

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA TATU**

**Kikao cha Kumi na Saba – Tarehe 27 Aprili, 2021**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nawaomba tukae. Tunaendelea na Kikao chetu cha Kumi na Saba leo lakini ndani ya Mkutano wetu wa Tatu, Katibu.

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:**

Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA - K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) kwa mwaka wa fedha 2020/2021 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

**MHE. DKT. ALFRED J. KIMEA - K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kuhusu utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

**SPIKA:** Ahsante sana. Katibu.

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**SPIKA:** Tunaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI na swali la Mheshimiwa Prof. Patrick Ndakidemi, Mbunge wa Moshi Vijijini.

Na. 139

**Barabara ya Rau Madukani – Mamboleo - Shimbwe  
Juu - Moshi Vijijini**

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais wakati wa Kampeni za Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2015 ya ujenzi wa kiwango cha lami barabara yenye kilometa 13

kuanzia Rau Madukani – Mamboleo – Shimbwe Juu katika Jimbo la Moshi Vijijini?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri, David Silinde, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Profesa Patrick Alois Ndakidemi, Mbunge wa Jimbo la Moshi Vijijini, kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kutekeleza ahadi zilizotolewa na Waheshimiwa Marais walizozitoa katika Awamu zote. Katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 na 2019/2020 Serikali imeendelea kujenga kipande cha barabara chenye urefu wa mita 288 kwa kiwango cha lami kwa gharama ya shilingi milioni 190 kwa barabara ya Rau Madukani – Mamboleo - Shimbwe Juu. Aidha, katika mwaka wa fedha 2018/2019, barabara hi ilifanyiwa matengenezo ya muda maalum yenye urefu wa kilometa 9 kwa kiwango cha changarawe ambayo iligharimu shilingi milioni 148.85. Vilevile katika mwaka wa fedha 2021/2022 barabara hii imetengewa bajeti ya shilingi milioni 10 kwa ajili ya matengenezo ya sehemu korofi yenye urefu wa kilometa 2.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea na ujenzi na matengenezo ya barabara nchini ikiwemo Moshi Vijijini kwa kadri ya upatikanaji wa fedha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Profesa Ndakidemi, swali la nyongeza.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa fursa ya kuuliza maswali ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kutokana na jiografia ya Mkoa wa Kilimanjaro, niseme ukweli kwamba changamoto yetu kubwa

kule Kilimanjaro ni barabara hasa Jimbo langu la Moshi Vijijini na wakati wa mvua kama huu kuna mafuriko makubwa sana. Naomba nimuulize Naibu Waziri ni lini Serikali itaanza ujenzi wa barabara ya TPC – Mabogini – Kahe yenye urefu wa kilometa 11.4 na kumalizia zile za *Kibosho Shine* - Kwa Raphael - *International School* - Kiboriloni - Sudini – Kidia?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, Serikali ilishasema ingeanza upembuzi yakinifu wa barabara ya Uru – Mamboleo - Materuni yenye kilometa 10.2, ni lini Serikali itafanya zoezi hilo. Ahsante. (*Makofi*)

**SPIKA:** Sasa Profesa, kwenye swali lako la msingi lilihusu hii barabara ya kilometa 13 kwenye nyongeza umeuliza barabara zingine kabisa, hii wala hujaigusa maana yake umeridhika na swali. Kwa hiyo, Naibu Waziri, jibu lile la pili.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu maswali madogo ya nyongeza ya Mheshimiwa Profesa Patrick Alois Ndakidemi, Mbunge wa Moshi Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama ulivyoniongoza, umeniomba nimjibu Mheshimiwa Mbunge kuhusu ni lini upembuzi yakinifu utaanza katika barabara ya Uru – Mamboleo – Materuni yenye urefu wa kilometa 10.2.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Rais makini kabisa Mama Samia Hassan Suluhu, tumesikiliza maombi ya Mheshimiwa Mbunge. Kwa sababu ameomba tu upembuzi yakinifu na nafahamu mpaka muda huu *TARURA* wananisikiliza ni agizo langu kwao kwamba sasa watenge fedha waanze upembuzi yakinifu kwa ajili ya barabara hiyo ili iweze kujengwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia hizo barabara nyingine zote ambazo ameziainisha, Serikali imesikia tutaziweka katika Mpango kuhakikisha zinakamilika kwa wakati. Ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Bado tuko TAMISEMI, swali la Mheshimiwa Felista Deogratus Njau.

Na. 140

### **Kero ya Mafuriko Jimbo la Kawe**

**MHE. FELISTA D. NJAU** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kutatua tatizo la mafuriko katika maeneo ya Mbweni Teta, Bunju Basihaya, Kunduchi, Nyamachabes, Ununio na Mikocheni katika Jimbo la Kawe?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa David Silinde, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Felista Deogratus Njau, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua changamoto ya mafuriko katika maeneo ya Mbweni Teta, Bunju Basihaya, Kunduchi, Nyamachabes, Ununio na Mikocheni katika Jimbo la kawe. Serikali kupitia Mradi wa kuboresha Miundombinu katika Jiji la Dar es Salaam (*DMDP*) imetenga shilingi bilioni 8.4 kwa ajili ya ujenzi wa mfereji wa maji ya mvua wenye urefu wa kilomita 8.89 katika Kata ya Mbweni. Awamu ya pili ya mradi huu itajumuisha mifereji ya maji ya mvua katika maeneo ya Kunduchi, Nyamachabes, Ununio na Mikocheni.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kujenga na kukarabati miundombinu ya barabara, madaraja na mifereji ya maji ya mvua ili kuondoa kero ya mafuriko katika maeneo mbalimbali Jijini Dar es Salaam ikiwemo Jimbo la Kawe.

**SPIKA:** Swali la nyongeza, nimekuona Mheshimiwa Felista.

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa sababu mpaka sasa kuna kaya kumi ambazo maji yameingia ndani na hawana pa kuishi katika Mtaa wa Ununio, Serikali ina mkakati gani wa dharura kabla ya kutekeleza mradi huu alioutaja ili kuhakikisha wananchi hawa wanapata mahali pa kuishi na sehemu zile nilizoainisha zinapata majibu mapema? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kilio hiki ni cha nchi nzima kwa maana matatizo haya yamekuwa yanajirudia kila eneo la nchi; ni lini basi Serikali itaweka mikakati madhubuti ya kujenga mifereji imara ili basi maeneo haya maji yaweze kuelekezwa kwenda kwenye maziwa, mito hata bahari ili kuepuka adha ya magonjwa ya milipuko pia na adha kwa wananchi? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Naibu Waziri-TAMISEMI, Mheshimiwa David Silinde, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE)** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu maswali madogo mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Felista Deogratius Njau, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza alikuwa anaomba kujua upi ni mkakati wa dharura katika eneo la Ununio ambao Serikali imeuweka kuhakikisha tunatatua tatizo hilo la mafuriko. Nimuambie tu kabisa kwamba Serikali iko kazini na baada ya janga hili inafanya tathmini ya mwisho kuhakikisha kwamba tunasaidia maeneo hayo hususan maeneo ya Ununio katika Kata hizo ambazo Mheshimiwa Mbunge ameziainisha.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili Mheshimiwa Mbunge ameuliza ni lini Serikali itaweka mikakati madhubuti kuhakikisha kwamba tunaondoa majanga haya hususan kwa kujenga mifereji. Nimhakikishie kabisa kwamba sasa hivi moja ya mkakati mkubwa ambao Serikali unao katika kila barabara tunayojenga tunaambatanisha na ujenzi wa miundombinu hususan mifereji. Kwa hiyo, hiyo ni sehemu ya mikakati ambayo ipo na tutaendelea kufanya hivyo. Kwa kadri fedha zitakavyopatikana tutajenga mifereji mikubwa pamoja na midogo kuhakikisha janga la mafuriko nchi nzima katika maeneo yote ambayo tunayasimamia hayapatwi na hii adha ambayo Mheshimiwa Mbunge ameianisha. Ahsante sana.

**SPIKA:** Bado tuko Wizara hii hii, tunaendelea na swali la Mheshimiwa Aloyce John Kamamba, Mbunge wa Buyungu.

Na. 141

**Ahadi ya Barabara ya Kilometa Tatu Katika  
Mji wa Kakonko**

**MHE. ALOYCE J. KAMAMBA** aliuliza:-

Mwaka 2015 wakati wa Kampeni, Mhe. Rais aliahidi kujenga barabara ya kilometa tatu katika Mji wa Kakonko ambao ndiyo Makao Makuu ya Wilaya.

Je, kwa nini ahadi hiyo haijatekelezwa na ni lini sasa itatekelezwa?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Naibu Waziri-TAMISEMI, Mheshimiwa David Silinde, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa

Aloyce John Kamamba, Mbunge wa Jimbo la Buyungu, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali imeanza kutekeleza ahadi ya aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tano, Hayati Dkt. John Joseph Pombe Magufuli kwa awamu. Katika mwaka wa fedha 2020, Serikali imeanza ujenzi wa barabara yenye urefu wa mita 630 kwa kiwango cha lami katika Mji wa Kakonko itakayogharimu shilingi milioni 500. Ujenzi huu umefikia asilimia 80 na unatarajiwa kukamilika mwezi Mei 2021.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya barabara nchini ikiwemo Wilaya ya Kakonko kwa kadri ya upatikanaji wa fedha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kamamba, Mbunge wa Kakonko, tafadhali.

**MHE. ALOYCE J. KAMAMBA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Ujenzi huu ni ahadi ya muda mrefu, ni miaka sita sasa lakini kama ambavyo ameweza kutoa majibu utekelezaji wake umeanza kwa kuweka kifusi katika Mji ule wa Kakonko. Ni miezi minne sasa shughuli za biashara katika Mji ule hazifanyiki, je, Serikali iko tayari angalau kifusi kiweze kusawazishwa katika maeneo yale ili wananchi waendeleo na shughuli zao wakati taratibu hizo nyingine zikifanyika?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, barabara ya Kakonko – Kinonko – Nyakayenze - Muhange na Kasanda - Gwanumpu - Mgunzu ni barabara ambayo iko chini ya *TARURA*. Barabara hii imeharibika sana pamoja na kwamba ni maeneo ambayo yana uzalishaji mkubwa, wananchi hawawezi kusafirisha mazao yao. Je, nini jibu la Serikali kuhusiana na suala hili? Ahsante. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Aloyce John Kamamba, Mbunge wa Buyungu. Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Profesa Ndakidemi wakati wewe unalia na lami ya nyongeza Moshi mwenzako anaomba kilometa 3 katikati



ya Kakonko ambayo ndiyo Makao Makuu ya Mji. Sisi Kongwa pia tunaomba kilometa 2 au 3 katikati ya Mji, ndiyo muone *disparity* katika nchi yetu ilivyo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu maswali madogo mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Aloyce John Kamamba, Mbunge wa Jimbo la Buyungu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge anaiuliza Serikali kwamba ni kwa nini sasa tuisambaze kile kifusi ili shughuli zingine ziendele. Kama nilivyoeleza katika jibu langu la msingi ni kwamba barabara ile inajengwa kwa kiwango cha lami, kwa hiyo, kile kifusi ni sehemu tu ya *process* za kukamilisha barabara ile. Kama tulivyojibu kwenye jibu la msingi kwamba kufikia mwezi Mei, yaani mwezi ujao ile barabara itakuwa imekamilika kwa kiwango cha lami kwa sababu *TARURA* wako kazini. Hapa napozungumza wanasikia, nina hakika hilo zoezi litakuwa linaendelea na kazi inafanyika.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ameanisha barabara ambazo zimeharibika sana na kuiomba Serikali iweze kuzifanyia kazi. Nimwambie tu kwamba tutatuma wataalam wetu waende wakafanye tathmini na baada ya hapo nafikiri sisi na *TARURA* katika ngazi ya Halmashauri ya Wilaya ya Kakonko tutakaa pamoja kuhakikisha barabara hiyo inajengwa ili kuondoa hiyo adha ambayo wananchi wanaipata. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante.

Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea, naomba niwataarifu kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu hatuko naye hapa mjengoni kwa sasa, shughuli za Kiserikali mlizonazo zipelekeni kwa Mheshimiwa William Lukuvi, nashukuru sana. (*Makofi*)

Nimekuona Mheshimiwa Asia Halamga, swali la nyongeza.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa ahadi hii ya Mheshimiwa Rais ya ujenzi wa barabara kule Kakonko inafanana kabisa na ahadi ya Mheshimiwa Rais katika barabara ya Boay – Gidas hadi Getasam, Wilaya ya Hanang, lakini barabara ya Boay – Gidas, barabara ya Babati Vijijini: Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi huu wa barabara kwa kiwango cha lami?

Mheshimiwa Spika, kwa sababu, sasa hivi barabara hiyo imekuwa ni chakavu kabisa na haiwezi kupitika: Je, Serikali inatuhidi nini hata kutusaidia kwa kiwango cha changarawe? Ahsante sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa TAMISEMI, Mheshimiwa Silinde, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Ambacho amejaribu kukiainisha Mheshimiwa Mbunge; ni lini Serikali itaanza kukamilisha ahadi za Mheshimiwa Rais, Hayati Dkt. John Pombe Magufuli na Marais wote waliotangulia na hapa amejaribu kuainisha barabara katika maeneo ya Hanang na Babati Vijijini.

Mheshimiwa Spika, nikuhakikishie kwamba mpaka sasa hivi Ofisi ya Rais, TAMISEMI pamoja na Serikali kwa ujumla tumeanza mchakato wa kuziainisha ahadi zote zilizotolewa na viongozi wakubwa nchini. Baada ya hapo tutazifanyia tathmini, tutazitenga katika mipango yetu na kuziwekea bajeti ili kuhakikisha kila ahadi ambayo kiongozi mkubwa aliahidi inatekelezwa na kwa wakati ili kuhakikisha kwamba tunawasaidia wananchi, hususan maeneo yale ambayo yana-*involve* sana uzalishaji mkubwa kwa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante. Wizara ya Kilimo Waheshimiwa Wabunge, swali la Mheshimiwa Neema William Mgaya.

Na. 142

### **Zao la Parachichi Kuwa Zao la Mkakati**

**MHE. NEEMA W. MGAYA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuliingiza zao la parachichi katika mazao ya kimkakati kutokana na zao hilo kuiingiza nchi fedha za kigeni?-

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo. Naibu Waziri Kilimo, Mheshimiwa Hussein Bashe tafadhali, kuhusiana na zao la parachichi.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Neema William Mgaya, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, parachichi ni miongoni mwa mazao ya bustani ambayo yanapewa kipaumbele katika Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (*ASDP II*) kutokana na umuhimu wake katika kuongeza kipato na lisho kwa wakulima na jamii kwa ujumla. Zao hilo ni miongoni mwa mazao yanayokua kwa kasi na limeonesha mafanikio makubwa.

Mheshimiwa Spika, aidha, mauzo ya parachichi nje ya nchi yameongezeka kutoka tani 3,279 mwaka 2015 hadi tani 9,000 mwaka 2018. Mauzo hayo yameilingizia Taifa kiasi cha Dola za Marekani milioni 8.5 kutokana na masoko ya nchi za Ufaransa, Uholanzi, Uingereza na Kenya.

Mheshimiwa Spika, zao la parachichi limeingizwa tayari kuwa miongoni mwa mazao ya kimkakati na wizara ipo katika hatua za awali za mapendekezo ya kuanzishwa

kwa Mamlaka ya Mazao ya Bustani (*Hotculture Development Authority*) ambayo itakuwa na jukumu la kusimamia mazao ya bustani likiwemo zao la parachichi ili kuongeza tija na kukidhi mahitaji ya soko la ndani, kikanda na Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali inaendelea kukamilisha mkakati wa kuendeleza tasnia ya mazao ya bustani ya mwaka 2021 – 2030 utakaotumika kama dira ya kuwekeza katika Sekta ya *Horticulture* itakayojumuisha zao la parachichi. Mkakati huo umehusisha wadau wote muhimu kwenye mnyororo wa thamani wa mazao ya *horticulture*.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha gharama za usafirishaji wa mazao ya *horticulture* ikiwemo parachichi zinapungua, Serikali ipo katika hatua za awali kuanzisha Kituo cha Huduma za Biashara ya Mazao ya Kilimo (*Agricultural Logistics Hub*) kwenye eneo la ekari 20 katika ukanda maalum wa uwekezaji (*Export Processing Zone – EPZ*) Kurasini, Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, kwa kushirikiana na sekta binafsi, TAHA kwa maana ya TPSF, TAHA na Wizara ya Viwanda na Biashara, kituo hicho kitakuwa ni kituo cha huduma ya pamoja (*One Stop Centre*) chenye wataalam na miundombinu ya mnyororo wa baridi (*cold chain*) wa kuhifadhi mazao kabla ya kusafirishwa kwenda nje ya nchi kwa bei nafuu tofauti na hali ilivyo sasa ambapo baadhi ya mazao hulazimika kusafirishwa kupitia Uwanja wa Ndege wa Nairobi ama Bandari ya Mombasa kwa kuwa na mindombinu thabiti.

Mheshimiwa Spika, kutekelezwa kwa mkakati wa kuendeleza mazao ya bustani na kuanzishwa kwa mamlaka ya kusimamia mazao hayo likiwemo zao la parachichi kutaongeza tija na mchango mkubwa katika pato la mkulima na Taifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Neema, swali la nyongeza.

**MHE. NEEMA W. MGAYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. Nataka kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa kuna umuhimu na mmeshaanza kufanyia kazi suala la *Kurasini Logistic Hub* kwa ajili ya mazao ya *horticulture* ili kuweka mfumo huo wa *cold chain*; Serikali mmejipanga vipi kwa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini kwa sababu, ndiko wakulima wakubwa wa zao hili la parachichi waliko? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Serikali imejipanga vipi kuhakikisha kwamba wanaweka mfumo wa ubaridi kwenye reli ya *TAZARA* ili kuendelea kuwasaidia wakulima hawa kusafirisha parachichi zao kwa bei nafuu kwenda kule Kurasini kwa ajili ya kupelekwa nje kwa kutumia Bandari ya Dar es Salaam; na vilevile kuhakikisha kwamba parachichi zao na mazao mengine ya mbogamboga yanafika yakiwa na ubora?

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kuna umbali wa kutoka Nyanda za Juu Kusini mpaka Kurasini kule Dar es Salaam kitu ambacho bado kinaweza kukasababisha mazao yale yakakosa ubora: Je, mmejipanga vipi kama Serikali kuhakikisha kwamba mnaweka mfumo wa ubaridi katika mabehewa haya ya *TAZARA*?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Kwa kuwa zao hili limeonyesha linaingiza pato kubwa Tanzania; Serikali imejipanga vipi kuhakikisha kwamba wakulima wale wanaendelea kulima kwa ubora kwa kuwapelekea mbolea na kuwasimamia katika suala zima la uzalishaji wa zao la parachichi?

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri Kilimo, mmejipangaje?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba zao la parachichi na *subsector* ya *horticulture* ni moja kati ya sekta zinazokua kwa kiwango kikubwa na inaajiri

watu wengi sana hasa vijana, akina mama na *middlemen* wameanza kwenda katika maeneo haya. Tunafanya nini?

Mheshimiwa Spika, cha kwanza, hivi karibuni Wizara ya kilimo kupitia Waziri wetu, Profesa Mkenda amekutana na *representative* wa *European Business Council* kwa ajili ya ku-*attract private sector* kuja kuwekeza kwenye *cold chain* ikiwemo mabehewa yenye ma-*fridge* kwa ajili ya reli ya TAZARA na hata reli yetu kuelekea upande wa Kaskazini kwa sababu ni maeneo ya uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, vilevile *pilot* katika Wilaya ya Njombe, tumeanzisha *centre* ya kwanza ambayo imekuwa ni mradi uliofanywa na Wizara ya Kilimo, Tanzania *Horticulture Association* na Halmashauri ya Njombe kuweka *park house* ya kwanza ikiwa ya majaribio na imeonesha mafanikio.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa kama Wizara tunaangalia uwezekano wa ku-*attract* sekta binafsi ili iweze kuwekeza katika maeneo haya ambayo yanakuwa kwa kiwango kikubwa na wengi wameonesha *appetite* na wamekuja kuongea nasi. Nasi tunatumia Bunge lako Tukufu kuwaomba na kuendelea kuwahamasisha wawekezaji wa Kitanzania waweze kuwekeza. Hata hivyo Kurasini itaunganishwa na Njombe ili tuweze ku-*process* katika *primary level* na tuweze kupeleka Kurasini kwa ajili ya kuingiza kwenye meli.

Mheshimiwa Spika, kuhusu tumejipanga vipi kwenye kuwasaidia wakulima; sasa hivi hatua ambayo tunachukua na lilitolewa agizo na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba katika maeneo yote ya uzalishaji hasa ya maeneo ya Nyanda za Juu Kusini, halmashauri zote zimeagizwa zitenge maeneo kwa ajili ya kuzalisha miche ambayo itatumika kuwagawia wakulima.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi wakulima wananunua karibu na shilingi 5,000/= kwa mche mmoja, lakini hatua ya pili tuliyochukua kwenye eneo la miche ni kwamba, tumeanza kuwasajili wazalishaji wote wa miche ambao ni

wazalishaji wadogo wadogo na kuwaunganisha na kituo chetu cha Uyole ili kuweza ku-*protect* mbegu ya hasi ambayo ndiyo mbegu yenye thamani kubwa katika soko la dunia.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Wizara sasa hivi tunavyomalizia huu mkakati wa kutokea 2021 mpaka 2030, itakuwa ni *road map* ambayo itaonesha ushiriki wa Serikali, ushiriki wa sekta binafsi na hatua tutakazochukua kwa ajili ya kuhakikisha kwamba sekta hii tunailinda na kuipatia vivutio vyote ili viweze kumsaidia mkulima na kuongeza pato la Taifa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Musukuma nimekuona, kuna parachichi huko pia?

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa zao la parachichi ni zao ambalo linasifika na linaingiza kipato kikubwa kwenye Taifa letu, ni sawa sawa kabisa na zao la nanasi lililoko jimboni kwangu. Zao hili linaonekana kama tunda tu la kuliwa holela holela, lakini ukienda kwenye masoko kama Dubai linauzwa mpaka dola 30 wakati kwetu Usukumani linauzwa shilingi 200/= mpaka shilingi 500/=.

Je, Wizara mmejipangaje kutusaidia wakulima wa mananasi, hasa kwenye Jimbo la Geita Vijijini ili nalo liwe na soko kama soko la parachichi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya, mananasi, Mmejipangaje Wizara ya Kilimo? Naibu Waziri Kilimo, Mheshimiwa Bashe.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, Mkoa wa Geita ni mmoja kati ya mikoa inayozalisha nanasi na vilevile katika mikoa mingine kama ya Pwani, Wilaya ya Chalinze na Wilaya ya Bagamoyo ni miongoni mwa wilaya zinazozalisha nanasi kwa kiwango kikubwa. Hatua tunayochukua sasa hivi kama Wizara, cha kwanza, ili kuweza ku-*meet international standards* na mazao yetu ya matunda yaweze kuuzwa katika masoko ya Kimataifa na vilevile

yaweze kukidhi mahitaji ya viwanda vyetu vya ndani vya *juice*; hatua tunayochukua sasa hivi kama Wizara, tumewaagiza *TARI* ili kuweza kuzalisha mbegu ambazo zitakidhi viwango vya viwanda na kukidhi ubora unaostahili kuweza kumsaidia mkulima.

Mheshimiwa Spika, changamoto tuliyonayo katika *subsector* ya matunda ya nanasi na machungwa, kwa muda mrefu kumekuwa hakuna uwekezaji wa kutosha tuliofanya kama nchi katika eneo hili kwa sababu lilikuwa halionekani kama ni eneo la kimkakati. Kama Wizara, sasa hivi sekta ya matunda na mbogamboga imepewa kipaumbele kikubwa na tumeagiza *TARI* Selian kuwa ndiyo kituo halisi kwa ajili ya kufanya *research and development*.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti yetu Mungu akijalia mwezi ujao mtaona kwamba, uwekezaji tunauweka katika *research and development* ili mazao ya mananasi na matunda yaweze kukidhi mahitaji ya soko la ndani na soko la Kimataifa na viwanda vyetu viweze kupata matunda wanayostahili.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi tuna soko la Shinyanga, Jambo amefungua kiwanda cha ku-*process* nanasi. Tunamhakikishia Mheshimiwa Musukuma, mimi mwenyewe nitachukua hatua ya kuwaunganisha wakulima wake moja kwa moja waweze kuuza kwa Jambo pale Shinyanga. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Musukuma kule duniani wanataka vinanasi vile vidogo vidogo, tena vichunguchungu wala siyo vitamu. Sijui hawa wenzetu Ulaya wana matatizo gani? Yale ya kwako makubwa kuliko kichwa changu yale, hayana soko sana, yana soko hapa Dodoma kwa Wagogo hapa.

Mheshimiwa Mbunge wa Kasulu Vijijini, Mheshimiwa Augustine Vuma Holle, uliza swali lako kwa Wizara ya Mambo ya Ndani.



Na. 143

**Mgogoro wa Ardhi Kambi ya Wakimbizi  
Nyarugusu**

**MHE. ALOYCE J. KAMAMBA K.n.y. MHE. AUGUSTINE V. HOLLE** aliuliza:-

Kumekuwa na mgogoro wa ardhi wa muda mrefu baina ya Kambi ya Wakimbizi ya Nyarugusu na Kata ya Makere:-

Je, ni lini Serikali itatatua mgogoro huo?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Hamza Khamis Khamis, majibu tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya ndani ya Nchi, naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Augustine Vuma Holle, Mbunge wa Kasulu Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Wakimbizi ya Nyarugusu ilianzishwa mwaka 1996 kwa ajili ya kupokea wakimbizi kutoka nchi ya *DRC*. Wakati wa uanzishwaji wa kambi hiyo hakukuwa na mgogoro wa ardhi kwa sababu lilikuwa ni eneo lisilotumika. Aidha, pamoja na eneo la kambi, Serikali ilitenga eneo lingine la kambi kwa ajili ya wakimbizi iwapo eneo la awali litazidiwa.

Mheshimiwa Spika, kadiri ya muda ulivyoenda, wananchi walianza kuvamia eneo la akiba kwa lengo la kuwatumia wakimbizi kama vibarua katika shughuli za kilimo katika eneo hilo. Kwa kuzingatia maelezo hayo, ni wazi kuwa hakuna mgogoro wa ardhi baina ya Kambi ya Nyarugusu na Kata ya Makere, bali ni suala la uelewa ambapo wananchi wanaendelea kuelimishwa juu ya matumizi sahihi ya eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na jitihada za kumaliza tatizo la wakimbizi nchini kwa kuwarejesha wakimbizi makwao kwa kushirikiana na Jumuiya za Kimataifa na nchi wanazotoka wakimbizi hao. Baada ya wakimbizi hao kuondoka maeneo yote ya kambi za wakimbizi yatarejeshwa Serikalini ili mamlaka zinazohusika ziweze kuyapangia matumizi stahiki.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge wa Buyungu, uliza swali la nyongeza.

**MHE. ALOYCE J. KAMAMBA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza. Kutokana na kuwepo kwa mgogoro huo kwa muda mrefu, Mheshimiwa Waziri yuko tayari sasa kwenda eneo lenyewe la mgogoro ili aweze kujionea hali halisi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Je, ikidhihirika kwamba katika utaratibu huo wa kugawa mipaka kuna makosa ambayo yatakuwa yamejitokeza wakati huo: Serikali iko tayari kuchukua hatua kwa wale ambao watakuwa wamekiuka taratibu za utoaji mipaka?

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo mawili, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Hamza Khamis Khamis.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, swali la kwanza la Mheshimiwa Kamamba ni: Je, nipo tayari kwenda katika eneo hilo ili nikajionee mwenyewe huo mgogoro? Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, ndani ya kipindi hiki cha Bunge la Bajeti nikipata nafasi ambayo itaniruhusu kuweza kwenda kwa sababu ni sehemu ya wajibu wangu kuyajua, kuyaona na kusikiliza changamoto za wananchi, nimhakikishie tu kwamba naenda kupanga ratiba na nitajitahidi nimjulishe tuweko pamoja ili kwa kushirikiana na maafisa kutoka hiyo Idara ya Wakimbizi, tuone namna ambavyo tunaenda kutatua hiyo

changamoto ambayo kwa sasa wananchi inawakabili. Kwa hiyo, kwa ufupi ni kwamba, nipo tayari kufuatana naye kwenda katika eneo.

Mheshimiwa Spika, swali lingine ni: Je, ikidhihirika kama kuna makosa kuna watu wamefanya mambo mengine, mengine, Serikali ipo tayari kuchukua hatua? Serikali ipo kwa ajili ya kuwatetea, kuwasemea na kwa ajili ya kutatua changamoto za wananchi. Tumegundua kuna baadhi ya mambo yanafanywa na baadhi ya maafisa au baadhi ya watu ambayo yanavunja utaratibu na sheria katika maeneo haya. Kama Serikali tuko tayari kuchukua hatua ili kuhakikisha kwamba wengine wawe ni funzo na wasiendeleo kufanya makosa hayo.

Mheshimiwa Spika, kikubwa nimwambie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba wakimbizi hawa tuliamua kuwapokea kwa sababu ya Mkataba wa Kimataifa ambao tuliukubali sisi wenyewe, kwamba ikitokea machafuko katika nchi fulani, basi kama wakija na tuki-*prove* kwamba kweli kuna tatizo, sisi tunawapokea.

Mheshimiwa Spika, pia tulikubaliana kwamba migogoro ikimalizika katika maeneo yao, sisi tupo tayari kuwarejesha katika maeneo yao kwa kushirikiana na mashirika na kwa kushirikiana na nchi zao.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimwambie tu kwamba eneo hili ikitokea wakimbizi hawa wameondoka na ikawa hakuna machafuko, maana yake ni kwamba eneo hili tutalirejesha kwa Serikali, halafu Serikali itaona namna ya kufanya. *Unless* ikitokea fujo nyingine huko kwenye nchi za wenzetu ikawafanya wakimbizi waje, tutawapokea na kuwahifadhi.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

**SPIKA:** Ahsante. Tuelekee katika Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Swali la Mheshimiwa Angelina Adam Malembeka, uliza swali lako. (*Makofi*)

Na. 144

### Huduma ya Ulinzi kwa SUMA JKT

**MHE. ANGELINA ADAM MALEMBEKA** aliuliza:-

Je, ni gharama kiasi gani na taratibu gani hutumika ili kupata huduma za ulinzi za SUMA JKT?

**SPIKA:** Majibu ya Serikali kwenye swali hilo, Mheshimiwa *Engineer* Elias John Kwandikwa, Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, tafadhali.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Angelina Adam Malembeka, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, huduma ya Ulinzi toka *SUMA JKT Guard* inapatikana kupitia njia kuu nne, ikiwemo:-

(1) Idara ya masoko kutembelea wadau wa huduma ili kutangaza shughuli za kampuni;

(2) Mteja mwenyewe kuwasilisha barua za maombi ya kupatiwa huduma ya ulinzi;

(3) Kampuni imesajiliwa katika mfumo wa manunuzi ya Serikali ya *TANEPS* ambapo wadau, hasa Taasisi za Serikali hutumia kutangaza zabuni.

(4) Ushiriki katika mchakato wa zabuni shindanishi zinazotangazwa kupitia magazeti na vyombo vya habari.

Mheshimiwa Spika, naomba nifafanue zaidi kuwa gharama ya kupata huduma za ulinzi za *SUMA JKT Guard* kwa mlinzi mmoja bila silaha ni shilingi 590,000 kwa mwezi ikijumuisha *VAT*, lakini silaha moja ni shilingi 129,800 hivyo mlinzi akiwa na silaha, gharama yake ni shilingi 719,800 kwa mwezi.

Huduma ya mlinzi mmoja kwa maeneo ya migodini ni shilingi 944,000/= ikiwa ni pamoja na VAT kwa mwezi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Malembeka.

**MHE. ANGELINA ADAM MALEMBEKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Swali langu la kwanza; kwa kuwa Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Tano Hayati Dkt. John Pombe Magufuli alitoa maagizo, taasisi na kampuni za Serikali kutumia Kampuni ya Ulinzi ya SUMA JKT. Je, hadi sasa ni makampuni mangapi au Taasisi ngapi za umma au Serikali zinazotumia Ulinzi wa SUMA JKT? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili; je ni fedha kiasi gani hadi sasa Kampuni ya SUMA JKT inadaidai kwa wateja wake? Ahsante. (*Makofi*)

**SPIKA:** Hilo la pili sina uhakika nalo sana, Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi - Mheshimiwa Elias Kwandikwa, majibu tafadhali.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali ya nyongeza la Mheshimiwa Angelina Malembeka kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze na kumshukuru sana Mheshimiwa Malembeka kwa namna ambavyo anafuatilia maelekezo ya viongozi wakuu, lakini pia kufuatilia maendeleo hususan ya *SUMA JKT*. Kwa kujibu maswali yake niseme tu baada ya maelekezo ya Amiri Jeshi Mkuu Hayati Dkt. John Pombe Magufuli kuyatoa juhudi zimefanyika mpaka sasa idadi ya malindo 443 tunayo, ikiwemo malindo 259 ya Taasisi za Serikali na Mashirika ya Umma na malindo 184 ya watu binafsi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali lake la pili, ni kweli kwamba baada ya maelekezo yale tumefanya ufuatiliaji kama Wizara kulikuwa na rekodi ya madeni ya shilingi bilioni kama kumi na mbili na milioni mia tano (12,500,000,000) hivi,

lakini baada ya uhakiki, deni hilo lilikuwa kwenye bilioni kumi na mbili na milioni tisini na sita (12,096,000,000), lakini kwa juhudi zilizofanyika asilimia 70 ya madeni yale ya kama bilioni nane na milioni mia tano (8,500,000,000) hivi zimeshalipwa. Bado tunalo deni kama la bilioni tatu nukta tano (3,500,000,000). Kwa hiyo, niendeleo kuwashukuru wateja wetu kwa kutupa kazi, lakini niwashukuru pia kwa kuendelea kufanya malipo.

Mheshimiwa Spika, pia niwaombe wateja wetu waendeleo kufanya malipo ya madeni haya kwani yapo manufaa makubwa kwamba tunapokusanya fedha hizi tunaendelea kuongeza ajira mbalimbali kwa vijana wetu lakini pia kadri tunavyoongeza huduma hizi za ulinzi, usalama kwenye mitaa unaongezeka kwa sababu pale ambapo tuna walinzi wetu wa SUMA JKT, ni msaada mkubwa kwa maeneo pia ya jirani na malindo yao. Kwa hiyo tunaendelea kupata manufaa makubwa, lakini kubwa zaidi pia tunaongeza uchumi katika nchi yetu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Tuelekee Madini sasa nimwite Mheshimiwa Mbunge wa Ngara, Mheshimiwa Ndaisaba Ruhoro.

Na. 145

### **Wananchi wa Ngara Kunufaika na Uchimbaji wa Madini ya Nickel**

**MHE. NDAISABA G. RUHORO** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba Wananchi wa Jimbo la Ngara wananufaika na uchimbaji wa Madini ya *Nickel* unaotarajia kuanza katika eneo la Kabanga?

**SPIKA:** Majibu wa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Madini, Profesa Shukrani Manya, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ndaisaba George Ruhoro, Mbunge wa Jimbo la Ngara, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Mbunge Mheshimiwa Ndaisaba kwa jinsi ambavyo anafanya ufuatiliaji kuhakikisha kwamba, wananchi wake wa Jimbo la Ngara wananufaika na mradi tarajiwa wa uchimbaji. Serikali imefanya mageuzi makubwa katika Sekta ya Madini kupitia Marekebisho ya Sheria ya Madini ya mwaka 2017 na kutungwa kwa sheria mpya za usimamizi wa rasilimali za Taifa kwa manufaa ya wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Madini, Sura 123, imeweka bayana kuwa, makampuni yote ya uchimbaji madini ni lazima yawasilishe mpango wa ushirikishwaji wa Watanzania katika miradi ya uchimbaji kwa maana ya *local content plan* ambao ni lazima ubainishe manufaa yatakayopatikana kwa wananchi kutokana na uanzishwaji wa miradi ya madini. Hivyo, kwa kuzingatia matakwa hayo ya Sheria, Serikali itahakikisha kwamba inachambua kikamilifu mpango utakaowasilishwa na Kampuni ya Tembo *Minerals Corporation Limited* inayotarajia kuwekeza katika mradi mkubwa wa uchimbaji wa madini ya *nickel* katika Jimbo la Ngara na kuusimamia kwa kushirikiana na Mamlaka zingine za Serikali kuhakikisha kuwa unatekelezwa na unaleta manufaa kwa wananchi wa Ngara na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, mbali na suala hili la *local content*, wananchi wa maeneo yanayozunguka mradi watanufaika kama ambavyo makampuni mengine yote yanafanya kupitia malipo ya ushuru wa Huduma kwa maana ya *Service Levy* lakini pia na miradi itakayotekelezwa kupitia mpango wa *Corporate Social Responsibility* kwa maana ya *CSR*.

Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Tume ya Madini itaandaa mpango mahsusi wa uendeshaji wa semina elekezi kwa wananchi wa Halmashauri ya Ngara na halmashauri yenyewe na maeneo jirani ili kuwawezesha kubaini fursa zilizopo ikiwa ni pamoja na bidhaa na huduma mbalimbali

ambazo wataweza kuzitoa katika mradi huo ili waweze kujiongezea kipato. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ndaisaba, swali la nyongeza tafadhali.

**MHE. NDAISABA G. RUHORO:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; kwa kuwa eneo hili la Kabanga *Nickel* kuna leseni nyingi zimechukuliwa hivi karibuni kuzunguka eneo hili. Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba leseni hizi zilizochukuliwa hazitazuia uwekezaji wa msingi wa Tembo *Nickel*?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kwa vile kuna tathmini ilifanyika hapo awali kwa ajili ya kutoa fidia kwa wananchi wanaoishi kuzunguka mgodi huu na kwa vile tathmini hii ambayo ilishafanyika, ilifanyika kipindi kirefu na hivyo imeshapoteza uhalali; je, Serikali ina mpango gani wa kurudia kufanya tathmini ili wananchi wanaounguka Mgodi huu wa Kabanga ambao kwa sasa unaitwa Tembo *Nickel* waweze kupata fidia? Ahsante. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Majibu wa maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Madini, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Ndaisaba, Mbunge wa Jimbo la Ngara, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, uwepo wa leseni zinazozunguka mradi tarajiwa wa uchimbaji wa Tembo *Nickel*, ni kwamba mtu anapokuwa amepewa leseni ana eneo ambalo lipo katika *coordinates* na kwa maana hiyo anachimba katika eneo lake na uwepo wa leseni nyingine zozote zinazozunguka eneo la mradi hauna uhusiano wa kuzuia uchimbaji wa mtu aliye na leseni yake. Ni sawa na upangaji tu wa nyumba mtu ana kiwanja chake utaingia nyumbani kwako na mimi nitaingia nyumbani kwangu.



Mheshimiwa Spika, nimhakikishe Mbunge kwamba kuwepo kwa leseni nyingine zozote zilizotolewa siku za karibuni hazitazuia kamwe uchimbaji unao tarajiwa wa mradi wa *Nickel*.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili ni kuhusu tathmini; ni kweli kwamba tathmini ilishafanyika siku za nyuma na ikipita miezi sita mara nyingi tathmini hiyo kisheria inaonekana kwamba haifai na hivyo inabidi kurudiwa. Katika miradi yote ya uchimbaji mkubwa hakuna mradi ulioanza bila kufanya tathmini na wananchi kulipwa malipo stahiki. Siku zote tunawaelekeza watu hawa wanaofanya miradi mikubwa ya uchimbaji waweze kuwa na *social license*, kwamba waweze kuwa na mahusiano mazuri na jamii inayowazunguka.

Kwa hiyo tutawaelekeza Tembo *Mineral Corporation* kwamba warudie kufanya tathmini na walipe fidia ili hatimaye mradi uweze kuanza. (*Makofi*) Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba Wananchi wa Jimbo la Ngara wananufaika na uchimbaji wa Madini ya Nickel unaotarajia kuanza katika eneo la Kabanga.

**SPIKA:** Tunaendelea na Maliasili na Utalii, swali la Mheshimiwa Joseph George Kakunda, Mbunge wa watu wa Sikonge.

Na.146

### **Wafugaji Kutopewa Risiti za Kielektroniki Wanapoingia Hifadhini – Sikonge**

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA** aliuliza:-

Je, ni kwa nini Serikali haitumii risiti za kielektroniki inapotoza faini za kuingiza mifugo kwenye Hifadhi zilizopo Sikonge.

**SPIKA:** Majibu wa swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Mary Francis Masanja, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Joseph George Kakunda, Mbunge wa Sikonge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu ya Sheria ya Wanyamapori Na.5 ya Mwaka 2009, ni kosa kwa mtu yeyote akiwemo mfugaji kuingiza mifugo kwenye maeneo yaliyohifadhiwa. Serikali iliweka sheria hii sio kwa ajili ya kujipatia mapato bali kudhibiti uharibifu ikiwemo uvamizi, ujangili na uingizaji wa mifugo ndani ya maeneo hayo kwa lengo la kuyatunza.

Mheshimiwa Spika, katika jitihada za kudhibiti upotevu wa mapato, Serikali ilianzisha mfumo wa *TEHAMA* kwa ajili ya utoaji wa leseni au vibali, ukusanyaji wa takwimu na mapato ya vyanzo mbalimbali vya Sekta ya Maliasili na Utalii unaoitwa *MNRT Portal* ambao umefungamanishwa na Mfumo wa *Government electronic Payment Gateway* yaani *GePG* kwa ajili ya kutoa *Control Number* inayomwezesha mteja sasa yeyote yule kulipa. Aidha, baada ya kufanya malipo hayo mfumo wa *MNRT Portal* unatoa risiti ambazo zinatambulika na Mamlaka ya Mapato Tanzania yaani *TRA*.

Mheshimiwa Spika, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa risiti zinazotolewa na mfumo huu ni halali kwa malipo ya Serikali sawa na zinazotolewa na mfumo wa *Electronic Fiscal Devices* yaani *EFDs*.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Kakunda, swali.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu ya Serikali ambayo yametolewa vizuri kwa ufasaha, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; sina tatizo na risiti za *MNRT Portal*, tatizo langu ni kwa nini mtozaji wa faini asipewe *post* maalum ili atoe risiti halali badala ya zile za kuandikwa kwa mkono?

Mheshimiwa spika, swali la pili, kwa nini Serikali isitoe mwongozo kwa halmashauri na *WMAs* zote ili fedha zilipwe kwenye *control number* maalum benki badala ya kubeba kwenye mabegi na kwenda kulipia porini? Ahsante sana.

**SPIKA:** Looo! Pesa zinabebwa wenye sandarusi, majibu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili. (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kakunda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza ameongelea ni kwa nini tusitoe risiti za kielektroniki badala ya kutoa risiti za mkono. Kama ambavyo nimejibu kwenye jibu langu la msingi ni kwamba miongozo yote ya sasa tunayofanya ni kwamba Serikali inapokea mapato ya aina yeyote ile kutumia risiti za *EFD* na kwa upande wa Maliasili na Utalii tunatumia hiyo *MNRT Portal* ambayo ndio tunayopokelea fedha kwa kutumia *control number*.

Mheshimiwa Spika, suala analoliongelea Mheshimiwa Mbunge ni kwenye hizi Jumuiya za Hifadhi ya Wanyamapori ambazo zinasimamiwa na Serikali za Mitaa kupitia halmashauri na tunazieleleza sasa halmashauri kwa kuwa fedha zake za jumuiya hizi zinakaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali waangalie sasa utaratibu wa kuhakikisha kwamba malipo yote yanayotokana na faini yapitie kwenye utaratibu wa Serikali yaani *EFD*.

Mheshimiwa Spika, kwenye upande wa mwongozo, mwongozo tulishautoa na utekelezaji wake unaendelea kufanyika isipokuwa usimamizi tu kama ambavyo amesema Mheshimiwa Mbunge kwamba imeonekana kuna wananchi wanabeba fedha kwenye mifuko. Tunatoa maelekezo sasa kwa halmashauri ambazo zinasimamia hizi jumuiya kuhakikisha kwamba usimamizi wa fedha za Serikali unapitia kwenye mifumo ya *TEHAMA* iliyoainishwa na Serikali, ambayo kwa Maliasili na Utalii tunatumia *MNRT Portal* ambayo inakusanya kwa kutoa *control number* na kwa wale

wanaotumia *EFD*, basi Halmashauri zisimamie suala hilo ili fedha hizi sasa ziweze kufika kwenye Mifuko husika na ubadhilifu usiweze kujitokeza. Naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mbunge wa Sikonge kule porini kule mtandao upo kule Sikonge msituni kule? Mheshimiwa Vita Kawawa nilikuona, halafu nimemwona Mheshimiwa Dkt na nimekuona Ester Bulaya.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kuwa tatizo la mifugo kuingia katika hifadhi za Sikonge linafanana kabisa na tatizo lililopo katika Wilaya ya Namtumbo kwenye eneo la Hifadhi ya Selous au sasa hivi Mwalimu Nyerere, mifugo mingi iliyofukuzwa kutoka Morogoro imeingia katika hifadhi hiyo na kuharibu *ecology* ya tembo na sasa tembo wamekuwa wanakuja katika vijiji wanapoishi wananchi na jana wameuwa Imam wa Msikiti katika Kijiji cha Luhangano, Kata ya Mputa, Je, Serikali itafanya nini kuondoa mifugo hiyo na kutuletea askari wakae kule moja kwa moja kuzuia tembo kuleta madhara ya vifo kama yaliyotolea jana?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Waziri Mwenyewe, samahani, Mheshimiwa Waziri majibu, tafadhali.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Kawawa kwa kazi nzuri anayowafanya wananchi wa Jimbo la Namtumbo.

Mheshimiwa Spika, ni kweli tumekuwa na changamoto ya mifugo kuingia katika hifadhi ambayo inasukuma wanyamapori wakiwemo tembo kuja sasa kwenye maeneo ya wananchi. Tunaendelea na *operation* ya kuondoa mifugo hiyo na kuwarudisha tembo katika maeneo yao stahiki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, *operations* zinaendelea jana tu tumefanya *operation* katika Wilaya ya Tunduru na msiba anaosema katika Kijiji cha Mputa tayari Maafisa

Wanyamapori watawa wapo Mputa hivi sasa kushughulikia suala hilo. Naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri mbona umenyamaza kuhusu fidia. Tunaendelea. Mheshimiwa Ester Bulaya nilikuona.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kumekuwa na *double standard*, mifugo inapoingia hifadhini sio tu wanatozwa fidia na wengine ni fidia kubwa na hata wale wafugaji wamekuwa wakipata mateso, lakini tembo wanapokwenda kuharibu mazao ya wananchi na nyumba za wananchi fidia yake ni kidogo, hususan wananchi wa Serengeti, Wananchi wa Tamau, wananchi wa Nyamatoke, Wananchi wa Kunzugu wote hao wapo kando kando ya Hifadhi ya Mbuga Serengeti. Je, ni lini sasa Serikali itarekebisha fidia ya tembo wanapoharibu mazao au mali za wananchi ili iendane na hali halisi kuliko ilivyo hivi sasa fidia ya Shilingi 100,000/= *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Mary Francis Masanja, tafadhali, usawa uko wapi?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ester Bulaya, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru sana Mbunge wa Viti Maalum Ester Bulaya kwa swali lake zuri. ni kweli kumekuwa na changamoto hii ya kwamba wafugaji wanatozwa fedha kubwa kwa maana ya kiwango ambacho kimewekwa kwenye sheria zetu hizi lakini inapokuja kwa mwananchi inaonekana kwamba Serikali haioni umuhimu.

Mheshimiwa Spika, lakini nimtoe wasi wasi Mheshimiwa Esther kwamba sisi tunachofanya ni kukemea uingizaji wa mifugo kwenye hifadhi na niwaombe wananchi ambao wanaishi kwenye maeneo ya pembezoni mwa hifadhi tembo hawa wanaangalia ni nini ulichopanda

kwenye maeneo hayo na tunawahamasisha wananchi wapande pilipili lakini pia waweke mizinga ya nyuki.

Mheshimiwa Spika, nasema hivyo hawa tembo na Wanyama wengine wana Serikali yao na Serikali yao hii na wenyewe wanajadili kama ambavyo tunajadili sisi hapa. Na ukumbuke maeneo mengi ambayo ni ushoroba wa wanyama sisi wananchi ndiyo tumeenda kuwafata kule hata wao wanatushangaa kwamba kwanini sisi maeneo yetu wananchi wameyasogelea. Ndivyo sasa sisi kama Serikali tunajitahidi angalau kuwa tunawaondoa wale tembo kuwarudisha kwenye maeneo ya hifadhi. Lakini tutambue kwamba wananchi ndiyo tunaowafuata hawa tembo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, lengo la kutoza hiki kiwango ni kuzuia hawa wafugaji sasa kutoingiza mifugo yao kwenye hifadhi, na niombe Waheshimiwa kwenye hili tushirikiane lisionekane kama ni la Wizara ya Maliasili ya Utalii sheria hizi tumezitunga sisi wenyewe na utekelezaji wake basi tutekeleze sisi wenyewe. Wafugaji wanaaswa kutoingiza mifugo yao kwenye maeneo ya hifadhi ahsante.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge nawaona lakini muda hauko upande wetu. Mheshimiwa Mbunge wa Longido nilikuwa nimekuahidi tangu mwanzo unaswali kwa Serikali ya tembo? (*Kicheko*)

**MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA:** Mheshimiwa Spika, ndiyo, ndiyo kabisa!

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na nitumie fursa hii kuiasa Wizara ya Maliasili na Utalii kwamba wanapofanya kila jitihada kuzuia mifugo isiingie ndani ya hifadhi hawafanyi juhudi kuzuia wanyama wasiingie ndani ya maeneo ya jamii.

Mheshimiwa Spika, kwa taarifa hiyo watambue pia kwamba mifugo na wanyamapori wote ni wanyama kuna maeneo ambayo wanaingiliana vizuri kiasi kwamba hata

ningependekeza kwamba maeneo ambayo hamna wanyamapori kama misitu asili mifugo waruhusiwe kulisha kwasababu wanatengeneza mazingira ya ekolojia ya majani katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, swali langu ni kwamba kwa vile kuna hako kafuta jasho au kifuta machozi hawa wanyama wanapoingilia katika maeneo ya jamii.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba hicho kifuta machozi au kifuta jasho kinawahishwa kwasababu kuna tabia ya kuiweka mpaka hata mtu anakuja kupewa ameshasahau na maumivu aliyoyapata?

**SPIKA:** Jibu la swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Maliasili na Utalii Mheshimiwa Mary Masanja.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ni kweli wananchi wanapokutana na adha hii ya tembo kuingia kwenye mashamba yao Wizara ya Maliasili na Utalii ina utamaduni wa kulipa kifuta jasho, na kifuta jasho kinategemea ni aina gani ya uharibifu uliofanyika.

Mheshimiwa Spika, kuna waliopata adha ya kupoteza maisha, lakini kuna wale ambao wamepoteza mazao huwa tunafanya tathmini pale tu ambapo tembo wanakuwa wameingia kwenye maeneo hayo na baada ya kufanya tathmini basi Serikali huwa inachukua jukumu la kulipa kifuta jasho.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka huu wa fedha tumetenga bilioni mbili kwa ajili ya kulipa kifuta jasho. Nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge kifuta jasho cha aina yoyote ambacho kinatokana na uvamizi wa tembo Serikali itakilipa ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana swali la mwisho kwa siku ya leo Waheshimiwa Wabunge ni la Mheshimiwa Antipas Zeno Mgungusi Mbunge wa Malinyi kwa Wizara hii hii ya Maliasili na Utalii Mheshimiwa Mgungusi tafadhali.

Na. 147

**Eneo Lililotwaliwa na TAWA Mwaka 2017 Malinyi**

**MHE. ANTIPAS Z. MGUNGUSI** aliuliza:-

Sehemu kubwa iliyokuwa ikitumika kwa shughuli za uchumi katika Wilaya ya Malinyi imetwaliwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA) mwaka 2017 ambapo waliweka mipaka maarufu kama "TUTA LA 2017" bila kushirikisha wananchi.

Je, Serikali haioni haja ya kurejea na kufanya upya mapitio shirikishi ya mipaka ya eneo hilo?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo bado tuko maliasili na utalii, Mheshimiwa Naibu Waziri tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii napenda kujibu swali la Mheshimiwa Antipas Zeno Mgungusi, Mbunge wa Malinyi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, maeneo yanayozungumziwa na Mheshimiwa Mbunge ni sehemu ya Pori Tengefu la Kilombero lililoanzishwa mwaka 1952 na kuhuishwa kwa Tangazo la Serikali Na. 269 la mwaka 1974 likiwa na ukubwa wa Kilomita za mraba 6,500. Eneo hilo vile vile ni sehemu ya ardhi oevu yenye umuhimu kitaifa na kimataifa kutokana na kuhifadhi bioanuai mbalimbali na zilizo adimu duniani kama vile mnyama aina ya Puku. Aidha, Bonde hilo huchangia takriban asilimia 62.5 ya maji yote ya Mto Rufiji na hivyo kuwa chanzo muhimu cha maji kwa mradi tarajali wa kufua umeme wa maji wa Julius Nyerere.

Mheshimiwa Spika, aidha tuta linalozungumziwa liliwekwa mwaka 2012 hadi 2013 kwa lengo la kuokoa kiini cha Bonde la Mto Kilombero kutokana na uharibifu mkubwa wa mazingira uliokuwa unaendelea.



Mheshimiwa Spika, ni kweli Serikali kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii mwaka 2017 ilifanya mapitio ya mipaka ikiwa ni hatua mojawapo ya kuangalia uwezekano wa kurekebisha mipaka (GN) ili iendane na hali halisi kwani kwa asilimia kubwa eneo la hifadhi lilikuwa limeathiriwa na shughuli za kilimo na ufugaji. Suala hili lilipelekwa kwenye Kamati ya Mawaziri Nane iliyoundwa na Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Tano. Utekelezaji wa mapendekezo hayo umeshafanyika na muda si mrefu wananchi watajulishwa maamuzi ya Kamati hiyo.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa rai kwa Mheshimiwa Mbunge pamoja na wananchi wa Wilaya ya Malinyi waendeleo kuwa na subira wakati utekelezaji wa maamuzi ya Baraza la Mawaziri ukiendelea kufanyiwa kazi, naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mgungusi.

**MHE. ANTIPAS Z. MGUNGUSI:** Mheshimiwa Spika, katika Bunge la Februari nilitoa ombi kutokana na majibu hayo kwamba Kijiji cha Ngombo ambacho kinatajwa kihame tuliomba tuko radhi kipunguziwe ukubwa wa mipaka na kupunguza mifugo Zaidi ya 90% ili wananchi waweze kubaki sehemu iliyobaki ichukuliwe kwa ajili ya uhifadhi.

Mheshimiwa Spika, lakini pia eneo kubwa la Jimbo huo mpaka wa 2017 tuliomba tupewe walau mita 700 kama siyo kilomita 1 kwa ajili ya shughuli za kiuchumi kwa maana umbali sehemu ambayo tunafanya shughuli mpaka mto ni mrefu sana tofauti na ambavyo inasemwa kiujumla. Kwa hiyo, je Serikali iko radhi kuridhia maombi haya?

Mheshimiwa Spika, la pili, majibu ya Naibu Waziri kuhusu wanashughulikia hii Tume ya Mawaziri nane ni tangu mwaka jana wanasema tunashughulikia tutajibu tutajibu watu tuko *pending* hatufanyi shughuli za kilimo, hatujui hatma yetu. Lini hasa Serikali itatoa msimamo wa mwisho juu ya jambo hili ili tuendeleo kuwaza mambo mengine tulimalize?

Mheshimiwa Spika, la tatu, kwa wale ambao tayari wameshalima Wizara inaridhia kipindi hiki tuweze kuvuna? Ahsante

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri mwenyewe majibu ya maswali hayo na moja la upendeleo.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ningependa kutoa ufafanuzi kwa Mheshimiwa Antipas kwamba mipaka ya Bonde Tengefu la Kilombero iliwekwa mwaka 1952 kwa GN Namba 107 na ikarejewa mwaka 1997. Mipaka hiyo haijawahi kurekebishwa mpaka sasa kilichofanyika ni wananchi wa maeneo mbalimbali kuvamia maeneo hayo na kutokana na uvamizi huo Serikali ikachukua hatua ya kuunda kamati maalum ya Mawaziri ikiongozwa na Waziri Mwandamizi Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi ambapo taarifa yake imefikia hatua ya mwisho tunaenda kutoa tathimini.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo maombi hayo yote tayari Mawaziri walishakwenda kule wamefanya tathimini ripoti iko tayari na watajulishwa wananchi. Kuhusiana na kulima hatuwezi kuendelea mtu kulima ndani ya hifadhi. Kwasababu mpaka unajulikana unaposema unaomba tulime maana yake unataka tulime ndani ya hifadhi madhara ya kulima ndani ya hifadhi hii ni kuhujumu mradi wa umeme wa Mwalimu Nyerere. Kwa hiyo, tsubiri maelekezo ya kamati maalum ya Baraza la Mawaziri tutajua hatma ya suala hili.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri maswali kwa siku ya leo tuishie hapo na leo ni siku ya Wizara ambayo tunatakiwa tumalize leo leo Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira. Kwa hiyo, mambo yetu yatakuwa ni mbio mbio kidogo.

Naomba niwatambue wageni wawili wa Mheshimiwa Spika ambao ni viongozi Waandamizi wa kutoka Benki inayoitwa *ECO Bank* wa kwana ni Mkuu wa Kitengo cha Biashara wateja binafsi Ndugu Salma Mkambala karibu sana Salma na wa pili ni Meneja Mahusiano Wateja Maalum

Jackline Nyangoe karibuni sana. Waheshimiwa Wabunge Ndugu zetu wa *ECO Bank* wako na banda hapo Msekwa kwa nyuma ambalo wanatoa huduma na matangazo kuhusu *services* wanazozitoa. Wananiambia wanazo ofa nzuri sana kwa wakati wenu watembeleeni *ECO Bank*.

Pia kuna wapiga kura kutoka Kongwa ule Kijiji cha Hembahemba Jimbo la Kongwa wakiongozwa na Ndugu Chrisphine Mguli karibuni sana Bungeni lakini kipekee naomba asimame Sophia karibu sana Sophia na mchumba wako karibuni sana ahsante sana Sophia ni binti yetu kutoka kule Kongwa binti wa mkulima wetu mmoja kule ambaye anasoma kule Marekani na kijana huyu toka Kenya ndiyo mchumba amemchumbia Sophia karibu sana karibuni sana. *(Makofi)*

Nasema hilo mwingine anaweza akaliona kama ni *joke* kwamba tunao wakulima sasa ambao wanaweza kusomesha Watoto nje ya nchi mpaka Marekani kwa kulipa wao wenyewe ni maendeleo makubwa sana haya katika kilimo na kutoka maeneo makame kama haya ya Dodoma lakini bado watu wanaweza kuwa na uwezo kama huo ambao baadhi yetu hapa mnaweza mkahema ni jambo jema.

Wageni wengine wa Mheshimiwa Spika ni viongozi tisa wa Jumuiya ya Wanafunzi wa sita vilivyochini ya Wizara ya Maliasili wakiongozwa na Ndugu Shindawangoni Mbiro wale wa kutoka Olemotonyi, Mweka na Vyuo vingine karibuni sana sana Bungeni na wale mnaotoka Mweka basi na mimi nilikuwa mmoja wenu enzi hizo karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni watano wa Mheshimiwa Selemani Jafo Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira ambao ni viongozi mbalimbali wa Wizara hiyo wakiongozwa na Katibu Mkuu Mary Ngelela Maganga karibu sana Katibu Mkuu hongera sana. *(Makofi)*

Lakini pia yumo Naibu Katibu Mkuu Mohamed Hamis Abdullah ahsante, yumo Mwenyekiti wa Bodi ya Baraza la

Taifa la Mazingira *NEMC* Profesa Asinath Chagu karibu sana Profesa. Yuko Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Hifadhi ya Mazingira *NEMC* Dkt Samwel Gwamaka Mafwenga na pia yupo Ndugu Thabit Idarus Faina ambaye ni Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa pili wa Rais karibuni sana leo siku yenu karibuni muwasilize Waheshimiwa Wabunge. (*Makofi*)

Mgeni wa Mheshimiwa Catherine Magige ambaye ni mshauri wa Rais wa Zambia katika mambo ya mawasiliano ya kimtandao Ndugu Thedy Ladislaus karibu sana Thedy mshauri wa Rais katika masuala ya mawasiliano karibu sana. (*Makofi*)

Wageni wanane wa Mheshimiwa Rashid Shangazi ambao ni watumishi kutoka Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu Jijini Dar es Salaam wakiongozwa na Mkurugenzi Mtendaji Ndugu Anna Henga karibuni sana *Legal and Human Right Centre*. (*Makofi*)

Wageni wanne wa Mheshimiwa Bupe Mwakang'ata ambao ni viongozi wa Chama Cha Wakulima wa zao la parachichi kutoka Mkoani Mbeya wakiongozwa na Johnson Mwita karibuni sana na bahati nzuri mmesikia majibu ya parachichi toka Serikalini leo hapa muendeleze kilimo hicho. (*Makofi*)

Wageni watatu wa Mheshimiwa Almas Maige ambao ni wapiga kura wake kutoka Uyui Mkoani Tabora wakiongozwa na Ndugu Shigela Kateraji Hoya karibuni sana yupo Mheshimiwa *yaya kwibeja* yupo hajambo kabisa.

Mgeni wa Mheshimiwa Balozi Dkt Pindi Chana kutoka Zanzibar ambaye ni Mbunge Mstaafu Ndugu Parmukh Singh Hoogan, Mheshimiwa Singh yuko wapi leo yupo ee hajafika. Huyu Mheshimiwa ndiye aliyewezesha kubadilisha kanuni bahati mbaya hajaja leo na kilemba chake tukaweza kuruhusu katika Kanuni za Bunge kilemba cha Singasinga kuwa sehemu ya vazi rasmi alipoingia wakati huo ilikuwa hairuhusiwi kwa hiyo ilibidi akae nje kwa muda mpaka tubadili kanuni kwanza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati ana wageni ambao ni wahitimu wa Vyuo vya Kilimo na Mifugo kutoka Mkoani Iringa wakiongozwa na Ndugu Peter Lawrence wale wahitimu karibuni sana sana karibuni sana wahitimu wanam-*beep* Waziri kwamba bwana tupo tumehitimu lakini mambo bado mnahitajika sana tulieni tu.

Wageni watano wa Mheshimiwa Janel James Ntate ambao ni wana maombi wa Mkoa wa Dodoma wakiongozwa na Ndugu Elice Mkunwa wana maombi wa Dodoma karibuni sana mliombe Taifa, muombeeni Rais wetu mliombe na Bunge letu pia.

Wageni watano wa Mheshimiwa William Tate Olenasha Naibu Waziri wa Mambo ya Nje ni wapiga kura wake wa Mheshimiwa Ole Nasha, kutoka Jimbo la Ngorongoro wakiongozwa na Ndugu Ibrahim Sakayi karibuni sana wale wa kutoka Ngorongoro. (*Makofi*)

Wageni watano wa Mheshimiwa Benaya Kapinga ambao ni wapiga kura wake kutoka Jimbo la Mbinga wakiongozwa na Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga Ndugu Bahati Mbele karibuni sana watu kutoka Mbinga. (*Makofi*)

Wageni watatu wa Mheshimiwa Mrisho Gambo wapiga kura wake kutoka Jimbo la Arusha Mjini wakiongozwa na Ndugu Shinga Sepeta karibuni sana. (*Makofi*)

Mgeni wa Mheshimiwa Halima Mdee ambaye ni Ndugu yake kutoka Dar es Salaam Ndugu Tecla Selemani karibu sana Tecla. (*Makofi*)

Wageni watano wa Mheshimiwa Irene Ndyamukama ambao ni wana maombi wa Mkoa wa Dodoma wakiwa na Aksa Mnyamiti karibuni sana.

Nina tangazo la Mheshimiwa Shally Raymond kwamba kwa nafasi yake ya Mwenyekiti wa *TWPG* anaomba Wabunge wanawake kwamba leo tarehe 27 mara baada

ya kuahirisha kikao cha Bunge kutakuwa na mafunzo kwa Wabunge wanawake katika Ukumbi wa Msekwa saa saba, kuna mafunzo kule na mambo yanayohusu utaratibu yako sawasawa, kwa hiyo msikose.

Mheshimiwa Anna Lupembe Mwenyekiti wa *chapel* ya Bunge anaomba wale waumini wote mkutane kwa shughuli za Ibada leo mchana baada ya kuahirisha shughuli za Bunge.

Katibu wa Bunge anaomba niwatangazieni Waheshimiwa Wabunge kwamba Waziri Mkuu hili nimeshalitangaza la Mheshimiwa Lukuvi ahsante sana. Katibu tuendeleo.

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

### **HOJA ZA SERIKALI**

#### **MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022**

**SPIKA:** Basi tunaingia sasa Waheshimiwa Wabunge kama alivyosema Katibu wetu, ambapo tunaenda kuwaombeni Waheshimiwa Wabunge mkubali mapendekezo ya makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano. Kwa hiyo, moja kwa moja nimuite Mheshimiwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Mheshimiwa Selemani Said Jafo. Mheshimiwa Jafo hongera sana karibu Makao Mapya karibu sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS,  
MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, baada ya Bunge lako Tukufu, kupokea taarifa ya mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda Biashara na Mazingira na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba Sheria kuhusu mapitio ya utekelezaji wa bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa mwaka wa fedha 2021/2022 na malengo ya Ofisi kwa mwaka wa fedha 2021/2022 naomba kutoa hoja

kwamba Bunge lako Tukufu sasa likubali kupokea, kujadiliana kupitisha makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa mwaka 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, naomba taarifa yangu hii yote iingie katika *Hansard* za Bunge kama nilivyowasilisha mezani.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema na baraka kwa kuendelea kunijalia afya njema na kuniwezesha kuwasilisha Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira kwa mwaka 2021/2022 mbele ya Bunge lako Tukufu. Kipekee namshukuru sana Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuonesha imani yake kubwa kwangu na kuniteua kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais mwenye dhamana ya Muungano na Mazingira. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa masikito makubwa, napenda kutumia fursa hii kutoa pole kwa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano, Mheshimiwa Job Yustino Ndugai na familia ya Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, pamoja na Watanzania wote kwa kuondokewa na mpendwa wetu, Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Msiba huu ni pigo kubwa kwa taifa letu kutokana na uongozi wake mahiri, uchapakazi na uzalendo uliotukuka kwa Taifa. Mwenyezi Mungu ampumzishe marehemu wetu mahali pema peponi, Amina. Aidha, napenda kutoa pole kwa Taifa kwa kuondokewa na Viongozi Wakuu, Mheshimiwa Maalim Seif Sharif Hamad, aliyekuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanziba, na Balozzi Mhandisi John Kijazi, aliyekuwa Katibu Mkuu Kiongozi. Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi.

Mheshimiwa Spika, vilevile, napenda kutoa pole kwako binafsi Spika wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na familia za marehemu kwa kifo cha

Mheshimiwa Atashasta Nditiye aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Muhambwe na Mheshimiwa Martha Umbulla aliyekuwa Mbunge Viti Maalum. Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi.

Mheshimiwa Spika, kwa dhati, naomba kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kuapishwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu wa Taifa letu. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango kuteuliwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vilevile, napenda kutoa pongeza kwa Balozi Hussein Kattanga kwa kuteuliwa kuwa Katibu Mkuu Kiongozi na Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri wote walioteuliwa kwa nafasi mbalimbali za uongozi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kuenzi na kuudumisha Muungano wetu. Kipekee namshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake na maelekezo anayotupa katika kusimamia masuala ya Muungano na uhifadhi wa mazingira. Uongozi wake thabiti unadhihirishwa na matokeo ya kazi nzuri inayofanywa ya kuudumisha Muungano wetu pamoja na kuhifadhi na kusimamia mazingira nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Mbunge na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa hotuba yake nzuri ambayo imetoa mwelekeo wa kisera katika utekelezaji wa shughuli za Serikali kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022. Aidha, nampongeza kwa uongozi weke dhabiti katika kusimamia shughuli za Serikali ndani na nje ya Bunge letu Tukufu. Vilevile, nawashukuru Waheshimiwa Mawaziri wote kwa ushirikiano walionipa katika utekelezaji



wa majukumu ya kusimamia shughuli zangu za Muungano na Mazingira.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani na pongezi za dhati kwa Bunge lako Tukufu kwa kazi nzuri linaloifanya katika kipindi chote cha uongozi wako. Aidha, nakupongeza wewe binafsi Mheshimiwa Job Yustino Ndugai, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuliongoza Bunge letu kwa heshima na busara kubwa, nikupongeze sana kwa dhati ya moyo wangu. Aidha, napenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wote wa Kamati za Bunge kwa kusaidia kuliongoza Bunge letu Tukufu kwa weledi na uadilifu mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara Mheshimiwa David Kihenzile na Kaimu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, pamoja na wajumbe wote wa Kamati ambao kwa pamoja wameipokea, kujadili na kupitisha Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka 2020/2021 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa mwaka 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, sasa naomba kutoa taarifa ya utekelezaji wa kazi za Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kipindi cha mwaka 2020/2021 na malengo ya mwaka 2021/22.

Mheshimiwa Spika, mapitio ya utekelezaji wa mipango na bajeti kwa mwaka 2020/2021. Ofisi imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia matakwa ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977; Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025; Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2020/2021– 2025/2026; Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi – CCM (2020 – 2025); Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 1997; Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2004; Ajenda ya Maendeleo ya Afrika 2063, Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030 na

Maelekezo na Miongozo mbalimbali inayotolewa na Viongozi Wakuu wa nchi.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Makamu wa Rais ina mafungu mawili ya kibajeti ambayo ni Fungu 26 kwa ajili ya Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais na Fungu 31 kwa ajili ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2020/2021, jumla ya shilingi 8,759,191,000.00 ziliidhinishwakwa ajili ya Fungu 26. Kati ya fedha hizo, shilingi 7,734,965,000.00 zilikuwa ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na shilingi 1,024,226,000.00 zilikuwa za Mishahara. Kwa upande wa Fungu 31, shilingi 19,230,964,000.00 ziliidhinishwa. Kati ya fedha hizo shilingi 11,581,534,000.00 zilikuwa za Matumizi ya Kawaida na shilingi 7,649,430,000.00 zilikuwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia 31 Machi, 2021, jumla ya shilingi 7,251,890,892.63 zilipokelewa kwa ajili ya kutekeleza majukumu yaliyo chini ya Fungu 26. Kati ya fedha hizo, shilingi 6,501,079,893.00 zilipokelewa kwa ajili ya Matumizi Mengineyo, sawa na asilimia 84 ya fedha za Matumizi Mengineyo zilizoidhinishwa na shilingi 750,811,000. kwa ajili ya Mishahara, sawa na asilimia 73.3 ya fedha za Mishahara zilizoidhinishwa. Hadi kufikia 31 Machi 2021 Fungu 31 lilipokea jumla ya shilingi 9,957,762,762. kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, mchanganuo wa fedha hizo ni kama ifuatavyo; shilingi 3,398,928,620.00 kwa ajili ya Matumizi Mengineyo, sawa na asilimia 68.7 ya fedha za Matumizi Mengineyo zilizoidhinishwa; shilingi 2,074,366,175.00, mishahara ya watumishi wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira zilizopokelewa sawa na asilimia 58.4 ya fedha zilizoidhinishwa; na shilingi 1,974,095,525. mishahara ya watumishi wa Ofisi ya Makamu wa Rais, sawa na asilimia 64 ya fedha za mishahara zilizoidhinishwa. Aidha, shilingi 2,510,372,442.00 zilipokelewa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo, sawa na asilimia 35.6 ya fedha za maendeleo zilizoidhinishwa.

Mheshimiwa Spika, tarehe 26 Aprili, 2021, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeadhimisha miaka 57 tangu kuasisiwa kwa Muungano wa Tanganyika na Zanzibar. Muungano umetupatia mafanikio lukuki katika nyanja za kijamii, kiuchumi na kisiasa ambayo yanaendelea kuwanufaisha wananchi wa pande mbili za Muungano kwa kuwapa fursa za kuishi kwa amani na kufanya shughuli mbalimbali za kimaendeleo popote katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Muungano huu adimu na adhimu umeendelea kudumu na kimsingi umekuwa ndio nyenzo muhimu ya utambulisho, amani, upendo, umoja na mshikamano wa Taifa letu. Hivyo kuulinda, kuudumisha na kuenzi ni jukumu letu sote.

Mheshimiwa Spika, kwa masuala ya Muungano, Ofisi iliratibu kikao cha kusaini Hati Tano za Makubaliano ya kuondoa hoja za Muungano zilizopatiwa ufumbuzi kwenye orodha ya Hoja za Muungano kilichofanyika katika Ukumbi wa Mikutano Ikulu, Dar es Salaam tarehe 17 Oktoba, 2020. Hoja zilizosainiwa ni: - Ushirikishwaji wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwenye Masuala ya Kimataifa na Kikanda; Ushiriki wa Zanzibar katika Jumuiya ya Afrika Mashariki; Gharama za Kushusha Mizigo Bandari ya Dar es Salaam kwa mizigo inayotoka Zanzibar; utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia; na utaratibu wa Vikao vya Kamati ya Pamoja vya SMT na SMZ vya kushughulikia masuala ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kutekeleza miradi ya maendeleo pande zote mbili za Muungano ambayo inawanufaisha wananchi kwa kuongeza kipato, kutoa ajira za muda, kuboresha elimu, kuboresha huduma za kijamii ikiwemo maji, afya na miundombinu. Miradi hiyo ni:- Mfuko wa Maendeleo ya Jamii *TASAF III*; Mradi wa Kuongeza Tija na Uzalishaji wa Zao la Mpunga - ERPP; Mradi wa Udhhibiti Uvuvi na Maendeleo Shirikishi Kusini Magharibi ya Bahari ya Hindi; Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara Tanzania (MKURABITA); Mpango wa Kupanua Usikivu wa Shirika la Utangazaji Tanzania; Mkakati wa Kudhibiti Sumu Kuvu Tanzania; na Mradi wa Kurejesha Ardhi Iliyoharibika na

Kuongeza Usalama wa Chakula Katika Maeneo Kame ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha miaka mitano 2015 - 2020 ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii - *TASAF III*, katika mzunguko wa kwanza ulipangiwa kiasi cha shilingi 1,087,960,454,968.00 kwa Tanzania Bara na shilingi 15,907,907,009.00 kwa Zanzibar. Kati ya fedha hizo, shilingi 1,079,227,845,129.00 zilitumika Tanzania Bara na shilingi 44,931,869,941.00 zilitumika Zanzibar. Programu ya *TASAF III* ilitekelezwa katika Halmashauri 159 Tanzania Bara na Wilaya zote za Zanzibar. Programu hii imekuwa na mafanikio makubwa kwa wananchi wa pande mbili za Muungano, ambapo ruzuku zinazotolewa kwa walengwa zimewasaidia kupata mahitaji ya msingi yakiwemo ya chakula, mahitaji ya shule kwa watoto na miradi midogo midogo ya kujiongezea kipato.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili ulizinduliwa mwezi Februari, 2020 na utagharimu takriban shilingi trilioni 2.032. Kati ya fedha hizo, shilingi trilioni 1.919 zitatumika Tanzania Bara na shilingi bilioni 112.9 zitatumika Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Kuongeza Tija na Uzalishaji wa Zao la Mpunga ulitekelezwa kwa miaka mitano (2015 - 2020) kwa dola za Marekani milioni 22.9 ambapo Tanzania Bara ilipangiwa Dola za Marekani milioni 16.5 na kwa upande wa Zanzibar dola za Marekani milioni 6.4. Lengo la mradi lilikuwa ni kuongeza uzalishaji wa mpunga ili kukidhi mahitaji ya ndani na kuongeza wigo wa mauzo ya nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Udhubiti Uvuvi na Maendeleo Shirikishi Kusini Magharibi mwa Bahari ya Hindi unatekelezwa katika maeneo ya Pwani ya Bahari ya Hindi kwa upande wa Tanzania Bara na katika Wilaya zote za Zanzibar pamoja na Ukanda wa Uchumi wa Bahari Kuu kwa kipindi cha 2005 - 2021. Lengo kuu la mradi huu ni kuimarisha usimamizi madhubuti wa uvuvi katika ngazi ya kikanda, kitaifa

na kijamii. Mradi unafadhiliwa na Benki ya Dunia kupitia mkopo nafuu wa dola za Marekani 36,000,000. Mradi umefanikisha yafuatayo; kuanzishwa kwa mfumo wa ukusanyaji na uhifadhi wa takwimu za uvuvi na mtandao wake kwa ajili ya wananchi kujipatia taarifa za uvuvi kwa muda husika; Kupatikana kwa Mpango Mkuu wa Miaka 15 wa Usimamizi na Uendelezaji wa Uvuvi; na Udhamini wa masomo ya wanafunzi katika Ngazi ya Uzamili na Uzamivu katika fani ya uvuvi ambapo jumla ya wanafunzi watano ngazi ya Uzamili (*Masters*) na wanafunzi watatu katika ngazi ya Uzamivu (*Ph.D*) wamenufaika na mpango huu.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara Tanzania (MKURABITA) unatekeleza shughuli za urasimishaji Tanzania Bara na Zanzibar. Katika kipindi cha miaka mitano mradi huu ulipangiwa kiasi cha shilingi 14,487,477,054 kwa upande wa Tanzania Bara na shilingi 1,050,451,000 kwa upande wa Zanzibar. Kati ya fedha hizo, shilingi 5,009,846,218 zimetumika Tanzania Bara na shilingi 566,390,250 zimetumika Zanzibar. MKURABITA umekuwa na faida kubwa kwa wananchi kwani wameweza kurasimisha rasilimali na biashara wanazomiliki na kuzitumia kupata mitaji, mikopo na hatimaye kuongeza kipato; Kuongezeka kwa Pato la Taifa kutokana na ongezeko la shughuli mbalimbali za uzalishaji mali; Kuongezeka kwa wigo wa walipa kodi na matumizi bora ya ardhi; Kuimarika kwa utawala bora kutokana na kuboresha mifumo ya kisheria na kitaasisi ambayo itarahisisha upatikanaji wa huduma kwa wananchi; na Viwanda vidogo vya kusindika mazao kuanzishwa katika maeneo ya vijijini baada ya wakulima waliorasimishiwa ardhi kujengewa uwezo.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pia, inafadhili Mpango wa Kupanua Usikivu wa Shirika la Utangazaji Tanzania (*TBC*) ambapo katika Bajeti ya Maendeleo, *TBC* imekuwa ikipatiwa fedha na Serikali kwa ajili ya upanuzi wa usikivu wa redio. Katika kipindi chca miaka mitano (2015 -2020). Mpango huu ulitumia shilingi 5,243,000,000.00 kwa upande wa Tanzania Bara na shilingi 375,000.00 kwa upande wa Zanzibar. Mpango huu

umewezesha wananchi kuhabarishwa, kuelimishwa na kuburudishwa kupitia vipindi vilivyoandaliwa kwa uweledi.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira na Muungano) inatekeleza Mradi wa Kurejesha Ardhi Iliyoharibika na Kuongeza Usalama wa Chakula Katika Maeneo Kame ya Tanzania - wenye thamani ya Dola za Marekani milioni 7.156 na utatekelezwa katika kipindi cha 2017 - 2022. Maeneo ya utekelezaji wa mradi huu kwa Tanzania Bara ni Dodoma, Tabora, Singida na Mwanza. Kwa upande wa Zanzibar mradi unatekelezwa katika Wilaya ya Michweni na Kaskazini Pemba.

Mheshimiwa Spika, Serikali zote mbili zimeweka utaratibu wa vikao vya kisekta vya ushirikiano kwa Wizara, Idara na Taasisi zisizo za Muungano. Lengo la kufanya vikao hivyo ni kuimarisha ushirikiano kwa manufaa ya Watanzania. Vikao hivyo vimekuwa vikijadili masuala ya kisekta kwa kubadilishana ujuzi, utaalamu na uzoefu kupitia mfumo, masuala ya sera na ushiriki katika masuala ya kimataifa. Aidha, katika kipindi hiki vimefanyika vikao kumi (10) vya Ushirikiano baina ya Wizara/Idara na Taasisi zisizo za Muungano zinazoshabihiana kimajukumu.

Mheshimiwa Spika, ofisi imeendelea kuelimisha umma kuhusu umuhimu na faida zinazotokana na Muungano kupitia vyombo vya habari ikiwemo redio, televisheni, magazeti, mitandao ya kijamii na jarida la Ofisi ya Makamu wa Rais. Ofisi iliandaa na kufanya kikao kazi cha Wabunge 50 wa Majimbo ya Zanzibar ambacho kilifanyika tarehe 12 Februari, 2021 kwa lengo la kujenga uelewa wa pamoja kuhusu Mfuko wa Kuchochea Maendeleo yaani Mfuko wa Jimbo.

Mheshimiwa spika, Uhifadhi na Usimamizi Endelevu wa Mazingira. Kwa mwaka wa fedha 2021, Ofisi kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa maendeleo imetekeleza mambo mbalimbali ikiwemo yafuatayo. Moja, ofisi imekamilisha mapitio ya Sera ya Taifa ya Mazingira 1997 na kuandaa Rasimu ya Sera mpya ya Mazingira 2024. Mbili, Ofisi imefanya mapitio ya Mpango Kazi wa Taifa wa Hifadhi wa Mazingira

ya Mwaka 2013 - 2018 na kuandaa Mpango Kazi mpya ya Taifa wa Hifadhi ya mazingira ya Mwaka 2021-2026. Tatu, Ofisi imekamilisha mapitio ya Kanuni ya Usajili wa Wataalamu wa Mazingira za mwaka 2005. Lengo la mapitio haya ni kuongeza ufanisi na tija katika mchakato wa tathimini ya athari ya mabadiliko ya tabia nchi yaani *TAM*. Nne, Ofisi imeendelea na jitihada ya kupunguza matumizi ya mkaa unaotokana na miti na kuhamasisha matumizi ya nishati mbadala ikiwemo pamoja na matumizi ya gasi, mkaa mbadala, umeme na biogasi. Tano, Ofisi kwa kushirikiana na wadau imeandaa Kanuni za Hifadhi ya Maeneo lindwa nchini ili kusimamia maeneo ambayo yatakuwa yakitangazwa kuwa ni maeneo lindwa na nyeti.

Mheshimiwa Spika, kufuatia Tamko la Serikali la Kupiga Marufuku Uzalishaji, Uingizaji, Uuzaji, Usambazaji, Usafirishaji nje ya nchi na Utumiaji wa Mifuko ya Plastiki nchini kuanzia tarehe 1 Juni, 2019, katika mwaka wa fedha 2020/2021, Ofisi kwa kushirikiana na Shirika la Viwango Tanzania (*TBS*) imeandaa viwango vya ubora vya mifuko mbadala ya plastiki aina ya *Non-woven* ambavyo vitasaidia kudhibiti ubora wa mifuko hiyo. Viwango hivyo vimeshasambazwa kwa viwanda 30 vinavyojihusisha na uzalishaji na usambazaji wa mifuko hiyo.

Mheshimiwa Spika, ofisi imeendelea kuratibu shughuli za Mfuko wa Mabadiliko ya Tabianchi uliopo chini ya Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi. Shughuli zilizofanyika ni pamoja na kuwezesha Benki ya CRDB ambayo imepewa ithibati katika mfuko huo kuandaa programu ya kujenga uwezo wa sekta ya kilimo na kuandaa miradi ya kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi. Programu hii ina thamani ya dola za Marekani 610,500 na utekelezaji wake utaanza katika kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, ofisi kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais-TAMISEMI imeendelea kuratibu utekelezaji wa kampeni ya kitaifa ya upandaji na utunzaji wa miti inayoelekeza kila Halmashauri ya Wilaya kutenga maeneo na kupanda miti milioni 1.5 kila mwaka. Katika kipindi cha mwaka 2019/2020, idadi ya miti iliyopandwa ni 197,623,843 na iliyostawi ni

159,282,897 sawa na asilimia 80.6. Napenda kuchukua fursa hii kuzitaka Halmashauri zote ambazo hazikutimiza lengo hili kuhakikisha zinachukua hatua za makusudi kufikia azma hii katika mwaka ujao.

Mheshimiwa Spika, ofisi imeendelea kuratibu utekelezaji wa Kampeni ya Kuifanya Dodoma kuwa ya Kijani. Katika kipindi hiki, takriban miche 71,782 ilipandwa katika maeneo mbalimbali ya Jiji la Dodoma.

Mheshimiwa Spika, Ofisi imeendelea kutoa elimu kwa Umma kuhusu uhifadhi na usimamizi wa mazingira kupitia njia mbalimbali ikiwa ni pamoja na vyombo vya Habari, maadhimisho mbalimbali ya Kitaifa na kimataifa, ziara za viongozi, semina za Wabunge wa Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira na mashindano ya insha kwa wanafunzi.

Mheshimiwa Spika, ifikapo tarehe 5 Juni kila mwaka, dunia inadhimisha Siku ya Mazingira Duniani. Kwa mwaka 2021, maadhimisho hayo Kimataifa yatafanyika nchini Pakistani na kaulimbiu itakuwa, "Kuongoa Mfumo Ikolojia." Kitaifa, maadhimisho hayo yatafanyika Mkoani Dodoma na kaulimbiu ya Kitaifa itakuwa, "Tutumie Nishati Mbadala, Kuongoa Mfumo Ikolojia."

Mheshimiwa Spika, Ofisi imeanza kuandaa maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani ambayo kilele chake itakuwa ni tarehe 5 Juni, 2021.

Mheshimiwa Spika, kupitia maadhimisho hayo, Makamu Rais wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, atazindua Kampeni Kabambe ya Uhifadhi na Usafi wa Mazingira. Lengo la kampeni hiyo ni kuongeza nguvu katika kuwaleta pamoja wadau wote na wananchi katika masuala ya uhifadhi na usafi wa mazingira. Kampeni hiyo itakuwa na tuzo mbalimbali kwa taasisi, makundi na mtu mmoja mmoja watakaoshinda katika vigezo mbalimbali vya uhifadhi na usafi wa mazingira. *(Makofi)*



Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021, Ofisi imeendelea kuratibu utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004 katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Katika kipindi hiki, Maafisa Mazingira 48 kutoka Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri za Lindi, Mtwara, Mbeya, Songwe, Rukwa, Katavi na Ruvuma walipatiwa mafunzo mbalimbali kuhusu hifadhi ya mazingira hususan tathmini ya athari kwa mazingira kimkakati.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021, Ofisi imepitia Taarifa ya Tathmini ya Mazingira Kimkakati kuhusu Mradi wa Uzalishaji wa Umeme wa Maji wa Kikonge katika Mto Ruhuhu Mkoani Ruvuma na Njombe na kutoa kibali cha utekelezaji wake (*SEA Approval Notice*). Aidha, Ofisi imeendelea kufuatilia utekelezaji wa mipango ya usimamizi wa mazingira ya tathmini za mazingira kimkakati zilizopitishwa.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021, Ofisi iliendelea kutekeleza mradi wa kuhimili mabadiliko ya tabianchi kupitia mifumo ya ikolojia ambapo kiasi cha shilingi 1,380,000,000/= kilitumika. Kazi zilizotekelezwa ni pamoja na kuandaa mfumo wa kielektroniki wa usimamizi wa taarifa na elimu kuhusu kukabiliana mabadiliko ya tabianchi; kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi katika vijiji 14 katika Wilaya za Simanjiro, Kishapu, Mpwapwa na Mvomero; na kuanzisha vitalu vya miche 114,416 katika Wilaya za Mvomero (miche 40,000), Simanjiro (miche 45,416), Kishapu (miche 3,000) na Mpwapwa (miche 26,000).

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021, Ofisi iliendelea kutekeleza mradi wa kujenga uwezo wa taasisi na jamii kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi kwenye maeneo ya kaskazini mwa nchi ambapo kiasi cha shilingi 80,500,000 zilitumika kukamilisha malipo ya kazi zilizosalia.

Mheshimiwa Spika, kazi zilizotekelezwa katika kipindi hiki ni pamoja na; ujenzi wa skimu mbili za usambazaji wa maji safi na salama kwenye Vijiji vya Kambi ya Simba,

Makuyuni na Jipe Wilayani Mwanga; ujenzi wa mfereji wa kisasa wa umwagiliaji wenye urefu wa mita 1,800 katika Kijiji cha Mabilio Wilaya ya Same na ufungaji wa mitambo miwili ya Hali ya Hewa katika Wilaya za Same na Mwanga kwa lengo la kutoa taarifa za uhakika za hali ya hewa.

Mheshimiwa Spika, Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (*NEMC*); katika mwaka wa fedha 2020/2021, Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (*NEMC*) kama msimamizi mkuu wa uzingatiji na utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Sura 191 limeendelea kutekeleza majukumu yake kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, naomba taarifa yangu yote iingie katika *Hansard*.

Mheshimiwa Spika, baada ya kueleza taarifa hiyo sasa, naomba Bunge lako liweze kupitia kitabu changu kama nilivyowasilisha hapo miradi mbalimbali itakayotekelezwa katika mwaka wa fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nchi yetu ni ya Muungano ambao una umuhimu wa kipekee kwa Taifa letu na umekuwa ni utambulisho wa Taifa letu na kielelezo cha umoja wetu katika kudumisha amani, mshikamano na usalama wa nchi yetu. Mwaka huu Muungano wetu unatimiza miaka 57 tangu kuasisiwa kwake. Ninatoa wito kwa Watanzania wote kuendelea kuuthamini, kuenzi, kuulinda na kuudumisha Muungano kwa lengo la kusukuma mbele maendeleo ya kiuchumi, kijamii na kisiasa kwa faida za pande zote mbili za Muungano.

Mheshimiwa Spika, chini ya uongozi wa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan na kiongozi wetu, Dkt. Isdor Philip Mpango, akiwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Dkt. Hussein Mwinyi, akiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, tunapenda kushukuru sana kwa kazi yao kubwa ya kuendelea kuenzi Muungano wetu.

Mheshimiwa Spika, maendeleo endelevu na uchumi wa viwanda haviwezi kupatikana bila kutunza na kuhifadhi mazingira. Kutokana na umuhimu huu, ni jukumu la kila Mtanzania kuhakikisha kuwa mazingira na maliasili za nchi yetu zinalindwa na kuhifadhiwa ipasavyo. Napenda kutoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge pamoja na wananchi kwa ujumla, kuunga mkono juhudi za Serikali katika kulinda na kuhifadhi mazingira kwa manufaa ya kizazi cha sasa na kijacho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili Ofisi iweze kutekeleza majukumu na malengo yaliyopangwa, ninaomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu liidhinishhe maombi ya fedha, jumla ya shilingi 28,708,348,000.00 kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Fungu 26 – Ofisi ya Makamu wa Rais; ninaomba Bunge lako Tukufu liidhinishhe Makadirio ya Matumizi ya shilingi 8,719,076,000.00 ikiwa ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Kati ya fedha hizi, shilingi 984,111,000.00 ni fedha za mishahara ya watumishi na shilingi 7,734,965,000.00 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Spika, Fungu 31 – Ofisi ya Makamu wa Rais; katika fungu hili ninaomba Bunge lako Tukufu liidhinishhe jumla ya shilingi 19,989,272,000.00. Kati ya fedha hizi, shilingi 13,138,484,000.00 ni kwa ajili matumizi ya kawaida na shilingi 6,850,788,000.00 ni fedha za miradi ya maendeleo. Bajeti ya matumizi ya kawaida inajumuisha shilingi 6,773,706,000.00 fedha za mishahara; na shilingi 6,364,778,000.00 ni fedha za matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Spika, fedha za mishahara zinajumuisha kiasi cha shilingi 3,021,908,000.00 mishahara ya watumishi wa Ofisi ya Makamu wa Rais na kiasi cha shilingi 3,751,798,000.00 ni mishahara ya watumishi wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira. Aidha, fedha za miradi ya maendeleo zinajumuisha fedha za ndani shilingi 4,280,000,000.00 na shilingi 2,570,788,000.00 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**HOTUBA YA WAZIRI WA NCHI OFISI YA MAKAMU WA RAIS  
KUHUSU MAKADIRIOYA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA  
2021/22 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**


*Mhe. Selemani Saidi Jafo(Mb.),  
Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais  
Muungano na Mazingira*

**A. UTANGULIZI**

**1. Mheshimiwa Spika**, baada ya Bunge lako Tukufu kupokea taarifa iliyowasilishwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa mwaka 2020/21; na Malengo ya Ofisi ya mwaka 2021/22, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu sasa likubali kupokea, kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa mwaka 2021/22.

**2. Mheshimiwa Spika**, awali ya yote ninapenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema na baraka kwa kuendelea kunijalia afya njema na kuniwezesha kuwasilisha Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira kwa mwaka 2021/22 mbele ya Bunge lako Tukufu. Kipekee ninamshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuonesha imani yake kwangu na kuniteua kuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais mwenye dhamana ya Muungano na Mazingira.

**3. Mheshimiwa Spika**, kwa masikito makubwa napenda kutumia fursa hii kutoa pole kwa Mheshimiwa **Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa **Job Yustino Ndugai(Mb.)**Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano, na Familia ya **Dkt. John Pombe Joseph Magufuli**, pamoja na Watanzania wote kwa kuondokewa na mpendwa wetu, Hayati **Dkt. John Pombe Joseph Magufuli**, aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.



*Hayati Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli alipokuwa akihutubia wakati akifungua Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania jijini Dodoma enzi za uhai wake.*



*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe.Samia Suluhu Hassan akimpa mkono wa pole Mama Janeth Magufuli nyumbani kwake jijini Dar es Salaam Machi 19, 2021.*

**4. Mheshimiwa Spika**, msiba huu ni pigo kubwa kwa taifa letu kutokana na uongozi wake mahiri, uchapakazi na uzalendo uliotukuka kwa Taifa. Mwenyezi Mungu ampumzishe mahali pema peponi, Amina. Aidha, napenda kutoa pole kwa Taifa kwa kuondokewa na Viongozi Wakuu, Mheshimiwa Maalim **Seif Sharif Hamad**, aliyekuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, na **Balozi Mhandisi John Kijazi**, aliyekuwa Katibu Mkuu Kiongozi. Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi.

**5. Mheshimiwa Spika**, Vilevile, napenda pia kutoa pole kwako Spika na familia za marehemu kutokana kifo cha Mheshimiwa **Atashasta Nditiye** aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Muhambwe na **Martha Umbula** aliyekuwa Mbunge viti maalum. Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi.

**6. Mheshimiwa Spika**, kwa dhati naomba kutoa pongezi kwa Mheshimiwa **Samia Suluhu Hassan** kwa kuapishwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu. Aidha, ninampongeza Mheshimiwa **Dkt. Philip Isdor Mpangokwa** kuteuliwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vile vile, napenda kumpongeza **Balozi Hussein A. Kattangakwa** kuteuliwa kuwa Katibu Mkuu Kiongozi na Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri wote walioteuliwa kushika nafasi mbalimbali za uongozi wa nchi yetu.

**7. Mheshimiwa Spika**, ninapenda kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa **Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa **Dkt. Hussein Ali Mwinyi**, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuuenzi na kuudumisha Muungano wetu.



*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan akizungumza na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Hussein Ali Mwinyi alipofanya ziara Zanzibar.*

Kipekee nashukuru sana Mheshimiwa **Dkt. Philip Isdor Mpango** Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake na maelekezo anayotupa katika kusimamia masuala ya Muungano na kuhifadhi Mazingira. Uongozi wake thabiti unadhihirishwa na matokeo ya kazi nzuri inayofanywa ya kuudumisha Muungano wetu pamoja na kuhifadhi na kusimamia Mazingira nchini.



*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango akizungumza na Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira Mhe. Selemani Jafo kushoto na Naibu Waziri wake Mhe. Hamad Hassan Chande Jijini Dodoma.*

**8. Mheshimiwa Spika**, ninamshukuru na kumpongeza Mheshimiwa **Kassim MajaliwaMajaliwa (Mb.)**, Waziri Mkuuwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa hotuba yake nzuri ambayo imetoa mwelekeo wa kisera katika utekelezaji wa shughuli za Serikali kwa kipindi cha mwaka 2021/22. Aidha, ninampongeza kwa uongozi wake thabiti katika kusimamia shughuli za Serikali ndani na nje ya Bunge lako Tukufu. Vilevile, ninawashukuru Waheshimiwa Mawaziri wote kwa ushirikiano walionipa katika kutekeleza majukumu ya kusimamia shughuli za Muungano na Mazingira.



*Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa*

**9. Mheshimiwa Spika**, ninapenda kutoa shukrani na pongezi za dhati kwa Bunge lako Tukufu kwa kazi nzuri ambayo linaifanya katika kipindi cha uongozi wako. Aidha, ninakupongezawewe binafsi Mheshimiwa **Job Yustino Ndugai(Mb.)**, Spikawa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuliongoza Bunge letu kwa hekima na busara kubwa. Ninampongeza pia Mheshimiwa **Dkt. Tulia Ackson Mwansasu (Mb.)**, Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wa Bunge kwa kukusaidia kuliongoza Bunge letu kwa weledi na uadilifu.

**10. Mheshimiwa Spika**, ninapenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya



Viwanda, Biashara na Mazingira, Mheshimiwa **David Kihenzile** na Kaimu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa **Najma Murtaza Giga** (Mb.), pamoja na Waheshimiwa wajumbe wa Kamati hizo kwa kupokea, kujadili na kupitisha Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka 2020/21 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa mwaka 2021/22.

**11. Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, sasa ninaomba kutoa taarifa ya utekelezaji wa kazi za Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kipindi cha mwaka 2020/21 na malengo ya mwaka 2021/22.

#### **B. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2020/21**

**12. Mheshimiwa Spika**, Ofisi imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia matakwa ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977; Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025; Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2020/21– 2025/26); Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi – CCM (2020– 2025); Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 1997; Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2004; Ajenda ya Maendeleo ya Afrika 2063 (*Africa Agenda 2063*), Malengo ya Maendeleo Endelevu (*Sustainable Development Goals – SDG 2030*); na Maelekezo na Miongozo mbalimbali inayotolewa na Viongozi Wakuu wa nchi.

#### **Bajeti Iliyoidhinishwa kwa Mwaka 2020/21**

**13. Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Makamu wa Rais ina mafungu mawili ya kibajeti ambayo ni Fungu 26 kwa ajili ya Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais na Fungu 31 kwa ajili ya Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira.

#### **Fungu 26**

**14. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2020/21, jumla ya Shilingi **8,759,191,000.00** ziliidhinishwakwa ajili ya Fungu 26. Kati ya fedha hizo, Shilingi **7,734,965,000.00** zilikuwanikwa ajili ya

Matumizi Mengineyo na Shilingi **1,024,226,000.00** zilikuwa za Mishahara.

### Fungu 31

**15. Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa Fungu 31, Shilingi **19,230,964,000.00** ziliidhinishwa. Kati ya fedha hizo Shilingi **11,581,534,000.00** zilikuwa za Matumizi ya Kawaida na Shilingi **7,649,430,000.00** zilikuwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Bajeti ya Matumizi ya Kawaida inajumuisha fedha za mishahara kiasi cha Shilingi **3,083,994,000.00** kwa watumishi wa Ofisi ya Makamu wa Rais, Shilingi **3,550,488,000.00** ni Mishahara ya Watumishi wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC). Na Fedha za Matumizi Mengineyo ni Shilingi **4,947,052,000.00**

### Fedha Zilizopokelewa Hadi 31 Machi, 2021

#### Fungu 26

**16. Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia 31 Machi 2021, jumla ya Shilingi **7,251,890,892.63** zilipokelewa kwa ajili ya kutekeleza majukumu yaliyo chini ya **Fungu 26**. Kati ya fedha hizo, Shilingi **6,501,079,893.00** zilipokelewa kwa ajili ya Matumizi Mengineyo, sawa na asilimia **84** ya fedha za Matumizi Mengineyo zilizoidhinishwa na Shilingi **750,811,000.00** kwa ajili ya Mishahara, sawa na asilimia **73.3** ya fedha za Mishahara zilizoidhinishwa.

#### Fungu 31

**17. Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia 31 Machi 2021 Fungu 31 lilipokea jumla ya Shilingi **9,957,762,762.00** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo. Mchanganuo wa fedha hizo ni kama ifuatavyo: Shilingi **3,398,928,620.00** kwa ajili ya matumizi mengineyo, sawa na asilimia **68.7** ya fedha za matumizi mengineyo zilizoidhinishwa; Shilingi **2,074,366,175.00**, mishahara ya watumishi wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira zilipokelewa sawa na

asilimia **58.4** ya fedha zilizoidhinishwa; na Shilingi **1,974,095,525.00** mishahara ya watumishi wa Ofisi ya Makamu wa Rais, sawa na asilimia **64** ya fedha za mishahara zilizoidhinishwa. Aidha, Shilingi **2,510,372,442.00** zilipokelewa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo, sawa na asilimia **35.6ya** fedha za maendeleo zilizoidhinishwa.

**Kazi zilizotekelezwa katika mwaka 2020/21**

### **MASUALA YA MUUNGANO**

**18. Mheshimiwa Spika**, tarehe 26 Aprili, 2021, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeadhimisha miaka 57 tangu kuasisiwa kwa Muungano wa Tanganyika na Zanzibar. Muungano, umetupatia mafanikio lukuki katika nyanja za kijamii, kiuchumi na kisiasa ambayo yanaendelea kuwanufaisha wananchi wa pande mbili za Muungano kwa kuwapa fursa za kuishi kwa amani na kufanya shughuli mbalimbali za kimaendeleo popote katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Muungano huu adimu na adhimu umeendelea kudumu na kimsingi umekuwa ndio nyenzo muhimu ya Utambulisho, Amani, Umoja na Mshikamano wa Taifa letu. Hivyo kuulinda, kuudumisha na kuenzi ni jukumu letu sote.

***Kuratibu Vikao vya Kamati ya Pamoja ya SMT na SMZ ya Kushughulikia Masuala ya Muungano***

**19. Mheshimiwa Spika**, kikao cha Sekretarieti ya Kamati ya Pamoja ya SMT na SMZ kilifanyika Dodoma tarehe 6 Julai, 2020 kwa ajili ya kutathmini utekelezaji wa maagizo yaliyotolewa katika kikao cha Kamati ya Pamoja ya SMT na SMZ kilichofanyika Dodoma tarehe 9 Februari, 2019. Kikao hicho kilishauri kifanyike kikao cha kusaini hati za hoja Tano (5) ambazo zimeshapatiwa ufumbuzi ili ziondolewe kwenye orodha ya Hoja za Muungano.

**20. Mheshimiwa Spika**, Ofisi iliratibu kikao cha kusaini Hati Tano (5) za Makubaliano ya kuondoa hoja za Muungano zilizopatiwa ufumbuzi kwenye orodha ya Hoja za Muungano

kilichofanyika katika Ukumbi wa Mikutano Ikulu, Dar es Salaam tarehe 17 Oktoba, 2020. Hoja zilizosainiwa ni: - Ushirikishwaji wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) kwenye Masuala ya Kimataifa na Kikanda; Ushiriki wa Zanzibar katika Jumuiya ya Afrika Mashariki; Gharama za Kushusha Mizigo Bandari ya Dar es Salaam kwa Mizigo inayotoka Zanzibar; Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia; na Utaratibu wa Vikao vya Kamati ya Pamoja ya SMT na SMZ ya Kushughulikia Masuala ya Muungano.



*Hafla ya utiaji saina Hati Tano (5) za Makubaliano ya kuondoa hoja za Muungano zilizopatiwa ufumbuzi kwenye orodha ya Hoja za Muungano, iliyofanyikatarehe 17 Oktoba 2020, Ikulu Dar es Salaam.*

**21. Mheshimiwa Spika**, pia, zipo hoja saba (7) ambazo zimeshapatiwa ufumbuzi na zinasubiri kupata ridhaa ya Kikao cha Kamati ya Pamoja ya SMT na SMZ kama ilivyoainishwa katika Utaratibu wa Vikao vya Kamati ya Pamoja ya SMT na SMZ Aya ya 2.2 (b). Hoja hizo ni: - Tatizo la Usimamizi wa Ukokotoaji na Ukusanyaji wa Kodi kwenye Huduma za Simu unaofanywa na ZRB; Changamoto za uingizaji wa maziwa kutoka Zanzibar; Kuchelewa kusainiwa kwa Mkataba wa Ujenzi wa Barabara ya Chake Chake hadi Wete – Pemba ambapo Serikali imesaini Mkataba huo na *Saudi Fund* tarehe

19 Aprili, 2020; Kuchelewa kusainiwa kwa Mkataba wa Mradi wa Ukarabati wa Hospitali ya Mnazi Mmoja, pia, Serikali imesaini Mkataba na *Saudi Fund* tarehe 19 Aprili, 2020; Uvuvi kwenye Ukanda wa Uchumi wa Bahari Kuu ambapo Sheria ya Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu, Sheria Na. 5 ya mwaka 2020 imetungwa na Bunge la 11 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Sheria hiyo imeshaorodheshwa (*Listing/noting*) na Baraza la Wawakilishi tarehe 23 Februari, 2021; Uteuzi wa Makamu Mwenyekiti wa Mahakama ya Rufaa za Kodi (TRAT) kutoka Zanzibar; na Uteuzi wa Mjumbe wa *Deposit Insurance Board* (DIB) kutoka Zanzibar.

### ***Kuratibu Masuala ya Kiuchumi na Kijamii***

**22. Mheshimiwa Spika**, Ofisi ilifanya ziara ya kikazi Tanzania Bara na Zanzibar kuanzia tarehe 18 Agosti hadi tarehe 1 Septemba, 2020 ambapo jumla ya Taasisi kumi na mbili (12) zilitembelewa. Lengo la ziara lilikuwa ni kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya Taasisi za Muungano na Miradi ya Maendeleo inayotekelezwa pande mbili za Muungano. Ziara hizo zinasaidia kubaini mafanikio na changamoto zilizopo kwenye Taasisi za Muungano hususan upande wa Zanzibar pamoja na kuzihimiza Taasisi ambazo hazijafungua Ofisi Zanzibar zifungue ili kusogeza huduma karibu na wananchi. Taasisi za Muungano zikitekeleza majukumu yake ipasavyo, zitapunguza au kuondoa changamoto za Muungano na kuleta taswira halisi ya Muungano.

**23. Mheshimiwa Spika**, Taasisi zilizotembelewa katika pande mbili za Muungano ni:- Bodi ya Mikopo kwa Wanafunzi wa Elimu ya Juu; Tume ya Pamoja ya Fedha; Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania; Mamlaka ya Mapato Tanzania; na Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara Tanzania (MKURABITA). Aidha, Taasisi zilizotembelewa Tanzania Bara ni:- Mamlaka ya Elimu Tanzania; Tume ya Vyuho Vikuu; Shirika la Viwango Tanzania; na Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba. Aidha na Taasisi zilizotembelewa Zanzibar ni:- Tume ya Sayansi na Teknolojia; Benki Kuu ya Tanzania, Tawi la Zanzibar; na Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu.

**24. Mheshimiwa Spika**, Ofisi pia ilitembelea miradi mitatu (3) ya maendeleo, Zanzibar (Unguja na Pemba). Lengo la ziara ilikuwa ni kuhakikisha wananchi wa Zanzibar wanaendelea kunufaika na matunda ya Muungano. Miradi iliyotembelewa ni pamoja na: - Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF III); Mradi wa Kuongeza Tija na Uzalishaji wa Zao la Mpunga (ERPP); na Mradi wa Udhhibiti Uvuvi na Maendeleo Shirikishi Kusini Magharibi ya Bahari ya Hindi (SWIOFish).

**25. Mheshimiwa Spika**, Serikali imeendelea kutekeleza miradi ya maendeleo pande zote mbili za Muungano ambayo inawanufaisha wananchi kwa kuongeza kipato, kutoa ajira za muda, kuboresha elimu, kuboresha huduma za kijamii ikiwemo maji, afya na miundombinu. Miradi hiyo ni:- Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF III); Mradi wa Kuongeza Tija na Uzalishaji wa Zao la Mpunga (ERPP); Mradi wa Udhhibiti Uvuvi na Maendeleo Shirikishi Kusini Magharibi ya Bahari ya Hindi (SWIOFish); Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara Tanzania (MKURABITA); Mpango wa Kupanua Usikivu Shirika la Utangazaji Tanzania; Mkakati wa Kudhibiti Sumu Kuvu Tanzania; na Mradi wa Kurejesha Ardhi Iliyoharibika na Kuongeza Usalama wa Chakula Katika Maeneo Kame ya Tanzania.

**26. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha miaka mitano (2015 - 2020) ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF III), mzunguko wa kwanza ulipangiwa kiasi cha shilingi **1,087,960,454,968.00** kwa Tanzania Bara na **45,907,907,009.00** kwa Zanzibar. Kati ya fedha hizo, shilingi **1,079,227,845,129.00** zilitumika Tanzania Bara na shilingi **44,931,869,941.00** zilitumika Zanzibar. Programu ya TASAF III ilitekelezwa katika Halmashauri 159 Tanzania Bara na Wilaya zote za Zanzibar. Programu hii imekuwa na mafanikio makubwa kwa wananchi wa pande mbili za Muungano, ambapo ruzuku zinazotolewa kwa walengwa zimewasaidia kupata mahitaji ya msingi yakiwemo ya chakula, mahitaji ya shule kwa watoto na miradi midogo midogo ya kujiongezea kipato.



*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Selemani Jafo na Naibu Waziri Mhe. Hamad Hassan Chande wakikagua mradi wa ukumbi wa kufanyia mitihani katika skuli ya Fujoni iliyopo Zanzibar kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF III).*

**27. Mheshimiwa Spika**, Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili ulizinduliwa mwezi Februari, 2020 na utagharimu takriban shilingi trilioni **2.032**. Kati ya fedha hizo, shilingi trilioni **1.919** zitatumika Tanzania Bara na shilingi bilioni **112.9** zitatumika Zanzibar.

**28. Mheshimiwa Spika**, Mradi wa Kuongeza Tija na Uzalishaji wa Zao la Mpunga (ERPP) ulitekelezwa kwa muda wa miaka mitano (2015 - 2020) kwa Dola za Marekani milioni **22.9** ambapo Tanzania Bara ilipangiwa Dola za Marekani milioni **16.5** na kwa upande wa Zanzibar Dola za Marekani milioni **6.4**. Lengo la mradi lilikuwa ni kuongeza uzalishaji wa mpunga ili kukidhi mahitaji ya ndani na kuongeza wigo wa mauzo ya nje ya nchi.

Kwa upande wa Tanzania Bara, mradi umetekelezwa katika Mkoa wa Morogoro kwenye Halmashauri za Wilaya ya Kilombero, Kilosa, Mvomero, Morogoro, Malinyi na Ulanga.

Kwa upande wa Zanzibar, mradi unatekelezwa katika skimu za umwagiliaji za:- Kibonde Mzungu; Mtwango; Koani; Mchangani; Bandamaji (Unguja); Machigini; Kwalempona; Ole; Dobi – 1; na Dobi – 2 (Pemba).

Baadhi ya mafanikio ya mradi huu ni:- Kuwawezesha wakulima kuzalisha mpunga mara mbili kwa mwaka hivyo kuongeza uhakika wa chakula na kipato; na Kuongeza uzalishaji kutoka tani 1.6 kwa hekta hadi tani 6 kwa msimu mmoja.

**29. Mheshimiwa Spika**, Mradi wa Udhubiti Uvuvi na Maendeleo Shirikishi Kusini Magharibi mwa Bahari ya Hindi (*SWIOFish*) unatekelezwa katika maeneo ya Pwani ya Bahari ya Hindi kwa upande wa Tanzania Bara na katika Wilaya zote za Zanzibar pamoja na Ukanda wa Uchumi wa Bahari Kuu (*EEZ*) kwa kipindi cha 2005 - 2021. Lengo kuu la mradi huu ni kuimarisha usimamizi madhubuti wa uvuvi katika ngazi ya kikanda, kitaifa na kijamii. Mradi unafadhiliwa na Benki ya Dunia kupitia mkopo nafuu wa Dola za Marekani **36,000,000.00** kwa mgawanyo ufuatao:- Wizara ya Mifugo na Uvuvi (SMT) Dola za Marekani **17,280,000.00**; Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi (SMZ) Dola za Marekani **11,520,000.00**; na Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu Dola za Marekani **7,200,000.00**.



*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mhe. Selemani Jafo akikagua Mradi wa Udhubiti Uvuvi na Maendeleo Shirikishi Kusini Magharibi ya Bahari ya Hindi (South West Indian Ocean Fisheries Governance and Shared Growth - SWIOFish) katika eneo la Nungwi, Zanzibar*



**30. Mheshimiwa Spika**, Mradi umefanikisha yafuatayo:- Kuanzishwa kwa mfumo wa ukusanyaji na uhifadhi wa takwimu za uvuvi na mtandao wake kwa ajili ya wananchi kujipatia taarifa za uvuvi kwa muda husika; Kupatikana kwa Mpango Mkuu wa Miaka 15 wa Usimamizi na Uendelezaji wa Uvuvi; Kuongezeka kwa ukataji wa leseni za uvuvi na vyombo vya uvuvi kutoka asilimia 15% mwaka 2016/17 hadi asilimia 35% mwaka 2020; na Udhamini wa masomo ya wanafunzi katika Ngazi ya Uzamili na Uzamivu katika fani ya uvuvi ambapo jumla ya wanafunzi watano (5) ngazi ya Uzamili (Masters) na wanafunzi watatu (3) katika ngazi ya Uzamivu (PhD) wamenufaika na mpango huu.

**31. Mheshimiwa Spika**, Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara Tanzania (MKURABITA) unatekeleza shughuli za urasimishaji Tanzania Bara na Zanzibar. Katika kipindi cha miaka mitano (2015 - 2020), mradi huu ulipangiwa kiasi cha shilingi **14,487,477,054** kwa upande wa Tanzania Bara na shilingi **1,050,451,000** kwa upande wa Zanzibar. Kati ya fedha hizo, shilingi **5,009,846,218** zimetumika Tanzania Bara na shilingi **566,390,250** zimetumika Zanzibar.

**32. Mheshimiwa Spika**, MKURABITA umekuwa na faida kubwa kwa wananchi kwani wameweza kurasimisha rasilimali na biashara wanazomiliki na kuzitumia kupata mitaji, mikopo na hatimaye kuongeza kipato; Kuongezeka kwa Pato la Taifa kutokana na ongezeko la shughuli mbalimbali za uzalishaji mali; Kuongezeka kwa wigo wa walipa kodi na matumizi bora ya ardhi; Kuimarika kwa utawala bora kutokana na kuboresha mifumo ya kisheria na kitaasisi ambayo itarahisisha upatikanaji wa huduma kwa wananchi; na Viwanda vidogo vya kusindika mazao kuanzishwa katika maeneo ya vijijini baada ya wakulima waliorasimishiwa ardhi kujengewa uwezo.

**33. Mheshimiwa Spika**, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pia, inafadhili Mpango wa Kupanua Usikivu wa Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) ambapo katika Bajeti ya Maendeleo, TBC imekuwa ikipatiwa fedha na Serikali kwa ajili ya upanuzi wa usikivu wa redio. Katika kipindi chca miaka mitano (2015 -2020). Mpango huu ulitumia shilingi

**5,243,000,000.00** kwa upande wa Tanzania Bara na shilingi **375,000,000.00** kwa upande wa Zanzibar. Mpango huu umewezesha wananchi kuhabarishwa, kuelimishwa na kuburudishwa kupitia vipindi vilivyoandaliwa kwa uweledi.

**34. Mheshimiwa Spika**, Mkakatiwa Kudhibiti Sumu Kuvu Tanzania ulianzishwa baada ya sumu ya aflotoxin kwenye vyakula kuathiri watu takriban 65 na kusababisha vifo vya watu 19 katika mkoa ya Dodoma na Manyara. Sumu hii inapatikana katika mimea ya mahindi na karanga na kusababisha madhara pale mlaji anapotumia vyakula hivyo. Mkakati huu umepangwa kutekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia Juni, 2019 na hadi mwezi Mei, 2023. Mkakati unatekelezwa kwenye Wilaya 18 katika Mkoa 10 ya Tanzania Bara na Zanzibar. Mradi una jumla ya Shilingi **69,929,845,314.00** kwa Tanzania Bara na Shilingi **6,313,684,686.00** kwa Zanzibar.

**35. Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) inatekeleza Mradi wa Kurejesha Ardhi Iliyoharibika na Kuongeza Usalama wa Chakula Katika Maeneo Kame ya Tanzania - LDFS wenye thamani ya Dola za Marekani milioni **7.156** na utatekelezwa katika kipindi cha 2017 - 2022. Mgawanyo wa fedha hizi ni Dola za Marekani milioni **5.706** kwa Tanzania Bara na Dola za Marekani milioni **1.45** kwa Zanzibar. Mradi una lengo la kuboresha mifumo ikolojia ya kilimo ambayo itawezesha kuongeza uzalishaji wa chakula; na kuboresha mazingira na usimamizi endelevu wa mifumo ikolojia inayochangia kutoa huduma muhimu za uzalishaji kwenye maeneo ya ardhi, maji, misitu na bioanuai kwa madhumuni ya kuboresha uzalishaji. Maeneo ya utekelezaji wa mradi huu kwa Tanzania Bara ni Dodoma, Tabora, Singida na Mwanza. Kwa upande wa Zanzibar mradi unatekelezwa katika wilaya ya Michweni, Kaskazini Pemba.

**36. Mheshimiwa Spika**, Ofisi imeratibu gawio la Fedha za Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo Zanzibar, Misaada ya Kibajeti (GBS) kwa SMZ, ambapo. Hadi kufikia Machi, 2021 jumla ya shilingi bilioni **25.75** zimepelekwa SMZ kwa mchanganuo ufuatao: - Mfuko wa Kuchochea

Maendeleo ya Jimbo shilingi bilioni **1.40**; Mfuko wa misaada ya kibajeti (GBS) shilingi bilioni **9.5** na Kodi ya mapato (PAYE) inayotokana na mishahara shilingi bilioni **15.75**

***Kuratibu masuala yasiyo ya Muungano ili kuimarisha ushirikiano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar***

**37. Mheshimiwa Spika**, Serikali zote mbili zimeweka utaratibu wa vikao vya kisekta vya ushirikiano kwa Wizara, Idara na Taasisi zisizo za Muungano. Lengo la kufanya vikao hivyo ni kuimarisha ushirikiano kwa manufaa ya Watanzania. Vikao hivyo vimekuwa vikijadili masuala ya kisekta kwa kubadilishana ujuzi, utaalamu na uzoefu kupitia mafunzo, masuala ya sera na ushiriki katika masuala ya kimataifa. Aidha, katika kipindi hiki vimefanyika vikao kumi (10) vya Ushirikiano baina ya Wizara/Idara na Taasisi zisizo za Muungano zinazoshabihiana kimajukumu.

***Kutoa Elimu ya Muungano kwa Umma***

**38. Mheshimiwa Spika**, Ofisi imeendelea kuelimisha umma kuhusu umuhimu na faida zinazotokana na Muungano kupitia vyombo vya habari ikiwemo redio, televisheni, magazeti, mitandao ya kijamii na jarida la Ofisi ya Makamu wa Rais.

**39. Mheshimiwa Spika**, Ofisi iliandaa na kufanya kikao kazi cha Wabunge 50 wa Majimbo ya Zanzibar tarehe 12 Februari, 2021 kwa lengo la kujenga uelewa wa pamoja kuhusu Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo.



*Sehemu ya Waheshimiwa Wabunge wakifuatilia mawasilisho ya mada hukusu Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo.*

## HIFADHI NA USIMAMIZI ENDELEU WA MAZINGIRA

**40. Mheshimiwa Spika**, maendeleo ya nchi yetu yanategemea matumizi endelevu ya mifumo-ikolojia na maliasili zilizopo nchini. Shughuli zisizoendelevu zinazochangia kwa kiasi kikubwa uharibifu wa mazingira nchini ni pamoja na: kilimo na ufugaji usioendelevu; ukataji wa miti hovyoy, uchimbaji holela wa madini; na shughuli zisizoendelevu za utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi, uzalishaji viwandani na migodini. Shughuli hizi husababisha uchafuzi wa mazingira, upotevu wa bioanuai, ongezeko la viumbe vamizi, ukosefu wa maji safi na salama, na mabadiliko ya tabianchi.

**41. Mheshimiwa Spika**, katika kukabiliana na changamoto za uharibifu wa mazingira nchini, Ofisi imeendelea kusimamia utekeleza Sera, Sheria, Mikakati mbalimbali ya hifadhi ya mazingira, Mikataba ya Kimataifa na Kikanda ya Mazingira na Miradi ya hifadhi ya mazingira. Katika kutekeleza azma hiyo, kwa mwaka 2020/21, Ofisi kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imetekeleza yafuatayo: -

- (i) **Utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Mazingira 1997, Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2004, Miongozo na Kanuniza Usimamizi wa Mazingira**

### **Sera ya Taifa ya Mazingira 1997**

**42. Mheshimiwa Spika**, Ofisi imekamilisha mapitio ya Sera ya Taifa ya Mazingira (1997) na kuandaa Rasimu ya Sera mpya ya Mazingira (2020). Lengo ni kuhuisha sera na kujumuisha maeneo mapya ya kimazingira kama vile kuongezeka kwa viumbe vamizi, taka za kielektroniki, matumizi ya kemikali na bioteknolojia ya kisasa yasiyo salama, kukua kwa shughuli za utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia pamoja na uwekezaji katika miradi ya Mazingira.

**43. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka 2020/21, Ofisi imefanya mapitio ya Mpango Kazi wa Taifa wa Hifadhi ya

Mazingira wa Mwaka 2013-2018 na kuandaa Mpango Kazi Mpya wa Taifa wa Hifadhi ya Mazingira wa Mwaka 2021-2026. Lengo la mapitio hayo ni kuhisha changamoto na masuala mapya ya mazingira yaliyobainishwa katika Taarifa ya Tatu ya Hali ya Mazingira ya mwaka 2019; Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo (2021 - 2026); Ilani ya CCM (2020 – 2025), Malengo ya Maendeleo Endelevu 2015 – 2030; Mikataba na itifaki za kimataifa za usimamizi wa mazingira ambazo Serikali imeridhia katika kipindi cha 2013 - 2020; na Programu za Kikanda (EAC na SADC) za kuhifadhi na usimamizi wa mazingira.

### ***Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Mwaka 2004***

**44. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2020/21, Ofisi kwa kushirikiana na wadau imefanya marekebisho madogo ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira kifungu cha 194 kuhusu utaratibu wa kufifisha makosa kwenye usimamizi wa mazingira. Marekebisho hayo yanalenga kupunguza mlolongo wa kupeleka kesi mahakamani zinazohusu mazingira pale ambapo mtuhumiwa ameridhia kulipa faini kulingana na kosa husika kwa mkaguzi wa mazingira. Maboresho hayo yataanza kutumika mara baada ya kupitishwa na Bunge lako tukufu.

### ***Kanuni na Miongozo ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2004***

**45. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka 2020/21, Ofisi imekamilisha mapitio ya Kanuni ya Usajili wa Wataalam wa Mazingira za mwaka 2005. Lengo la mapitio haya ni kuongeza ufanisi na tija katika mchakato wa Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM). Aidha, Ofisi imeendelea kufanya marekebisho ya Kanuni tatu (3) za: Udhhibiti wa Taka Hatarishi za mwaka 2019; Udhhibiti wa Kemikali Zinazomong'onyoa Tabaka la Ozoni za mwaka 2007; na za Wakaguzi wa Mazingira za mwaka 2009. Vilevile, Ofisi imeanza maandalizi ya kanuni mpya (3) za: Udhhibiti wa Taka za Kieletroniki za mwaka 2021; Hifadhi ya Maeneo Lindwa na Nyeti za mwaka 2021 na za Udhhibiti wa Kemikali Zinazodumu

kwenye Mazingira kwa Muda Mrefu za mwaka 2021. Pia, Ofisi inakamilisha maandalizi ya Mwongozo wa Udhambi wa Taka Ngumu kwa Kutumia Dhana ya Punguza, Tumia Tena na Rejeleza ili kuboresha utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira. Marekebisho ya kanuni hizi yataanza kutumika mara baada ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali.

**(ii) Hifadhi ya Bioanuai**

***Mwongozo wa Matumizi ya Eneo la Hifadhi ya Mita 60 kutoka kwenye Vyanzo vya Maji***

**46. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2020/21, Ofisi imekamilisha Mwongozo wa Taifa wa Matumizi Endelevu ya Eneo la Hifadhi la Mita 60 kutoka kwenye fukwe za bahari na maziwa, kingo za mito na Mabwawa. Lengo la Mwongozo huo ni kuweka utaratibu wa matumizi endelevu ya ardhi kwa shughuli zinazoweza kuruhusiwa na zisizoruhusiwa kufanyika katika maeneo hayo ili kuchangia katika kukuza uchumi na ustawi wa jamii. Mwongozo huu utanza kutumika mara baada ya kuridhiwa na wadau wote.

***Mkakati na Mpango-kazi wa Kitaifa wa Kutatua changamoto za Viumbe Vamizi***

**47. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka 2020/21, Ofisi imesambaza Mkakati na Mpango-Kazi wa Kitaifa wa Kutatua changamoto za viumbe vamizi kwa wadau kwa ajili ya utekelezaji. Aidha, kupitia Mkakati huo, Wizara za Kilimo; Mifugo na Uvuvi; na Taasisi ya Utafiti wa Viuatilifu zimeandaa mipango ya miaka mitano (2020 - 2025) ya kutekeleza Mikakati iliyobainishwa katika Mkakati na Mpango-kazi wa Kitaifa.

***Kupunguza Matumizi ya Mkaa Utokanao na Miti***

**48. Mheshimiwa Spika**, Katika kipindi cha mwaka 2020/21, Ofisi imeendelea na jitihada za kupunguza matumizi ya mkaa unaotokana na miti na kuhamasisha matumizi ya nishati mbadala ikiwa ni pamoja na:gesi, mkaa mbadala, umeme na bayogesi.



Katika kipindi hiki, Ofisi imeendelea kushirikiana na Taasisi za Serikali kuandaa Mipango-kazi ya kila taasisi ya kupunguza matumizi ya nishati ya kuni na mkaa kwa ajili ya kupikia. Hadi mwezi Februari, 2021 jumla ya Taasisi (11) zimeandaa mipango hiyo. Taasisi hizo ni: Jeshi la Magereza, Jeshi la Kujenga Taifa, Jeshi la Wananchi Tanzania, Uhamiaji, Kurugenzi ya Huduma ya Wakimbizi; Chuo cha Msitu Olmotony; Chuo cha Mafunzo ya Uhifadhi wa Maliasili kwa Jamii; Chuo cha Taifa cha Utalii; Chuo cha Mafunzo ya Ufugaji Nyuki Tabora; Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori Mweka; Chuo cha Viwanda vya Misitu; na Chuo cha Taaluma za Wanyamapori zimeandaa na kuwasilisha Mipango-kazi ya kupunguza matumizi ya kuni na mkaa.

### ***Usimamizi wa Maeneo Lindwa na Nyeti***

**49. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka 2020/21, Ofisi kwa kushirikiana na wadau imeandaa Kanuni za Hifadhi ya Maeneo Lindwa Nchini ili kusimamia maeneo ambayo yatakuwa yakitangazwa kuwa ni maeneo lindwa na nyeti. Aidha, Ofisi kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI katika Mikoa ya Singida na Mara imetambua na kuweka mipaka katika maeneo matatu (3) yaliyopendekezwa kuwa maeneo nyeti na lindwa ya mazingira. Maeneo hayo ni: Ziwa Singidani, Kindai na Munangi mkoa wa Singida na Mlima Mkendo Mkoani Mara

(iii) Udhhibiti wa Uchafuzi wa Mazingira  
*Udhhibiti wa Mifuko ya Plastiki*

**50. Mheshimiwa Spika**, kufuatia Tamko la Serikali la Kupiga Marufuku Uzalishaji, Uingizaji, Uuzaji, Usambazaji, Usafirishaji nje ya nchi na Utumiaji wa Mifuko ya Plastiki nchini kuanzia tarehe 1 Juni, 2019, katika mwaka wa fedha 2020/21, Ofisi kwa kushirikiana na Shirika la Viwango Tanzania (TBS) imeandaa viwango vya ubora vya mifuko mbadala wa plastiki aina ya Non-woven (*TZS 2303: Non-woven bags - specification*) ambavyo vitasaidia kudhibiti ubora wa mifuko hiyo. Viwango hivyo vimeshasambazwa kwa viwanda 30 vinavyojihusisha na uzalishaji na usambazaji wa mifuko hiyo.

**51. Mheshimiwa Spika**, Katazo la matumizi ya mifuko ya plastikilimeibua changamoto mpya ambapo vifungashio vya plastiki vimeanza kutumika kama vibebeo na hivyo kuchangia kuongezeka kwa uchafuzi wa mazingira. Aidha, kumekuwepo na changamoto ya matumizi ya vifungashio vya plastiki visivyokidhi viwango vya ubora. Katika kukabiliana na changamoto hizi Serikali lilitoa tamko la kusitisha matumizi ya vifungashio vya plastiki kama vibebeo vya bidhaa; na kutoa kipindi cha mpito cha miezi mitatu kuanzia tarehe 8 Januari 2021 kuviondoa sokoni vifungashio vya plastiki visivyokidhi viwango vya ubora.



*Pichani: Vifungashio vilivyobadilishwa matumizi na kutumika kama vibebeo vya bidhaa kinyume cha sheria.*



### ***Usimamizi wa Taka Hatarishi***

**52. Mheshimiwa Spika**, katikamwaka 2020/21, Ofisi imetoa jumla ya vibali **251** ambapo vibali **246** ni vya kukusanya, kuhifadhi na kusafirisha taka hatarishi ndani ya nchi na vibali **5** vya kusafirisha taka hizo nje ya nchi. Aidha, katika kuboresha utaratibu wa utoaji wa vibali, Ofisi imeandaa Mwongozo wa Utoaji Elimu kwa Umma kuhusu Udhhibiti na Usimamizi wa Taka Hatarishi utakaowezesha wadau mbalimbali kupata uelewa kuhusu udhibiti na usimamizi wa taka hatarishi. Katika kipindi hicho kiasi tani **143,000** za chuma chakavu kilikusanywa na tani **1,898** za chuma chakavu zilisafarishwa nje ya nchi.

#### **(iv) Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi**

##### ***Mkakati wa Taifa wa Mabadiliko ya Tabianchi***

**53. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka 2020/21, Ofisi kwa kushirikiana na wadau, imekamilisha mapitio ya Mkakati wa Mabadiliko ya Tabianchi wa mwaka 2012 ili kujumuisha masuala muhimu yaliyojitokeza kitaifa na kimataifa, ikiwa ni pamoja na: Mpango wa tatu wa maendeleo wa Taifa 2021/22-2025/26; Changamoto za mabadiliko ya tabianchi zilizobainishwa katika taarifa ya tatu ya mazingira 2019; Makubaliano ya Paris ya mwaka 2015 kuhusu kuongeza juhudi za kukabiliana na mabadiliko ya Tabianchi; Malengo ya Maendeleo Endelevu 2015-2030; Makubaliano ya Umoja wa Afrika kuhusu Afrika tunayoitaka na Mikakati ya nchi za Jumuiya za Kusini mwa Afrika na Jumuiya ya Afrika Mashariki kuhusu mabadiliko tabianchi. Mkakati mpya wa Mabadiliko ya Tabianchi ya mwaka 2021 – 2026 unatarajiwa kuzinduliwa na kuanza kutumika katika mwaka wa fedha 2021/22.

##### ***Mfuko wa Mabadiliko ya Tabianchi (GCF)***

**54. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka 2020/21, Ofisi imeendelea kuratibu shughuli za Mfuko wa Mabadiliko ya Tabianchi (GCF) uliopo chini ya Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa mabadiliko ya tabianchi. Shughuli zilizofanyika ni pamoja nakuwezesha Benki ya CRDB ambayo imepewa

ithibati katika mfuko huo kuandaa programu ya kujenga uwezo wa sekta ya kilimo kuanda miradi ya kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi. Programu hii inathamani ya Dola za Marekani **610,500**nautekelezaji wake utaanza katika kipindi cha mwaka wa fedha 2021/22.

#### **(v) Kukabiliana na Uharibifu wa Ardhi**

##### ***Kampeni ya Upandaji Miti milioni 1.5 kwa Kila Halmashauri kwa Mwaka***

**55. Mheshimiwa Spika**Katika kipindi cha mwaka 2020/21, Ofisi kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais-TAMISEMI imeendelea kuratibu utekelezaji wa kampeni ya kitaifa ya upandaji na utunzaji wa miti inayoelekeza kila Halmashauri ya Wilaya kutenga maeneo na kupanda miti milioni **1.5** kila mwaka. Katika kipindi cha mwaka 2019/20, idadi ya miti iliyopandwa ni **197,623,843** na iliyostawi **159,282,897** sawa na asilimia **80.6**.Napenda kuchukua fursa hii kuzitaka Halmashauri zote ambazo hazikutimiza lengo hili kuhakikisha zinachukua hatua za makusudi kufikia azma hii katika mwaka ujao.

##### ***Kampeni ya Kuifanya Dodoma kuwa ya Kijani***

**56. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka 2020/21, Ofisi imeendelea kuratibu utekelezaji wa Kampeni ya Kuifanya Dodoma kuwa ya Kijani. Katika kipindi hiki, takriban miche **71,782** ilipandwa katika maeneo mbalimbali ya Jiji la Dodoma.



*Afisa Mazingira Mkuu kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais Dkt. Paul Deogratius akipanda mti katika eneo la Chuo Kikuu cha Dodoma ikiwa ni sehemu ya kampeni za kuifanya nchi kuwa ya kijani.*

### ***Mpango wa Taifa wa Kupambana na Kuenea kwa Jangwa na Hali ya Ukame***

**57. Mheshimiwa Spika**, Katika kipindi cha mwaka 2020/21, Ofisi imepitia Mpango wa Taifa wa Kupambana na Kuenea kwa Hali ya Jangwa na Ukame. Lengo la mapitio haya ni kuhuisha changamoto za uharibifu wa ardhi zilizobainishwa katika Taarifa ya Tatu ya Hali ya Mazingira ya mwaka 2019.

#### **(vi) Elimu kwa Umma Kuhusu Uhifadhi wa Mazingira**

**58. Mheshimiwa Spika**, Katika kipindi cha mwaka 2020/21, Ofisi imeendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu hifadhi na usimamizi wa mazingira kupitia njia mbalimbali ikiwa ni pamoja na vyombo vya habari; maadhimisho mbalimbali ya kitaifa; kimataifa; ziara za Viongozi; Semina kwa wabunge wa Kamati ya Bunge ya Viwanda Biashara na Mazingira; na mashindano ya insha kwa wanafunzi. Maeneo yaliyotolewa elimu ni pamoja na: Mabadiliko ya Tabianchi; Usimamizi taka ngumu; Usimamizi wa taka hatarishi; Matumizi ya nishati mbadala; Hifadhi ya Tabaka la Ozoni; Matumizi ya zebaki katika shughuli za wachimbaji wadogo; Viumbe vamizi; Sheria na Kanuni za usimamizi wa mazingira; Miradi ya hifadhi ya mazingira; Mikataba ya kimataifa ya mazingira; na Taarifa ya Hali ya Mazingira nchini. Aidha, katika kipindi hiki Ofisi imeendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu Katazo la Mifuko ya Plastiki kupitia vipindi vya redio na runinga, mitandao ya kijamii na magazeti pamoja na kufanya mikutano ya kimkakati na wazalishaji, wasambazaji na watumiaji wa vifungashio vya plastiki.

#### ***Maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani***

**59. Mheshimiwa Spika**, ifikapo tarehe 5 Juni kila mwaka, Dunia huadhimisha Siku ya Mazingira Duniani. Kwa mwaka 2021, maadhimisho hayo Kimataifa yatafanyika nchini Pakistani na Kauli Mbiu itakuwa, "***Kuongoa Mfumo Ikolojia***" (***Ecosystem Restoration***). Kitaifa, maadhimisho hayo yatafanyika mkoani Dodoma, na Kauli Mbiu ya Kitaifa itakuwa ni, "***Tutumie Nishati Mbadala, Kuongoa Mfumo Ikolojia***".

**60. Mheshimiwa Spika**, katika kuadhimisha siku hii kitaifa, shughuli mbalimbali za uhamasishaji zimepangwa kufanyika ikiwa ni pamoja na: kuendesha kongamano la mazingira kuhusu hifadhi ya vyanzo vya maji, matumizi ya nishati mbadala na usimamizi wa taka ngumu; kuendesha mijadala katika Vyombo vya Habari kuhusu maadhimisho hayo na Kauli Mbiu husika; na kufanya usafi wa mazingira katika maeneo mbalimbali nchini.

**61. Mheshimiwa Spika**, Ofisi imeanza kuandaa maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani ambayo kilele chake itakuwa ni tarehe 5 Juni, 2021. Kupitia maadhimisho hayo, Mheshimiwa Makamu Rais wa Serikali ya jamhuri ya Muungano wa Tanzania, atazindua Kampeni Kabambe ya Uhifadhi na Usafi wa Mazingira. Lengo la Kampeni hiyo ni kuongeza nguvu katika kuwaleta pamoja wadau wote na wananchi katika masuala ya uhifadhi na usafi wa mazingira. Kampeni hiyo itakuwa na Tuzo mbalimbali kwa Taasisi, Makundi na mtu mmoja mmoja watakaoshinda katika vigezo mbalimbali vya uhifadhi na usafi wa mazingira.

**(vii) Kuimarisha usimamizi wa shughuli za hifadhi na usimamizi wa mazingira katika Sekta na Mamlaka za Serikali za Mitaa**

**62. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka 2020/21, Ofisi imeendelea kuratibu utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004 katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Katika kipindi hiki, maafisa mazingira 48 kutoka Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri za Lindi, Mtwara, Mbeya, Songwe, Rukwa, Katavi na Ruvuma walipatiwa mafunzo mbalimbali kuhusu hifadhi ya mazingira hususan Tathmini ya Athari kwa Mazingira Kimkakati (TMK).

**(viii) Tathmini na Ukaguzi wa Mazingira**

**63. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka 2020/21, Ofisi imepitia Taarifa ya Tathmini ya Mazingira Kimkakati kuhusu Mradi wa Uzalishaji wa Umeme wa Maji wa Kikonge katika mto Ruhuhu mkoani Ruvuma na Njombe na kutoa kibali cha utekelezaji wake (*SEA Approval Notice*). Aidha, Ofisi

imeendelea kufuatilia utekelezaji wa Mipango ya Usimamizi wa Mazingira ya Tathmini za Mazingira Kimkakati zilizopitishwa.

***(ix) Utekelezaji wa Miradi ya Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira na mabadiliko ya Tabianchi***

**64. Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2020/21, Ofisi iliendelea kutekeleza miradi ya hifadhi na usimamizi wa mazingira. Katika kipindi hiki jumla ya miradi mitatu (3) ilitokelezwa kama ifuatavyo: -

*i) Mradi wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi Kupitia Mifumo ya Ikolojia*

**65. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka 2020/21, Ofisi iliendelea kutekeleza Mradi wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi Kupitia Mifumo ya Ikolojia ambapo kiasi cha shilingi **1,380,000,000** kilitumika. Kazi zilizotekelezwa ni Pamoja na: kuandaa mfumo wa kielektroniki wa usimamizi wa taarifa na elimu kuhusu kukabiliana mabadiliko ya tabianchi; kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi katika vijiji **14** katika wilaya za Simanjiro, Kishapu, Mpwapwa na Mvomero nakuanzisha vitalu vya miche **114,416** katika wilaya za Mvomero (miche 40,000), Simanjiro (miche 45,416), Kishapu (miche 3,000), na Mpwapwa (miche 26,000).



*Moja ya Kitalu cha miche **114,416** katika wilaya ya Mvomero*

ii) Mradi wa Kujenga Uwezo wa Taasisi na Jamii Kuhimili Athari za Mabadiliko ya Tabianchi Kwenye Maeneo ya Kaskazini mwa Nchi

**66. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka 2020/21, Ofisi iliendelea kutekeleza Mradi wa Kujenga Uwezo wa Taasisi na Jamii Kuhimili Athari za Mabadiliko ya Tabianchi Kwenye Maeneo ya Kaskazini mwa Nchi ambapo kiasi cha shilingi **80,500,000** zilitumika kukamilisha malipo ya kazi zilizosalia. Kazi zilizotekelezwa katika kipindi hiki ni Pamoja na: Ujenzi wa skimu mbili (2) za usambazaji wa maji safi na salama kwenye vijiji vya kambi ya Simba, Makuyuni na Jipe Wilaya ya Mwanga; ujenzi wa mfereji wa kisasa wa umwagiliaji wenye urefu wa mita 1800 katika kijiji cha Mabilioni Wilaya ya Same; ufungaji wa mitambo miwili (2) ya Hali ya Hewa katika Wilaya za Same na Mwanga kwa lengo la kutoa taarifa za uhakika za hali ya hewa; kutoa mafunzo ya mabadiliko ya tabianchi kwa viongozi wa halmashauri na wataalam katika hamashauri za Mwanga na Same; kutoa mafunzo kwa vikundi vya wakulima kuhusu uendeshaji endelevu wa Skimu ya umwagiliaji katika kijiji cha Mabilioni Wilaya ya Same; na kuhuisha masuala ya mabadiliko ya Tabianchi katika mipango na miongozo ya wilaya za Same na Mwanga.



Mitambo miwili (2) ya Hali ya Hewa katika Wilaya za Same na Mwanga kwa lengo la kutoa taarifa za uhakika za hali ya hewa

iii) *Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Ardhi ya Bonde la Ziwa Nyasa*

**67. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka 2020/21 Ofisi imeendelea kuratibu utekelezaji Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Ardhi ya Bonde la Ziwa Nyasa ambapo kiasi cha shilingi **230,165,952.84** kilitumika. Kazi zilizotekelezwa ni pamoja na: kuendesha mafunzo kuhusu matumizi ya majiko banifu kwa kaya **40** na kuwezesha utengenezaji wa majiko banifu **96** katika wilaya za Nyasa na Mbinga; kuelimisha vijiji **26** kuhusu uanzishaji na uimarishaji wa jumuiya za watumia maji katika Bonde la Ziwa Nyasa katika Halmashauri za Wilaya ya Mbinga Vijiji (**16**) na Nyasa (Vijiji 10); na kufanya utafiti wa shughuli mbadala za kujiongezea kipato kwa vijiji vitatu (**3**) kwa kila halmashauri za wilaya tano (5) za Nyasa, Mbinga, Kyela, Ludewa na Makete.



*Mfano wa majiko banifu yaliyotengenezwa katika kaya za wilaya za Nyasa na Mbinga*

***Miradi mipya ya Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira iliyopitishwa***

**68. Mheshimiwa Spika**, Ofisi imefanikiwa kupata fedha kutoka kwa wafadhili kwa miradimipya 3 ambayo itaanza utekelezaji kabla ya mwisho wa mwaka wa fedha 2020/21. Miradi hiyo ni kama ifuatavyo:-



i. Mradi wa Kupunguza Hewa Ukaa inayosababishwa na Ukataji na Uharibifu wa Misitu wenye thamani ya Shilingi Bilioni 2 na unatekelezwa Kitaifa. Lengo Kuu la mradi huo ni kujenga uwezo wa kitaasisi ikiwemo Ofisi ya Makamu wa Rais, Wizara za Kisekta, *NEMC* na Mamlaka za Serikali za Mitaa katika kupunguza Hewa Ukaa ifikapo Mwaka 2022;

ii. Mradi wa Kujenga Uwezo wa Kitaasisi wa Kutekeleza Sheria ya Usimamizi wa Mazingira. Mradi huu ni wa miaka 3 (2020-2023) na unatekelezwa kwa gharama ya Shilingi Bilioni 6.9 kwa ufadhili wa Serikali ya Sweden. Lengo kuu la Mradi huo ni kuimarisha uwezo wa Taasisi na Mamlaka husika ikiwemo mifumo na nyenzo za kisasa katika kusimamia utekelezaji na uzingatiaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira; na

iii. Mradi wa Usimamizi Jumuishi wa Mfumo Ikolojia na urejeshwaji wa Uoto Asili na Hifadhi ya Bionuai. Mradi huoni wa kipindi cha miaka 5 (2021 hadi 2026) na unafadhiliwa na Mfuko wa Mazingira Duniani (*Global Environment Facility – GEF*) kwa gharama ya Dola za Marekani 11,205,872. Lengo la mradi huu ni kuimarisha usimamizi jumuishi wa Mfumo Ikolojia na kurejesha Uoto wa asili na Hifadhi ya Bionuai katika Wilaya za: Chunya, Iringa, Kasulu, Kibondo, Mbarali, Mpanda Mpimbwe, Waging’ombe, Sumbawanga na Uvinza.

## **BARAZA LA TAIFA LA HIFADHI NA USIMAMIZI WA MAZINGIRA**

**69. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2020/21, Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira kama msimamizi mkuu wa uzingatiaji na utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Sura 191 limeendelea kutekeleza majukumu yake kama ifuatavyo:-

### ***Ukaguzi wa Maeneo ya Uwekezaji na Mazingira***

**70. Mheshimiwa Spika**, Baraza limefanya kaguzi katika miradi **1,910** inayojumuisha viwanda, migodi, mabomba ya mafuta, mitambo ya gesi na mafuta, mitambo ya nishati ya umeme, maghala ya kemikali na taka zenye madhara, vituo vya mafuta, na masoko. Changamoto kubwa za kimazingira



zilizojitokeza kufutia ukaguzi ni: kutiririsha majitaka kwenye mazingira ikiwemo vyanzo vya maji na makazi ya watu; Matumizi yasiyo endelevu ya rasilimali kama misitu ya asili kwa ajili ya nishati na ujenzi; Ukosefu wa mifumo ya kuhifadhi taka ngumu; Uzalishaji wa hewa chafu; na Uzalishaji na usambazaji wa mifuko mbadala isiyokidhi viwango. Baraza lilitoa maelekezo kwa wenye miradi kurekebisha kasoro zilizoonekana.



*Ukaguzi wa hali ya mazingira katika mradi wa kufua umeme wa Julius Nyerere Wilayani Rufiji.*

### ***Udhibiti wa taka zenye madhara***

**71. Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka 2020/21, Baraza limepokea maombi **16** ya usimamizi wa uteketezaji wa taka zenye madhara ambapo kiasi cha tani **324** za taka zenye madhara zimeteketazwa zikiwemo dawa, kemikali na bidhaa za viwandani zilizokwisha muda wake wa matumizi.

### ***Usajili wa Miradi na Utoaji wa Vyeti vya Mazingira***

**72. Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka 2020/21, Baraza limesajili jumla ya miradi **1,206**. Kati ya miradi iliyosajiliwa miradi ya TAM ni **733** na miradi ya Ukaguzi wa Mazingira ni **473**. Aidha, katika kipindi hicho vyeti vya TAM **591** vilitolewa.

### ***Ufuatiliaji wa Miradi Mikubwa ya Uchimbaji na Uchenjuaji wa Madini***

**73. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2020/21, Baraza limefanya ufuatiliaji wa miradi **10**, migodi **9** na mtambo mmoja wa uchenjuaji wa dhahabu. Taarifa ya ukaguzi imeainisha maeneo ya kuboresha kwenye Sheria, Kanuni na Miongozo ili kuwa na usimamizi madhubuti wa shughuli za uchimbaji na uchenjuaji madini.



*Wataalamu kutoka Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) wakifanya Ukaguzi katika Mgozi wa Dhahabu wa North Mara*

### ***Usajili wa Wataalam Elekezi wa Mazingira***

**74. Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka 2020/21, Baraza limefanya uchambuzi wa wataalam elekezi na kuandaa orodha ya wataalam elekezi wenye sifa na kuweka kwenye tovuti ya Baraza. Orodha hiyo ina wataalam elekezi **191** (kati yao **120** ni eneo TAM na **71** katika eneo la Ukaguzi wa Mazingira) na makampuni 108 (katika eneo la TAM **66** na **42** katika eneo la Ukaguzi wa mazingira) waliokidhi vigezo. Hatua hii itawarahisishia wawekezaji katika kuwapata wataalam elekezi kwa ajili ya TAM na ukaguzi wa mazingira.

### ***Elimu kwa Umma Kuhusu Hifadhi ya Mazingira***

**75. Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka wa Fedha 2020/21, Baraza limetoa elimu ya mazingira kupitia vyombo vya habari

nakutoa mafunzo kwa Wakaguzi wa Mazingira 16 kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Aidha, Baraza lilifanya Mikutano miwili 2 ya kusikiliza wadauna mikutano minne 4 ya mashauriano pamoja na kushiriki katika maadhimisho mbalimbali.



*Mkutano wa wamiliki wa Baa na Kumbi za starehe jijini Dar es Salaam ulioandaliwa na NEMC kutoa elimu juu ya uchafuzi wa kelele kwenye mazingira.*

## **Tathmini na Usimamizi wa Mifumo Ikolojia**

**76. Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka 2020/21, Baraza liliandaa Mwongozo wa kufanya tathmini ya mifumo ikolojia ya milima na vilima (*Mountain Ecosystem Assessment Framework*)lengo ni kuwa na mfumo mmoja wa kufanya tathmini ya milima na vilima nchini. Aidha, mwezi Disemba 2020 majaribio ya kutathmini ufanisi wa mwongozo huo yalifanyika katika baadhi ya milima katika mkoa wa Iringa kwa lengo la kuuboresha kabla ya kuanza kutumika.

## **Maandalizi ya Miradi**

**77. Mheshimiwa Spika**,katika Mwaka 2020/21, Baraza limeidhinishiwa miradi minne (4) na Mfuko wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabiachi.Miradi hiyo ambayo itanza utekelezaji kabla ya mwisho wa mwaka wa fedha 2020/21 ni pamoja na:

- i. Mradi wa kuhimili mabadiliko ya tabianchi kwenye jamii za wafugaji na wakulima wilaya ya Kongwa wenye thamani ya Dola za Marekani 1,200,000;
- ii. Mradi wa kimkakati wa uvunaji maji katika maeneo kame ya ukanda wa kati wenye thamani ya Dola za Marekani 1,280,000;
- iii. Mradi wa kuhimili mabadiliko ya tabianchi miongoni mwa jamii za Pwani kutoka Zanzibar wenye thamani ya Dola za Marekani 1,000,000; na
- iv. Mradi wa kuhimili mabadiliko ya tabianchi Bunda (*Bunda Climate Resilient and Adaptation Project*) wenye thamani ya Dola za Marekani **1,400,000**.

#### **MASUALA YA UTAWALA NA MAENDELEO YA WATUMISHI**

**78. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa Fedha 2020/21 Ofisi imeendelea kusimamia Sheria, Kanuni, Taratibu, Miongozo na Maadili ya Utumishi wa Umma na imewezesha watumishi kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi. katika kipindi hiki jumla ya watumishi **14** wamewezeshwa kuhudhuria mafunzo mbalimbali ambapo watumishi wanne (**4**) walihudhuria mafunzo ya muda mrefu, watumishi watatu (**3**) Walihudhuria mafunzo ya muda mfupi na watumishi saba (**7**) wamepatiwa mafunzo ya awali baada ya kuajiriwa kwa mujibu wa Sheria. Aidha, Ofisi imeendelea kuboresha mazingira ya utendaji kazi kwa kuwezesha upatikanaji wa vitendea kazi kwa kadiri fedha zilivyopatikana.

**79. Mheshimwa Spika**, Ofisi imeendelea kuimarisha maadili, Utawala Bora, ushirikishwaji wa vyama vya wafanyakazi na dhana ya ushirikishwaji na uwajibikaji wa watumishi mahala pa kazi. Aidha sekta binafsi imeshirikishwa katika utoaji wa huduma na bidhaa katika Ofisi ili kuendeleza dhana ya ushirikishwaji wa Sekta Binafsi.

#### **CHANGAMOTO NA MIKAKATI ILIYOPO**

**80. Mheshimiwa Spika**, pamoja na Ofisi ya Makamu wa Rais kuendelea kutekeleza majukumu yake, ilikabiliwa na changamoto kadhaa zikiwemo;-

- i. Uwepo wa tofauti ya Sheria kwa pande mbili za Muungano, hukwamisha utekelezaji wa baadhi ya maamuzi yanayofikiwa katika kutatua changamoto za Muungano;
- ii. Kutokutekelezwa kikamilifu kwa Mfumo wa Kitaasisi wa Usimamizi wa Mazingira katika ngazi ya Wizara za Kisekta na Mamlaka za Serikali za Mitaa;
- iii. Uelewa mdogo wa jamii kuhusu Muungano na hifadhi na usimamizi wa masuala ya mazingira; na
- iv. Uzingatiaji mdogo wa jamii kuhusu sheria, kanuni na taratibu za hifadhi na usimamizi wa mazingira.

**81. Mheshimiwa Spika**, katika kukabiliana na changamoto hizi, Ofisi ilichukua hatua zifuatazo:- Kuendelea na majadiliano baina ya SMT na SMZ kuhusu changamoto za kisheria; Kuendelea na majadiliano kati ya Ofisi ya Makamu wa Rais na Ofisi ya Rais-TAMISEMI kuhusu kuimarisha Muundo wa Ofisi ya Rais-TAMISEMI katika kuratibu shughuli za uhifadhi na usimamizi wa mazingira;kuanza utekelezaji wa mradi wa Kujenga Uwezo wa Utekelezaji wa Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004, ambao pamoja na mambo mengine utaimarisha mfumo wa kitaasisi wa usimamizi wa mazingira katika Wizara za Kisekta na Mamlaka za Serikali za Mitaa; kuendelea na majadiliano na Wizara za Kisekta kuhusu kuimarisha uratibu wa masuala ya mazingira katika sekta husika; na kuendelea kutoa elimu kwa umma juu ya masuala ya Muungano na hifadhi na usimamizi wa mazingira.

## MALENGO NA MAOMBI YA FEDHA ZA MATUMIZI YA KAWAIDA NA MAENDELEO KWA MWAKA 2021/22

### MASUALA YA MUUNGANO

***Kuratibu Vikao vya Kamati ya Pamoja ya SMT na SMZ ya Kushughulikia Masuala ya Muungano***

**82. Mheshimiwa Spika**,kwa mwaka wa fedha 2021/22, Ofisi itaendelea Kuratibu utatuzi wa changamoto zilizobakia na zitakazojitokeza katika utekelezaji wa masuala ya Muungano

kupitia Vikao vya Kamati ya Pamoja ya SMT na SMZ ya Kushughulikia Masuala ya Muungano. Vikao hivi vitafanyika katika ngazi zifuatazo: - Kikao kimoja (1) cha Kamati ya Pamoja ya SMT na SMZ; Kikao kimoja (1) cha Mawaziri wa SMT na SMZ; Vikao viwili (2) vya Makatibu Wakuu wa SMT na SMZ; Vikao vinne (4) vya Sekretarieti ya Kamati ya Pamoja ya SMT na SMZ; na Vikao vya Kamati Ndogo za Fedha, Uchumi na Baishara na Kamati ya Sheria, Katiba na Utawala.

***Kuratibu Masuala ya Kiuchumi na Kijamii***

**83. Mheshimiwa Spika**, Ofisi itaendelea kuratibu masuala ya kiuchumi na kijamii kwa kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa programu na miradi ya maendeleo inayotekelezwa pande mbili za Muungano ikiwa ni pamoja na kuratibu utekelezaji wa miradi inayotekelezwa kwa fedha za Kuchochea Mfuko wa Jimbo, Zanzibar na kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa Taasisi za Muungano.

***Kuratibu masuala yasiyo ya Muungano ili kuimarisha ushirikiano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar***

**84. Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2021/22, Ofisi itaendelea na uratibu wa masuala yasiyo ya Muungano kupitia vikao vya ushirikiano vya Wizara, Idara na Taasisi za SMT na SMZ zisizo za Muungano zenye majukumu yanayoshabihiana.

***Kutoa Elimu ya Muungano kwa Umma***

**85. Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2021/22, Ofisi itaendelea kutoa elimu ya Muungano kwa umma kwa makundi tofauti ya kijamii kupitia: - Redio; Luninga; Makala za magazeti; Makongamano ya Muungano; na mitandao ya kijamii.

**HIFADHI NA USIMAMIZI ENDELEU WA MAZINGIRA**

**Vipaumbele vya Mwaka 2021/22**

**86. Mheshimiwa Spika**, katika jitihada za kuhakikisha kuna hifadhi endelevu ya mazingira mwaka 2021/22, Ofisi imepanga kutekeleza vipaumbele sita (6), ambavyo

ni:Kuimarisha usimamizi wa shughuli za hifadhi na usimamizi wa mazingira katika ngazi ya Serikali za Mitaa; Kuhamasisha matumizi ya Nishati mbadala; Kulinda na kutunza Vyanzo vya maji; Udhhibiti wa taka ngumu; Kuendelea kuratibu utekelezaji wa Mpango-kazi wa Taifa wa kupunguza matumizi ya zebaki kwa wachimbaji wadogo wa dhahabu nchini; na Kuendelea kufuatilia utekelezaji wa sheria ya usimamizi wa mazingira katika migodi na viwandani.

**Kazi zilizopangwa kutekelezwa kwa mwaka 2021/22**  
***Kuimarisha usimamizi wa shughuli za hifadhi na usimamizi wa mazingira katika ngazi ya Serikali za Mitaa***

**87. Mheshimiwa Spika**,Ofisi itaendelea na hatua za uimarishaji wa usimamizi wa shughuli za hifadhi na usimamizi wa mazingira katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Katika kipindi hiki, Ofisi itaratibu vikao vya mashirikiano baina ya Ofisi ya Makamu wa Rais na TAMISEMI kwa lengo la kuimarisha katika utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2004.

***Kuhamasisha Matumizi ya Nishati Mbadala***

**88. Mheshimiwa Spika**,Ofisi itaendelea kuhamasisha matumizi ya nishati mbadala. Shughuli zitakazotekelezwa ni pamoja na:kuandaa Mkakati wa Nishati Mbadala ya Kuni na Mkaa kwa ajili ya kupikia; na kuendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu matumizi ya nishati mbadala hususan kwa taasisi zinazotumia kuni na mkaa kwa ajili ya kupikia zikiwemo magereza, polisi, na taasisi za elimu. Katika kipindi hiki, Ofisi itaendelea na ufuatiliaji wa utekelezaji wa mipango iliyowekwa na taasisi mbalimbali kuhusu matumizi ya nishati mbadala.

***Hifadhi ya Vyanzo vya Maji***

**89. Mheshimiwa Spika**,Ofisi itaendelea kuratibu utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa kuhifadhi mazingira ya Ardhi na Vyanzo vya Maji nchini 2019 – 2024 na kutoa elimu ya usimamizi na hifadhi ya mazingira kuhusu hifadhi ya vyanzo vya maji. Aidha,

kwa kushirikiana na Wizara ya Maji na Mamlaka za Serikali za Mitaa, Ofisi itaendelea kutekeleza miradi ambayo Pamoja na masuala mengine inalenga hifadhi ya vyanzo vya maji ikiwemo: -

(i) Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Ardhi ya Bonde la Ziwa Nyasa unaotekelezwa katika Halmashauri za Wilaya za Ludewa, Makete, Kyela, Nyasa na Mbinga;

(ii) Mradi wa Usimamizi Jumuishi wa Mfumo Ikolojia na urejeshwaji wa Uoto Asili na Hifadhi ya Bionuai unaotekelezwa katika Halmashauri za Wilaya za Chunya, Iringa, Kasulu, Kibondo, Mbarali, Mpanda, Mpimbwe, Waging'ombe, Sumbawanga, na Uvinza.

(iii) Mradi wa Kurejesha Ardhi iliyoharibika na kuongeza Usalama wa Chakula katika maeneo kame ya Tanzania unaotekelezwa katika Halmashauri za Wilaya zaKondo, Mkalama, Nzega, Magu na Micheweni (Kaskazini Pemba); na

(iv) Mradi wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi Kupitia Mifumo ya IkolojiaWilaya za Mvomero, Simanjiro, Kishapu, Mpwapwa na Kaskazini A (Kaskazini Unguja).

### ***Udhibiti wa taka ngumu***

**90. Mheshimiwa Spika**, katika kuimarisha usimamizi na udhibiti wa taka ngumu, Ofisi itatekeleza shughuli zifuatazo: kufuatilia utekelezaji wa Mwongozo wa Usimamizi na Udhibiti wa Taka Ngumu kwa kutumia dhana ya Punguza, Tumia tena na Rejeleza; kuratibu utekelezaji wa miradi ya majaribio wa usimamizi na udhibiti wa taka za katika Jiji la Dodoma na Dar es Salaam; kuendelea kutoa elimu ya usimamizi na hifadhi ya mazingira kuhusu udhibiti wa taka ngumu; kuendelea kufuatilia utekelezaji wa Katazo la Matumizi ya Mifuko ya Plastiki na Tamko kuhusu Marufuku ya Vifungashio vya plastiki visivyokidhi viwango; kuandaa Mkakati mahsusi wa kuhamasisha uanzishwaji na utumiaji wa madampo ya kisasa (*Sanitary Landfills*); na kuandaa Mwongozo wa Wajibu wa



Wazalishaji Kudhibiti Taka zinazozalishwa kutokana na bidhaa wanazozizalisha.

***Kuratibu utekelezaji waMpango-kazi wa Taifa wa kupunguza matumizi ya zebaki kwa wachimbaji wadogo wa dhahabu nchini***

**91. Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza Mpango-kazi wa Taifa wa kupunguza matumizi ya zebaki kwa wachimbaji wadogo wa dhahabu nchini, Ofisi itaendelea kutoa elimu kuhusu matumizi ya zebaki kwa wachimbaji wadogo wa dhahabu na kuhamasisha matumizi ya teknolojia mbadala wa zebaki. Aidha, kwa kushirikiana na Mamlaka husika, Ofisi itaandaa Mkakati wa udhibiti wa athari za zebaki kwa afya ya binadamu na mazingira; itaainisha na kufanya tathmini ya maeneo yenye shughuli nyingi za uchimbaji mdogo wa dhahabu kwa kutumia zebaki na kuweka mikakati ya kuyarejesha katika hali yake ya asili; na kutoa mafunzo kwa mamlaka zinazohusika na udhibiti wa zebaki kuhusu namna ya kudhibiti uingizaji, matumizi na utupaji wa taka zitokanazo na zebaki nchini.

***Kufuatilia Utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2004 katika migodi na viwanda***

**92. Mheshimiwa Spika**, Ofisi kwa kushirikiana na wadau itaendelea kufuatilia na kufanya ukaguzi katika migodi na viwanda kuhusu uzingatiaji wa sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004 katika viwanda na migodi. Aidha, Ofisi itaendelea kutoa elimu kwa wenye viwanda na migodi kuhusu kuweka mifumo ya kutibu majitaka kabla ya kuyatiririsha katika mazingira.

***Kutekeleza Mradi wa Kuimarisha Miundombinu ya Mazingira katika Maeneo Mablimali Nchini***

**93. Mheshimiwa Spika**, Katika kipindi hiki Serikali itaendelea na utekelezaji wa miradi ya kuimarisha miundombinu ya mazingira ikiwemo vizimba vya kukusanya Taka Ngumu, Madampo, kujenga kingo za kuzuia maji katika bahari,

maziwa na mito, kujenga uzio katika maeneo lindwa na kuboresha. Aidha, miradi mingine itahusisha ujenzi wa visima, mabwawa ya kulishia mifugo na mabwawa ya kuifadhi maji yenye kemikali inayotokana shughuli za wachimbaji wadogo katika maeneo ya migodi.

### ***Masuala mengine yatakayotekelezwa***

**94. Mheshimiwa Spika**, masuala mengine yatakayotekelezwa ni pamoja na: -

(i) Kukamilisha na kuanza kutekelezwa kwa Sera mpya ya Taifa ya Mazingira ya Mwaka (2020) na mkakati wa utekelezaji;

(ii) Kufanya mapitio ya Mpango Mkakati wa Hifadhi ya Bioanuai nchini;

(iii) Kuandaa mwongozo wa Kisekta wa Tathmini ya Athari kwa Mazingira;

(iv) Kuandaa mwongozo wa Upandaji miti nchini na kusimamia Kampeni ya Kitaifa ya Upandaji miti milioni 1.5 kwa mwaka kwa kila Wilaya;

(v) Kuendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu hifadhi ya mazingira, mabadiliko ya tabianchi, viumbe vamizi, biounuai, hifadhi ya vyanzo vya maji, na uzingatiaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2004;

(vi) Kufuatilia utekelezaji wa Mikakati na Mipango ya hifadhi ya mazingira, na miongozo ya usimamizi wa mazingira nchini ikiwa ni pamoja na Mkakati wa kuhifadhi mazingira ya bahari, ukanda wa Pwani, maziwa, mito na mabwawa 2019 – 2024; Mkakati wa Taifa wa kuhifadhi mazingira ya Ardhi na Vyanzo vya Maji nchini 2019 – 2024; Mkakati wa Usimamizi wa Kemikali na Taka nchini 2020 - 2025; na Mkakati wa Mabadiliko ya Tabianchi 2021 – 2026; na Mkakati na Mpango-kazi wa Taifa wa Viumbe vamizi 2019 -2024;

(vii) Kuandaa mwongozo wa usimamizi wa mazingira katika utekelezaji wa uchumi wa bluu;

(viii) Kukamilisha maandalizi ya miradi mitano (5) ya hifadhi na usimamizi wa mazingira chini ya ufadhili wa Mfuko wa Dunia wa Mazingira-GEF;

(ix) Kukamilisha maandalizi ya kanuni sita (6) na kutunga Kanuni mpya tano (5) za Sheria ya Usimamizi wa Mazingira.

***Kuendelea kutekeleza miradi ya hifadhi na usimamizi wa mazingira***

**95. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2021/22, Ofisi itaendelea kutekeleza miradi ya hifadhi na usimamizi wa mazingira. Katika kipindi hiki jumla ya miradi tisa (9) itatekelezwa kama ifuatavyo: -

*i. Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Ardhi ya Bonde la Ziwa Nyasa*

**96. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2021/22, kiasi cha shilingi **392,388,000.00** kimetengwa kutekeleza kazi zifuatazo: Kujenga uwezo wa vikundi vya wakulima na wadau wengine katika matumizi bora ya ardhi; Kuwezesha uzalishaji endelevu wa mkaa na matumizi ya majiko banifu; Kuwezesha usimamizi endelevu wa vyanzo vya maji; Kuwezesha makundi ya wanawake na vijana katika uwekezaji mdogo wa kilimo biashara; Kuwezesha usimamizi shirikishi wa misitu; Kuendesha mafunzo kwa ya shamba darasa kwa wakulima; Kuendesha mafunzo kwa vikundi vya wavuvi kuhusu uvuvi endelevu; Kuendesha mafunzo kwa wakulima kuhusu upandaji miti kibiashara; Kuendesha mafunzo kwa wachimbaji wadogo kuhusu uchimbaji endelevu madini; na Kuwezesha makundi ya wakulima kufanya ziara za mafunzo kuhusu kilimo endelevu.

*ii. Mradi wa Usimamizi Jumuishi wa Mfumo Ikolojia na urejeshwaji wa Uoto Asili na Hifadhi ya Bionuai*

**97. Mheshimiwa Spika**, Mradi huu ni wa kipindi cha miaka 5 (2021 hadi 2026) unafadhiliwa na Mfuko wa Mazingira Duniani

(*Global Environment Facility – GEF*) kwa gharama ya Dola za Marekani **11,205,872**. Lengo la mradi huu ni kuweka mikakati ya usimamizi jumuishi wa Mfumo Ikolojia na urejeshwaji wa Uoto Asili na Hifadi ya Bionuai katika Wilaya za: Chunya, Iringa, Kasulu, Kibondo, Mbarali, Mpanda Mpimbwe, Waging'ombe, Sumbawanga, na Uvinza.

**98. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2021/22 jumla ya Shilingi **500,000,000.00**. zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza mradi huu. Kazi zitakazotekelezwa ni hizi zifuatazo: Kuendesha mafunzo kwa maafisa wa Halmashauri zinazotekeleza mradi kuhusu utekelezaji wa shughuli za mradi; Kuanzisha jumua tano (5) za mifumo ya ushirikishaji wa jamii katika uhifadhi wa wanyamapori na misitu; Kutekeleza kilimo kinachozingatia mabadiliko ya tabianchi; na Kujenga miundombinu sita (6) ya maji kwa ajili ya binadamu na mifugo yakiwemo Malambo na visima.

*iii. Mradi wa Kujenga Uwezo wa Kutekeleza Mkataba wa Montreal Kuhusu Udhhibiti wa Kemikali Zinazomong'onyoa Tabaka la Ozoni*

**99. Mheshimiwa Spika**, Mradi huu unafadhiliwa na Mfuko wa Utekelezaji wa Itifaki ya Montreal (*Multilateral Fund for Implementation of Montreal Protocol*) kupitia Shirika la Mazingira la Umoja wa Mataifa (UNEP) kwa gharama ya Shilingi 213,900,000.00. Lengo la Mradi ni kujenga uwezo wa Kitaasisi kuwezesha utekelezaji wa Itifaki ya Montreal Kuhusu Udhhibiti wa Kemikali Zinazomong'onyoa Tabaka la Ozoni.

**100. Mheshimiwa Spika**, Katika Mwaka 2021/22 kiasi cha Shilingi **50,000,000.00** zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza kazi zifuatazo:- Kufuatilia utekelezaji wa Kanuni za ODS hususan kwenye matumizi ya kemikali zinazomong'onyoa Tabaka la Ozoni; Kufanya vikao na Taasisi za Serikali kuhusu udhibiti wa kemikali zinazomong'onyoa Tabaka la Ozoni; na kukuza uelewa wa jamii kuhusu utekelezaji wa Mkataba wa Vienna na Itifaki ya Montreal kuhusu Udhhibiti wa Kemikali Zinazoharibu Tabaka la Ozoni.

*iv. Mradi wa Kutekeleza Mpango wa Kitaifa wa Utekelezaji wa Mkataba wa Stockholm Unaohusu Kemikali Zinazodumu katika Mazingira kwa Muda Mrefu*

**101. Mheshimiwa Spika**, Mradi huu unafadhiliwa na Mfuko wa Dunia wa Mazingira (GEF) kwa gharama ya Shilingi **1,876,567,700** chini ya usimamizi wa Shirika la Mazingira la Umoja wa Mataifa (UNEP). Mradi unatekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano (2017 hadi 2022). Lengo la mradi ni kulinda afya ya binadamu na mazingira kutokana na athari za kemikali zinazodumu kwenye mazingira kwa muda mrefu.

**102. Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka 2021/22 kiasi cha Shilingi **300,000,000.00** zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza kazi zifuatazo: kukusanya sampuli za mafuta ya kwenye transfoma Zanzibar na kusafirisha Afrika Kusini kwa ajili ya uchunguzi wa kimaabara; Kukamilisha rasimu ya Kanuni za Usimamizi wa kemikali zinazodumu kwenye mazingira kwa muda mrefu (POPs); Kukusanya sampuli za hewa na kusafirisha nje ya nchi kwa uchunguzi wa kimaabara; Kukusanya sampuli za maji na kufanya uchunguzi wa kimaabara nchini; Kuwezesha uanzishwaji wa kanzidata ya kemikali zitokanazo na uchomaji taka; na Kufanya kikao cha wadau cha kuainisha fursa za urejelezaji wa taka ngumu.

*v. Mradi wa Kurejesha Ardhi iliyoharibika na kuongeza Usalama wa Chakula katika maeneo kame ya Tanzania*

**103. Mheshimiwa Spika**, mradi huu ni wa miaka mitano (2017-2022) na unafadhiliwa na Mfuko wa Dunia wa Mazingira (*Global Environment Facility*) kupitia Mfuko wa Kimataifa wa Maendeleo ya Kilimo (*International Fund for Agricultural Development*) na unatekelezwa kwa gharama ya Shilingi **15,599,999,340.00**. Lengo la mradi ni kuboresha mifumo ya kiikolojia ambayo itawezesha kuongeza uzalishaji wa chakula na hivyo kuchangia moja kwa moja kuboresha mazingira katika eneo husika na unategemea kuongoa hekta 9,000 za ardhi zilizoharibika katika Halmashauri za wilaya za Kondoa (Dodoma), Mkalama (Singida), Nzega (Tabora), Magu (Mwanza) na Micheweni (Kaskazini Pemba).

**104. Mheshimiwa Spika**Kwa kipindi cha Mwaka 2021/22 kiasi cha Shilingi **500,000,000.00** kwa ajili ya kutekeleza kazi zifuatazo: - Kuendesha mafunzo ya shamba darasa kwa maafisa ugani, Kamati ya Maliasili; vikundi vya watumiaji maji na Kamati za vijiji za mipango ya matumizi ya ardhi; Kuwezesha kufanya tathmini shirikishi ya misitu kwa ajili ya kuandaa mpango shirikishi wa usimamizi wa misitu katika jamii za Wahadzabe katika wilaya ya Mkalama; na Kujenga miundombinu ya maji ikiwemo malambo, visima na mifumo ya kuvuna maji ya mvua.

*vi. Mradi wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi Kupitia Mifumo ya Ikolojia*

**105. Msheshimiwa Spika**, Mradi huu ni wa kipindi cha miaka mitano (5) (2018 hadi 2022) na unatekelezwa kwa gharama ya Shilingi **17,413,835,900** kwa ufadhili wa Mfuko wa Dunia wa Mazingira (*Global Environment Facility - GEF*). Lengo la mradi ni Kuongeza uwezo wa kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi katika jamii za vijijini nchini Tanzania kwa kuimarisha mifumo ya ikolojia katika Wilaya za Mvomero (Morogoro), Simanjiro (Manyara), Kishapu (Shinyanga), Mpwapwa (Dodoma) na Kaskazini A, (Kaskazini Unguja).

**106. Msheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2021/22 ya kiasi cha Shilingi **800,000,000.00** kwa ajili ya kutekeleza kazi zifuatazo: - Kuanzisha maeneo ya malisho katika Wilaya za Mpwapwa, Simanjiro, Mvomero na Kishapu; Kuwezesha hifadhi ya mito katika Wilaya ya Mvomero; Kukarabati malambo sita (6) na kuanzisha maeneo nane (8) ya uhifadhi wa malisho endelevu katika maeneo ya mradi; Kuotesha vitalu vya miti 390,000 ili kuboresha Lindimaji; Kuongoa ardhi iliyoharibika na kuboresha Kingo za mito; Kuwezesha utekelezaji wa kilimo kinachozingatia mabadiliko ya tabianchi; Kuwezesha uanzishaji wa shughuli mbadala kwa ajili ya kuhimili mabadiliko ya tabianchi; na Kuendesha mafunzo kwa maafisa wa Serikali za Mitaa kuhusu kuhimili mabadiliko ya tabianchi kwa kutumia mifumo-ikolojia

*vii. Mradi wa Majaribio wa Kikanda wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi katika Bonde la Ziwa Victoria*

**107. Msheshimiwa Spika**, Mradi huu unatekelezwa katika wilaya ya Magu. Lengo la mradi huu ni kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi. Lengo la mradi huu ni kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi. Katika kipindi cha mwaka 2021/22 kiasi cha Shilingi **128,400,000.00** kimetengwa kwa ajili ya kutekeleza kazi zifuatazo:- Ukarabati wa kisima katika kijiji cha Sekoture ili kuwezesha kilimo cha umwagiliaji kwa wakulima wadogo; Kuchimba na kujenga kisima katika shule ya msingi Busaranga katika kijiji cha Ng'haya; Kujenga na kuboresha mifumo ya uvunaji maji ya mvua katika shule ya Sekondari Ng'haya na kuanzisha kitalu cha miti; na Kuwezesha miradi ya majaribio ya kilimo cha misitu ili kuhimili mabadiliko ya tabianchi katika kijiji cha Ng'haya.

*viii. Mradi wa Kupunguza Hewa Ukaa inayosababishwa na Ukataji na Uharibifu wa Misitu*

**108. Msheshimiwa Spika**, Mradi huu unatekelezwa Kitaifa na lengo la mradi ni kujenga uwezo wa kitaasisi katika kupunguza Hewa Ukaa ifikapo Mwaka 2022. Katika kipindi cha mwaka 2021/22 kiasi cha Shilingi **100,000,000.00** kimetengwa kwa ajili ya kutekeleza kazi zifuatazo: Kujenga uwezo wa kitaasisi katika kusimamia na kuratibu shughuli za kupunguza hewa ukaa inayotokana na ukataji na uharibifu wa misitu; Kuhuisha Mkakati wa Kupunguza Uharibifu wa Misitu na Ukataji Miti katika sera na mipango; Kukamilisha mwongozo wa Taifa wa Kupunguza Hewa Ukaa inayosababishwa na Ukataji na Uharibifu wa Misitu; na Kujenga uwezo wa wataalam katika sekta za: Misitu, Maliasili, Nishati, Kilimo, Mifugo, Ardhi na Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kuibua na kuandaa maandiko ya miradi ya kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi.

*ix. Mradi wa Kujenga Uwezo wa Kitaasisi wa Kutekeleza Sheria ya Usimamizi wa Mazingira*

**109. Msheshimiwa Spika**, Mradi huu ni wa miaka 3 (2020-2023) na unatekelezwa kwa gharama ya Shilingi Bilioni **6.9** (Dola za

Marekani Milioni 3) kwa ufadhili wa Serikali ya Sweden.Lengo kuu la Mradi ni kuimarisha uwezo wa Taasisi na Mamlaka husika ikiwemo mifumo na nyenzo za kisasa katika kusimamia utekelezaji na uzingatiji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira.

**110. Mheshimiwa Spika**, Katika kipindi cha mwaka 2021/22 kiasi cha Shilingi **200,000,000.00** kimetengwa kwa ajili ya kutekeleza kazi zifuatazo: - Kufanya tathmini ya utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004; Kuandaa kanuni 15 na miongozo 15 inayohitajika kwa ajili ya kuboresha usimamizi na utekelezaji wa Sheria husika; Kuweka mfumo wa kimtandao wa kutoa vibali vya mazingira (Tathmini ya Mazingira Kimkakati; na vibali vya taka za vifaa vya umeme na kielektroniki).

#### **MASUALA YA UTAWALA NA MAENDELEO YA WATUMISHI**

**111. Mheshimiwa Spika**,kwa mwaka 2021/22 Ofisi imepanga kupandisha vyeo watumishi **26** kwa kuzingatia utendaji wao wa kazi na miundo inayotawala kada zao na watumishi **56** wataajiriwa.

**112. Mheshimiwa Spika**, Ofisi itaendelea kusimamia Sheria, Kanuni, Taratibu, Miongozo na kuimarisha Maadili na Utawala Bora katika Utumishi wa Umma. Aidha, Ofisi itaendelea kutoa elimu kuhusu masuala ya UKIMWI, Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza, ushauri nasaha, kupima afya kwa hiari na kutoa huduma stahiki kwa watakojitokeza na kuthibitika kuwa na maambukizi ya VVU. Pia Ofisi itaendelea kuboresha mazingira ya utendaji kazi kwa kuhakikisha uwepo wa vitendea kazi, samani za Ofisi na stahili za watumishi.

#### **BARAZA LA TAIFA LA HIFADHI NA USIMAMIZI WA MAZINGIRA**

**113. Mheshimiwa Spika**,katika mwaka 2021/22, Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira litaendelea kushirikiana na mamlaka nyingine katika kushughulikia udhibiti wa uchafuzi wa Mazingira katika maeneo mbalimbali ya kijamii na uzalishaji ili kuwa na maendeleo endelevu. Katika kipindi hicho, Baraza limepanga kufanya mapitio ya TAM kwa miradi



**3,000** itakayosajiliwa kwa ajili ya kupata vyeti vya TAM/ Ukaguzi.

**114. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2021/22, Baraza litaendelea kujenga uwezo kwa wadau hususan Serikali za Mitaa kwa kutoa mafunzo kwa maafisa na wakaguzi wa mazingira, na elimu kwa umma ili waweze kusimamia utekelezaji wa sheria ya mazingira katika maeneo yao.



*Mkurugenzi Mkuu wa NEMC Dkt. Samwel Gwamaka akitoa elimu kwa wachimbaji wa mchanga.*

### **Uanzishwaji naUhifadhi wa Maeneo Lindwa/Nyeti**

**115. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2021/22 Baraza kwa kushirikiana na Halmashauri husika litaandaa Mipango ya usimamizi wa maeneo ambayo yatakuwa yametangazwa kuwa Maeneo Nyeti ya Mazingira. Aidha, Baraza kwa kushirikiana na Halmashauri husika litaendelea kuainisha maeneo mengine ili yaweze kutangazwa kuwa Maeneo Nyeti ya Mazingira. Vile vile, Baraza litashiriki kuandaa miongozo ya usimamizi wa mazingira katika maeneo lindwa na nyeti (EPAs) na (ESAs).

## **Usimamizi na Uratibu wa Miradi**

**116. Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka 2021/22, Barazalitaendelea kufuatilia shughuli za kuhimili mabadiliko ya tabianchi na kufanya mapitio ya miradi inayowasilishwa na wadau na kuiwasilisha kwenye Mfuko wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi iweze kupata ufadhili. Aidha, Baraza litaendelea kuwajengea uwezo wadau ili kuandaa maandiko ya miradi inayokubalika kuombewa fedha. Vilevile, Baraza litaandaa taarifa mbalimbali zinazohitajika kukamilisha mchakato wa kupata ithbati katika mfuko mwingine wa mabadiliko ya tabianchi wa GCF.

### ***Mradi wa Kudhibiti Uchafuzi wa Mazingira kutokana na Matumizi ya Zebaki***

**117. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2021/22, Baraza litaanza kutekeleza mradi wenye thamani ya Dola za Kimarekani Milioni **7.33** unaofadhiliwa na Mfuko wa Mazingira wa Dunia (GEF) kupitia Benki ya Dunia na '*Environmental Management and Pollution Management Project (EHPMP)*'. Mradi huu unalenga kupunguza madhara ya kimazingira na afya yanayotokana na matumizi ya Zebaki miongoni mwa wachimbaji wadogo wa dhahabu (Artisanal and Small-Scale Gold Miners-ASGM). Mikoa itakayohusika katika utekelezaji ni Geita, Mwanza, Mara, Shinyanga, Singida, Mbeya na Songwe.

### ***Kusogeza huduma kwa wananchi, Kujengea uwezo Watumishi na Kuboresha Mapato ya Baraza***

**118. Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka 2021/22, Baraza litaendelea kuzijengea uwezo ofisi za kanda kwa kuongeza vitendea kazi na watumishi, na kuboresha mifumo ya TEHAMA ili kuongeza ufanisi katika utoaji huduma katika kanda za Baraza.

## HITIMISHO NA SHUKRANI

**119. Mheshimiwa Spika**, nchi yetu ni ya Muungano ambao una umuhimu wa pekee kwa Taifa na umekuwa ni utambulisho wa Taifa letu na kielelezo cha umoja wetu katika kudumisha Amani, Mshikamano na Usalama wa nchi yetu. Mwaka huu Muungano wetu unatimiza miaka 57 tangu kuasisiwa kwake. Ninatoa wito kwa Watanzania wote kuendelea kuuthamini, kuuenzi, kuulinda na kuudumisha Muungano kwa lengo la kusukuma mbele maendeleo ya kiuchumi, kijamii na kisiasa kwa faida za pande zote mbili za Muungano.

**120. Mheshimiwa Spika**, chini ya uongozi wa Rais wetu, Mheshimiwa **Samia Suluhu Hassan**, Makamu wa Rais, Mheshimiwa **Philip Isdor Mpango**, na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa **Dkt. Hussein Ali Mwinyi**, Muungano wetu unaendelea kuimarika na kushamiri. Chini ya uongozi wao mahiri, hakuna changamoto yoyote inayoweza kutufarakanisha, kututenganisha wala kuturudisha nyuma. Katika mwaka 2021/22, Ofisi na Serikali kwa ujumla itaendelea kuyafanyia kazi mambo yote yanayoleta changamoto katika utekelezaji wa masuala yanayohusu Muungano na kutoa elimu kuhusu Muungano ili uendelee kuimarika.

**121. Mheshimiwa Spika**, maendeleo endelevu na uchumi wa viwanda haviwezi kupatikana bila kutunza na kuhifadhi mazingira. Kutokana na umuhimu huu, ni jukumu la kila Mtanzania kuhakikisha kuwa mazingira na maliasili za nchi yetu zinalindwa na kuhifadhiwa ipasavyo. Ninapenda kutoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge pamoja na wananchi kwa ujumla kuunga mkono juhudi za Serikali katika kulinda na kuhifadhi mazingira kwa manufaa ya kizazi cha sasa na kijacho.

**122. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2021/22, Ofisi itaendelea kutoa miongozo katika nyanja mbalimbali kwa lengo la kuhifadhi mazingira kwa kuangalia mifumo ikolojia, mifumo ya uzalishaji mali, na mifumo ya uchumi ya matumizi

ya rasilimali asili. Vilevile Ofisi, imejipanga kuipa elimu ya mazingira kipaumbele kwa jamii ili kuhakikisha mazingira yanalindwa na kutunzwa.

## SHUKRANI

**123. Mheshimiwa Spika**, ninaomba nitumie nafasi hii kuwashukuru walionisaidia kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Ofisi. Shukrani zangu za dhati na za kipekee ni kwa Mheshimiwa **Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake na maelekezo aliotupatia kuhusu majukumu yetu. Aidha, ninamshukuru Mheshimiwa **Dkt Philip Isdor Mpango**, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa busara na uongozi wake makini unaotuwzesha kutekeleza majukumu yetu. Ninapenda kumshukuru Mheshimiwa **Hamad Hassan Chande (Mb.)**, Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, kwa ushirikiano anaonipa katika utekelezaji majukumu ya kila siku.

**124. Mheshimiwa Spika**, Vilevile, ninapenda kuwashukuru **Mary Ngelela Maganga**, Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Rais; **Mohamed Abdallah Khamis**, Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Baraza la Hifadhi ya Mazingira, **Prof. Mhandisi Esnati O. Chagguna**, wajumbe wa Bodi, **Dkt. Samuel Mafwenga**, Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira; Wakuu wa Idara na Vitengo; na Wafanyakazi wote wa Ofisi ya Makamu wa Rais na Baraza kwa mchango wao katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Ofisi na Baraza. Pia ninawashukuru wale wote waliotuwzesha kutekeleza majukumu ya Ofisi kwa kipindi kilichopita, na ambao wamesaidia katika kuandaa Mpango na Bajeti ya mwaka 2021/22.

**125. Mheshimiwa Spika**, Ofisi imefanikisha utekelezaji wa majukumu yake kwa kushirikiana na Washirika wa Maendeleo. Ninapenda kuwataja baadhi ya washirika wa maendeleo ambao Ofisi imefanya nao kazi kwa karibu kama ifuatavyo: Serikali ya Norway; Serikali ya Canada; Serikali ya Sweden; Serikali ya Italia; Serikali ya Jamhuri ya Watu wa

Korea; Umoja wa Nchi za Ulaya (*European Union - EU*); Shirika la Mpango wa Maendeleo la Umoja wa Mataifa (*United Nations Development Programme - UNDP*); Shirika la Mazingira la Umoja wa Mataifa (*UNEP*); Mfuko wa Mazingira wa Dunia (*Global Environment Facility - GEF*); Benki ya Maendeleo ya Afrika (*African Development Bank - AfDB*); Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo ya Viwanda (*United Nations Industrial Development Organization - UNIDO*); Shirika la Uhifadhi wa Mazingira Duniani (*World Wide Fund for Nature – WWF*); Mfuko wa Kimataifa wa Kuendeleza Kilimo (*International Fund for Agricultural Development - IFAD*); Mfuko wa Mabadiliko ya Tabianchi (*Green Climate Fund - GCF*); Shirika la Kilimo na Chakula Duniani (*Food and Agriculture Organization - FAO*); Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Ujerumani (*GiZ*); Kikundi cha Washirika wa Maendeleo kinachoshughulikia Mazingira (*Development Partners Group on Environment - DPGE*); Asasi Zisizo za Kiserikali (*AZISE*); na Sekta Binafsi. Aidha, ninapenda nitumie fursa hii kuwaomba Washirika wa Maendeleo kuendelea kutoa ushirikiano katika kipindi kijacho ili tuweze kufanikiwa zaidi katika kulinda na kuimarisha Muungano wetu na kulinda na kuhifadhi mazingira yetu.

## MAOMBI YA FEDHA

**126. Mheshimiwa Spika**, ili Ofisi iweze kutekeleza majukumu na malengo yaliyopangwa, ninaomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu liidhinisha maombi ya fedha jumla ya Shilingi **28,708,348,000.00** kama ifuatavyo:

### Fungu 26: Makamu wa Rais

**127. Mheshimiwa Spika**, ninaomba Bunge lako Tukufu liidhinisha Makadirio ya Matumizi ya Shilingi **8,719,076,000.00** ikiwa ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida kwa Mwaka 2021/22. Kati ya fedha hizi, Shilingi **984,111,000.00** ni fedha za Mishahara ya watumishi na Shilingi **7,734,965,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo.

**Fungu 31: Ofisi ya Makamu wa Rais**

**128. Mheshimiwa Spika**, katika fungu hili ninaomba Bunge lako Tukufu, liidhinishe jumla ya Shilingi **19,989,272,000.00**. Kati ya fedha hizi, Shilingi **13,138,484,000.00** ni kwa ajili Matumizi ya Kawaida na Shilingi **6,850,788,000.00** ni fedha za Miradi ya Maendeleo. Bajeti ya Matumizi ya Kawaida inajumuisha Shilingi **6,773,706,000.00** fedha za Mishahara na Shilingi **6,364,778,000.00** fedha za Matumizi Mengineyo. Fedha za Mishahara zinajumuisha kiasi cha Shilingi **3,021,908,000.00** Mishahara ya Watumishi wa Ofisi ya Makamu wa Rais na kiasi cha Shilingi **3,751,798,000.00** ni Mishahara ya Watumishi wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira. Aidha, fedha za Miradi ya Maendeleo zinajumuisha fedha za Ndani Shilingi **4,280,000,000.00** na Shilingi **2,570,788,000.00** ni fedha za nje.

**129. Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:**  
Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Ahsante sana Mheshimiwa Jafo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira). Tunakushukuru sana kwa kusoma hotuba yako kwa umakini na ufasaha mkubwa. *(Makofi)*

Sasa naomba nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Joseph Mhagama, tafadhali karibu sana. *(Makofi)*

Sasa ili kuokoa muda kwa sababu bajeti hii ni ya siku moja, naomba Wenyekiti mwende moja kwa moja kwenye maoni na ushauri wa Kamati.

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA:**

Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba Taarifa hii ya Kamati iliyowasilishwa Mezani iingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Spika, mnamo tarehe 28 Machi, 2021, Kamati ilipokea na kuchambua Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais – Muungano pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mafungu Mawili ya Ofisi hiyo, kwa kuzingatia vipaumbele vya Bajeti hiyo kama vilivyoainishwa na Mtoa Hoja, ambavyo viliridhiwa na Kamati.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Kamati kuridhishwa na uhalisia wa vipaumbele hivyo, Kamati inaishauri Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) kuhakikisha kwamba, utekelezaji wa vipaumbele hivyo unaakisi mwendelezo wa kuimarisha na kuulinda Muungano wetu kwa manufaa ya Watanzania wote kwa kudumisha udugu, umoja na mshikamano wa Watanzania wa pande zote mbili za Muungano.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendeleza jitihada za kutatua changamoto mbalimbali za Muungano, hususan, kuendelea kurahisisha mwingiliano wa kibiashara baina ya pande mbili za Muungano kwa kuzitafutia ufumbuzi changamoto mbalimbali za kikodi na za kisheria kwa manufaa ya Serikali za pande zote mbili na wananchi wa pande zote mbili.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa randama unabainisha kwamba kwa kipindi cha mwaka 2021/2022, Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais (Fungu 26) inatarajia kutumia jumla ya shilingi 8,719,070,000.00 kwa matumizi ya kawaida. Kiasi hicho ni pungufu ya shilingi 40,511,000.00 sawa na asilimia 0.46 ya bajeti ya matumizi ya kawaida kwa mwaka 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, aidha, hakuna mapato yanayotarajiwa kukusanywa chini ya Fungu 26 kwa mwaka 2021/2022 na hakuna bajeti ya maendeleo kwa kuwa muundo wa Ofisi Binafsi haujikiti katika majukumu hayo.

Mchanganuo wa bajeti ya kawaida kwa Fungu 26 ni kama inavyoainishwa katika jedwali la pili.

Mheshimiwa Spika, Fungu 31 (Muungano), Makadirio ya Bajeti ya Matumizi ya Kawaida; randama ya awali iliyowasilishwa mbele ya Kamati ilibainisha kuwa, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ilikuwa imeomba jumla ya shilingi bilioni 6.26 ili kutekeleza majukumu yake, bajeti ambayo kwa maoni ya Kamati ilionekana kuwa ni ndogo ukilinganisha hali halisi ya mahitaji ya Ofisi hiyo katika kutekeleza vipaumbele vyake, kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, hivyo, Kamati ilishauri ipasavyo na kutokana na vikao vya Kamati ya Bajeti, bajeti ya matumizi ya kawaida kwa Fungu 31 imeongezeka kwa shilingi 882,497,000.00 na hivyo kwa sasa maombi ya bajeti hiyo ni shilingi 7,144,332,560.00, ikijumuisha maboresho ya bajeti ya matumizi mengineyo kutoka bilioni 4.04 hadi kufikia shilingi 4,920,868,560.00. Mchanganuo wa mtiririko wa bajeti ya matumizi ya kawaida kwa Fungu 31, unabainishwa katika jedwali la tatu.

Mheshimiwa Spika, kwa mchanganuo huo, tafsiri ya kiuchambuzi ni kwamba kumekuwepo ongezeko la shilingi 241,221,000.00, ambayo ni sawa na ongezeko la asilimia 3.49 ukilinganisha na bajeti iliyoidhinishwa na Bunge chini ya Fungu hili kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Mpango wa Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2021/2022 (Fungu 31); kwa mwaka wa fedha 2021/2022, bajeti ya miradi ya maendeleo imeongezeka kwa shilingi 2,880,000,000.00 hadi kufikia shilingi 3,880,000,000.00 ya fedha za ndani, tofauti na shilingi bilioni moja kwa mwaka 2020/2021. Tafsiri ya ongezeko hilo ni kwamba, bajeti ya miradi ya maendeleo imeongezeka kwa asilimia 388 ya bajeti ya maendeleo kwa mwaka unaoisha.

Mheshimiwa Spika, randama inabainisha kuwa, fedha za miradi ya maendeleo zinazoombwa ni kwa ajili ya



utekelezaji wa miradi ifuatayo: Shilingi bilioni tatu zitatumika kwenye ukarabati na ujenzi wa Ofisi na Makazi ya Makamu wa Rais Wete (Pemba), Kilimani (Dodoma) na Tungu (Zanzibar), na; shilingi 880,000,000.00, zimepangwa kutumika katika ununuzi wa magari yatakayorahisha utekelezaji wa majukumu ya Ofisi hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa mchanganuo huo, jumla ya bajeti inayoombwa kuidhinishwa na Bunge kwa Fungu 31, kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ni shilingi 11,024,332,560.00, kwa kuzingatia mchanganuo uliobainishwa hapo juu, wenye kujumuisha bajeti ya matumizi ya kawaida na bajeti ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, hivyo, bajeti ya jumla kwa Fungu 31 imeongezeka kwa shilingi 4,121,221,000.00, ongezeko ambalo ni sawa na asilimia 59.7 ya bajeti ya Fungu hili kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, Kamati inakubaliana na ongezeko hilo ambalo lina lengo la kukamilisha utekelezaji wa miradi ya kuboresha Ofisi na Makazi ya Ofisi ya Makamu wa Rais, pamoja na manunuzi ya vifaa vya utekelezaji wa majukumu ya Ofisi hiyo, kwa pande zote mbili za Muungano.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa kutoa maoni na ushauri wa Kamati kuhusu masuala mbalimbali ya kibajeti na utekelezaji yaliyojitokeza katika uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais, (Muungano) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, pamoja na Kamati kuridhishwa kwa kasi kubwa ya utekelezaji wa maoni na mapendekezo ya Kamati yaliyotolewa kwa Ofisi ya Makamu wa Rais, (Muungano) katika mwaka wa fedha 2020/2021, ikiwa ni pamoja na kuendelea kuzingatia uwiano wa ajira katika taasisi za Muungano, katika kuajiri Watanzania kutoka pande mbili za Muungano, Kamati, inaendelea kushauri kuwa, Serikali izingatie misingi ya haki za usawa wa kijinsia katika nafasi mbalimbali za ajira katika Taasisi za Muungano kwa

kuendelea kuhakikisha kwamba, kunakuwepo uwiano sawa wa Watanzania wanaume na wanawake kutoka Zanzibar wanaopata nafasi sawa za ajira katika taasisi za Muungano.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Kamati kupongeza juhudi za Ofisi ya Makamu wa Rais, (Muungano) katika kushirikiana na mamlaka husika za pande mbili za Muungano katika kutatua changamoto mbalimbali katika sekta ya biashara baina ya pande mbili za Muungano, Kamati inaendelea kushauri kwamba, Serikali ifanye jitihada za ziada katika kuhakikisha changamoto za kifedha na za kikodi zinazolalamikiwa na wananchi wa pande zote mbili za Muungano, zinapatiwa ufumbuzi kwa wakati, hatua ambayo itachochea ukuaji wa uchumi kwa mwananchi mmoja mmoja na kwa manufaa ya Serikali zote mbili. Aidha, Serikali iendeleee na juhudi hizo katika kubaini changamoto mpya zinazoweza kuibuka na kuzitatua kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali imepokea ushauri wa Kamati kuhusu uboreshaji wa magari na vitendea kazi vingine chini ya Ofisi hii, kwa kuanza kutenga fedha kwa ajili ya manunuzi ya magari kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Kamati inaishauri Serikali kuendelea na utekelezaji wa mpango wake wa kuongeza na kuboresha vitendea kazi chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais, (Muungano) kwa kutoa fedha hizo kwa wakati, kwa lengo kurahisisha utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi hiyo kwa wakati na kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kukupongeza wewe kwa umahiri wako katika kazi ya kuliendesha Bunge la Kumi na Mbili katika kuishauri vyema Serikali kwa manufaa ya wananchi wa Tanzania. Aidha, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha Maoni ya Kamati kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Naibu Spika, Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, Mbunge, kwa weledi na umahiri wake katika kukusaidia kuongoza Bunge. Ninaipongeza pia Kamati yako ya Uongozi kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kukushauri na kukusaidia kuendesha

shughuli za Bunge la Kumi na Mbili. Wote kwa pamoja tunawaomba afya na uzima katika kutekeleza majukumu waliyopewa.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza na kumshukuru aliyekuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mheshimiwa Umyy Mwalimu, Mbunge, kwa ushirikiano wake mzuri katika kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ikiwemo uchambuzi wa bajeti hii kwa ufanisi uliokusudiwa. Aidha, ni imani ya Kamati kuwa, Waziri wa Nchi aliyepo kwa sasa, Mheshimiwa Selemani Jafo, Mbunge; Naibu Waziri, pamoja na Watendaji Wakuu na Wataalam wote wa Ofisi ya Makamu wa Rais, wataendelea kutoa ushirikiano wa kutosha katika kutekeleza ushauri wa Kamati na Bunge lako Tukufu kwa Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kwa ushirikiano na michango mizuri wakati wa kupitisha na kuchambua bajeti hii. Naomba majina yao kama yaliyo katika taarifa hii yaingie katika Taarifa Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa lakini si kwa umuhimu, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndugu Stephen Kagaigai kwa kuiwezesha Kamati kukamilisha kazi yake bila kukwama. Aidha, napenda kuwashukuru Wakurugenzi na Wasaidizi wote wa Katibu wa Bunge kama walivyotambuliwa kwenye taarifa hii kwa kufanikisha shughuli za Kamati kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naliomba Bunge lako Tukufu sasa lijadili na kuidhinisha makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano, Fungu Na. 26 na 31 kwa mwaka wa fedha 2020/2021- 2022 kama ilivyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri hivi punde.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA  
SHERIA KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA OFISI YA  
MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO) KWA MWAKA WA FEDHA  
2020/2021; PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU  
MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI HIYO KWA  
MWAKA WA FEDHA 2021/2022 KAMA ILIVYOWASILISHWA  
MEZANI**

---

**1.0 UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa **Kanuni ya 118 (9)** ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais-Muongano kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

**Mheshimiwa Spika**, Kifungu cha 6 (2) (c) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, kimeipa Kamati ya Katiba na Sheria jukumu la kusimamia shughuli za Ofisi ya Makamu wa Rias - Muungano.

Aidha, Kifungu cha 7(1) (a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, kinatoa jukumu kwa Kamati zote za Kisekta kushughulikia bajeti za Wizara inazozisimamia. Jukumu hili la Uchambuzi wa Bajeti linaendana sambamba na jukumu la ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 kwa mujibu wa Kanuni ya **Kanuni ya 117(1) na (2)**.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa **Kanuni ya 118 (4)** ya Kanuni za Kudumu za Bunge, inatoa sharti kuwa, kabla ya taarifa za utekelezaji na Makadirio ya Matumizi ya Wizara kujadailiwa Bungeni, zichambuliwe na Kamati za Bunge za Kisekta, hivyo, naomba kutoa taarifa kwa Bunge lako Tukufu kwamba, Kamati ya Katiba na Sheria imechambua Mafungu Mawili (2) ya Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais-Muongano, na kuridhia kuwa mapendekezo hayo ya Bajeti kwa mwaka wa

Fedha 2021/2022 kama ilivyowasilisha na Mtoa Hoja, yanafaa kujadiliwa na kuridhiwa na Bunge. Mafungu hayo ni:-

i) **Fungu 26** - Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais, na

ii) **Fungu 31** - Ofisi ya Makamu wa Rais,

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa hii inatoa maelezo kuhusu maeneo Manne yafuatayo:-

i) Uchambuzi kuhusu utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha unaoisha;

ii) Uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021;

iii) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais – Muungano kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022; na

iv) Maoni na Ushauri wa Kamati.

## **2.0 UCHAMBUZI KUHUSU UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021**

### **2.1 Fungu 26: Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais.**

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia Muundo na Majukumu ya Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais (Muungano), hakukuwa na Bajeti ya Miradi ya Maendeleo katika Fungu hili, kwa kuzingatia Muundo na Majukumu yake.

### **2.2 Fungu 31: Utekelezaji wa Mradi wa ukarabati wa Makazi ya Makamu wa Rais-Tunguu Zanzibar**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2020/2021, kamati ilibaini uwepo wa madai ya Wakandarasi wanao husika na ujenzi wa mradi huu, ambao walikuwa wanadai kiasi cha **Shilingi Bilioni Moja (1,000,000,000.00)**. Kutokana na

changamoto hiyo, Kamati ilishauri kwamba, Wakandarasi hao walipwe kiasi hicho cha fedha kutoka kwenye Bajeti ya fungu hilo kwa mwaka wa fedha unaoisha, kama ilivyoidhinishwa na Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, kwa kipindi cha Julai, 2020 hadi Machi, 2021, Ofisi ya Makamu wa Rais-Muungano imepokea madai yenye jumla ya **Shilingi Milioni Mia Nane Thelathini na Moja, Laki Tano Hamsini na Sita Eflu, Mia Mbili Sitini na Nane, na Senti Arobaini na Mbili (831,556,268.42)**, kutoka kwa Wakandarasi hao, ambapo, kwa mujibu wa taarifa za randama, hadi kufikia Machi, 2021, kiasi hicho cha fedha kimelipwa kwa mujibu wa madai hayo, ambacho ni sawa na **asilimia 83** ya bajeti yote iliyoidhinishwa na Bunge, kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo. Hivyo, Kamati inaipongeza Hazina kwa kulipa kwa wakati kiasi hicho cha fedha, kwa kuzingatia ushauri wa Kamati. Aidha, Kamati inashauri kuwa, Ofisi ya Makamu wa Rais-Muungano ikamilishe taratibu za kupokea kiasi kilichobaki kutoka hazina ili wakamilishe utatuzi wa changamoto hiyo, kabla ya tarehe 30 Juni, 2021.

### **3.0 YATOKANAYO NA UCHAMBUZI WA TAARIFA YA OFISI YA MAKAMU WA RAIS-MUUNGANO KUHUSU UTEKELEZAJI WA MPANGO WA BAJETI NA UZINGATIAJI WA MAONI YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021.**

**Mheshimiwa Spika**, mnamo tarehe 28 Machi, 2021, Kamati ilipokea na kuchambua Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 na uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo, kwa mujibu wa **Kanuni ya 117 (2)** ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuhusu yatokanayo na uchambuzi huo kama ifuatavyo:-

#### **3.1 Uchambuzi wa Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021**

##### **3.1.1 Upatikanaji wa fedha za Matumizi ya Kawaida kwa FUNGU 26: Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais;**

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, katika kipindi cha kuanzia Mwezi Julai, 2020 hadi mwezi Februari, 2021, Fungu 26 lilipokea jumla ya **Shilingi Bilioni Tano, Milioni Mia Saba Sitini, Laki Saba Eflu, Mia Saba Tisini na Tatu na Senti Sitini na Mbili (5,760,700,793.62)**, kwa ajili ya Mshahara na Matumizi Mengineyo, ambacho ni sawa na **asilimia 65.7** ya Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya Fungu hilo. Mchanganuo wa mwenendo wa upatikanaji wa Fedha za Matumizi ya Kawaida kwa **Fungu 26**, umebainishwa na **Jedwali la 1**.

**Jedwali la 1: Fedha Zilizopokelewa na Kutumika hadi Februari, 2021**

	Fedha Zilizopokelewa	% ya Zilizopokelewa	Fedha Zilizotumika	% ya Fedha Zilizotumika
Matumizi	5,066,284,193.2	87.9	5,034,521,663.46	99.1
Mshahara	674,161,900.00	11.9	1,715,416,000.00	30.0
<b>Jumla</b>	<b>5,740,446,093.2</b>	<b>100</b>	<b>5,729,998,563.46</b>	<b>99.5</b>

Machi, 2021

ni kwamba, Ofisi ya Makamu wa Rais katika robo tatu ya mwaka wa fedha 2020/2021 ni wakumbusha

### 3.1.2 Upatikanaji wa fedha za Matumizi ya Kawaida kwa FUNGU 31: Ofisi ya Makamu wa Rais

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, katika mwaka wa fedha 2020/2021, **Fungu 31** lilipangiwa kukusanya kiasi cha **Shilingi milioni Sita, Laki Nane Eflu (6,800,000)** kutokana na mauzo ya zabuni. Hata hivyo, randama inaonesha kuwa, hadi kufikia Februari, 2021 hakuna mapato yoyote yaliyokusanywa

Aidha, uchambuzi umebaini kuwa, katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Februari, 2021 Ofisi hiyo ilipokea jumla ya **Shilingi**

**Bilioni Nne, Milioni Mia Moja Arobaini na Moja, Laki Moja na Tisa Elfu, Mia Tano Tisini na Tatu, na Senti Sitini na Sita (4,141,109,593.66)** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, ambayo ni sawa na **asilimia 65.70** ya fedha iliyoidhinishwa.

**Mheshimiwa Spika**, kwa uchambuzi huo ni kwamba, upatikanaji wa fedha za Matumizi ya kawaida kwa **Fungu 31** ni wa kuridhisha.

*Mheshimiwa Spika, Maoni ya Kamati ni kwamba hali hii ya upatikanaji wa fedha kwa wakati inatakiwa kuendelea na kuzingatwa na Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, ili kurahisisha usimamizi na utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano kwa wakati na kwa ufanisi zaidi. Kwa hatua hii, Kamati inaipongeza Hazina na Serikali kwa Ujumla kwa kutoa Fedha za Matumizi ya Kawaida kwa wakati.*

#### **4.0 UCHAMBUZI WA MAKADIRIO YA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022**

**Mheshimiwa Spika**, Mnamo tarehe 28 Machi, 2021, Kamati ilipokea na kuchambua Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais – Muungano pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mafungu Mawili ya Ofisi hiyo, kwa kuzingatia vipaumbele vya Bajeti hiyo kama vilivyoainishwa na Mtoa Hoja, ambavyo viliridhiwa na Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na Kamati kuridhishwa na uhalisia wa vipaumbele hivyo, Kamati inaishauri Ofisi ya Makamu wa Rais-Muungano kuhakikisha kwamba, utekelezaji wa vipaumbele hivyo uakisi mwendelezo wa kuimarisha na kuulinda Muungano wetu kwa manufaa ya Watanzania wote kwa kudumisha Udugu, Umoja na Mshikamano wa Watanzania wa pande zote mbili za Muungano.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendeleza jitihada za kutatua changamoto mbalimbali za Muungano, hususan, kuendelea kurahisisha mwingiliano wa kibiashara baina ya Pande mbili za Muungano kwa kuzitafutia



ufumbuzi changamoto mbalimbali za kikodi na kisheria kwa manufaa ya Serikali za pande zote mbili na wananchi wake kwa ujumla.

#### 4.1 Fungu 26: Makadirio ya Bajeti ya Matumizi

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi wa randama unabainisha kuwa, kwa kipindi cha mwaka 2021/2022, Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais (**Fungu 26**) inatarajia kutumia jumla ya **Shilingi Bilioni Nane, Milioni Mia Saba Kumi na Tisa, na Sabibi la Sita Eflu (8,719,076,000.00)** kwa matumizi ya kawaida. Kiasi hicho ni **pungufu ya Milioni Arobaini, Laki Moja Kumi na Tano Eflu (40, 115, 000)**, sawa na asilimia 0.46 ya bajeti ya Matumizi ya kawaida kwa 2020/2021.

Aidha, hakuna mapato yanayotarajiwa kukusanywa chini ya Fungu 26 kwa mwaka 2021/22, na hakuna bajeti ya maendeleo kwa kuwa muundo wa Ofisi Binafsi haujiki katika majukumu hayo. Mchanganuo wa Bajeti ya Kawaida kwa Fungu 26 ni kama inavyobainishwa katika **Jedwali la Pili:-**

#### Jedwali la 2: Mchanganuo wa Maombi ya Bajeti ya Matumizi ya Kawaida (FUNGU 26), kwa Mwaka 2021/2022

FUNGU	Makadirio ya Mwaka 2021/22		JUMLA
	Mishahara	Matumizi Mengineyo	
1001	984,111,000.00	7,734,965,000	<b>8,719,076,000.00</b>

Chanzo: Taarifa ya WN-OMRMMZ ya tarehe 28 Machi, 2021

#### 4.2 Fungu 31 (MUUNGANO); Makadirio ya Bajeti ya Matumizi ya Kawaida

**Mheshimiwa Spika**, Randama ya awali iliyowasilishwa mbele ya Kamati ilibainisha kuwa, Ofisi ya Makamu wa Rais-Muungano kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ilikuwa imeomba jumla ya **Shilingi Bilioni 6.26** ili kutekeleza majukumu yake, bajeti ambayo, kwa maoni ya Kamati ilionekana kuwa ni ndogo ukilinganisha hali halisi ya mahitaji ya Ofisi hiyo katika

kutekeleza vipaumbele vyake, kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

Hivyo, Kamati ilishauri ipasavyo, na kutokana na Vikao vya Kamati ya Bajeti, bajeti ya Matumizi ya Kawaida kwa Fungu 31 imeongezeka kwa **Shilingi Milioni Mia Nane Themanini na Mbili, Laki Nne Tisini na Saba Eflu (882,497,000.00)** na hivyo kwa sasa maombi ya Bajeti hiyo ni **Shilingi Biloni Saba, Milioni Mia Moja Arobaini na Nne, Laki Tatu Thelathini na Mbili Eflu, Mia Tano Sitini (7,144,332,560)**, ikijumuisha maboresho ya Bajeti ya Matumizi mengineyo kutoka **Biloni 4.04** hadi kufikia **Shilingi Biloni Nne, Milioni Mia Tisa Ishirini, Laki Nane Sitini na Nne Eflu, Mia Tano Sitini (4,920,868,560.00)**. Mchanganuo wa mtiririko wa Bajeti ya Matumizi ya kawaida kwa Fungu 31, inabainishwa katika **Jedwali la tatu**.

**Jedwali la Tatu: Mchanganuo wa Makisio ya Bajeti ya Matumizi ya Kawaida kwa Mwaka 2021/2022**

Kifungu	Idara/Kitengo	Mshahara	Matumizi Mengineyo	Jumla
1001	Utawala na Rasilimali Watu	961,864,000	2,823,901,560	3,785,765,560
1002	Uhasibuna Fedha	213,288,000	157,929,000	371,217,000
1003	Sera na Mpango	237,784,000	478,199,000	715,983,000
1004	Mawasiliano Seikalini	45,080,000	153,705,000	198,785,000
1005	Ukaguzi wa Ndani	98,412,000	143,612,000	242,024,000
1006	Uhunzi na Ugavi	106,068,000	190,053,000	296,121,000
1007	Tehama	114,020,000	259,635,000	373,655,000
1008	Hudumaza Sheria	176,936,000	175,800,000	352,736,000
2001	Mungano	270,012,000	538,034,000	808,046,000
	<b>Jumla</b>	<b>2,223,464,000</b>	<b>4,920,870,560</b>	<b>7,144,332,560</b>

**Chanzo: Taarifa ya WN-OMRMMZ ya tarehe 28 Machi, 2021**

Kwa mchanganuo huo, tafsiri ya kiuchambuzi ni kwamba, kumekuwepo ongezeko la **Shilingi Milioni Mia Mbili Arobaini na Moja, Laki Mbili Ishirini na Moja Eflu (241,221,000)**, ambayo ni sawa na ongezeko la **asilimia 3.49** ukilinganisha na bajeti iliyoidhinishwa na Bunge chini ya Fungu hili kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021.

#### **4.2.1 Uchambuzi wa Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 (FUNGU 31).**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2021/2022, bajeti ya Miradi ya Maendeleo imeongezeka kwa **Shilingi Bilioni Mbili, Milioni Mia Nane Themanini Eflu (2,880,000,000.00)** hadi kufikia **Shilingi Bilioni Tatu, Milioni Mia Nane Themanini Eflu (3,880,000,000)** ya fedha za ndani, tofauti na **Shilingi Bilioni Moja** kwa mwaka **2020/2021**.Tafsiri ya ongezeko hilo ni kwamba, bajeti ya miradi ya Maendeleo imeongezeka kwa **asilimia 388** ya Bajeti ya Maendeleo kwa Mwaka unaoisha.

**Mheshimiwa Spika**, randama inabainisha kuwa, fedha za Miradi ya maendeleo zinazoombwa ni kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ifuatayo:-

**a) Shilingi Bilioni 3** zitatumika kwenye ukarabati na ujenzi wa Ofisi na Makazi ya Makamu wa Rais Wete-Pemba, Kilimani – Dodoma na Tunguu – Zanzibar,na

**b) Shilingi Milioni Mia Nane Themanini Eflu (880,000,000)**, zimepangwa kutumika katika ununuzi wa magari yatakayorahisisha utekelezaji wa majukumu ya Ofisi hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mchanganuo huo, jumla ya bajeti inayoombwa kuidhinishwa na Bunge kwa Fungu 31, kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 ni **Shilingi Bilioni Kumi na Moja, na Milioni Ishirini na Nne,Laki Tatu Thelathini na Mbili Eflu (11,024,332,560.00)**, kwa kuzingatia mchanganuo uliobainishwa hapo juu, wenye kujumuisha bajeti ya Matumizi ya Kawaida na bajeti ya Miradi ya Maendeleo.

Hivyo, bajeti ya jumla kwa **Fungu 31** imeongezeka kwa **shilingi Bilioni Nne, Milioni Mia Moja Ishirini na Moja, Laki Mbili Ishirini na Moja Efu (4,121,221,000)**, ongezeko ambalo ni sawa na **asilimia 59.70** ya bajeti ya Fungu hili kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inakubaliana na ongezeko hilo ambalo lina lengo la kukamilisha utekelezaji wa miradi ya kuboresha Ofisi na makazi ya Ofisi ya Rais, pamoja na manunuzi ya vifaa vya utekelezaji wa majukumu ya Ofisi hiyo, kwa pande zote mbili za Muungano.

## 5.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika**, ninaomba sasa kutoa maoni na ushauri wa Kamati kuhusu masuala mbalimbali yaliyojitokeza katika uchambuzi wa Taarifa ya utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 pamoja na Taarifa za Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 wa Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano kama ifuatavyo:-

i) **Mheshimiwa Spika**, pamoja na Kamati kuridhishwa kwa kiasi kikubwa na utekelezaji wa maoni na mapendekezo ya Kamati yaliyotolewa kwa Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) katika Mwaka wa Fedha 2020/2021, ikiwa ni pamoja na kuendelea kuzingatia uwiano wa ajira katika taasisi za Muungano, katika kuajiri Watanzania kutoka pande mbili za Muungano, Kamati, inaendelea kushauri kuwa, Serikali izingatie misingi ya haki za kijinsi katika nafasi mbalimbali za ajira katika Taasisi za Muungano, kwa kuendelea kuhakikisha kwamba, kunakuwepo uwiano sawa wa Watanzania wanaume na wanaweke kutoka Zanzibar, wanaopata nafasi sawa za ajira katika taasisi hizo za Muungano.

ii) **Mheshimiwa Spika**, pamoja na Kamati kupongeza juhudi za Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) katika kushirikiana na Mamlaka husika za pande mbili za Muungano katika kutatua changamoto mbalimbali katika Sekta ya biashara baina ya pande mbili za Muungano, Kamati inaendelea

kushauri kwamba, Serikali ifanye jitihada za ziada katika kuhakikisha changamoto za kifedha na za kikodi zinazolalamikiwa na Wananchi wa pande zote mbili za Muungano, zinapatiwa ufumbuzi kwa wakati, hatua ambayo itachochea ukuaji wa Uchumi kwa Mwananchi mmoja mmoja na kwa manufaa ya Serikali zote mbili. Aidha, Serikali iendelee na juhudi hizo katika kubaini changamoto mpya zinazoweza kuibuka na kuzitatua kwa haraka.

iii) **Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa Serikali imepokea ushauri wa Kamati kuhusu uboreshaji wa magari na vitendea kazi vingine chini ya Ofisi hii, kwa kuanza kutenga vyedha kwa ajili ya manunuzi ya magari kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, Kamati inaishauri Serikali kuendelea na utekelezaji wa mpango wake wa kuongeza na kuboresha vitendea kazi chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais-Muungano kwa kutoa fedha hizo kwa wakati, kwa lengo kurahisisha utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi hiyo kwa wakati na kwa ufanisi zaidi.

## 6.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, napenda nikupongeze kwa umahiri wako katika kasi ya kuliendesha Bunge la Kumi na Mbili (12) katika kuishauri vema Serikali kwa manufaa ya Wananchi wa Tanzania, Aidha, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha Maoni ya Kamati kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kumpongeza Naibu Spika, Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, Mb, kwa weledi na umahiri wake katika kukusaidia kuongoza Bunge. Niipongeze pia Kamati yako ya Uongozi kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kukushauri na kukusaidia kuendesha shughuli za Bunge la Kumi na Mbili. Wote kwa pamoja tunawaomba afya na uzima katika kutekeleza majukumu mliyopewa.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kumpongeza na kumshukuru aliyekuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais, Mhe. Ummy Mwalimu, (Mb), kwa ushirikiano wake mzuri katika kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ikiwemo

uchambuzi wa Bajeti hii kwa ufanisi uliokusudiwa. Aidha, ni imani ya Kamati kuwa, Waziri wa Nchi aliyepo kwasasa, Mhe.Suleiman Jafo (Mb), pamoja na Watendaji Wakuu na Wataalam wote wa Ofisi ya Makamu wa Rais wataendelea kutoa ushirikiano wa kutosha katika kutekeleza ushauri wa Kamati na Bunge lako Tukufu kuhusu Ofisi ya Makamu wa Rais-Muungano.

**Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya pekee napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano na michango yao mizuri wakati wa kupitia na kuchambua Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano.

**NAOMBA MAJINA YAO KAMA YALIVYO KATIKA TAARIFA HII YAINGIE KATIKA TAARIFA RASMI YA BUNGE (HANSARD).**

1. Mhe. Najma Murtaza Giga, Mb. – **Makamu Mwenyekiti**
2. Mhe. Abdullah Ali Mwinyi, Mb. – Mjumbe
3. Mhe. Emmanuel Adamson Mwakasaka, Mb. – Mjumbe
4. Mhe. Wanu Hafidh Ameir, Mb.-Mjumbe
5. Mhe. Joseph Anania Tadayo, Mb.-Mjumbe
6. Mhe. Edward Olelekaita Kisau, Mb -Mjumbe
7. Mhe. Zainabu Athumani Katimba, Mb,-Mjumbe
8. Mhe. Ng’wasi Damas Kamani, Mb,-Mjumbe
9. Mhe. Lemburis Saputu Mollel Noah, Mb, -Mjumbe
10. Mhe. Asha Abdallah Juma, Mb, -Mjumbe
11. Mhe. Elibariki Immanuel Kingu, Mb, -Mjumbe
12. Mhe. Omar Ali Omar, Mb, -Mjumbe
13. Mhe. Suma Ikenda Fyandomo, Mb, -Mjumbe
14. Mhe. Suma Ikenda Fyandomo, Mb, -Mjumbe
15. Mhe. Joseph Kizito Mhagama, Mb, -Mjumbe
16. Mhe. Salum Mohammed Shaafi, Mb.-Mjumbe
17. Mhe. Ahmed Juma Ngwali Dedi, Mb,-Mjumbe
18. Mhe. Agnesta Lambert Kaiza, Mb,-Mjumbe
19. Mhe. Yahaya Omary Massare, Mb,-Mjumbe
20. Mhe. Jackline Ngonyani Msongozi, Mb, -Mjumbe
21. Mhe. Hussein Nassor Amar, Mb, -Mjumbe
22. Mhe. Khadija Shaaban Taya, Mb,-Mjumbe
23. Mhe.Agnes Elias Hokororo, Mb,-Mjumbe

**Mheshimiwa Spika**, mwisho kabisa lakini si kwa umuhimu napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, **Ndg. Stephen Kagaigai** kwa kuiwezesha Kamati kukamilisha kazi yake bila kukwama. Aidha, napenda kumshukuru Mkurugenzi wa Kamati za Bunge Ndg. Athuman Hussein, Wakurugenzi Wasaidizi Ndg. Gerald S. Magili na Ndg. Michael Chikokoto, Katibu wa Kamati hii, Ndg. Stanslaus Kagisa, na Msaidizi wa Kamati Ndg. Raheli Masima kwa kuihudumia vyema Kamati pamoja na kukamilisha taarifa hii kwa wakati. Napenda kuwashukuru Makatibu Muhtasi wa Idara ya Kamati za Bunge kwa kuchapa taarifa hii. Napenda pia kuwashukuru Watendaji wote wa Idara na Vitengo husika vya Ofisi ya Bunge, kwa kuhakikisha kwamba Taarifa hii inatoka kwa wakati na kwa ubora.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo naliomba Bunge lako Tukufu sasa lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais -Muungano, kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 kama yalivyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri hivi punde.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja hii.

Najma Murtaza Giga, (Mb).

**MAKAMU MWENYEKITI**

**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA**

27 Aprili, 2021

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mhagama kwa kupitia hotuba ya Kamati ya Katiba na Sheria vizuri sana. Sasa naomba nimwite Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira na yeye aweze kutupatia ushauri wake.

Baada ya Mwenyekiti huyu, basi Mheshimiwa Ahmed Abdulwakil atakuwa mchangiaji wa kwanza, Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud atafuatia. Pia mwasilishaji nakuomba

uende kwenye Maoni na Mapendekezo ya Kamati moja kwa moja. Karibu sana Mheshimiwa Shigongo.

**MHE. ERIC J. SHIGONGO – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, napokea maelekezo yako ya kwamba niende moja kwa moja kwenye Maoni na Uchambuzi wa Mpango. Najua nikienda moja kwa moja hapo Mungu hatafurahi kwa sababu nitakuwa sijamshukuru kwa kunipa nafasi ya kusimama hapa leo nikiwa naweka historia. Kwa hiyo, naomba tu unipe dakika moja au mbili niweze kutoa shukrani zangu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kusimama hapa leo, naomba nichukue nafasi hii kwanza kumshukuru Mungu wa Mbinguni ambaye kwa utaratibu wake huwainua watu kutoka kwenye mavumbi na kuwakalisha juu. Naomba nikushukuru sana wewe mwenyewe kwa uongozi wako mzuri kwa Bunge na nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Spika kwa uongozi mzuri kwa Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwako wewe naomba nizungumze machache kuhusiana na wewe na kwa sababu wiki moja iliyopita ulishangaa kwamba watu wa Kanda ya Ziwa nao wana bandari. Naomba nichukue nafasi hii kukupongeza wewe kwa namna ambavyo umewaletea heshima kabila ya Wagogo. Kwa sababu huko nyuma mimi nilikuwa najua kazi ya Wagogo ilikuwa ni moja tu, kukaa kando ya barabara na kuuza maji, lakini kwa sababu ya kazi uliyofanya imewainua sana Wagogo kama alivyofanya Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kuwainua Wakwere. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba pia niishukuru sana sana familia yangu, mke wangu na watoto kwa namna ambavyo wameniunga mkono mpaka kufika hapa siku ya leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nimpongeze sana Rais Samia Suluhu Hassan kwa namna alivyoanza kuihudumia nchi



yetu. Tumepata Rais mwanamke na naomba nichukue nafasi hii kuwahakikishia Watanzania wote ya kwamba nchi yetu ipo kwenye mikono salama kwa sababu ipo chini ya Mama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Biblia inasema wazi kabisa kwamba Adamu aliumbwa baada ya kuumbwa akalala usingizi na ubavu wake ukachuliwa akaumbwa mwanamkwe na mwanamke huyo akapuliziwa pumzi ya uhai kwa mara ya pili. Kwa hiyo hii ni ishara kwamba wanawake wanazo nguvu, wanao uwezo wa kuongoza na hawahitaji kutiliwa mashaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwanasayansi mwingine kule Marekani alifanya utafiti akagundua kwamba wanawake *wana-emotional intelligence* zaidi ya wanaume, kwa hiyo hii ni ishara ya kwamba wanawake wanaweza kuongoza na wanaume wote tuliopo hapa ndani naomba tuwaunge mkono wakina mama ili nchi yetu iweze kupata kusongambe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Buchosa, naomba niwashukuru sana kwa kunipa kura nyingi ambazo hatimaye zimenifikisha ndani ya Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo, sasa naomba nisome uchambuzi wa Mpango wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya mwaka wa fedha 2021/2022. Uchambuzi wa Malengo na Mpango; Kamati imepitia maelezo ya Waziri kuhusu kazi zilizopangwa kutekelezwa kwa mwaka wa fedha 2020/2021 kwa lengo la kujiridhisha na tija inayoweza kupatikana katika utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2021/2022. Malengo yaliyochambuliwa yanahusu utekelezaji wa shughuli za umma unaokasimiwa katika kifungu 5001. Aidha, Kamati ilitaka kujiridhisha kama malengo yote yalizingatia ipasavyo majukumu ya msingi ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Idara ya Mazingira.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya uchambuzi huo yanaonyesha kuwa malengo pamoja na vipaumbele

vilivyoanishwa kwa mwaka wa fedha 2021/2022 yanaendana na majukumu ya msingi ikiwemo kuzingatia Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, jukumu la kuimarisha usimamizi wa shughuli za uhifadhi wa mazingira katika ngazi ya Serikali za Mitaa linaendana na majukumu ya msingi ya Idara ya Mazingira. Aidha, jukumu hilo linaendana na Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa mwaka 2020 kama ilivyofanunuliwa katika aya 191 ukurasa wa 250 hadi 251 wa Ilani.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Makadirio na Mapato; katika mwaka wa fedha wa 2021/2022, hakuna mapato yanayotarajiwa kukusanya chini ya Fungu 31, Idara ya Mazingira, lakini Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira (NEMC) ambao lipo chini ya Ofisi hii linalenga kukusanya jumla ya shilingi bilioni ishirini na tano, na milioni thelathini na nane (25,038,000,000) katika vyanzo mbalimbali vya ndani vya baraza.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi unaonyesha kuwa, kiasi kinacholengwa kukusanya kimeongeza kwa asilimia 17.73 ikilinganishwa na malengo ya makusanyo ya baraza ya mwaka wa fedha 2020/2021. Kuongezeka kwa lengo la makusanyo hakuazingatia mwenendo hafifu wa makusanyo ya mapato ya mwaka wa fedha 2020/2021 linalokamilika kwa asilimia 53.86 hadi kufikia robo ya tatu ya mwaka wa fedha. Kwa hali hiyo lengo hili linaweza lisiwe na uhalisia

Mheshimiwa Spika, kutokana na uchambuzi huo ni maoni ya Kamati kuwa ipo haja ya Baraza kuongeza wigo wa ukusanyaji wa ada na tozo za mazingira. Jambo hili linawezekana kwa kuongeza ufuatiliaji katika ulipaji tozo pamoja na kudhibiti mianya ya uvujaji wa mapato hayo.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Bajeti ya Matumizi; Kamati ilijulishwa kuwa katika mwaka wa fedha wa 2021/2022, jumla ya Shilingi bilioni nane, milioni mia tisa na sitini na

sita, laki tisa na thelathini na tisa, mia nne arobaini bila senti (8,966,936,440.00) zinaombwa chini ya Fungu 31 - Idara ya Mazingira kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya uhifadhi na usimamizi wa mazingira. Mchanguo wa fedha hizo unaonekana katika jedwali namba 4.1 kwenye taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi ulibainisha yafuatayo:-

(i) Kiasi cha makadirio ya matumizi ya mwaka wa fedha 2021/2022 ni pungufu kwa asilimia 27.28 ikilinganishwa na bajeti ya mwaka 2020/2021. Tafsiri ya upungufu huo ni nini? Ni kuwa utekelezaji wa majukumu ya Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira utaathirika kwa kiwango cha karibu asilimia 27 ikilinganishwa na mpango wa mwaka unaoisha.

(ii) Upungufu...

**SPIKA:** Sasa nenda kwenye ushauri wa Kamati moja kwa moja.

**MHE. ERIC J. SHIGONGO – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, Ushauri wa Kamati; baada ya kupokea Taarifa Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo na Kuchambua Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais – Idara ya Mazingira kwa mwaka 2020/2021, pamoja na mapendekezo ya Mapato na Matumizi ya fedha kwa mwaka 2021/2022, Kamati ina maoni na ushauri ufuatao kwa Serikali:-

(i) Mfumo wa Kitaasisi wa Usimamizi wa Mazingira; Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004 imeweka mfumo wa kitaasisi katika ngazi ya Sekta na Serikali za Mitaa. Sheria hiyo inataka kila Sekta ikiwemo Ofisi ya Rais, TAMISEMI kuwa na kitengo cha Usimamizi wa Shughuli za Uhifadhi Mazingira. Kamati inasisitiza kuwa sekta zote zizingatie Sheria ya Usimamizi wa Mazingira kwa kuanzisha kitengo maalum kwa ajili ya kuratibu na kusimamia masuala ya mazingira.

(ii) Mfuko wa Taifa wa Dhamana ya Uhifadhi wa Mazingira; kwa kuwa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004 imetaka uanzishwe Mfuko wa Taifa wa Dhamana ya Uhifadhi wa Mazingira na kwa sababu vyanzo vya mapato vya Mfuko huo vilikwishaa inishwa na kuwasilishwa Serikalini, wakati sasa umefika kwa Serikali kuuwezesha Mfuko huu kuanza kufanya kazi.

(iii) Elimu ya Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira; pamoja na juhudi mbalimbali zinazofanywa za kujenga uelewa wa jamii kuhusu umuhimu wa mazingira ya kijamii bado uelewa ni mdogo na hivyo kamati inaendelea kuisisitiza kuwa Serikali iwezeshe Ofisi ya Makamu wa Rais – Idara ya Mazingira kirasilimali fedha na watu ili wawafikie wananchi wengi na kuwapa elimu ya mazingira.

(iv) Mapitio ya Sera ya Taifa ya Mazingira; Sera ya Taifa ya Mazingira iliyopo sasa ni ya zamani, jambo ambalo linakwamisha masuala mengi ya utekelezaji wa shughuli za mazingira, kulingana na hali halisi ya sasa, ikiwemo uendeshaji wa Mfuko wa Mazingira. Kamati inaendelea kuisisitiza kuwa Serikali kukamilisha mchakato wa mapitio na maboresho ya Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 1997 ili kuwezesha Ofisi hii kufanya mabadiliko mbalimbali, yakiwemo mabadiliko ya Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004, hivyo kurahisisha utekelezaji wa masuala mbalimbali yaliyokwama ikiwemo Mfuko wa Taifa wa Mazingira.

(v) Upatikanaji na Utumiaji wa Nishati Mbadala; Uharibifu wa Mazingira unatokana na ukataji wa miti kwa ajili ya kuni na mkaa unaendelea kwa kasi nchini mwetu. Hivyo, Kamati inashauri kuwa Serikali iwahamasishe wananchi kuendelea kupanda miti kwa muda mrefu na ile ya muda na pia Serikali ihimize uwekezaji katika kuzalisha mkaa unaotokana na takataka.

(vi) Matumizi ya Kemikali hatarishi aina ya Zebaki; uingizaji holela wa utumiaji wa kemikali ya zebaki nchini kutokana na kuwepo kwa wachimbaji wadogo wa dhahabu wanaotumia kemikali hiyo unaathiri kwa kiasi kikubwa afya

na ustawi wa wachimbaji hao. Madhara ya matumizi ya kemikali hiyo yanatokana na wachimbaji wengi kuitumia bila kuwa na nyenzo za kujikinga kutoka na zebaki. Vile vile maji yanayotumika kusafisha dhahabu yakiwa yamechanganyika na zebaki yanatiririka kwenye vyanzo vya maji kama vile mito na kuingia katika maziwa. Watu wanapotumia maji hayo hujikuta afya zao zinaathirika. Hivyo, kutokana na hali hiyo Kamati inashauri kuwa Ofisi ya Makamu wa Makamu Rais – Mazingira ishirikiane na:-

(a) Ofisi ya Mkemia Mkuu kudhibiti uingizwaji wa zebaki nchini.

(b) Usimamizi wa matumizi ya zebaki kwa wachimbaji wadogo wa dhahabu nchini uendelezwe.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali itafute teknolojia mbadala ambayo wachimbaji hao wataitumia ili kuachana na matumizi ya Zebaki.

(vii) Taarifa ya hali ya Mazingira nchini; kifungu 175(1) cha Sheria ya Mazingira 2004 kinamtaka Mkurugenzi wa Mazingira kuandaa na kutoa taarifa juu ya hali ya mazingira nchini kila baada ya miaka miwili na kuiwasilisha Bungeni. Hata hivyo, uzoefu unaonyesha kuwa upo ugumu wa kutekeleza masharti hayo, jambo linalosababisha kuwasilishwa kwa taarifa hiyo kwa mwaka 2008, 2014 na 2019. Kwa sababu hiyo, taarifa ya kwanza na pia ya tatu hazikuweza kuzingatia masharti ya kuwasilishwa baada ya miaka miwili. Kwa msingi huo basi, Kamati inashauri kuwa Serikali iandae mapendekezo ya marekebisho ya kifungu hicho kwa kuongeza muda wa kutoa ripoti kufikia miaka mitano.

(viii) Tathmini ya Athari za Mazingira (*Environmental Impact Assessment*); Sheria ya Mazingira inaelekeza kabla ya kuanza kutekeleza mradi eneo lolote lile lazima ifanyike tathmini ya athari za mazingira zinazoweza kujitokeza baada ya mradi kuanzishwa. Kazi hii inafanywa na Washauri Waelekezi. Kamati inashauri kuwa NEMC iwasimamie

Washauri Elekezi sambamba na kutoa mwongozo kuhusu gharama za kufanya tathimini hiyo. Kufanya hivyo kutawezesha gharama zinazotozwa kuwa halisi na zinazolingana na miradi uliopo badala kuwa kubwa ilivyo sasa na kukwamisha kuanzishwa kwa miradi.

Mheshimiwa Spika, hitimisho; naomba kuchukua fursa hii kukushukuru na kukupongeza sana kwa kuendelea kuliongoza Bunge letu kwa weledi mkubwa. Vilevile naomba kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Naibu Spika kwa weledi na umahiri wake katika kukusaidia kuongoza vikao vya Bunge hili la Kumi na Mbili.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira ambao wameweza kutoa maoni, michango na mawazo yao mbalimbali, wakati wa kupitisha na kuchambua bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais – Mazingira na hatimaye kuandaa na kukamilisha taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Umy Mwalimu, aliyekuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mazingira na Naibu wake Mheshimiwa Mwita Waitara kwa ushirikiano walioupatia Kamati. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Selemani Jafo na Naibu Waziri wake Mheshimiwa Hamad Hassan Chande aliyekuwa Mjumbe wa Kamati hii kabla ya kuteuliwa kwa namna wanavyofanya kazi zao.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndugu Stephen Kagaigai, Mkurugenzi wa Idara ya Kamati Bwana Athuman Hussein, Mkurugenzi Msaidizi Bwana Michael Chikokoto, Makatibu wa Kamati: Zainabu Mkamba, Bi Mwajuma Ramadhani pamoja na Msaidizi wa Kamati Bi. Grace Mwenye kwa kuratibu shughuli za Kamati.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo sasa naomba kulishauri Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Fungu 31 - Idara ya Mazingira kwa mwaka wa fedha

2021/2022 ambayo ni kiasi cha shilingi bilioni nane, milioni mia tisa sitini na nne, laki tisa thelathini na tisa, bila senti (shilingi 8,964,939,440.00) kama alivyofafanua mtoa hoja pamoja na maoni ya Kamati hii.

Mheshimiwa Spika, naomba ripoti yote hii iingie katika *Hansard* za Bunge.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIAHARA NA MAZINGIRA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA UHIFADHI NA USIMAMIZI WA MAZINGIRA CHINI YA OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA) FUNGU 31 – IDARA YA MAZINGIRA KWA MWAKA 2020/2021 PAMOJA NA MAONI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA MWAKA 2021/2022 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

---

## 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika**, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetupa afya, uzima na nafasi nyingine ya kukutana hapa Dodoma katika Mkutano huu wa Tatu wa Bunge la Kumi na Mbili.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu wa Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, sasa naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) **Fungu 31 – Idara ya Mazingira** kwa Mwaka **2020/2021** pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fungu hili kwa ajili ya Uhifadhi na Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira kwa Mwaka Fedha **2021/2022**.

**Mheshimiwa Spika**, nilikumbushe Bunge lako tukufu kuwa msingi wa Taarifa hii ni majukumu ya Kamati kwa mujibu wa

Kifungu cha 7(a) cha Nyogeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, pamoja na masharti ya Kanuni ya 118 (4) ya Kanuni za Bunge. Kanuni hizo kwa pamoja zimeweka masharti kuwa kabla ya taarifa ya utekelezaji na Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, hususan Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira kujadailiwa Bungeni, ilipaswa kuchambuliwe na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira. Nililijulishe Bunge lako tukufu kuwa Uchambuzi huo ulifanyika baada ya ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa katika uhifadhi na usimamizi wa Mazingira.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kusimama hapa, naomba nitoe pole kwa watanzania wote kwa kuondokewa na aliekuwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Hayati John Pombe Joseph Magufuli. Ambaye amemaliza safari yake kwa uongozi uliotukuka.

**Mheshimiwa Spika**, vilevile naomba nimpongeze mama yetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuwa Rais wa sita wa nchi yetu, tunaimani nae na tuna uhakika atatuongoza vyema na kuzidi kupata maendeleo kama nchi.

**Mheshimiwa Spika**, Maudhui ya Taarifa hii yanagawanyika katika maeneo makuu manne yafuatayo:-

- i) Matokeo ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo
- ii) Uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa ya Idara ya Mazingira kwa mwaka wa fedha 2020/2021;
- iii) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya kwa ajili ya Usimamizi na uhifadhi wa Mazingira kwa mwaka wa fedha 2021/2022; na
- iv) Maoni na ushauri wa Kamati unaotokana na uchambuzi na ufuatiliaji wa majukumu ya usimamizi na uhifadhi wa mazingira.



## **2.0 MATOKEO YA UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021**

**Mheshimiwa Spika**, ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ulitokana na masharti ya Kanuni ya 117(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge iliyotaka siku zisizozidi saba zitumike kwa ukaguzi wa miradi ya maendeleo. Kamati ilizingatia masharti hayo na kupanga kutembelea miradi miwili ya usimamizi wa mazingira. Hata hivyo, ratiba ya kutembelea miradi hiyo haikukamilika kutokana na msiba mkubwa uliolipata taifa letu. Pamoja na ratiba ya ziara kutokamilika, awali Kamati ilikwishapokea taarifa ya utekelezaji wa miradi hiyo. Kwa msingi huo, naomba kulijulisha Bunge kuhusu yaliyobainika katika uchambuzi pamoja na maoni ya jumla kuhusu utekelezaji wa miradi ya maendeleo inayohusu usimamizi na uhibiti wa Mazingira.

### **2.1 Yaliyobainika katika Uchambuzi**

**Mheshimiwa Spika**, nilikumbushe Bunge lako tukufu kuwa katika mwaka wa fedha 2020/2021 Ofisi ya Makamu wa Raisi - Mazingira Fungu **31**, ilidhinishiwa shilingi **7,049,430,000.00** kwa ajili ya kutekeleza Miradi mbalimbali ya Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira Ofisi ya Makamu wa Rais – Idara ya Mazingira chini ya Baraza la taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira (*NEMC*). Maeneo mawili ambayo Kamati ilipatafursa ya kupokea taarifa ya utekelezaji wake ni pamoja na:-

i) Mradi wa kuhimili mabadiliko ya Tabianchi kwa kutumia mifumo Ikolojia vijijini (Ecosystem – Based Adaptation for Rural Resilience in Tanzania - *EBARR*) – Zanzibar Kaskazini 'A' ambao utekelezaji wake ulianza mwaka 2018 na unatarajiwa kuisha 2022. Hadi Februari, 2021, mradi ulikuwa umepokea Shilingi **402,798,103.00** ambayo ni sawa na asilimia **36** ya fedha iliyodhinishwa na Bunge. Kiwango hicho cha upatikanaji wa fedha kinaonesha utekelezaji hafifu wa mradi huu, tofauti na ilivyotarajiwa na Bunge wakati wa kupitisha bajeti kwa mwaka wa fedha 2020/2021; na kuashiria kutokamilika kwa mradi kama ilivyotarajiwa;

**Mheshimiwa Spika**, changamoto zinazoambatana na utekelezaji wa mradi huu na kupelekea kuchukua muda mrefu ni kupatikana mshauri elekezi (Local NGO) mwenye sifa na uzoefu katika maeneo ya mradi, ukosefu wa maji ya bomba katika maeneo yaliyopendekezwa kwa ajili ya uanzishaji wa vitalu na kutosajiliwa kwa vikundi vilivyoainishwa. Kamati inasisitiza Serikali kushughulikia changamoto zilizopo ili mradi uendelee, kwani muda uliobaki wa kutekeleza mradi ni mfupi na sehemu kubwa ya mradi bado haijatekelezwa.

ii) Shughuli za Usimamizi wa Mazingira katika Mto Nyakasangwa na Mito mingine – Dar es Salaam, Changamoto za kimazingira zilizojitokeza katika mto Nyakasangwa na baadhi ya mito mingine jijini Dar es Salaam ni uchimbaji holela wa mchanga na utupaji wa taka ngumu ndani na pembezoni mwa mto. Kutokana na changamoto hizo inapelekea mito kupoteza kina chake cha asili na kuongezeka kwa upana wa mito hivyo kuleta athari kwenye makazi ya watu kama vile mafuriko.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Serikali kuongeza kasi katika kuandaa muongozo ambao utatoa maelezo ya jinsi gani shughuli hii itafanyika bila ya kuharibu mazingira na zitakuwa endelevu. Jambo hili liende sambamba na kufanya vipimo vya kingo za mito, kuweka mipaka ya kudumu na kuainisha maeneo sahihi ya upatikanaji wa mchanga ambayo yatatumiwa na wananchi na matumizi ya miradi ya kimkakati.

## ***2.2 Maoni ya Jumla kutokana na uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo***

**Mheshimiwa Spika**, matokeo ya uchambuzi wa taarifa hiyo yamebainisha mambo yafuatayo:-

i) Hadi kufikia mwezi Februari ambapo ni asilimia 66.7 ya kipindi cha utekelezaji, kiasi cha pesa zilizopokewa kwa ajili ya kugharamia mradi kuhimili mabadiliko ya Tabianchi kwa kutumia mifumo lkolojia vijijini ni asilimia 36.6 tu kiasi cha fedha kilichoidhinishwa na Bunge lako tukufu. Hali hii ni ishara mbaya kwa utekelezaji wa bajeti kwa ajili ya miradi

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na matokeo hayo Kamati ina maoni ya jumla kuhusu utekelezaji wa miradi ya maendeleo inayohusu usimamizi na uhifadhi wa mazingira kama ifuatavyo:-

i) Ufanisi na tija ya NEMC, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara ya Nishati na Mamlaka za Bonde kwenye kusimamia mazingira katika kudhibiti uchimbaji wa mchanga kwenye mito yote nchini unahitajika ili kuepusha kutanuka na kupungua kwa kina cha mito hiyo.

ii) Utaratibu wa utoaji wa vibali vya uchimbaji wa mchanga katika maeneo ya mito unahitaji kuboreshwa kwa njia ya ushirikiano baina ya NEMC, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara ya Nishari na Mamlaka za Bonde; na

iii) Mafanikio katika utekelezaji wa mradi ya mazingira yanategemea kwa kiasi kikubwa uelewa wa wananchi ambao watapaswa kutoa ushirikiano kutokana na kuwa wanufanika wakuu.

### **3.0 UTEKELEZAJI WA MPANGO WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021**

**Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza masharti ya Kanuni ya 117(2) ya Kanuni za Bunge, Toleo la Juni, 2020, Kamati ilichambua Taarifa ya utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais – Idara ya Mazingira kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021. Uchambuzi huo uligusa mambo yafuatayo:-

i) utekelezaji wa mpango wa makusanyo ya mapato;

ii) upatikanaji wa fedha kwa kuoanisha na bajeti iliyoidhinishwa na Bunge;

iii) Utekelezaji wa majukumu yaliyopangwa; na

iv) Uzingatiaji wa ushauri wa Kamati uliotolewa Bungeni

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifanya uchambuzi kwa kutumia taarifa zilizowahi kuwasilishwa kwenye Kamati ikiwemo taarifa ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo pamoja na mahojiano wakati wa vikao. Matokeo ya Uchambuzi huo ni kama ifuatavyo:-

### **3.1 Uchambuzi wa Taarifa kuhusu Ukusanyaji wa Mapato ya serikali**

**Mheshimiwa Spika**, Baraza la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira – NEMC kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 lilipanga na kuridhiwa na Bunge likusanye kiasi cha Shilingi **20,600,000,000.00**. Uchambuzi unaonesha kuwa hadi kufikia Machi, 2021, Baraza lilikuwa limekusanya Shilingi **11,094,417,333.18**, kiasi hicho ni sawa na asilimia **53. 86** ya lengo la makusanyo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipata mashaka kuhusu uwezekano wa Baraza kufikia lengo ifikapo tarehe 30 Juni, 2021. Hata hivyo, maelezo ya serikali yalionesha kuwa lengo la makusanyo linaweza kufikiwa kutokana na kuongezeka kwa wateja. Pamoja na maelezo hayo, ni maoni ya Kamati kuwa upungufu wa rasilimali watu unaoikabili NEMC unaweza kuwa umechangia pamoja na mambo mengine, ukusanyaji hafifu wa mapato ya serikali.

### **3.2 Upatikanaji wa fedha kutoka Hazina**

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 Bunge liliidhinisha Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais – Idara ya Mazingira, Fungu 31 kiasi cha fedha kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 01.

**Jedwali Na. 3:1 Muhtasari wa Mchanganuo wa Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya kuhifadhi na Kusimamia Mazingira**

UFAFANUZI	KIASI CHA FEDHA	% YA BAJETI
Jumla	12,327,852,440.00	100
Matumizi kawaida ya	5,278,422,440.00	43
Matumizi Maendeleo ya	7,049,430,000.00	57

**Chanzo:** Randama ya Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilifanya ulinganisho wa kiasi cha fedha zilizopokewa na Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge. Muhtasari wa matokeo ya Uchambuzi huo unaonekana katika Jedwali Na. 3:2

**Jedwali Na. 3:2 Ulinganisho wa Bajeti iliyoidhinishwa na Kiasi cha fedha iliyopokewa**

Mchanganuo	Bajeti iliyoidhinishwa	Kiasi kilichopokewa	% ya Bajeti
Jumla	12,327,852,440.00	5,410,228,413.54	44
Matumizi kawaida ya	5,278,422,440.00	2,899,855,971.54	55
Matumizi Maendeleo ya	7,049,430,000.00	2,510,372,442.00	36

**Chanzo:** *Randama ya Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira*

**Mheshimiwa Spika,** Matokeo ya Uchambuzi yanaonesha kuwa -

i) Pesa iliyoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya shughuli za kusimamia na kudhibiti mazingira kwa ujumla ilipatikana kwa mtiririko usioridhisha. Hadi kufikia mwezi Februari, 2021 pesa iliyopatikana ilikuwa ni asilimia **44** ya bajeti. Upatikanaji huo wa fedha katika kipindi ambacho ni asilimia **66.7** ya muda wa utekelezaji, unaonesha kuwa utekelezaji wa Bajeti hauendani na matarajio ya Bunge kuhusu matumizi kwa ajili ya udhibiti, uhifadhi na usimamizi wa mazingira.

ii) Fedha zilizopatikana kwa ajili matumizi ya kawaida ambazo zinakusudiwa kutumika katika uendeshaji wa shughuli za udhibiti, uhifadhi na usimamizi wa mazingira hadi kufikia mwezi Februari 2021, ni asilimia **55** tu ya bajeti iliyoidhinishwa. Kwa kuwa kipindi hicho ni zaidi ya nusu ya kipindi cha utekelezaji, upatikanaji huo wa fedha unatoa tafsiri kwamba, uendeshaji wa shughuli za usimamizi, udhibiti na uhifadhi wa mazingira haukuendana na matarajio ya Bunge.

iii) Upatikanaji wa fedha kwa ajili kugharamia miradi ya maendeleo inayolenga kuimarisha udhibiti, uhifadhi na usimamizi wa mazingira ulifikia asilimia **36** ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa ajili hiyo. Kiwango hicho, ni fedha za nje bila kujumuisha fedha za ndani ambazo hazikupatikana hata kidogo. Hali hii inatoa picha kuwa kuendelea kudhibiti na kusimamia mazingira ni jambo lenye utegemezi mkubwa wa fedha za nje. Utegemezi kwa kiwango hicho, unaweza kutafsiriwa kuwa hakuna juhudi za kutosha kumudu mipango ya kusimamia na kudhibiti mazingira kwa maendeleo endelevu.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa mwenendo huo wa upatikanaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mpango na bajeti kwa ajili ya kudhibiti, kuhifadhi na kusimamia mazingira, Kamati inasisitiza kuwa, bado kuna umuhimu wa kutoa uzito unaostahili katika kugharimia shughuli za udhibiti, uhifadhi na usimamizi wa mazingira. Kinyume cha kufanya hivyo, ni hatari katika kuliwezesha taifa kupata na kudumu na maendeleo endelevu.

### ***3.3 Utekelezaji wa kazi zilizopangwa kwa mwaka 2020/2021***

**Mheshimiwa Spika**, Kwa kuzingatia majukumu ya Kamati hii, uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa kazi za Usimamizi na Uhifadhi wa Mazingira zilizopangwa kutekelezwa kwa mwaka wa fedha **2020/2021** ulifanyika. Jumla ya kazi Ishirini na sita (26) zilipangwa kutekelezwa na idara ya Mazingira na Baraza (NEMC). Napenda kuliarifu Bunge hili kuwa kazi zote zilizopangwa zimeripotwa kutekelezwa. Hata hivyo, uchambuzi umeonesha yafuatayo:-

i) Mchakato wa mapitio ya mwongozo wa Taifa wa matumizi endelevu ya ardhi eneo la Hifadhi ya Mita 60 kutoka kwenye fukwe za Bahari na Maziwa, kingo za mito na mabwawa unakwenda kwa kasi ndogo kuliko inavyopaswa;

ii) Kazi ya kutoa elimu kwa Umma kuhusu umuhimu wa kuhifadhi na kutunza Mazingira haifanyiki kwa kiasi cha kuwezesha tija kwa wakati. Kwa mfano, bado wananchi wengi hawajaelimishwa kwa kiwango cha kutosha kuzingatia *Sheria ya Mazingira* ya Mwaka 2004; na

iii) Utekelezaji wa kampeni za Upandaji na utunzaji wa miti, hususani katika maeneo ambayo yameathirika sana na ukame, hauzingatii umuhimu wa ufuataliaji. Jambo hili, linasababisha matokeo ya kampeni kutokuwa na tija inavyostahili.

### ***3.4 Uzingatiaji wa Ushauri wa Kamati kuhusu Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira Mwaka wa Fedha 2020/2021.***

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa kupitia na kuchambua taarifa ya utekelezaji wa Ofisi ya Makamu wa Rais – Mazingira kwa mwaka wa fedha **2020/2021**, Kamati ilitoa ushauri kwenye maeneo tisa (9). Naomba kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa Serikali imejitahidi kuzingatia ushauri wa Kamati na kutekeleza maagizo hayo, uchambuzi unaonesha kuwa:-

i) Uzingatiaji wa Ushauri kuhusu usimamizi na Udhibiti wa Taka ngumu, utiririshaji wa maji taka toka viwandani na Taka hatarishi haufanyiki kwa kasi inayotakiwa. Kwa mfano, upatikanaji wa vibali vya usafirishaji wa taka hatarishi bado unakabiliwa na changamoto jambo linalosababisha taka hizo kuendelea kuwepo kwenye mazingira;

ii) Uratibu katika kuzisukuma Wizara, Taasisi, Mikoa pamoja na Halmashauri zote nchini kuwa na kitengo na kukiwezesha kifedha kutekeleza shughuli za uhifadhi wa mazingira kwa mujibu wa *Sheria ya Mazingira* ya mwaka 2004, haujafanikisha utekelezaji wa Sheria hii. Tafsiri ya hali hiyo ni kuwa mamlaka zilizotajwa hazijazingatia ipasavyo, Sheria iliyotungwa na Bunge.

iii) Mfuko wa Taifa wenye dhamana ya usimamizi wa Mazingira ulioanzishwa tangu mwaka 2007 haujaanza kufanya kazi ilivyotarajiwa. Mfuko huu umetimiza umri wa miaka kumi na nne unaotosha mototo kuzaliwa na kufika kidato cha pili, lakini bado haujaanza kufanya kazi;

#### **4.0 UCHAMBUZI WA MPANGO WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022**

##### ***4.1 Uchambuzi wa malengo/mpango***

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imepitia maelezo ya Waziri kuhusu kazi zilizopangwa kutekelezwa kwa mwaka wa fedha **2020/2021** kwa lengo la kujiridhisha na tija inayoweza kupatikana katika utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2021/2022. Malengo yaliyochambuliwa yanahusu utekelezaji wa shughuli za umma unaokasimiwa katika kifungu **5001**. Aidha, Kamati ilitaka kujiridhisha kama Malengo yote yalizingatia ipasavyo, majukumu ya msingi ya Ofisi ya Makamu wa Rais – Idara ya Mazingira.

**Mheshimiwa Spika**, matokeo ya uchambuzi huo yanaonesha kuwa malengo pamoja na vipaumbele vilivyoainishwa kwa Mwaka wa fedha **2021/2022**, vinaendana na majukumu ya msingi, ikiwemo kuzingatia Mpango wa tatu wa Maendeleo wa taifa na ilani ya uchaguzi. Kwa mfano, jukumu la kuimarisha usimamizi wa shughuli za uhifadhi na usimamizi wa mazingira katika ngazi ya serikali za mitaa, linaendana na majukumu ya msingi ya idara ya mazingira. Aidha, jukumu hilo linaendana na ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa ya mwaka 2020 kama ilivyofafanuliwa katika aya ya 191, ukurasa wa 250 hadi 251 wa Ilani.

##### ***4.2 Uchambuzi wa Makadirio ya mapato***

**Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka wa fedha 2021/2022, hakuna mapato yanayotarajiwa kukusanywa Chini ya **Fungu 31 – Idara ya Mazingira**, lakini Baraza la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira – *NEMC* ambalo lipo chini ya Ofisi hii, linalenga kukusanya jumla ya Shilingi **25,038,000,000.00** kutoka



katika vyanzo vya ndani vya Baraza. Uchambuzi unaoesha kuwa:

i) Kiasi kinacholengwa kukusanywa kimeongozeka kwa asilimia **17.73** ikilinganishwa na malengo ya makusanyo ya Baraza ya Mwaka wa Fedha 2020/2021; na

ii) Kuongezeka kwa lengo la makusanyo hakujazingatia mwenendo hafifu wa makusanyo ya mapato kwa mwaka wa fedha 2020/2021 lilokamilika kwa asilimia **53.86** hadi kufikia robo ya tatu ya Mwaka wa Fedha. Kwa hali hiyo lengo hili linaweza lisiwe na uhalisia.

**Mheshimiwa Spika**, Kutokana na uchambuzi huo, ni maoni ya Kamati kuwa ipo haja ya Baraza kuongeza wingo wa ukusanyaji wa ada na tozo za mazingira. Jambo hilo linawezekana kwa kuongeza ufuatiliaji katika ulipaji wa tozo pamoja na kudhibiti mianya ya uvujaji wa mapato hayo.

#### **4.3 Uchambuzi wa Bajeti ya Matumizi**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilijulishwa kuwa katika mwaka wa fedha 2021/2022, jumla ya shilingi **8,964,939,440.00** zinaombwa chini ya **Fungu 31 – Idara ya Mazingira**, kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira. Mchanganuo wa fedha hizo unaonekana katika jedwali Na. 4:1.

**Jedwali Na. 4:1 Mchanganuo wa Makadirio ya Matumizi kwa mwamaka wa fedha 2021/2022**

Ufafanuzi	Makadirio 2021/22	% ya bajeti	Bajeti 2020/21	% ongezeko au upungufu
Jumla	8,964,939,440.00	100%	12,327,852,440.00	-27%
Kawaida	5,994,151,440.00	67%	5,278,422,440.00	14%
a) Mishahara	4,550,242,000.00	51%	4,369,742,000.00	4%
b)M/Mengineyo	1,443,909,440.00	16%	908,680,440.00	59%
Maendeleo	2,970,788,000.00	33%	7,049,430,000.00	-58%

**Chanzo:** Randama ya Fungu 31- Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi ulibainisha yafuatayo: -

i) Kiasi cha makadiro ya matumizi kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ni pungufu kwa asilimia **27.28** ikilinganishwa na Bajeti ya mwaka wa fedha 2020/2021. Tafsiri ya upungufu huo, ni kuwa utekelezaji wa majukumu ya Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira utaathirika kwa kiwango karibu sawa na asilimia 27 ikilinganishwa na mpango wa mwaka unaoisha.

ii) Upungufu wa Bajeti hii kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 unaathari zaidi fedha kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ambayo imepungua kwa asilimia **58** ikilinganisha na Bajeti ya Miradi ya Maendeleo ya Mwaka wa Fedha 2020/2021.

iii) Fedha za ndani zinazoombwa kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo ni kidogo ukilinganishwa na uhalisia wa hali ya mazingira nchini.

**Mheshimiwa Spika**, Ni maoni ya Kamati kuwa, fedha zinazotengwa kwa ajili ya shughuli za Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira bado hazitoshelezi kukabiliana na changamoto pamoja na uharibifu unaoendelea kujitokeza katika mazingira Nchi. Upo umuhimu wa Serikali kuongeza bajeti ya uhifadhi na usimamizi wa Mazingira hususani upande wa kutekeleza miradi ya maendeleo.

## **5.0 HALI YA MAZINGIRA**

**Mheshimiwa Spika**, hali ya Mazingira nchini iliyoripotiwa ndani ya taarifa ya Tatu ya Hali ya Mazingira ya Mwaka 2019 inatia wasiwasi, imeripotiwa kuwa Tanzania bara inakisiwa kuwa na jumla ya 48.1 milioni hekari za misitu ambayo ni asilimia 51 ya eneo lote. Kuna ukataji holela wa miti unaokadiriwa kuwa takribani hekta 469,420 kwa mwaka, na tatizo hili linaendelea kukua kwa kasi mwaka hadi mwaka nchi nzima. Moja ya sababu inayopelekea kuwa na ukataji mkubwa wa miti nchini ni umasikini kwani asilimia kubwa ya wataanzania wanategemea mazao ya misitu katika kutimiza mahitaji yao (livelihood). Shughuli za kila siku wanazozifanya ni kama vile kilimo, ufugaji, uokotaji wa kuni na utengenezaji wa mkaa na shughuli hizo zinaenda moja kwa moja na ukataji wa miti na uharibifu wa misitu.

**Mheshimiwa Spika**, mambo mengine yaliyoripotiwa kwenye taarifa hiyo ni kuongezeka kwa tishio la kupotea kwa aina mbalimbali ya viumbe hai (bioanuwai) na kuongezeka kwa viumbe vamizi. Taarifa za hivi karibuni zinakadiria kuwa zaidi ya viumbe vamizi 198 vinapatikana nchini ambapo inapelekea Tanzania kuwa ni nchi iliyoathirika zaidi Africa Mashariki na Kati. Viumbe Vamizi ni sababu ya pili inayopelekea kupotea kwa bioanuwai ukiacha kupotea kwa maeneo ya asili ya viumbe hai (habitat loss), mabadiliko ya tabia nchi (Climate change) na nyenginezo.

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na kuongezekana kwa uharibifu wa mazingira nchini, Kamati imebaini kuwa upo umuhimu wa Serikali kuongeza kasi na ufanisi katika Usimamizi na Uhifadhi wa Mazingira nchini, kutoa elimu kwa jamii itakayosaidia kupunguza matumizi yasiyo endelevu ya maliasili zetu na kuongeza uhamasishaji wa utumiaji wa teknolojia za kisasa zinazopunguza matumizi mabaya ya maliasili zetu.

## 6.0 USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika**, Baada ya kupokea taarifa ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo na kuchambua utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais – Idara ya Mazingira kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021, pamoja na mapendekezo ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, Kamati ina Maoni na Ushauri ufuatao kwa Serikali:-

### *6.1 Mfumo wa Kitaasisi wa Usimamizi wa mazingira*

**Mheshimiwa Spika**, Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004 imeweka mfumo wa kitaasisi katika ngazi ya sekta na Serikali za Mitaa. Sheria hiyo, inataka kila sekta ikiwemo Ofisi ya Rasi TAMISEMI kuwa na kitengo cha usimamizi wa shughuli za uhifadhi wa Mazingira. **Kamati inasisitiza kuwa sekta zote zizingatie Sheria ya Usimamizi wa Mazingira kwa kuanzisha kitengo maalumu kwa ajili ya kuratibu na kusimamia masuala ya mazingira.**

### ***6.2 Mfuko wa Taifa wa Dhamana ya Hifadhi ya Mazingira***

**Mheshimiwa Spika**, Kwa kuwa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004, imetaka uanzishwe mfuko wa Taifa wa Dhamana ya Hifadhi ya Mazingira na kwa sababu vyanzo vya mapato vya mfuko huo vilikwisha ainishwa na kuwasilishwa serikali, **wakati umefika sasa kwa serikali kuuwezesha Mfuko huu kuanza kufanya kazi yake kwa mujibu wa sheria.**

### ***6.3 Elimu ya Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira***

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na juhudi mbalimbali zinazofanywa za kujenga uelewa kwa jamii kuhusu umuhimu wa mazingira kijamii na kiuchumi, bado uelewa umekuwa mdogo na utunzaji wa mazingira bado hauridhishi katika jamii. **Kamati inaendelea kuisisitiza kuwa Serikali iwezesha Ofisi ya Makamu wa Rais – Idara ya Mazingira kirasilimali fedha na watu ili wawafikie wananchi wengi zaidi na waweze kuweka mpango mkakati ambao ni endelevu katika kuelelewa wananchi juu ya umuhimu wa uhifadhi wa mazingira.**

### ***6.4 Mapitio ya Sera ya Taifa ya Mazingira 1997***

**Mheshimiwa Spika**, Sera ya Taifa ya Mazingira iliyopo sasa ni ya zamani, jambo ambalo linalokwamisha masuala mengi ya utekelezaji wa shughuli za kimazingira kulingana na hali halisi ya sasa ikiwemo uendeshaji wa Mfuko wa Mazingira. **Kamati inaendelea kuisisitiza Serikali kukamilisha mchakato wa mapitio na maboresho ya Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 1997 ili kuwezesha Ofisi hii kufanya mabadiliko mbalimbali yakiwemo mabadiliko ya sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004, hivyo kurahisisha utekelezaji masuala mbalimbali yaliyokwama ikiwemo Mfuko wa Taifa wa Mazingira ulionzishwa tangu Mwaka 2007, ila unashindwa kutekeleza majukumu yake hadi sasa.**

### **6.5 Upatikanaji na Utumiaji wa Nishati mbadala**

**Mheshimiwa Spika**, uharibifu wa mazingira unaotokana na ukataji wa miti kwa ajili ya kuni na mkaa unaendelea kwa kasi kubwa ukilinganisha na kasi ya upandaji wa miti mipya. **Kamati inashauri kuwa:-**

i) Serikali iwahamasishe wananchi kuendelea kupanda miti ya muda mrefu na ile ya muda mfupi na kuendelea kusimamia uvunaji endelevu wa misitu yetu; na

ii) Serikali ihimise uwekezaji katika kuzalisha mkaa kutokana na takataka, utumiaji wa gesi pamoja na umeme ili kupunguza matumizi ya kuni na mkaa kwa wananchi na Taasisi zetu nchini.

### **6.6 Matumizi ya kemikali hatarishi – Zebaki**

**Mheshimiwa Spika**, uingizaji holela na utumiaji wa kemikali ya Zebaki nchini kutokana na kuwapo kwa wachimbaji wadogo wa dhahabu wanotumia kemikali hiyo, unaathiri kwa kiasi kikubwa afya na usatwi wa wachimbaji hao. Madhara ya matumizi ya kemikali hiyo yanatokana na wachimbaji wengi kuitumia bila ya kuwa nyenzo za kujinga kutokana na zebaki. Vilevile, maji yanayotumika kusafishia dhahabu yakiwa yamechanganyika na Zebaki, yanatiririka kwenye vyanzo vya maji kama vile mito na mawaziwa. Watu wanapotumia maji kutoka vyanzo hivyo vilivyochafuliwa na zebaki ya kuoshea dhahabu, huathirika kiafya na wakati mwingine kupata maradhi sugu yanayogharimu maisha yao.

**Mheshimiwa Spika**, Kutokana na hali hiyo, **Kamati inashauri kuwa:-**

i) Ofisi ya Makamu wa Rais – Mazingira ishirikiane na Ofisi ya Mkemia Mkuu kudhibiti uingizwaji na zebaki nchini;

ii) usimamizi na uratibu matumizi ya zebaki kwa wachimbaji wadogo wa dhahabu nchini uendelezwe na Ofisi ya Makamu wa Rais kwa pamoja na Ofisi ya Mkemia Mkuu; na

iii) Serikali itafute teknolojia mbadala ambayo wachimbaji hao wataitumia ili kuachana na matumizi ya zebaki.

### *6.7 Taarifa ya Hali ya Mazingira nchini*

**Mheshimiwa Spika**, Kifungu 175 (1) cha Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004 kinamtaka Mkurugenzi wa Mazingira kuandaa na kutoa taarifa juu ya Hali ya Mazingira nchini kila baada ya miaka 2 na kuiwasilisha Bungeni. Hata hivyo uzoefu unaonesha kuwa upo ugumu wa kutekeleza masharti hayo jambo lililosababisha kuwasilishwa kwa taarifa hiyo mwaka 2008, 2014 na 2019. Kwa sababu hiyo, taarifa ya kwanza, ya pila na ya tatu hazikuweza kuzingatia masharti ya kuwasilishwa baada ya miaka miwili. Kwa msingi huo, **Kamati inashauri kuwa Serikali iandae mapendekezo ya marekebisho ya kifungu hicho kwa kuongeza muda wa kutoa ripoti kufikia miaka 5.**

### *6.8 Tathmini ya Athari ya Mazingira (Environmental Impact Assessment)*

**Mheshimiwa Spika**, sheria ya mazingira inaelekeza kabla ya kuanza kutekeleza miradi kwenye eneo fulani lazima ifanyike Tathmini ya Athari ya Mazingira zinazoweza kujitokeza kama mradi unaweza kutekelezwa sehemu husika. Kazi hii inafanywa na washauri elekezi ambao wanatoza fedha nyingi kufanya hiyo kazi hivyo kukwamisha kuanza kwa baadhi ya miradi kwa kuwa inaongeza kwa kiasi kikubwa gharama ya mradi. **Kamati inashauri kwamba NEMC iwasimamie washauri elekezi sambamba na kutoa mwongozo kuhusu gharama za kufanya Tathmini hiyo. Kufanya hivyo kutawezesha gharama zinazotowza kuwa halisi na zinazolingana na mradi unaohusika.**

## **7.0 HITIMISHO**

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuchukua fursa hii kukushukuru na kukupongeza sana kwa kuendelea kuliongoza Bunge letu kwa weledi mkubwa. Vilevile, naomba kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Naibu Spika, kwa weledi na

umahiri wake katika kukusaidia kuongoza vikao vya Bunge hili la Kumi na Mbili.

**Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya pekee, napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira ambao wameweza kutoa maoni, michango na mawazo yao mbalimbali wakati wa kupitia na kuchambua Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais – Mazingira na hatimaye kuandaa na kukamilisha taarifa hii. Orodha yao ni kama inavyosomoka hapa chini: -

1. Mhe. David Mwakiposa Kihenzile, Mb – Mwenyekiti
2. Mhe. Eric James Shigongo, Mb M/Mwenyekiti
3. Mhe. Usonge Hamad Juma, Mb
4. Mhe. Martha Nehemia Gwau, Mb
5. Mhe. Cecil David Mwambe, Mb
6. Mhe. Eng. Ezra John Chiwelesa, Mb
7. Mhe. Lucy John Sabu, Mb
8. Mhe. Hawa Chakoma Mchafu, Mb
9. Mhe. Hamad Hassan Chande, Mb
10. Mhe. Daimu Iddi Mpakate, Mb
11. Mhe. Haji Makame Mlenge, Mb
12. Mhe. Issa Ally Mchungahela, Mb
13. Mhe. Askofu Josephat Mathias Gwajima, Mb
14. Mhe. Khatib Said Haji, Mb
15. Mhe. Boniphace Mwita Getere, Mb
16. Mhe. Maryam Omar Said, Mb
17. Mhe. Deodatus Philip Mwanyika, Mb
18. Mhe. Zulfa Mmaka Omary, Mb
19. Mhe. Jumanne Kibera Kishimba, Mb
20. Mhe. Nancy Hassan Nyarusi, Mb
21. Mhe. Salim Hassan Turkey Toufiq, Mb
22. Mhe. Shamsia Azizi Mtamba, Mb
23. Mhe. Antipas Zeno Mgungusi, Mb
24. Mhe. Dkt. Charles Stephen Kimei, Mb
25. Mhe. Dkt. James Kimea Alfred, Mb

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuchukua nafasi hii kumshukuru Mhe. Umy Mwalimu, Mb. aliyekuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu Rais-Muungano na Mazingira, na aliyekuwa

Naibu wake Mhe. Mwita Waitara, Mb, kwa ushirikiano walioipatia Kamati. Aidha, Nampongeza Mhe. Selemani Jafo, Mb. na Naibu Waziri wake Mhe. Hamad Hassan Chande, Mb, kwa kuteuliwa katika nafasi zao.

**Mheshimiwa Spika**, napenda pia kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Stephen Kagaigai, Mkurugenzi wa Idara ya Kamati Bw. Athumani Hussein, Mkurugenzi Msaidizi Bw. Michael Chikokoto, makatibu wa Kamati Bi. Zainab Mkamba na Bi Mwajuma Ramadhan pamoja na Msaidizi wa Kamati Bi. Grace Mwenye kwa kuratibu shughuli za Kamati hadi taarifa hii kukamilika.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema haya, naomba kulishauri Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais – Mazingira **Fungu 31 – Idara ya Mazingira** kwa Mwaka wa Fedha **2021/2022** ambayo ni kiasi cha Shilingi **8,964,939,440.00** kama alivyofafanua mtoa hoja pamoja na maoni ya Kamati hii.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

David Mwakiposa Kihenzile, (Mb)  
**MWENYEKITI**  
**KAMATI YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA**  
**NA MAZINGIRA**  
27 April, 2021

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Nakushukuru sana kwa kusoma taarifa yako vizuri kabisa. Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Shigongo ni mmoja wa Wabunge ambao ni vizuri kufuatilia historia zao *as a unique history in life*. Sitataka kusema, kwa kifupi hapa lakini kwa sababu tupo naye basi tujaribu kujifunza mapito



ambayo amepitia mpaka kufika hapa. Ni mmojawapo kati ya Wabunge ambao kwa kweli wana mafanikio makubwa sana kwa maana hiyo ya maisha aliyopitia tangu udogo mpaka kufika hapa. (Makofi)

Nimesikia habari ya Mwongozo.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Spika, hapa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hussein Nassoro nimekuona sasa.

### MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Spika, naomba Mwongozo wako kutokana na hali ya hewa iliyopo humu ndani, ubaridi umezidi na unaona viti vingi Wabunge imebidi watoke nje kwa ajili ya hali ya hewa. Kwa hiyo, naomba mwongozo wako. (Makofi)

**SPIKA:** Ahsante sana nitatoa mwongozo wangu baadaye kidogo tu, lakini vijana wangu wamesikia, naomba mfikishe meseji huko *wa-regulate temperature*. Ahsante sana. Tafsiri nyingine Waheshimiwa mnapokuja muwe mnasiliba. Mnaweka viwalo kwelikweli. Ukija na kakitenge tu tabu.

Katika taarifa ya Kamati wametukumbusha kwamba kuna taarifa ya hali ya mazingira nchini ambayo huwa inatakiwa tuletewe hapa Bungeni *periodically*. Ni kwa muda mrefu sijaona taarifa hii ikiletwa. Kwa hiyo Mheshimiwa Waziri hii ni *homework* mojawapo, tunaomba na kwa sababu wataalam wako wapo tuwaambie kabisa, jamani taarifa yetu tunaitaka sasa. Tunaidai kabisa sababu ni moja ya taarifa muhimu sana. Taarifa ya hali ya mazingira nchini inatuonyesha hali halisi itakavyokuwa.

Pia, kutokana na mambo yanavyoenda huenda ratiba ya bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi badala ya siku mbili ikawa siku moja, huenda, bado tuna-*consult* na *Chief Whip* tuone hali itakavyokuwa kwa sababu ya Ijumaa ni siku maalum kidogo na ili ratiba yetu

isiparaganyike huenda ikawa Jumatatu peke yake. Lakini bado hatujaamua, tukimaliza vizuri nitawatangazia rasmi.

Sasa tunaendelea na uchangiaji, nilishawataja wachangiaji wawili naomba twende kwa dakika saba saba tujaribu, tuone, tukiona kama inakuwa tabu kidogo basi mbele huko tutafanya dakika tano, tano, lakini tuanze na dakika saba na kengele italia moja tu ili uwe umemaliza kuzungumza.

Naanza na Mheshimiwa Ahmed Abdulwakil, atafuatiwa na Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud, atafuatiwa na Mheshimiwa Maryam Omar Said kutoka Chama cha CUF.

**MHE. AHMED YAHYA ABDULWAKIL:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, asubuhi ya leo baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye tupo katika mfungo, mimi naheshimu sana heshima hii ya kupewa kuwa mchangiaji wa mwanzo katika wizara hii ambayo ni ya uhai wa maisha yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kikawaida sina uchangiaji mkubwa sana maisha yote na nitatumia haitozidi dakika tatu, nne mpaka tano. Kwa hiyo nitasevu muda kusudu ajaye apate nafasi ya kuongea zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitaongea upande wa Mazingira *(Environment)*. Katika hotuba ya Mheshimiwa Rais, hapa alitumia dakika tatu, jinsi anavyojali na kuthamini mazingira. Kwa njia hii alipitia kiatu hiki kabla ya leo kufikia kuwa Rais wa Tanzania, kwa hiyo tumpongeze sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa ufadhili hapa kidogo ndiyo nataka Mheshimiwa Waziri atakapokuja ku-*wind up* hotuba yake, dunia imekuwa sana katika upande wa mazingira na mikutano mbalimbali inafanyika ulimwenguni kwa sababu ya kuhifadhi mazingira. Kwa hiyo, kwa upande wa Zanzibar kuna PECCA ukanda wa PECCA ni ukanda mali sana huu, ambao kwa namna moja au nyingine umeingia

katika ramani ya dunia pamoja na kisiwa cha Misali. Misali kuna kisiwa, kuna bahari na kuna bustani chini ya ulimwengu ambayo si nchi nyingine ni *natural*. Sasa lazima yalindwe kimazingira kwa hiyo tulikuwa na wasiwasi kama nchi kwamba vipi hali ya ufadhili wa kimazingira katika hizo sehemu ambazo kubwa zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ukiangalia katika uchumi, Tanzania tunakusudia kununua meli nane (8) za uvuvi; meli nne (4) Tanzania Bara na nne(4) Tanzania Visiwani.

Katika uvuvi, kuna siri kubwa sana ya kupata *harvest* yaani mavuno kwa kutumia matumbawe. Haya kama hayakuhifadhiwa kimazingira, mara nyingi samaki wanahama na kutakuwa hakuna pia samaki wenyewe tunaokusudia, meli itakuja na hatutavua. Sasa napenda kujua wakati Mheshimiwa Waziri akija ku-*wind up*, atueleze hali ya kimazingira ya matumbawe, nchi zote baina ya Zanzibar na Tanzania Bara ikoje kusudi tuweze kufaidi neema hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nyuma kuna mfuko ukiitwa, Mfuko wa Kusaidia Nchi Masikini katika Kuokoa Mazingira (*LDCF*). Sasa wakubwa duniani wana hiari yao kutusaidia au kutosaidia hali ikoje katika kupambana na hali hii na ufadhili, ili kusudi tuweze kuishi katika ustahi mazingira mazuri kwa nchi yetu? Ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Ahmed, lakini jina lako huwa linanipa tabu kidogo, unauhusiano gani na Mzee Abdulwakil?

**MHE. AHMED YAHYA ABDULWAKIL:** Mheshimiwa Spika, jina langu kamilifu naitwa Ahmed Yahya Abdulwakil Mbunge wa Kohani. Tunao uhusiano wa kijomba wa huko nyumbani. (*Makofi/Kicheko*)

**SPIKA:** Ahsante sana Ahmed.

**MHE. AHMED YAHYA ABDULWAKIL:** Sikutaka kuweka sawa ehe! Kusudi watu wakatishika, hamna! (*Kicheko*)

**SPIKA:** Kiti changu kimekuwa kikipata tabu kidogo. Nashukuru kwa ufafanuzi huo, Ndugu yangu Ahmed. Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud.

**MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD:** Mheshimiwa Spika, ahsante, kwanza napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuamsha salama siku hii ya leo. Nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa Hotuba yake nzuri yenye kuleta mustakabali mwema katika Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote naanza kuchangia kwenye sekta ya mazingira, nchi yetu ya Tanzania ni nchi ambayo ina Bara, ina na Visiwa kwa pande zote mbili za Muungano. Sisi tumerithi nchi yenye Bara na Visiwa, ni vyema na sisi tukawarithisha vitoto vyetu nchi ikiwa kamilifu, kama ilivyo kwa maana ya Bara na Visiwa vyake.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mabadiliko ya tabia nchi kuna changamoto kubwa katika maeneo ya fukwe na maeneo mengine ya maziwa kwamba, tayari bahari au maji yanapanda juu na kuyafikia maeneo ya makazi ya watu. Kuna visiwa duniani tayari vimeshapotea kwenye ramani ya dunia, kwa hivyo na sisi ni vyema tukahifadhi mazingira yetu ili visiwa vyetu visije vikapotea kwenye ramani ya dunia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye sekta hiyo hiyo ya mazingira tumeambiwa na kwenye Hotuba ya bajeti kwamba, Wizara ina mpango wa kuzuia utumiaji wa kuni, makaa. Lakini ni vyema pia, kuna baadhi ya uzalishaji mali katika sekta ya biashara, unatumia kuni nyingi na hivyo ni vyema tukaangalia hasa kwenye kukausha tumbaku. Tumbaku inatumia miti mingi katika kukausha. Ni vyema sasa Wizara ya Kilimo na Wizara ya Mazingira ikakaa pamoja, ili kuweka namna bora ya ukaushaji wa tumbaku kwa kutumia mashine nyingine za kisasa ambazo hazitumii kuni na mikaa na kukata miti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kuna Taasisi zisizo za Kiserikali nyingi tu, zinajihusisha na uhifadhi wa mazingira na uoto wa

asili. Ni vyema Taasisi hizo zikatambuliwa rasmi kwasababu, kuna baadhi ya Taasisi nimezikagua, wanatumia fedha zao mfukoni kuhifadhi mazingira na uoto wa asili. Wengineo wana misitu karibu ya heka (10), (15) wanahifadhi wenyewe uoto wa asili. Kwa hivyo, ni vyema katika hiyo mifuko inayokuja, ikaangalia pia na hizi Taasisi zisizo za Kiserikali iweze kutekeleza jukumu letu hili kwa pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikija kwenye upande wa Muungano, Muungano wetu jana umetimiza miaka (57) na leo imeongezeka siku moja. Muungano huu unakwenda haukutembea na ndio maana kila kitu kinachokuwa kinakuwa na changamoto zake. Na Muungano wetu unakuwa kwasababu kuna changamoto za makuzi. Naipongeza Serikali kwa kutatua changamoto mbalimbali ambazo zinajitokeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaiomba Serikali, iendelee na hatua hizo za kutatua changamoto hizo kwa wakati muafaka na kuzitangaza kwa wananchi. Kwasababu, wanufaika wa Muungano huu ni nchi na wananchi ni vyema pande zote mbili za Muungano zikafaidi matunda ya Muungano kwa maana Bara na Visiwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, changamoto mbalimbali zikitatuliwa wananchi watakuwa na furaha na Muungano wetu. Changamoto za kibiashara, changamoto za kiuchumi, changamoto za ajira kama zilivyosemwa. Mambo haya yakienda sambamba na sawia mambo mengi yatatatuliwa kutokana na changamoto za Muungano.

Mheshimiwa Spika, nikiendelea, Tanzania ni nchi ya amani, Tanzania viongozi wote walioanza kuasisi Tanzania kutokea Hayati Mzee Karume na Mwalimu Nyerere na viongozi wote waliofuatia, wameuimarisha Muungano wetu kwa vitendo na waliopo ni matumaini yetu watauendeleza kama walivyosema wenyewe, wameahidi. Mheshimiwa wetu Rais Samia, Makamu wa Rais, Rais wetu wa Zanzibar Dkt. Hussein Ali Mwinyi wako sambamba na maamuzi na mapendekezo ya watangulizi wao nawapongeza kwa hilo

na sisi tuko nyuma yao kuwaunga mkono, kuhakikisha Muungano huu unadumu milele na milele kwa faida yetu tuliopo na faida ya vizazi vijavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jina la Tanzania ni jina zuri sana, jina lenye haiba, jina lenye mvuto nampongeza aliyetunga jina hili la Tanzania kwa dhati ya moyo wangu. Jina limetupatia heshima kubwa sana, jina la Tanzania. Ni vyema sisi wananchi wa Tanzania tukatunza amani yetu ya Tanzania kama jina letu lilivyo lina mvuto wa haiba ya Tanzania.

Naomba tumpe muda Rais wetu, Makamu wa Rais na Waziri Mkuu watuletee maendeleo ya nchi yetu na kutekeleza majukumu yote yaliyoachwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kweli wako na dhamira ya dhati kabisa kuwaletea wananchi maendeleo. Si vyema kwa sasa hivi wakaanza kuwachokonoa, ni muda mfupi tu wana malengo makubwa, wana maono makubwa ya kutuletea maendeleo sisi watanzania. Naomba tuwape ushirikiano, tuwape imani zetu kama tulivyo. Kiungo kikubwa cha Muungano wetu kinaashiria pia kwenye hili Bunge lako.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru na ninakupongeza wewe na Naibu wako kwa kuliongoza Bunge letu hili vizuri kwa salama na Bunge letu tukatekeleza majukumu yetu kama tulivyopangiwa kutoka pande zote mbili za Muungano tukiwa wawakilishi wa wananchi wa pande zote mbili za Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nchi iko salama, mipaka ya nchi iko salama. Ni matumaini yangu kwamba, na sisi wananchi tutahakikisha kuunga mkono viongozi wetu na vyombo vyote vya usalama, kuhakikisha nchi yetu hii itakuwa salama kwa faida yetu na vizazi vijavyo.

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia, Tanzania ina jina kubwa na ina historia kubwa, Muungano wetu uendelee kudumu kwa maslahi yetu na vizazi vijavyo. Ahsante nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud msiomfahamu Khadija amewahi kuwa mjumbe wa Kamati Kuu kwa muda mrefu tu, maarufu huyu. Nilikutaja Mheshimiwa Maryam Omar Said na utafuatiwa na Mheshimiwa Bakari Hamad Bakari. Mheshimiwa Maryam.

**MHE. MARYAM OMAR SAID:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii na nikaweza kuchangia katika sehemu ya Bajeti ya Wizara ya Muungano na Mazingira. Zaidi nitajikita katika sehemu ya Mazingira lakini nitaenda zaidi katika sehemu ya Mazingira ya nchi kavu. Namshauri kwanza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, tusiangalie tu mazingira ya bahari bali tuende zaidi na mazingira ya nchi kavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye mazingira ya nchi kavu, ni vizuri kwamba tunasema tunashajihisha sana kwamba tupande miti, lakini naomba tushajihishe kupanda miti lakini pia tushajihishe kuitunza miti hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwenyewe binafsi ni mtu ambaye kwamba jimbo langu lipo katika mazingira hatari sana la miti ambayo kwamba ni mashamba ya Serikali. Mashamba haya ya Serikali yenye kilimo cha miti ya mipira, zamani ilikuwa ni mazuri yana faida kubwa kwa wananchi wangu wa Jimbo la Pandani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kwa sasa imekuwa ni changamoto kubwa sana ndani ya Jimbo langu la Pandani. Yale mashamba zamani yalishughulikiwa vizuri, yakafyekwa vizuri, kiasi ambacho kwamba ulikuwa unauona mti uliopo mwanzo wa kwenye heka mpaka mwisho wa heka. Lakini sasa mashamba yale yamevamiwa na miti ambayo kwamba, si rasmi na kufanya sasa mashamba yale yamegeuka kuwa mapori na kuwa sasa, yanahatarisha maisha ya wananchi wangu ndani ya Jimbo langu la Pandani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vitendo vingi vya uhalifu vinafanyika ndani ya mashamba hayo ya Serikali kutokana

na mazingira yaliyopo. Tunaona sasa imefika hadi hata mwanafunzi akitoka kwenye Shehia moja kwenda kwenye Shehia nyingine, ambapo kwamba anafuata huduma ya elimu inakuwa ni mtihani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wabakaji hutumia maeneo hayo kwa kutimiza matakwa yao, kitu ambacho kwamba sasa wananchi wangu wanaishi wakiwa roho juu. Namuomba sana Waziri pamoja na Naibu Waziri. Naibu Waziri analijua hili kwasababu, ni mtu ambaye kwamba yupo jirani yangu ndani ya Jimbo langu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, afike katika maeneo yale na aniangalie kwa jicho la huruma, lakini pia ayasimamie mazingira ya Jimbo lile, katika mashamba yale ili kuondoa changamoto zile. Yale ni mashamba ya Serikali leo kama Serikali tunashajihisha kupanda miti, lakini miti yetu wenyewe hatuitunzi, hivi tunafikiria kipi ambacho kwamba kitaendelea hapo baadaye? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata hiyo miti inayopandwa inaweza kuja baadaye ikawa changamoto pia kwa wananchi. Namuomba sana Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri hebu tuliangalie hili. Tuangalie mazingira ya bahari lakini pia tuje katika mazingira ya nchi kavu. Katika mashamba haya kumeshawahi kufanyika mauaji makubwa yaliyolitikisa Jimbo na Taifa kwa ujumla. Kijana mdogo tu, aliuliwa ndani ya mazingira haya, mara nyingi sana vinatokea vitendo vya ubakaji ndani ya mazingira haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sitaki kuzungumza mengi na sitaki nipoteze muda, niliona kama sikulisema hili hapa sitopata nafasi kulisema pengine na wananchi wataniandama kwa hili. Wataniuliza, ulipata nafasi kwa nini hukulichangia? Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, nakuombeni mfike katika mazingira yangu ya Jimbo na muweze kuniwekea mazingira sahihi kwa mashamba yale. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Maryam Omar Said, Mbunge wa Pandani eeeh! Mbunge wa Jimbo huyu! Hata



Mheshimiwa Chande Naibu Waziri anajua hilo. *(Kicheko/Makofi)*

Sasa anafuata Mheshimiwa Bakari Hamad Bakari atafuata Mheshimiwa Kassim Hassan Haji. Mheshimiwa Bakari, Karibu.

**MHE. BAKARI HAMAD BAKARI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema, kwa kutuamsha na kutufikisha hapa na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu. Pia kwa vile, ni mara yangu ya kwanza kusimama katika Bunge lako hili, naomba nichukue fursa hii kuishukuru Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, kwa kunipigia kura za kishindo na kushinda kuja kuliwakilisha Baraza hapa kwenye Bunge hili Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nije kwenye kuchangia Hotuba hii ya Wizara ya Muungano na Mazingira. Kwanza nianze kuwapongeza Waziri na Naibu Waziri kwa kuwasilisha Hotuba yao hii. Hotuba ambayo imesheheni mambo mazuri kwa mustakabali wa mazingira lakini kwa muungano wetu tukufu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niende kwenye hoja moja kwa moja kwenye masuala haya ya Muungano. Tarehe 17 Oktoba, 2020 Kamati zetu zile za Muungano kwa maana ya *SMT* na *SMZ* zilitiana saina kuziondoa hoja (5) za Muungano.

Mheshimiwa Spika, hoja hizi ya kwanza ilikuwa ni ushirikishwaji wa Serikali ya Zanzibar kwenye masuala ya Kimataifa na Kikanda. Lakini ushiriki wa Zanzibar kwenye masuala ya Afrika Mashariki, lakini pia ni uchimbaji na utafutaji wa mafuta na gesi asilia. Lakini pia, kuna jambo kubwa la gharama za mizigo kwa mizigo ile inayotokea Zanzibar kutua katika Bandari ya Dar es Salaam. Mambo haya ni mambo mema sana lakini yanabakia kwenye makaratasi. Kwa nini tunaona aibu, tunaona haya kuweza kuwaelimisha wananchi kufahamu mambo haya? Kufahamu kwanza, kabla ya kuondolewa changamoto hii ilikuwaje? Na baada ya

kuondolewa kuna umuhimu gani na changamoto hii sasa ikoje? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala la gharama za mizigo inayotoka bandari ya Zanzibar kuja bandari ya Dar es Salaam bado kwenye jambo hili kuna changamoto. Pamoja na kuondolewa hoja hii, hatujui kwamba, labda pengine ni suala la elimu, ama ni jambo gani hasa? Lakini kuna changamoto kubwa ambayo inasababishwa, inawezekana na *TRA* au sijui ni Taasisi gani pale ambayo inahusika na mambo hayo lakini sana sana nadhani ni *TRA*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwananchi mmoja mmoja anaondoka na mzigo wake mmoja pengine ni *TV* moja, anatoka nayo Zanzibar anakuja nayo Dar es Salaam akifika pale baada ya kutoa kodi Zanzibar anakuja tena kutoa kodi nyingine pale. Jambo hili naomba liangaliwe tena upya, kama ni jambo ambalo limeshaondolewa kwenye changamoto kwenye hoja hizi za Muungano lielimishwe limeondolewaje? Likoje? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunavyofahamu sisi ni kwamba, kwa mizigo ile inayotoka nje kwa mfano, labda magari Zanzibar ikifika inachajiwa asilimia 40 ya *Tax*. Lakini yanaposafirishwa huku Bara yanamaliziwa *difference* ambayo ni asilimia 60 lakini je. kwa mizigo hii midogo midogo hali ikoje? Naomba sana Waziri na Naibu Waziri waelimishwe jamii, wawaelimishwe watanzania kuhusu masuala haya, bado kuna changamoto kubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, changamoto nyingine ni ucheleweshwaji wa kuwekwa saina mikataba ya Kimataifa ambayo sana sana inahusu Zanzibar. Kwa mfano, ujenzi na ukarabati, kwanza kuna ukarabati wa Hospitali ya Mnazimmoja kule Unguja. Jambo hili limefadhiliwa na *Saudia Fund*, lakini mpaka leo bado haujulikani mustakabali wa jambo hili ukoje? Lakini kuna ujenzi wa barabara kubwa ambayo inatoka Chakechake-Pemba mpaka Wete, mpaka leo kila siku tunaambiwa tu kesho, kesho! Jambo hili kwa kweli linanisononesha. Nakuomba sana, namuomba Mheshimiwa

Waziri atakapokuja hapa atueleze jambo hili limefikia wapi? Na ni lini hasa jambo hili litaondolewa, litatatuliwa na barabara ile ya Chakechake-Uwete itapata ufumbuzi na kujengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimalizie jambo moja. Kuenzi, kuutunza na kuuthamini Muungano wetu ni pamoja na kuwathamini viongozi wa Muungano huu. Dkt. Omar Ali Juma alikuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lakini ukienda katika Kijiji chake kinasikitisha. Kwanza, kwenye kaburi lake ambalo amelazwa pale, utasikitika sana. Barabara ambayo inaunganisha kutoka barabara kubwa mpaka kufika kwenye kaburi lake ambayo pia barabara hiyo inaunganisha kwenda kwenye shule ambayo ipo kwa jina lake yeye Dkt. Omar Ali Juma barabara hiyo ni chakavu haipitiki. Tunaomba Serikali ilione jambo hili na ithamini kiongozi huyu amefanya kazi kubwa kwa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namuomba sana Waziri atakapokuja hapa aeleze ni mpango gani uliopo kwenye kuthamini mchango wa Dkt. Omar Ali Juma nakushukuru sana. Ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Bakar Hamad Bakar. Sasa ni zamu ya Mheshimiwa Kassim Hassan Haji na atafuatiwa na Mheshimiwa Khalifa Mohamed Issa.

**MHE. KASSIM HASSAN HAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Awali ya yote, nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uhai na uzima na kutuweka katika Mfungo wa Ramadhan tukiwa wazima na leo kushiriki katika Bunge lako hili Tukufu.

Mheshimiwa Spika, kwenye Ilani ya CCM, ukifungua kifungu cha 226 na 227 na ukurasa wa 276 – 277 inazungumzia mambo ambayo si ya Muungano lakini yanaleta faida katika kutatua changamoto za watu wetu zikishirikiana Serikali zetu mbili; yaani Serikali ya Muungano wa Tanzania (*SMT*) na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (*SMZ*). Kwanza, niipongeze

Wizara kwa kutatua baadhi ya changamoto kwa kuunganisha makampuni *BRELA* na *BPRA*. *Memorandum* ambayo wamefanya angalau inasaidia wafanyabiashara wakubwa wenye makampuni; mtu akiwa amesajili biashara yake Zanzibar, basi angalu wakija huku wanakubalika vile vibali vyao nao vinaweza kufanya kazi, niwapongeze kwa hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vilevile, tukiangalia kwenye *ZFDA* na *TBS* wamefanya vivyo hivyo kwa kuwasaidia wafanyabiashara wadogo wadogo. Mtu akichukua biashara yake Zanzibar akija nayo Bara, basi nayo inakwenda bila usumbufu na cheti chao kinakubaliwa na jambo hilo linakuwa jema kwa wafanyabiashara wetu wadogo wadogo. Niwapongeze kwa hayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini kidogo kuna shida moja, jambo hili tunaomba liende likafanyike katika *TBS* na *ZBS*. Tukizungumzia *ISO* kwenye *standard* katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tukienda kwenye *codex* inayotambulika ni moja tu; inatambulika *TBS*. Kwa hiyo, *ZBS* wanashindwa ku-*recognize* zile *ISO* ambazo wao wenyewe wanatakiwa waende wakazifanye kama ambazo wanazifanya *TBS*.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, kitu kimesajiliwa Zanzibar; *TBS* inatakiwa iwasaidie *ZBS* angalau kitu kile kikitoka nje ya Tanzania basi na wao kiende kikatambuliwe kiufasaha. Kwa hiyo, watu wetu ambao wanafanya biashara ndogo ndogo Zanzibar wanakosa fursa ya kupeleka bidhaa zao nje kwa sababu tu ya haya mambo madogo ambayo yapo na yanaweza kutatuliwa kwa kufanya *memorandum* ambazo wenzetu wa *ZFDA* na *TBS* walifanya lakini walifanya hao wa *BRELA* na *BPRA*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kama kauli yetu ya Muungano ya safari hii inavyosema, “Muungano wetu ni msingi imara katika mapinduzi ya kiuchumi” basi twende tukawasidie wafanyabiashara hao wadogo wadogo na wao waweze angalau kulipata soko la nje ya Tanzania kwa kuweza kufanya

biashara zao zikawa zinakwenda na wakiwa wanapata kipato cha mtu mmoja mmoja. Si haya tu na taasisi nyingine ambazo zinakwenda kufanya mambo kama haya ya ushirikiano, basi tuwaombe sana wazifanye hizi *memorandum* angalau kuwafanya watu hawa wote wawili waweze kufanya biashara sehemu yoyote ambayo itakuwa ipo bila matatizo yoyote. Ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Kassim Hassan Haji. Nilishakutaja Mheshimiwa Khalifa Mohamed Issa na utafuatiwa na Mheshimiwa Abdul-Hafar Idrissa Juma.

**MHE. KHALIFA MOHAMED ISSA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Awali ya yote nimshukuru Allah *Subhanallahu Wataallah* kwa kutujaalia uzima na afya na kuukabili huu Mwezi Mtukufu wa Ramadhan kwa salama. *Inshaallah* Mwenyezi Mungu atujaalie tuukamilishe kwa salama.

Mheshimiwa Spika, nataka nijikite katika jambo hili la mazingira kwa maana ni jambo muhimu sana katika uhai wa binadamu. Mazingira yanayotuzunguka yanaakisi uhai wa binadamu na viumbe hai ambao wapo ndani ya ardhi yetu hii tunayoishi. Kuharibika kwa mazingira au kuharibiwa; ni kuharibika kwa maisha ya binadamu na viumbe hai vilivyomo. Mazingira uharibiwa ama kwa makusudi au bila kujua na binadamu wenyewe katika maisha yao ya kila siku ya kutafuta riziki zao. Sasa ni juu ya Serikali kusimamia na kuona kwamba mazingira haya kwa namna yoyote hayawezi kuharibiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nikija katika Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Zanzibar ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na inajumuisha Visiwa vya Unguja na Pemba na visiwa vidogo vidogo ambavyo vimezunguka visiwa hivyo. Kwa hivyo, uwepo wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania unategemea pia uwepo wa Visiwa vya Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, tumeona mabadiliko ya tabia nchi yameathiri sana na kama nilivyosema mwanzo hata

matendo ya binadamu wenyewe ya siku kwa siku yameathiri mazingira yetu hivyo bahari imechukua sehemu kubwa sana. Tumeambiwa katika tafiti nyingi kwamba katika miaka 50 zaidi ya sentimeta 19 – 20 zimekuwa maji ya bahari kwa maana ya kwamba kina cha bahari kimekuja juu. Kwa hiyo, imeathiri visiwa vingi sana vya Zanzibar kwa maana ya Unguja na Pemba kutaka kutoweka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niruhusu nitoe mifano michache kwa Zanzibar ambapo ni ushuhuda wa wazi wa kuondoka kwa visiwa. Kwanza, kuna Kisiwa cha Mtambwemkuu ambacho kimo katika Jimbo langu; Kisiwa kile kinavamiwa kwa kasi sana na maji ya bahari kiasi kutishia watu kutaka kuhama katika maeneo yao. Mfano wa pili; katika Jimbo langu pia kuna sehemu inaitwa Tosawana. Sehemu hii ina mashamba ya mpunga; watu wanajitafutia riziki zao kwa kulima katika maeneo yale, lakini kwa kweli kila baada ya muda maji ya bahari yanavamia mashamba yale ikabidi watu kuhama. Kwa kweli *TASAF* katika kipindi cha miaka miwili iliyopita walijitahidi kujenga tuta pale lakini kwa sababu lile tuta halikujengwa kitaalam, wala halikusimamiwa baada ya muda mfupi limeyeyuka kwa hivyo bado maji yanaingia kwenye mashamba ya watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna mfano mwingine katika eneo la Jimbo langu hilo hilo, kuna sehemu tunaambiwa miaka 50 iliyopita au zaidi kidogo ilikuwa ni mashamba watu wanalima mpunga, maji baridi lakini leo huwezi kupita kwa mguu lazima upite kwa kidau. Hii ni kutokana na maji ya bahari kupanda kila kukicha. Kuna mfano kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge, Kisiwa cha Misali; Kisiwa cha Utalii; baada ya muda mfupi kinaweza kupotea kwa sababu ya kuvamiwa na maji. Kuna Kisiwa cha Mnemba pia Kisiwa cha Utalii, nacho kiko hatarini kukikosa. Jimbo la Mheshimiwa hapa Bandani kuna Shehia ya Mjananza kuna sehemu inaitwa Uvuni kuna wakulima zaidi ya 100; leo wamehama kwa sababu maji ya bahari kuvamia mashamba yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile katika Kisiwa Panza bahari inakaribia shule, kwa hiyo makazi ya watu yako hatarini

kuondoka. Mwambeshidi mashamba yamevamiwa na maji, Ukunda Kengeja, Mwambe Shamiani, Nanguji, kote watu wamejitahidi kupanda miti kwa jitihada zao lakini bado kasi ya maji ni kubwa kwa hiyo athari inaweza kutokea wowote.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa ushauri tu kwa Serikali, kipindi kilichopita tuliomba sana lakini haikuwezekana, naomba tena Waziri na wataalam wake watembelee maeneo haya ili wakague na kuona zile athari ili wajue hatua za kuchukua.

Mheshimiwa Spika, mwisho niseme...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Khalifa.

**MHE. KHALIFA MOHAMED ISSA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Huyu ni Mheshimiwa Khalifa Mohamed Issa. Sasa ni zamu ya Mheshimiwa Abdul-Hafar Idrissa Juma na atafuatiwa na Mheshimiwa Mwanakhamis Kassim Said.

**MHE. ABDUL-HAFAR IDRISSA JUMA:** Mheshimiwa Spika, naendelea kukushukuru na kumshukuru Mwenyezi Mungu kama desturi yangu kutokana na neema hii ya uhai na afya ambayo mara nyingi tunaendelea kupewa.

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie haraka haraka katika hotuba hii ya bajeti kuhusiana na masuala haya ya utatuzi wa masuala ya Muungano. Niipongeze sana Ofisi ya Makamu wa Rais kwa namna ambavyo imeendelea kupambana na masuala ya Muungano na wakafanikiwa kutatua baadhi ya changamoto za Muungano hasa hizi tano ambazo zimesemwa katika bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nigusie hasa hii kuhusu gharama za kushusha mizigo bandarini. Muungano huu pamoja na faida zake kama walivyotangulia kusema wachangiaji wenzangu; changamoto zitakazokuja kujitokeza kwa umri wake ni namna ambavyo wananchi wa upande mmoja wanafaidi fursa za upande mwingine kwa usawa ama katika nafasi ya kupeana *favour* kwa sababu ni Muungano. Zanzibar ina watu wasiozidi 1,600,000 kwa makadirio; lakini Dar es Salaam tu peke yake ambayo ndiyo geti kubwa la watu kutoka Tanzania Zanzibar kuingia Tanzania Bara ina watu takribani 5,000,000 kuelekea 6,000,000.

Kwa hiyo, utaona namna gani *potentiality* ya soko la kibiashara ilivyo kwa upande wa Zanzibar na Tanzania Bara, hasa kupitia geti la Dar es Salaam. Nipongeze sana kwa hatua hii, lakini iendelezwe haraka ika-*reflect* kwa wananchi wetu kama walivyosema wenzangu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, utatuzi huu unaweza ukaleta ufumbuzi wa kurahisisha biashara lakini Muungano huu ni wa watu. Mimi nakuthibitishia sijafanya utafiti lakini ni uhakika zaidi ya asilimia 70 ya familia za wananchi Zanzibar tuna Ndugu zetu upande wa Tanzania Bara moja kwa moja. Mimi binafsi yangu, baba na mama yangu wanaishi Tanzania Bara, kwa hiyo, kuna mambo mengi sana nayahitaji katika kuunganisha. Kwa hiyo, wakati wakitatua masuala ya kibiashara na watatue masuala ya kiubinadamu moja kwa moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, haifurahishi hata kidogo mtu anatoka Zanzibar, amebeba sukari kilo tano tu kwa ajili ya kumpelekea mzazi wake au jamaa yake Tanzania Bara akifika pale bandarini anasumbuliwa. Sasa wakifanya utatuzi katika jambo hili isemwe wazi; Wizara ya Muungano ikaweke bango pale bandari ya Zanzibar, iweke bango pale bandari ya Dar es Salaam waseme sukari mwisho kilo moja ama usibebe kabisa ishia hukohuko; TV usibebe kabisa, ukibeba fuata tararibu hizi za kibiashara. Kwa hiyo, ningetamani waseme pamoja na kuwapongeza kwa haya waliyoyafanya. (*Makofi*)



Mheshimiwa Spika, nizungumzie suala la *TASAF*. Zanzibar ina Shehia 338; mpaka sasa Shehia 204 ndizo ambazo zinapata ruzuku ile kwa watu wa kaya maskini. Natambua katika bajeti hii ilivyosomwa kuna mnyanyuko wa Shehia, miongoni mwa Shehia zitakazonufaika ambazo zilikuwa hazipati ni zile zilizopo katika Jimbo langu la Mtoni. Jimbo langu lina Shehia tano, Shehia tatu zilikuwa zinapata msaada wa kaya maskini; Shehia ya Sharif Musa na Shehia ya Kwagoa zilikuwa hazipati. Natambua katika bajeti hii Shehia hizo mbili zimekwenda kuonekana lakini natambua pia si Shehia zote 338 za Zanzibar zitakwenda kumulikwa na mradi wa *TASAF* katika awamu inayoendelea. Naomba sana Serikali yetu hii, iendelee kutunisha na kutafuta uwezo wa mfuko wa *TASAF* ili Shehia zote 338 katika Visiwa vya Unguja na Pemba vinufaike na mradi huu wa kunyanyua na kuziwezesha kaya maskini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Wabunge tulipewa semina kama ambavyo Mheshimiwa Waziri amesema kuhusiana na Mfuko wa Jimbo kwa kule Zanzibar; natamani semina hiyo hiyo pia wakapewe wale wasimamizi wa fedha zetu kwa upande wa Zanzibar. Tujue, sisi tumeambiwa mipaka yetu ya fedha hizi na wale wakaambiwe kwamba mipaka ya fedha hizi za Mfuko wa Bunge la Jamhuri ya Muungano ni huu ili tukienda kuongoza vile vikao vya matumizi wasije wakaona labda tunawaingilia katika baadhi ya mambo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia, napongeza sana jitihada zinazochukuliwa katika kutoa elimu, lakini pia mfanye tathmini ya elimu mnayoitoa kuhusu Muungano; je, inakidhi mahitaji ya kisasa ya mabadiliko ya teknolojia? Mnaweza mkatoa elimu lakini bado ikawa haiwafikii watu wengi kwa sababu bado tunanung'unika sana kuhusu Muungano kuliko neema zake.

Mheshimiwa Spika, naomba nielezee Kiti chako na Bunge hili raha za Muungano, mimi ni mmoja wa wanufaika maana mke wangu ni Mchaga wa Rombo. Muungano una mambo mengi mazuri. Kama elimu inatolewa, taarifa zinakwenda, sasa fanyeni *evaluation* namna mnavyopeleka

elimu na mabadiliko ya teknolojia. Ningetamani kila tunapopita tuone tunazungumzia raha za Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, unaona changamoto zinazojitokeza visiwa kuanza kuliwa, hatutegemei visiwa vyetu vije vifutike, lakini kama mabadiliko ya tabianchi ulimwenguni yakiendelea ni lazima athari ya kupotea visiwa itatokea, tutakwenda wapi? Tuyaseme haya wazi sasa kama Muungano unatupa fursa ya kutembea, unatupa fursa ya kujenga na kujianda kama yale tunayotaka kuyazuia yakishindikana tuweze kuishi upande huu bila bughudha yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa fursa hii, naipongeza Wizara hii lakini naendelea tu kuishajihisha, Shehia 338, tuko katika Shehia 204 sasa mmeongeza Jimbo la Mtoni, mkimaliza Shehia 2 sina kesi nanyi lakini Zanzibar zitimie Shehia zote 338; Zanzibar tuendeleo kula raha na kufaidi Muungano. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Abdul-Hafar Idrissa Juma. Kwa kweli umechangia vizuri sana kuhusu Muungano. Maana mtu unakaa hapa Dodoma miaka tano umetoka toka Zanzibar hata kupata mtoto wa Kigogo, hamna? Dada zangu wamekaa tu hapa, wavusheni waende visiwani huko tuimarisha Muungano. *(Kicheko)*

Tunaendelea na Mheshimiwa Mwanakhamis Kassim Said, atafuatiwa na Mheshimiwa Asya Mwadini Mohammed. *(Makofi)*

**MHE. MWANAKHAMIS KASSIM SAID:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia Wizara hii ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, niende moja kwa moja kwenye mchango wangu. Leo tunazungumza ni mwaka 57 wa Muungano wetu na tunasema Muungano huu tutaulinda na tutautetea na ndipo tunapozungumza tunasema mbili

zatosha, tatu za nini. Leo toka tulivyoanza kuchangia Muungano huu Wazanzibar ndiyo tumepangwa kuchangia. Kwa kweli inasikitisha na inaumiza kwa sababu huu Muungano siyo wa Wazanzibar peke yetu ni Muungano wa Tanzania nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini ukizungumza hapa ukisema leo ni miaka 57 Muungano huu asilimia kubwa sisi viongozi wenyewe hatuujui na tunashindwa kuuzungumzia, zaidi tukizungumzia Muungano tutauzungumzia kisiasa, kumbe Muungano huu ni tunu ya nchi yetu; ni moyo wa nchi yetu; ni mishipa ya nchi yetu. Sisi tunasema tunatoka Zanzibar lakini na sisi vitovu vyetu vipo huku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi baba ni Mpemba, mama ni Mzaramo. Tunapouzungumzia Muungano lazima tuzungumzie Muungano wa Watanzania; tuzungumzie Muungano wa wanyonge na tumzungumzie mtu wa chini.

Leo unapokwenda mikoani; utamkuta mwananchi kutoka Mtambwe lakini yupo Shinyanga na Shinyanga kule amewekeza kiwanda cha mchele lakini kuuzungumza Muungano kusema hajui, kwa sababu gani? Ni kwa sababu hatupewi elimu, wala wananchi hawapewi elimu kuhusu Muungano wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo unapokwenda mikoani, utamkuta mwananchi kutoka Mtambwe, lakini yupo Shinyanga; na kule amewekeza kiwanda cha mchele, lakini kuuzungumza Muungano, kuusemea hajui. Kwa sababu gani? Kwa sababu hatupewi elimu, wala wananchi hawapewi elimu ya Muungano wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri, kwenye utalii tunapeperusha vipeperushi vya utalii. Kwa nini na Muungano tusipeleke vipeperushi wananchi wakaufahamu Muungano huu? Tumenyamaza zaidi! Leo tunanyanyuka kuzungumza Habari za Muungano, tunashindwa. Tunazungumza zaidi kisiasa, lakini kuuzungumza ile ilivyo, tunashindwa. Wapi tunafaidika, hatupajui; wapi

tunakosea, hatujui; wapi tunapokwenda, hatujui. Tutayazungumza yale madogo madogo, lakini na makubwa yapo yanaumiza.

Mheshimiwa Spika, jimboni kwangu, Jimbo la Magomeni kuna wanawake hawana uwezo wa kwenda China, China yao ni Kariakoo, wanakwenda kuchukua madera, khanga, viatu wanaleta Zanzibar. Utakuta amekwenda na mwananchi kutoka Mwanza, atachuka mzigo wake ule atakwenda kuuza Mwanza, lakini mwanamke anayetoka Zanzibar Magomeni, anateseka akifika bandarini. Muungano huo, miaka 57, tunaomba mambo haya mdogo madogo yaondolewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hivi sisi ni wamoja, ni ndugu, ni wazaliwa wa damu moja na tumbo moja, wa baba mmoja. Wameshapita viongozi wengi katika nchi hii, lakini bado wanasema wataulinda na watautetea kwa nguvu zote. Nasi tunasema tutaulinda na tutautetea kwa nguvu zote. Tunasema mbili zatosha, tatu za nini? Hatuoni haya, hatuoni aibu wala hatujuti, tunasema Muungano utaendelea kwa yeyote atakayekuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikitoka hapo, Mheshimiwa Marehemu Dkt. Omary Ali Juma alikuwa ni Makamu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Alikuwa Waziri Kiongozi miaka minane, akawa Makamu wa Rais miaka saba. Alizikwa vizuri, kwa heshima zote, tunashukuru; lakini leo ukienda kwenye kaburi la Marehemu Dkt. Omary, inauma sana. Kwa kweli inatusikitisha. Mheshimiwa Dkt. Omary aliitumikia nchi hii kwa nguvu zake zote, hakuna ambalo hakujua. Alikuwa ni Mjumbe wa Kamati Kuu ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, leo Mheshimiwa Dkt. Omary kaburi lake lina uzio wa waya toka laipozikwa hadi leo. Maana kaburi lile utasema siyo Makamu wa Rais, kama nilillozikwa mie tu, nikaenda nikazikwa, nikawekewa kuti, watu wakaondoka. Kwa kweli inauma. Viongozi wetu waliopita tunawaacha. Tunawadhaliisha. Hii inauma, inakera. Wao wameanza, imefikia hivyo, wengine itakuwaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sina zaidi, naunga mkono hoja.  
(*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwanakhamis Said Kassim kwa hotuba yako nzuri kabisa. Sasa nimeshamtaja nadhani Mheshimiwa Asya Mwadini Mohamed, karibu na utafuatiwa na Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma.

**MHE. ASYA MWADINI MOHAMMED:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nakushukuru kwa kuweza kunipa nafasi, na mimi nichangie hotuba hii ya bajeti ya Wizara ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi ya kwanza kumpongeza Mheshimiwa Rais mama Samia Suluhu Hassan kwa juhudi zake za makusudi kwa kuweza kuuheshimisha Muungano huu.

Mheshimiwa Spika, ikiwa jana ni siku ya Muungano, aliweza kutoa fedha za Sherehe ya Muungano na kuzigawa kwa nchi mbili hizi. Kwa hiyo, nampongeza sana na ametutia moyo, ameonesha kweli ana nia ya kwenda kuusaidia Muungano huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la pili, mama huyu, Rais wetu pia anaboresha mawasiliano ya kidemokrasia, ameweza kumpa nafasi Mheshimiwa Rais wa Zanzibar Dkt. Hussein Mwinyi kwenda kumwakilisha katika Mkutano wa *SADC*. Imetoa faraja sana na ninampongeza sana, tunaona kweli njia iliyokuwa na magugu sasa inakwenda kuwa safi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na mazuri ambayo yameanza, napenda kulieleza Bunge lako Tukufu, kumekuwa na changamoto nyingi kupitia Muungano huu, hususan Wazanzibari wakilalamika kupitia mitandao mbalimbali na maeneo mengi. Mengi yanazungumzwa, lakini mimi napenda kulizungumza suala zima la mfuko wa pamoja wa Jamhuri ya Muungano wa Zanzibar. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, leo imezungumzwa hotuba...

**SPIKA:** Mheshimiwa Asya, umesema mfuko...

**MHE. ASYA MWADINI MOHAMMED:** Mheshimiwa Spika, mfuko wa pamoja wa Muungano. Umenielewa? (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, leo imekuja hotuba ya Bajeti ya Wizara hii, lakini hatukuona kwamba kuna kipengele ambacho kina uwezo wa kuuchambua mfuko huu ili kuyaweka mambo haya sawa kuutambua kwanza mfuko huu una kiasi gani? Pia mfuko huu mgawanyo wake uko vipi? Wazanzibari wana haki ya kupata asilimia ngapi? Wanadai kiasi gani? Tunaomba mfuko huu uwe unaletwa katika Bunge lako Tukufu na uwe unajadiliwa ili kuyaweka mambo haya wazi na kupuguza kelele za mitaani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuchangia katika kipengele cha mazingira. Yamezungumzwa mengi; kumekuwa na Idara ya Mazingira, mimi nitakwenda kujikita zaidi kwenye *issue* nzima ya mifuko ya plastiki. Serikali ilitoa tamko la kuzuia uingiaji wa mifuko ya plastiki hasa kwa watumiaji na wafanyabiashara ambao wapo ndani ya nchi yetu. Kwa masikitiko makubwa, mifuko inaendelea kutumika na watu wanaitumia, lakini kinachoniumiza, Serikali huwa inachukua hatua kwa wafanyabiashara wadogo wadogo ambao wako chini, wao kazi yao kuuza mboga za majani pamoja na nyama na vitu vingine, wanawakamata, wanawapiga *fine*, na kuwafanyia mambo mengi ambayo huwa siyo mazuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika jambo hili, wako vigogo ambao ndio wanaoingiza mifuko. Tukiendelea kuwakandamiza wananchi wa chini, hatujaweza kuwasaidia. Tunatakiwa twende tukawatafute wahusika na wanajulikana; waweze kusema na kutoa hili tamko ambalo limetoka kwamba lisifanyiwe *implementation* kwa wafanyabiashara wadogo, wakatafutwe ambao wamewekeza na wanaoingiza mifuko hiyo ndani ya nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tumekuwa tukiona mambo mengi, ni kwa sababu hao ambao wanaleta mifuko hii

wanahifadhiwa kwenye kwapa, lakini wanaumizwa hawa ambao wako chini. Suala hili kama tunahitaji kweli kuwasaidia Watanzania, basi Serikali hii ikaanze kuwashika hawa ambao wanaingiza mifuko hii ndani ya nchi yetu, ndipo wakamalizane na watu wa chini kwa sababu muuza mboga kama hajapewa yeye kifungashio cha mfuko wa plastiki, anakitoa wapi? Mtaji wa mboga ni shilingi 200,000/=. Kwa hiyo, lifanyiwe kazi kweli kweli. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili, ni kweli tumeamua kuondoa vifungashio vya plastiki ndani ya nchi yetu, lakini tumekuja na mbadala? Tunatoa vifungashio vya plastiki, je, tumeweza kuwapa mbadala hawa akina mama wanaouza mboga mboga au wauza nyama? Leo mtu anakwenda sokoni na shilingi 2,000/= yake anasema anataka kununua mchicha wa shilingi 500/=: dagaa zake za shilingi 500/= na kitu kingine. Mfuko wenyewe unauzwa shilingi 500/=. Kweli wataweza kuumudu? Kwa hiyo, Serikali inapoamua kupiga marufuku ya kitu fulani, kwanza wafanye utafiti, waje na *solution* ya kuweza kulisaidia Taifa hili ndipo wapangue hiyo mifuko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile elimu inahitajika sana na watu lazima waelimishwe kwamba tunaondoa mifuko ya plastiki kwa sababu ni hatarishi, wanyama wetu wanaweza wakala, lakini na hawa wanyama sisi tunakula nyama yake na vitu vingine vingi ili kuweza kulisaidia Taifa hili; lakini kutoka tu kusema kwamba tunaondoa mifuko bila kuwatafutia mbadala, bila kutoa taaluma, bila kuwakamata vigogo wanaotuingizia, jambo hili haliwezi kusaidia. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. ASYA MWADINI MOHAMMED:** Mheshimiwa Spika, unanipa dakika mbili? *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Malizia dakika moja.

**MHE. ASYA MWADINI MOHAMMED:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

Mheshimiwa Spika, la tatu,...

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Ah, unaona sasa Mheshimiwa Asya unanitia katika matatizo. (*Kicheko*)

Taarifa inatoka wapi Mheshimiwa? Ahsante, endelea. Mheshimiwa Asya ukae chini ili uandike hiyo taarifa vizuri, uzime hapo, maana taarifa nyingine hizi ni muhimu.

### T A A R I F A

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpa taarifa mchangiaji kwamba siyo jukumu la Serikali kumwelekeza mwananchi *alternative*. Zipo *alternatives* nyingi, tulikuwa nazo tangu zamani. Tuna mifuko ya kushona, tulikuwa tunashona tangu tuko watoto, ipo inatumika. Kwa hiyo, wananchi watumie hizo *alternatives*. Siyo lazima Serikali iwaoneshe *alternatives*, Mifuko ya plastiki haitakiwi, ni kazi ya Serikali kuizuia na wananchi watafute njia rahisi kwa ajili ya kupata vifungashio mbadala. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda kumpa taarifa hiyo mchangiaji. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Asya Mwadini Mohammed, taarifa hiyo unaipokea? (*Makofi*)

**MHE. ASYA MWADINI MOHAMMED:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Mimi leo nimefunga na huu ni mwezi Mtukufu wa Ramadhani. Nadhani nilikuomba dakika mbili kwa ajili ya kulisaidia Taifa hili. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ukurasa wa 128 umezungumza mambo mengi ambayo yanapaswa kusimamia katika Muungano huu. Kuna suala la ulinzi na usalama, lakini kwenye ulinzi na usalama kuna Wizara ambayo inahusika katika kitengo hiki. Wizara hii kwa upande wa Zanzibar haina Ofisi,



hivyo inasababisha wastaafu wanajeshi ambao ni mama zetu na bibi zetu ambao wanasubiri viinua mgongo, wanalazimika kusafiri kuja bara, kwenda Dodoma na sehemu nyingine kwa ajili ya kufuatilia mafao hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naishauri Serikali iweze kuwasaidia wastaafu hao maana waliitumikia nchi hii. Hivyo, kama waliitumikia wana haki zao sawa na wengine.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Hivi Mheshimiwa Mwanakhamis alishaongea eh! Alishaongea. Sasa Mheshimiwa Hawa Mchafu.

**MHE. HAWA M. CHAKOMA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi. Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu. Sambamba na hilo, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Jafo kwa uwasilishaji wake mzuri.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu nitapenda kujikita kwenye upande wa mazingira. Tanzania ni miongoni mwa nchi wanachama tulioridhia wa Mkataba wa Minamata kuhusiana na kemikali za zebaki. Ukisoma mkataba wa Minamata katika Ibara ya 13 imeainisha vyanzo na utaratibu wa upatikanaji wa rasilimali fedha ili kuweza kutekeleza mkataba huo. Baadhi ama sehemu ya vyanzo hivyo ni pamoja na kutenga bajeti ya Serikali, kutumia Mfuko wa Dunia wa Mazingira, washirika wa maendeleo pamoja na sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, nimeskiliza hotuba ya Mheshimiwa Waziri, sijang'amua kinagaubaga ni kwa namna gani tumetenga fedha za bajeti ya Serikali ili kutekeleza masuala yaliyomo kwenye mkataba wa Minamata. Tunaambiwa tunayo fursa kama nchi wanachama kuweza kupata fedha kutoka Mfuko wa Dunia wa Mazingira ili kuweza ku-*deal* na matumizi ya kemikali ya zebaki ambayo ni hatari sana na ni sumu kwa maisha ya binadamu. Mheshimiwa Spika, hivyo,

nitataka kujua, sisi kama nchi tumeitumiaje fursa hiyo ya kuweza kupata fedha kutoka katika Mfuko huo wa Mazingira ili kuweza kuwajengea uelewa watu wetu sambamba na kupunguza athari ama madhara yanayotokana na kemikali ya zebaki.

Mheshimiwa Spika, ninapoizungumzia zebaki ninapenda Bunge lako lifahamu kwamba hii ni kemikali hatari sana na ni sumu kubwa inayosababisha maradhi kwa binadamu ikiwemo ugonjwa katika mifumo ya *nerve* za fahamu, uzazi, upumuaji, magonjwa ya figo, moyo na saratani, lakini inadhoofisha viumbe hai majini pamoja na athari za kimazingira. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kemikali hii ya zebaki nimetangulia kusema kwamba ina madhara makubwa sana, nasi kama binadamu tunadhurika na kemikali hii kwa kuishika hususan pale tunapochenjua dhahabu, tunapovuta mvuke wenye zebaki, tunapokunywa au kula vyakula vyenye viambata vya zebaki.

Mheshimiwa Spika, hivyo ni vyema sasa Serikali yako ikatambua na kuona namna bora ya kushughulika na kupunguza matumizi ya kemikali hii. Nitaomba Bunge lako lijue kwamba jamii ya wachimbaji wadogo hususan wenzetu wanaotokea ukanda wa ziwa, hawa ndiyo waathirika wakubwa wa matumizi ya kemikali hii ya zebaki. Wanapofanya shughuli za uchenjuaji wa dhahabu maji yale yanayotiririshwa kwenda kwenye vyanzo vya maji hususan mito na maziwa kuelekea...

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Taarifa. Endelea tu wewe mwenye taarifa. Nimeshakuona sasa.

## TAARIFA

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Spika, naomba nimpe taarifa mzungumzaji kwamba miongoni mwa

waathirika wakubwa sana wa kemikali ya zebaki ni pamoja na wanawake ambao wanashughulika katika shughuli za uchimbaji mdogo wa madini katika migodi yetu hususan Kanda ya Ziwa. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Hawa Mchafu, unapokea taarifa hiyo?

**MHE. HAWA M. CHAKOMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Ninaipokea Taarifa hiyo. Ni kweli kabisa jamii ya wachimbaji wadogo pamoja na watu wanaotokea Ukanda wa Ziwa ndio wanaoathirika na matumizi ya kemikali hiyo ya zebaki.

Mheshimiwa Spika, nimeshasema, wakati wa shughuli ya kuchenjua dhahabu, yale maji yanayotiririka kwenda kwenye vyanzo vya maji, mito na maziwa ndipo pale maji yale yanapokuwa *contaminated* na kemikali hii ya zebaki...

**SPIKA:** Kumbe ndiyo maana akina Musukuma hawanenepi, zebaki tupu! (*Kicheko*)

Endelea Mheshimiwa Hawa. (*Kicheko*)

**MHE. HAWA M. CHAKOMA:** Mheshimiwa Spika, ndiyo Ndugu zetu hawa wa Ukanda wa Ziwa, hawa Wanyamwezi, Wasukuma watani zangu, wajuu zangu wanapojiweka katika hatari kubwa ya kupata maradhi ambayo nimeyataja hususan maradhi hayo ya saratani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ipo shaka; na *research* ambayo siyo rasmi ni kwamba leo ukienda katika Taasisi...

**SPIKA:** Mheshimiwa umesimama eh! Endelea Mheshimiwa Hawa.

**MHE. HAWA M. CHAKOMA:** Mheshimiwa Spika, ipo shaka ama hofu na niseme kwamba hii ni *research* lakini siyo rasmi kwamba leo ukienda katika Taasisi yetu ya saratani, pale *Ocean Road*, wagonjwa wengi na Ndugu wa wagonjwa

wengi wa pale, lugha na lafudhi inayozungumzwa pale, ni watani zangu Wasukuma.

Kwa maana hiyo, ni dhahiri shahiri, kufuatia shughuli hii, wenzetu wamejaaliwa kupata madini, lakini athari yake au madhara yake ni kujiweka kwenye hatari ya kupata maradhi ambayo nimeshayataja.

**SPIKA:** Yaani Mheshimiwa Hawa anasema, ukifika *Ocean Road* pale utasikia tu titiri titiri, unajua hao hao! (*Kicheko*)

**MHE. HAWA M. CHAKOMA:** Mheshimiwa Spika, unasikia tu *ng'wadila, ng'wadila*, wanakandamiza. Asilimia kubwa ya wagonjwa wa pale ni hawa watani wangu. Tafiti zinaonesha vifo vinavyotokana na ugonjwa wa saratani vimefikia asilimia 15. Asilimia 15 ya vifo, siyo vidogo katika nchi yetu. Hivyo nina mambo mawili ya kuishauri Serikali.

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza ninapenda kuishauri Serikali kwamba wakati umefika sasa kuja na njia mbadala ya kuchenjulia dhahabu na kuachana na hii kemikali ya zebaki.

Mheshimiwa Spika, ninaomba...

(*Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji*)

**SPIKA:** Malizia...

**MHE. HAWA M. CHAKOMA:** Mheshimiwa Spika, naomba kumalizia kwamba tunayo teknolojia ama njia mpya ya uchenjuaji dhahabu inayoitwa *cyanide*. Kwa hiyo, Ndugu zangu na Serikali naomba sana tuanze kutumia hii njia mpya, tuachane na zebaki ambayo ina madhara makubwa kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo. Ninashukuru, ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana, nakushukuru sana. Wakati unaongea Mchungaji Gwajima alikuwa anakutazama sana. Hilo ni tatizo kubwa sana Kanda ya Ziwa. Mnapaswa msimame, muungane, tuone namna bora zaidi ya kuendelea kuishauri Serikali kwa sababu kwa kweli tatizo la zebaki ni kubwa. Linaathiri kizazi na kizazi.

Pia Mheshimiwa Hawa Mchafu ameongelea namna ya kupata fedha kutoka *Millennium Challenge Account* au mifuko mingine yoyote ya mazingira, fedha ambazo tumeshasema tena na tena kwamba zikija baadhi yake zinakwama Wizara ya Fedha. Hivi kwa nini uombe nyingine wakati ulizopewa zenyewe zimekwama hapa hapa nyumbani? Sababu ya kukwama hizo fedha hapo Wizara ya Fedha ni nini? Kwa sababu Bunge tunaweza tukaweka *pressure*, lakini siyo vizuri tuweke *pressure* mahali ambapo hakuna sababu ya kuweka *pressure*.

Kwa hiyo, tunataka majibu kwa kweli, Mheshimiwa Waziri; fedha ambazo zimekuja kwa ajili ya mazingira zinakwama pale Wizara ya Fedha kwa sababu gani? Mpaka inafika mahali ambapo zinataka kurudishwa kule zilikotoka na huenda baadhi yake zimesharudi na tumeshalisemea sana hata kwenye Kamati ya Bajeti na kadhalika. Tunataka ufumbuzi wa jambo hilo, hela hiyo ni kwa ajili yetu, ni faida yetu na dunia nzima inachukua hizo hela, sasa kwa nini sisi ikifika hapa inakuwa nongwa? Tatizo ni nini hasa?

Mheshimiwa Khamis Mbarouk Amour, atafuatiwa na Mheshimiwa Mohammed Jumah Soud na Mheshimiwa Abdullah Mwinyi atafuatia. Mheshimiwa Khamis Mbarouk Amour, hayupo eeh?

Haya, endelea haraka haraka. Hama hapo nenda mahali pengine, wa karibukaribu jaribuni kumuwashia. Hamia hata upande wa pili, jaribuni huku, mwonesheni hata upande wa pili kama inafanya kazi.

**MHE. AMOUR KHAMIS MBAROUK:** Mheshimiwa Spika, tayari.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Jumah Mohammed Soud ajiandae.

**MHE. AMOUR KHAMIS MBAROUK:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii na hii Wizara kwa kweli viongozi wake wamekwenda shule sana. Nawaombea Mwenyezi Mungu *Subhanahu Wataala* awaongoze, lakini pia awape mwelekeo mwema katika kutuongoza Jamhuri hii ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, niishukuru Jamhuri hii ya Muungano wa Tanzania kwa kuwa hata jimboni kwangu pale wamenisaidia sana. Kuna majengo mazuri sana ambayo yamefadhiliwa na *UAE* na haya tumeletewa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa kweli, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni njema sana kwetu na tunaishukuru sana na tunashukuru viongozi wa Tanzania kwa kutufikiria jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naamini kwa kuwa wamekuwa na imani ya kutusaidia jambo hili, kuna mambo mengine mazuri wanaweza wakatusaidia kama vile barabara na hata ile bandari inayotegemewa kuwa bandari ya samaki kwa ajili ya zile meli nane zile zinazotegemewa kununuliwa kwa Tanzania, naamini itajengwa Tumbe kwa kwa sababu, pale itarahisisha sana biashara baina ya Tanzania na Kenya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nataka nichangie kuhusiana na mazingira. Jimbo la Tumbe na Jimbo la Konde yameathiriwa sana na bahari. Jimbo la Tumbe bahari imeshafika kwenye soko pale na lile soko limejengwa kwa gharama sana. Katika mchango wa lile soko ni Jamhuri ya Muungano ndio imechangia pale, lakini maji yakipanda juu lile soko linafikwa sasa hivi, kwa hiyo, wakati wowote ile bahari itachukua eneo kubwa la ardhi. Kwa hiyo, naomba sana Wizara hii ya Muungano ifikirie jambo hilo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri juzi alipokuwa akijibu swali alisema kwamba, kuzuia mambo yale

ni kwa gharama kubwa sana, lakini naamini kutuhamisha Pemba sio gharama kubwa sana. Kwa hiyo, atutafutie hata eneo lingine hapa Tanzania bara na ndio neema za Muungano hizo kwamba kile kisiwa kikizama sisi tuwe na mahali pa kukimbilia huku. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika jambo hilo hilo la mazingira, mimi sijui kule kwetu kuna tatizo gani la mazingira kwa sababu, mikoroshu inakatwa ovyo na Wizara hii ipo, miembe inakatwa ovyo. Yaani miti inakatwa kimsingi na hakuna ule ufuatiliaji wowote.

Sasa mazingira haya tunayozungumza hapa, sina hakika kwamba yanahusika huko, lakini kama yanahusika, namwomba sana kabisa Waziri na Naibu wake na kwa sababu Naibu Waziri yupo Pemba pale, basi siku moja aje Jimbo la Tumbwe tuangalie namna zao la mikoroshu linavyoathiriwa na miembe inavyokatwa. Sasa hivi wakati wowote kutakuwa jangwa na kukiwa jangwa maana yake ni kusema kwamba, bahari itaongeza *speed* ya kupanda juu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wazazi wetu, wazee wetu, waasisi wa Taifa hili, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Mzee Abeid Amani Karume, walivyofanya jambo hili la Muungano maana yake walifanya kwa nia safi kabisa. Huwezi ukafanya umoja kama huna nia safi. Hawa walikuwa na nia safi kabisa na wakawashawishi Watanzania waliokuwepo wakati ule wote wakaridhia kwamba, wafanye Muungano huu.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa nina masikitiko kidogo kwamba, watu wametumia nguvu kubwa sana kuuchafua Muungano huu. Sasa naiomba sana Serikali ifikirie namna kwanza ya kutupa, kwa sababu Bunge hili ni jipya sana, kutupa semina angalau mtu asishindwe cha kujibu wakati akiulizwa. Pia naiomba Wizara hii inayohusika na mambo ya Muungano kwa sababu, nilisoma eneo katika kanuni zetu kwamba, ile Mifuko ya Jimbo ikishapelekwa Zanzibar watu wanatakiwa ku-*report* nini kimefanyika kutokana na hiyo Mifuko.

Mheshimiwa Spika, sasa Mifuko ile imetumika katika miaka 25 hii iliyopita, kuanzia mwaka 1995 mpaka juzi kwa kweli, hatujaona faida yake. Sasa Mheshimiwa Waziri akija hapa atatuzeleza labda angalau kwa lile Jimbo la Tumbe tu ambalo natoka niwaambie nini kwamba, Jamhuri ya Muungano hapa ilileta fedha shilingi milioni 20 kila mwaka na ilifanyiwa jambo gani. Fedha hizi hizi ndio zilizotumika kuwashawishi wananchi kule Pemba na Zanzibar kwamba, Jamhuri ya Muungano ndio adui wa Wazanzibari. Limefanyika sana jambo hilo mpaka sasa hivi sawa na kusema tu kwamba, yani wengi wa wananchi wanaamini kwamba...

**MBUNGE FULANI:** Taarifa.

**SPIKA:** Bahati mbaya muda umeisha.

**MHE. AMOUR KHAMIS MBAROUK:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Khamis Mbarouk Amour. Nilishamtaja Mheshimiwa Mohammed Jumah Soud atafuatiwa na Mheshimiwa Abdullah Mwinyi.

Mheshimiwa Mohammed Jumah Soud.

**MHE. SOUD MOHAMMED JUMAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii kuweza kuchangia bajeti ya Mheshimiwa Waziri wa Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira. Naomba niende moja kwa moja kwenye masuala ya mabadiliko ya tabia nchi.

Mheshimiwa Spika, kama tunavyokumbuka kwamba, Tanzania imeridhia mkataba wa Paris wa Mabadiliko ya Tabianchi na halikadhalika katika utekelezaji wa shughuli mbalimbali za mabadiliko ya tabianchi Tanzania mwaka 2000 na kitu Tanzania iliandaa mkakati wa mabadiliko ya tabianchi, lakini kabla ya hapo Tanzania iliandaa mkakati wa kupunguza ongezeko la hewa ukaa kutokana na masuala mazima ya uharibifu na ukataji wa misitu hovyoy. Sasa namwomba tu Mheshimiwa Waziri atakapokuja aje atuambie



tu kwa kiasi gani wametokeleza ule mkakati wa mabadiliko ya tabianchi wa mwaka 2012 na wana mpango gani wa kufanya mapitio ya mkakati ule kwa sababu matatizo bado yanaendelea.

Mheshimiwa Spika, halafu pia nataka vilevile kumwomba Mheshimiwa Waziri, kama tunavyojua kwamba, hizi *documents* zimetumia fedha za Watanzania na kwa kiasi kikubwa inaonekana mara nyingi tukishakuzitayarisha zinabaki kwenye ma-*shelf* na utekelezaji wake unakuwa ni mtihani. Kwa hiyo, naomba tu hili lifanyiwe kazi.

Mheshimiwa Spika, pia kuna suala zima, ambalo wenzangu wameligusia hapa kuhusu fedha za mabadiliko ya tabianchi. Kuna Mifuko hii, Mfuko wa kwanza Mfuko wa Nchi Masikini wa Mabadiliko ya Tabianchi na kuna Mfuko wa *GCF wa Green Climate Fund*, lakini pia kuna Mfuko wa *Adaptation Fund*. Mifuko hii yote inasaidia nchi kuweza kutekeleza mikakati yake ya mabadiliko ya tabianchi na kuepukana na athari za mabadiliko ya tabianchi. Sasa nataka kujua tu kwa kiasi gani Wizara au Ofisi imejitahidi kuweza ku-*capitalize* hizi fedha na kuweza kutumika. Kwa hiyo, naomba atakapokuja Waziri aje atueleze tu tumepata fedha kiasi gani kwenye Mifuko hii yote mitatu na zimetumika kwa kiwango gani?

Mheshimiwa Spika, kuna sehemu vile vile ambayo ni muhimu pia, niliwahi kuuliza katika swali langu moja hapa Bungeni kwamba, fedha hizi matumizi yake hayako vizuri kimgawanyo baina ya Zanzibar na Tanzania Bara. Imekuwa zaidi ni kama huruma tu kwamba, fedha hizi zitumike Zanzibar na hizi zibaki zitumike Tanzania Bara.

Kwa hiyo naomba Waziri atakapokuja aje atujulishe vilevile kwa kiasi gani fedha hizi zimeweza kutumika upande wa Tanzania Visiwani na upande wa Tanzania Bara.

Mheshimiwa Spika, kuna sehemu moja ambayo ni muhimu kuizingatia. Fedha hizi hasa za *Adaptation Fund* na fedha za Mfuko wa Nchi Masikini kunakuwa kuna *allocation*

maalum ambayo inagawiwa kwa nchi. *Allocation* ile kama hukuitumia vizuri, basi inakwenda kwa nchi nyingine ambao wako *sharp* katika matumizi. Sasa nina wasiwasi kwamba, gawio letu la Tanzania hatulitumii vizuri kwa sababu, mara nyingi utaona ufuatiliaji wetu katika...

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Taarifa. Eeh, sawa nimekuona.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Naomba kumpa Taarifa mzungumzaji kwamba, anayosema ni sahihi na sisi kama Taifa tumeshindwa ku-*access* hizo *fund* kwa sababu, kuna *qualifications*; lazima uwe na taasisi ambazo ziko *accredited*, wakati nchi kama Kenya ina taasisi kama hizo 18 sisi nadhani tuna taasisi moja tu ambayo ni *NEMC*. Ndio maana tunakosa hizo fedha pamoja na kuwa fungu limetengwa kwa kila nchi. (*Makofi*)

**SPIKA:** Nakushukuru kwa *intervention* hiyo, lakini pamoja na taasisi hiyo moja hata hizo chache ambazo tumepata zinakwama Wizara ya Fedha. Ndio maana Waziri wa Fedha ajiandae siku ya Wizara yake nitakamata shilingi mimi mwenyewe ya mshahara wa Waziri wa Fedha. (*Kicheko/Makofi*)

Kabisa, yaani ni kitu ambacho kila wakati nauliza, hivi hata Spika basi mwambieni ili anyamaze. Kwa nini fedha inaombwa inakuja katika nchi yetu, Wizara ya Fedha mnakalia, eti kisa kamati inayoitwa kamati ya nini sijui, nini sijui inaitwa ile, wala sio ya madeni maana yake hii sio deni, hii ni *grant*; inaitwa kamati ya, sijui kamati gani, ninyi mnaielewa vizuri zaidi, eti hajakaa. Ni kamati ya wataalam ndani ya Wizara ya Fedha, hajakaa.

Fedha zina miaka miwili, zina miaka mitatu, zina mwaka. Hata Mheshimiwa Jafo tunamwonea tu maana hata yeye hazikwami kwake, zinakwama Wizara ya Fedha. Sasa Wizara ya Fedha waipate kabisa mapema, katika jambo hili

tunataka badiliko, kwamba mifuko iko, mapesa yako duniani ya kutusaidia mambo ya mazingira, halafu hizo chache zinazokuja kwanza hatupati za kutosha, hizo chache zinazokuja zinakwama Wizara ya Fedha kwa nini? *(Makofi)*

Tunataka wenzetu wataalam muandike zaidi tupate hizo fedha, hizo fedha ni za dunia nzima ni za mazingira. Tuweze kufaidika na sisi tuna shida kubwa ya mazingira, miti kukatwa hovyoy, makorongo kila mahali na matatizo ya fukwe, mmeleza ninyi wenyewe matatizo mengi sana, tufaidike na hizo fedha. Sio fedha ikifika Wizara ya Fedha, basi ina wenyewe pale Wizara ya Fedha, haiwezekani! Haiwezekani Bunge hili likakubali mambo ya namna hii. *(Makofi)*

Endelea Mheshimiwa, alikuwa anakuunga mkono kwenye mchango wako. Malizia dakika zako kama bado una ya kusema.

**MHE. SOUD MOHAMMED JUMAH:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Kwanza naikubali Taarifa na Wizara ya Fedha walianza mchakato wa *accreditation* karibu sasa hivi mwaka wa kumi na mpaka leo hawajafanikiwa kupata *accreditation*.

Kwa hiyo, ningepomba tu sijui kama hili Mheshimiwa Waziri atakuwa na nafasi nalo, lakini tulikuwa tunataka tupate vilevile ufafanuzi wa Wizara ya Fedha wamekwama wapi?

Mheshimiwa Spika, kwa sababu, wenzetu nchi mbalimbali...

**SPIKA:** Wizara ya Fedha au Ofisi ya Makamu wa Rais?

**MHE. SOUD MOHAMMED JUMAH:** Mheshimiwa Spika, Wizara ya Fedha wameanza mchakato wa *accreditation* wa kuweza ku-*access* fedha za *GCF*, huu ni mwaka wa kumi na imeshindikana. Tunashukuru Mungu angalau...

**SPIKA:** Miaka kumi hatujapata hela za *Global Climate Facility*.

**MHE. SOUD MOHAMMED JUMAH:** Mheshimiwa Spika, hatujawahi kupata hata siku moja, labda kupitia kwa Mashirika ya Umoja wa Mataifa. Kwa hiyo, hili nafikiri Wizara ya Fedha au Waziri wa Muungano, kwa sababu, yeye ndio *answerable* kwa masuala ya mabadiliko ya tabia nchi, basi ni vizuri wakaja wakatueleza wana mchakato gani kwa sababu, kama alivyozungumza mtoaji taarifa kwamba, kuna nchi zina karibu taasisi zaidi ya tano, sita, ambazo tayari zimeshakuwa *accredited* na zinaweza ku-*access* hizi *funds*, lakini sisi ndio kwanza *CRDB* na *CRDB* ilivyo kwa utaratibu wa benki watakopesha hawatatoa msaada moja kwa moja.

Mheshimiwa Spika, wale ambao watakuwa na uwezo wa kuweza kutoa *grant* moja kwa moja ingekuwa kama Wizara ya Fedha na kule Zanzibar walianza mchakato, lakini mpaka leo nako bado hawajafanikisha. Kwa hiyo, kwa ufupi Tanzania *capacity* yetu imekuwa ni ndogo na hizi fedha tutakuwa tukiona tu wenzetu wakizitumia, nchi nyingine, lakini sisi tutakuwa hatuna faida nazo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimalizie mchango wangu katika mchango wa *CSOs* asasi za kiraia. Kama unavyojua kwamba, asasi za kiraia na asasi za kikanda na za kimataifa nazo zina mchango wa kuweza kutupatia fedha kwa ajili ya kupambana na mabadiliko ya tabianchi. Kuna tatizo ambalo limekuwa likijitokeza kuna asasi ambazo zina wataalam kutoka nje ambao wamekuwa wakisaidia ku-*raise* hizi *funds*, lakini hawa wamekuwa wakipata matatizo ya kuzuiliwa vibali na wengine wameondoshwa nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ningepomba tukazisaidie hizi asasi kujengea uwezo na hawa wataalam kutoka nje wakija basi tuwape nafasi kuweza kusaidia kuchangia na ku-*raise* hizi *funds*.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Asante sana Mheshimiwa Mohammed Jumah Soud kwa kututoa tongotongo kwenye baadhi ya mambo

muhimu. Tunakushukuru sana Mheshimiwa Mohammed Jumah Soud.

Nilikutaja Mheshimiwa Abdullah Mwinyi na utafuatiwa na Mheshimiwa Mbunge wa Kondoa Mjini, Ali Makoa.

**MHE. ABDULLAH ALI MWINYI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Napenda kuanza mchango wangu kwa kutoa shukrani na kwa kuwapongeza sana Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa kazi nzuri na kwa uwasilishaji mzuri wa *report* hii ndani ya Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, pili, ningependa vilevile kumpongeza Mheshimiwa Mhagama kwa uwasilishaji wake wa *Report* ya Kamati. Ameweka mambo vizuri kabisa, sina shaka yoyote kwamba, kuna mambo mengine makubwa zaidi yanakuja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Soud amenifilisi kidogo katika mchango wake sasa mimi nitajikita katika jambo moja, moja ameshalizungumza kwa kina na nisingependa kulirudia na yeye amekuwa mahiri zaidi katika sekta yake hiyo ya masuala ya mazingira.

Mheshimiwa Spika, ningependa kujikita katika masuala ya yale mambo ambayo tunaita kero za muungano. Kero za Muungano imekuwa jambo la msingi kabisa ambalo hata Mheshimiwa Rais amelizungumzia mara mbili, tatu na kukabidhi kwa Mheshimiwa Makamu wa Rais, masuala ambayo bado hayajafanyiwa kazi yafanyiwe kazi kwa kipaumbele. Hata hivyo, ningependa kuzungumzia jambo moja ambalo lilishatafutiwa ufumbuzi, suala la mafuta na gesi, *extractive industry*.

Mheshimiwa Spika, mnapo mwaka 2014 mpaka 2015 suala hili lilikuwa moto sana na tukatolea maamuzi kwamba, suala la mafuta na gesi lisiwe suala la Muungano, kila upande ujitegemee. Jambo hili ni jema katika uendelezaji wa tasnia hii na hivi karibuni kwa bahati mbaya Ndugu zetu wa Msumbiji *Total* imejitoa, imetangaza juzi wamejitoa kuwekeza Msumbiji

kwenye *project* ya LNG. Bahati mbaya kwa Ndugu zetu kwa sababu ule mradi ulikuwa mkubwa ndio unasemekana ndio ulikuwa mradi mkubwa kabisa ambao ungeweza kutokea katika *Sub Saharan Africa* katika miaka yote iliyopita, lakini kwa sababu ya matatizo ya machafuko na ugaidi wameamua kujitoa na *investment* hiyo haitaendelea.

Mheshimiwa Spika, sasa msiba wa wenzetu ni faraja kwetu, lakini kuna changamoto moja ambayo lazima tuitazame. Ukiangalia yale makubaliano yetu ya ndani tuliyokubaliana kwamba, tasnia hii sio sekta ya Muungano na taasisi na sheria na asasi zikaundwa, huku upande wa bara zipo *TPDC*, *PURA* na mengineyo na Zanzibar zikafanywa hivyo hivyo na sheria ikaundwa na kuna watu ambao tayari wameshaingia katika kufanya utafiti, lakini kuna changamoto moja.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia Katiba yetu ukurasa wa 128 inazungumza, Mambo ya Muungano, jambo la 15. Naomba ninukuu kwa ruhusa yako, inasema ifuatavyo; "15. Maliasili ya mafuta pamoja na mafuta yasiyochujwa na ya motokaa na mafuta ya aina ya petroli na aina nyinginezo za mafuta au bidhaa na gesi asilia."

Mheshimiwa Spika, hiyo ni mojawapo ya vitu ambavyo vipo katika orodha ya muungano, Kikatiba, japokuwa sisi wenyewe tumekubaliana kwamba kila upande unajitegemea. Sasa suala la mafuta na gesi ni suala linalohusisha fedha nyingi sana, Mabilioni ya dola yanawekwa pale ili kuyatoa hayo mafuta na gesi.

Mheshimiwa Spika, japo kuwa sisi wenyewe tumekubaliana kwamba kila upande unajitegemea, sasa suala la mafuta ya gesi ni suala linalohusisha fedha nyingi sana, Mabilioni ya dola yanawekwa pale ili kuyatoa hayo mafuta na gesi.

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza mwekezaji yeyote atakayefanya kama ataweka mabilioni yake anafanya *legislative review* anatazama Sheria, Katiba na

Mikataba yote kuangalia anawezaje kufanya hivyo. Na mtu mwekezaji wa Kimataifa ambaye anataka kuweka mabilioni hata fanya hivyo kama kuna kuwa kuna tatizo kama hili. Kwasababu ukiangalia kikatiba suala hili bado ni la Muungano. Sheria zipo zinazosema kwamba inaruhusu upande wa pili na makubaliano ya Kiserikali mambo ya pili yaendeleo.

Mheshimiwa Spika, sasa kuna mgongano hapo bila huu mgongano kuurejebisha hakuna mwekezaji wa fedha nyingi atakayeweza kuweka fedha upande wa pili wa Muungano wa Zanzibar. Huku ipo bayana upande wa pili itashindikana, ningependa tu kumuomba Mheshimiwa Waziri alitazame hili hasa katika kipindi hiki ambacho fursa hii itakuwa moto, alitazame ajue jinsi gani tutalifanyia ufumbuzi suala hili kwa haraka iwezekanavyo ili uwekezaji mkubwa ule ambao tunautaka uweze kufanyika upande wa pili wa Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache ningependa tu kumshukuru tena Mheshimiwa Waziri kwa uwasilishaji mzuri na ningependa atoe maelezo katika hili ambalo nimeliweka hapa hadharani, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Abdullah Mwinyi kwa mchango wako, Mheshimiwa Ally Makoa nilishakutaja, atafuatiwa na Mheshimiwa Omar Ali Omar na Mheshimiwa Ali Hassan Omar King ajiandae.

**MHE. ALLY J. MAKOA:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii lakini niwapongeze Mheshimiwa Jafo na Mheshimiwa Chande kwa wasilisho lililo zuri kabisa kwenye bajeti yao. Nilikuwa naomba nichangie eneo dogo la mazingira wewe unafahamu mji wa Kondoa umekatiza mto mkubwa pale, sasa mto ule umehama kutoka njia yake ya asili kwenda mto mkondo mdogo.

Mheshimiwa Spika, huu ni msimu wa pili madhara yanayotokea kwenye mto ule ni makubwa sana nilikuwa naomba Wizara iweke fungu kwa ajili ya kuurudisha ule mto

kwenye mkondo wake wa asili. Kwasababu madhara ambayo yanatokea kwa hivi sasa kwanza maji ni mengi yana-*force* kuingia kwenye mkondo mdogo, mashamba ya watu yanaendelea kumegwa na maji yanaelekea kwenye nyumba za watu, kama hatujaudhibitwa kwa wakati mto ule maeneo ambayo yanakwenda kuathirika ni pamoja na shule za msingi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, shule ya msingi Mpalangwi eneo lote la kanisa la *Katholic* makaburi yaliyopo kule pamoja na Chuo cha Bustani, kwasababu mto wenyewe ule ni mdogo sana maji yanatafuta njia mbadala ya kupita, kwa sasa kwasababu ni mkondo mdogo maji yanaingia mashambani yanakwenda kuharibu mazao ya wananchi. Lakini sio hiyo tu miundombinu ya *TANESCO* pia ipo mashakani kwasababu zipo nguzo ambazo tayari na zenyewe zimekwisha kufikiwa na maji.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilikuwa naomba watenge fedha kwa ajili ya kurejesha ule mto katika chanzo chake cha asili. Aidha, Mheshimiwa Waziri aagize watu wa *NEMC* waende wakafanye tathmini mapema ili kuweza kuurejesha ule mto katika chanzo chake cha asili. Hasara nyingine inayojitokeza barabara ile inayotoka Iboni kuelekea Bolisa mpaka Gubali inakuwa haipitiki kwasababu Serikali itakuja kuingia gharama kubwa ya kujenga madaraja makubwa.

Mheshimiwa Spika, msimu wa mvua uliopita daraja ambalo lilijengwa na gharama kubwa na Serikali lilisombwa na maji zima zima kama lilivyo likahamishwa zaidi ya mita 200, kwa hiyo, pale fedha ya Serikali ilipotea kabla daraja halikuanza kujengwa, ni kwasababu ya nguvu ya maji ambayo ilikuwa inatoka kwenye mto mkubwa kwenda kwenye mto mdogo. Nilikuwa naomba tu eneo hili ili kuokoa hata shughuli za kiuchumi za wananchi wa kata ya Kondoa Mjini na Kata ya Bolisa kuelekea kata ya Kolo Gubadi zile barabara ili ziwe salama inabidi mto huu urejeshwe kwenye mkondo wake wa asili.



Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo ninakushukuru sana kwa nafasi hii ahsante sana naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Ally Makoa, nilishakutaja Mheshimiwa Omar Ali Omar utafuatiwa na Mheshimiwa Ali Hassan Omar King. Mheshimiwa Omar hayupo? haya tuendeleo Mheshimiwa King, Ahaa!! endelea nilikuwa sijakuona samahani.

**MHE. OMAR ALI OMAR:** Mheshimiwa Spika, nipo ahsante sana na mimi kunipa fursa ya kuchangia katika Wizara hii nyeti kabisa ya Muungano. Kwanza niwapongeze wote Mheshimiwa Waziri na Naibu wako, na zaidi nakupongeza zaidi Mheshimiwa Chande kwasababu ni mwenzangu ananijua tunajuana. Tunapiga shamvi pamoja katika maeneo yetu. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, lakini zaidi nijikite kwenye Wizara hii inayohusiana na mambo ya Muungano kwenye sehemu zaidi ya Elimu ya juu. Kama tunavyojua kwamba Wizara hii ni Wizara nyeti sana katika kujenga mustakabali wa Taifa letu. Kwa bahati nzuri ni mwalimu ninapotokea miaka 22 nimefundisha, na nimeona matokeo mengi ambayo tunapokuja kufanya kazi inayohusiana na mambo ya Muungano zaidi katika Wizara yetu ya Muungano kwenye Sekta ya Elimu kuna vitu ambavyo kidogo vinaleta ukanganyifu kwa sababu ni Wizara ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, maombi yangu, zaidi ni kwenye suala zima linalohusiana na watendaji, watendaji wanaotoka visiwani kuja kwa wenzetu huku bara, kuja kufanya shughuli nzima inayohusiana na shughuli za Muungano zaidi kwenye sekta hii inayohusiana na Elimu ambayo pia ni Wizara ya Muungano. Kwa kweli kwa upeo wangu nimeona kwamba mahusiano yetu yanakuja katika sekta nyingi sana zinazohusiana na Muungano. Nikiangalia katika sekta hii zaidi kwenye suala la upatikanaji wa *syllabus* ambazo tunakuwa tunakwenda nazo kule visiwani na bara kwa ujumla.

Tukiangalia kwenye *syllabus* zetu tunatakiwa tuwe na ulinganifu.

Mheshimiwa Spika, ulinganifu wetu unatakiwa kwenye *syllabus* ziwe zinalingana tokea *from standard one* au darasa la kwanza mpaka darasa la saba alafu tuje tuangalie *curriculum* yetu iendane sambamba na *curriculum* ile iliyopo bara ambayo ni ya kuanzia *form one* mpaka kufika madarasa ya juu zaidi *form six*.

Sasa hii ina ukanganifu mkubwa ukiangalia kwamba matokeo yanapotolewa wanafunzi wetu wengi wanakuwa wanafeli na wanafeli kwasababu mtaala unaotumika Zanzibar na Mtaala unaotumika huku Tanzania Bara unakuwa ni tofauti. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hii ni kuonyesha kwamba wanafunzi wetu wanaonekana kwamba siku zote wanashika nafasi ya mwisho zaidi Zanzibar, unasikia nafasi zile kumi za mwisho zinatoka Zanzibar, hii ni kwasababu kwamba sio kwamba wanafunzi hawana uwezo lakini wanauwezo mkubwa bali mitaala haiendi sambamba kwasababu kitengo kile kinachohusiana na elimu ya juu hakihusiana zaidi na kule Tanzania visiwani.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hili naomba sasa liangaliwe kwa kina kabisa ili kwamba mitaala yetu iende sambamba, kinachofanyika Tanzania visiwani *from standard one* hadi *standard seven* na sawasawa kiendane na bara na visiwani viwe ni vitu vinalingana, huo ndio mchango wangu siku ya leo kwenye suala zima la Muungano. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Nilikuwa bado nawaza habari ya kwamba alichangia Mheshimiwa mmoja, kwa mfano wa mama wawili; mmoja ametoka Shinyanga amenunua bidhaa Kariakoo anazipeleka bila tatizo lolote na ndio ukweli, halafu mwingine ametoka Zanzibar yeye anashughulishwa, nilikuwa najiuliza sababu yake ni nini? Kwasababu angalau basi bidhaa hizo zinazotoka Zanzibari kuja huku, kuna hilo sijui kodi zimefanyaje sijui nini na nini ambalo tunataka liwekwe sawa.

Lakini sasa hizo kodi zetu za bara hizo kubwa zimeshalipwa tayari, sasa mtu anapeleka mzigo Zanzibar yaani unamshughulisha kwa lipi yaani? Labda Waziri utatusaidia na hasa wale wa kitengo cha Muungano, haya ndio kilo mbili ya sukari yaani ni mambo yamesemwa humu bungeni kwa miaka, kwanini yasiishe haya mambo yakawekwa sawa tu vizuri, kwenye eneo la Muungano. Kama kweli bado yapo maana hatuna uhakika, Mheshimiwa Ali Hassan King. *(Makofi)*

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Spika, ahsante nashukuru kupata nafasi hii kwa ajili ya kuchangia katika Wizara yetu hii adhimu ni Wizara moja ambayo ina umuhimu mkubwa sana katika maisha yetu. Muungano wetu ni zaidi ya hapa ambapo kila mmoja wetu ametaja zile sifa.

Mheshimiwa Spika, nataka nimnukuu mwimbaji mmoja wa kizazi kipya anatokea kule Jang'ombe kwa Alinatu ni mtoto wa Khadija Kopa anaitwa Zuchu alisema kwamba "ladha yake msambaa shira ya kizanzibar" maana sasa hivi tayari... *(Makofi)*

**SPIKA:** Hebu iweke vizuri unajua Kiswahili huku bara na hasa Dodoma huku, ebu iweke vizuri tena amesemaje?

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Spika, anasema ladha yake msambaa shira ya kizanzibar, sasa maana yake kwamba tayari katika Muungano huu nikijamii zaidi tumeshachanganyika kiasi ambacho hata kubagua huwezi tena ni sawa sawa na mchanga ambao umeuchanganya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza niishukuru Wizara kwa kutaja haya mafanikio ambayo katika ukurasa wa 15 na 16 tulizungumza hapa mwaka juzi na mwaka jana, kwa kutosainiwa Mkataba wa SAUD BADEA ambao ulikuwa unahusisha shilingi za Kitanzania bilioni 26 kwa ajili ya barabara ya Chake Chake – Wete hivi sasa imeshasainiwa. Lakini pia tunashukuru kwa kusainiwa Mkataba pia wa Ukarabati wa Hospitali ya Mnazi Mmoja hilo nalo pia tunashukuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kupitia wewe kwanza nikushukuru wewe katika Bunge lako la 11 tulizungumzia hapa juu ya kutoa VAT katika umeme ambao TANESCO anauza kwa ZECO na kusamehewa deni la shilingi bilioni 22.9 na tulilizungumza hapa lakini tunashukuru Rais alilisikia na Mheshimiwa Rais Mungu amrehemu ampe mapokezi mema huko alipo, akasema analifuta deni lile na ile VAT imeondolewa, kwa hiyo, tunashukuru sana. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kuna neno moja ambalo ninataka niseme haya tunayoyasifu yote hapa leo na tunapata nguvu ya kuyasifu, huko nyuma tulikuwa tukiyataja kama ni changamoto na yalipofanyiwa kazi badala yake ndipo yamegeuka sasa yamekuwa ni sifa na yamekuwa ni ufanisi na yamekuwa mazuri na yanasifiwa kila mahali. Kwa hiyo, na haya ambayo tunayoyataja leo kama ni changamoto isionekane labda tunasema vitu vya ajabu, vitakapopatiwa ufumbuzi tutakuja kukaa katika wakati mwingine tutakuja kusifu kama ni mafanikio ambayo yamepatikana na kwasababu mwanzo tuliyataja kama changamoto. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunaomba Wizara ituchukuliwe, mimi ninaelezea changamoto moja, changamoto nayoelezea ni kuhusiana na bei ya umeme, lile jambo tulilozungumza kipindi kile lilikuwa lina *component* mbili; kulikuwa kuna VAT, lakini pia kulikuwa kuna bei ya umeme. Bei ya umeme ambayo TANESCO anaiuza ZECO ni bei ambayo ipo kubwa, bei ambayo inasababisha ZECO katika ku-*pack* zile bei za umeme aweze kuwafanyia wale wanaofanya biashara au watu wa viwanda apeleke mzigo mkubwa zaidi kwa kuwanusuru mtu mmoja mmoja au *individuals* ambao ni raia wa kawaida.

Mheshimiwa Spika, sasa bei ile inachosababisha; kama mtu ana kiwanda kule Zanzibar mfano kiwanda cha Soda *Zanzibar Bottlers*, na kama mtu ana kiwanda kule cha kukoboa kwa mfano kama vile *Zanzibar Milling* anaona bora atumie kiwanda kilichopo Tanzania Bara, na kile cha Zanzibar anakiacha kwasababu umeme analipa bei kubwa.

Mheshimiwa Spika sasa hicho ndicho kinachosababisha Zanzibar alikuwa na deni, pale wakati tunazungumza mwaka jana alikuwa na deni la shilingi bilioni 132, lakini deni hilo alilolikubali Zanzibar ni bilioni 65.7 ambapo hili amelipa bilioni 57.9, sasa limebakia takribani deni la bilioni saba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini deni ambalo Zanzibar hajalikuwani deni linalotokana na *kilowatt Amps* ambayo *per unit TANESCO* analuzia *ZECO* shilingi 16,000 lakini bei waliyokubaliana ni shilingi 8,000 ni *double* mara mbili zaidi. Kwa hiyo, hapo pana deni zaidi ya bilioni 66, sasa nini wazo langu ambalo ninalosema au maoni yangu au ushauri wangu, hili jambo katika ngazi ya watendaji alitujibu Waziri Mheshimiwa Kalemani mwaka jana kwamba tayari Wizara imekutana wameshazungumza wameshakubaliana lakini lipo katika *desk* la Muungano.

Mheshimiwa Spika, sasa tulikuwa tunaomba hili lifanyiwe kazi, na lifanyiwe kazi kwenye mambo mangapi? Kwenye mambo haya matatu ambayo ninayasema hapa sasa hivi, lifanyiwe kazi moja; hii bei ya *kilowatt amperes* ya 16,560 ibaki lilipwe lile lililokuwa la 8,647, ili hili lingine tunaomba lisamehewe. jingine bei ambayo imependekezwa sasa hivi na *EWURA* ya 157 ambayo ipo isitumike tunaomba bei ambayo *ZECO* wamependekeza ya kwa *unit* moja ikiwa ni *kilowatts per hour* 130 ikitumika bei hii itakuwa kutakuwa huko mbele hakuna mgogoro na hakutazalisha deni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ombi lingine la tatu kusamehewa kwa hizi Bilioni 66.5 kwasababu zimetokana na bei ambayo imekuwa *disputed* sasa hicho ndicho ambacho tulichokuja nacho, kwa hiyo hii ni changamoto, changamoto hii inafanya kwamba *ZECO* asiweze kuendelea kuuza umeme tujue maingira *ZECO* imeme anavyoununua, anavyoupokea, anavyoupoza, alafu anaupeleka kwa wanachi yeye mwenyewe. Ukimuzia kwa bei hii ambayo inafanana na ile ambayo mtu anapelekewa moja kwa moja nyumbani kwake au kiwandani kwake itakuwa haiwi-*fare price* na hapo ndipo kwenye mahusiano yetu na kuna kauli mbiu ambayo

imesemwa hapa katika sherehe hii ya Miaka 57 ya Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwamba Muungano wetu ni msingi imara wa mapinduzi ya kiuchumi kama ni msingi imara ya mapinduzi ya kiuchumi uchumi huu utatokana na viwanda vikifungwa viwanda Zanzibar msingi huo utakuwepo?

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Spika, nashukuru naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Ali Hassan Omar King kwa mchango wako, ila kitu kimoja haukusema tulipambana sana hapa bei wanayopewa *ZECO* ipungue mambo ya *VAT* na nini na nini na Mheshimiwa Dkt. Kalemani akashughulikia, likawa lakini *ZECO* hajawahi kupunguza bei kule kwa wazanzibar mmoja mmoja hilo nalo haujatupa mrejesho wake kwanini? Kwa hiyo, linatupa uvivu kidogo kuendelea kuweka presha endapo nae *ZECO* haonyeshi moja kwa moja kuna unafuu kwa watumiaji kule Zanzibar. Lakini wakati wa Bajeti ya Nishati basi amelisikia hili atusaidie Mheshimiwa Dkt. Kalemani kuliweka sawa mazungumzo haya yamefikwa wapi.

Waheshimiwa Wabunge uchangiaji wetu unaendelea vizuri bila tatizo lolote na nina nafasi nne tano kwa mwenye dukuduku yoyote ambaye anahisi angependa jioni ya leo aseme nitakapokaa hapa jioni basi niandikie ili tutambana bana Waziri dakika zake tutapata nafasi Waheshimiwa. Lakini jioni tutaanza na Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji, na Mheshimiwa Ameir Abdalla Ameir na Mheshimiwa Mwita Boniphace Getere watatanzishia maungumzo yetu jioni ya leo na hoja tutaihitimisha leo leo! *(Makofi)*

Kwa hatua hii basi ninaomba nisitize shughuli za Bunge hadi saa Kumi Kamili Jioni.

(Saa 7.02 Mchana Bunge lilitishwa hadi Saa Kumi Kamili Jioni)

(Saa 10.00 Jioni Bunge Lilirudia)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa Wabunge, majadiliano yanaendelea, nilishamtaja Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji atafuatiwa na Mheshimiwa Ameir Abdullah Ameir.

**MHE. MWANTUMU DAU HAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Awali ya yote, nimshukuru Mwenyezi Mungu kunijalia uzima na afya hata kurudi tena jioni hii na kuanza kuchangia hoja hii.

Mheshimiwa Spika, kwanza napongeza kusainiwa kwa hati tano za makubaliano ya kuondoa hoja za Muungano zilizopatiwa ufumbuzi mfano kushirikishwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwenye masuala ya kitaifa na kikanda. Suala hili tunashukuru sana kwamba limeondoa kero hizi na sasa hivi hivi tuko katika Muungano wa uhu na haki ambao hauwezi kupingika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nizungumzie kuhusu kuratibu masuala ya kiuchumi na kijamii hasa suala hili la *TASAF* Awamu hii ya Tatu. *TASAF* Awamu hii ya Tatu kuna jambo hawajalitekeleza na kipindi kile tulichopita walikuwa wanafanya semina kule Zanzibar na wanashirikisha Wakuu wa Mkoa, Wakuu wa Wilaya pamoja na viongozi wengine lakini pia walitushirikisha na sisi Wabunge wa Zanzibar tunapewa semina na kupata mafunzo elekezi ili kwenda kuwafanyia wajasiriamali. Kwa hiyo, naomba hizi semina zifanyike tena kwa hii awamu ya tatu na washirikishe viongozi kama vile walivyoshirikisha mwanzo.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie suala la mazingira. Kule kwetu katika Mkoa wetu wa Kusini kuna Kijiji kinaitwa Marumbi. Kijiji kile kutokana na tabianchi maji yakajaa hadi kufikia kubomoa makaburi kwa sababu kule wanazikia

maeneo pwani. Kwa hiyo, kutokana na tabianchi maji yalipanda juu na kuvunja makaburi yale. Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilichukua hatua lakini sehemu nyingine bado maji yanachimbuka. Kwa hiyo, naomba suala hili lifanyiwe kazi tena na kama kuna uwezekano Mheshimiwa Waziri tuungane twende katika Mkoa wa Kusini Kijiji cha Marumbi akaone hiki nachokiongelea ikiwa ni pamoja na upandaji wa koko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niendeleo kuchangia kuhusu suala la Bodi ya Mkopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu. Suala la mikopo ya elimu ya juu watoto wetu wanapokuwa wanataka mikopo hili suala linakuwa kubwa na linakuwa zito, wanahangaika kwa kuwaona kwa macho yetu mpaka wakaipata ile mikopo basi wanakuwa wako hoi. Kwa hiyo, naomba Bodi hii ifanye kazi zake vizuri, watoto wanapotaka mikopo ili kwenda kujisomea basi wafanyiwe kiurahisi. Wanapokwenda kule benki wasihangaika wapate pesa zao za mikopo na waende wakafanyie kazi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja asilimia mia. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji. Nilishamtaja Mheshimiwa Ameir Abdallah Ameir baada ya hapo tutakwenda Bara kwa Mheshimiwa Jackson Kiswaga.

**MHE. AMEIR ABDALLAH AMEIR:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametukutanisha hapa leo. Zaidi napenda kuwapongeza Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar ambao wamenipa imani kubwa na kunichagua kuweza kuliwakilisha Baraza katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile nitakuwa mtovu wa nidhamu kama sitawashukuru wananchi wa Jimbo langu walionichagua wa Jimbo la Mwanakwerekwe. Ni mara



yangu ya kwanza kuchangia humu ndani ndiyo maana natoa shukrani hizo.

Mheshimiwa Spika, niende katika mchango wangu na nitagusa mambo matatu. Kwanza nitagusia suala zima la historia ili watu wajue ni kwa kiasi gani huu Muungano una umuhimu katika maisha ya Watanzania kwa ujumla. Katika kipengele cha pili nitajaribu kueleza angalau mafanikio yaliyopatikana katika kila awamu; kuanzia awamu ya kwanza mpaka awamu ya tano ili pia tuone kwamba Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika suala zima la maendeleo ya kiuchumi linakua kwa hali ya juu.

Mheshimiwa Spika, katika historia mimi ni muumini wa faida kubwa zinazopatikana kutokana na Muungano huu. Naomba nitamke hilo wazi na sitatafuna maneno kwamba naziona faida kubwa zaidi na changamoto ambazo zinaelekea ukingoni katika kukamilishwa, kuratibiwa na kuondolewa kabisa. Nikianza katika historia yetu kidogo tu ni kwamba mahusiano ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar hayakuanza tarehe 26 Aprili, 1964 bali yalikuwa yameshajengeka tangu siku za nyuma. Kilele kile ilikuwa ni kuhitimisha tu lakini mahusiano ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar yalianza mbali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nieleze katika karne ya pili ambapo tulishuhudia biashara (*commercial contact*) ikifanyika baina ya Zanzibar na nchi zile za Uajemi kama Syria, Iraq, Iran ambao hawa sasa walileta bidhaa zao Zanzibar lakini zikifika Zanzibar zilikuwa zikiletwa maeneo ya ndani kwa Ndugu zetu huku Tanganyika tukishirikiana nao kwa pamoja. Kwa hiyo, hata suala la uchumi halikuanza leo; mashirikiano ya uchumi yalianza kipindi kirefu tangu siku za nyuma.

Mheshimiwa Spika, vilevile Profesa Felix Chami, Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam wakati anafanya utafiti wake wa *ecological excavation* katika eneo maarufu Zanzibar, Mkoa wa Kusini linaitwa Kuumbi *Cave*, naomba mnisikilize kwa makini sana Waheshimiwa Wabunge kuna jambo la msingi sana nataka kusema hapa; katika hili pango

Profesa aliweza kugundua kwamba binadamu pale aliishi miaka 30,000 iliyopita.

Vilevile iliweza kugundulika mifupa ya wanyama kama twiga, pundamilia na nyati. Sasa kwa akili ya kawaida unajiliza wanyama hawa wanapatikana *Tanzania Mainland* tu imekuwaje leo Profesa Chami katika utafiti wake akagundua wanyama wakubwa wakubwa walikuwa wanaishi maeneo ya Zanzibar. Hii ni kutokana na ile *theory* kwamba eneo lote hili lilikuwa moja lakini baadaye likatawanyika na likagawa visiwa vidogo vidogo vikiwemo vikubwa Zanzibar na vingine, nadhani jamani tumefahamiana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine Muungano huu wa Tanzania na Zanzibar naomba tuelewe kwamba ni wa kipekee sana ambapo ni nadra duniani kukuta Muungano umefanyika kwa siku 100 lakini Muungano wetu ulifanyika kwa siku 100 kama na siku 12 hivi kuonesha kwamba ulikuwa ni wa ridhaa, wa damu na wa udugu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, yalianza mashirikiano ya udugu, damu baadaye tukaja tukamalizia na suala la *documentation*. Msingi wa Muungano huu ni maridhiano na ridhaa na hiyari, kwa hiyo, ni vigumu sana kuona kwamba kuna siku Muungano huu utaweza kuvunjika, hilo jambo haliwezekani. Ni sawasawa na kusema mgonjwa wa akili achukue bunduki halafu apige mbu itawezekana wapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nachotaka kuzungumza ni kwamba tumepata baraka kubwa kutokana na Muungano huu, tumepata heshima kubwa duniani kutokana na Muungano huu, miungano mingi imeshavunjika lakini huu bado unadumu na unaendelea na utaendelea. Tumeona mfano Muungano wa Syria na Misri, tumeona Sudan ambayo imekatika na kuwa na Sudan ya Kusini na Sudan ya Kaskazini; tuna mifano mingi kama hiyo. Mfano mdogo tu *East Africa Community* tulianza nayo lakini baada ya muda ili- *collapse* kidogo kwa changamoto mbili, tatu ambazo hazikuwa-*handled* vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nawashukuru sana viongozi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwamba wanausimamia Muungano huu kidhati kabisa na tuna imani kubwa utadumu kwa maslahi ya pande zote mbili. Hakuna sababu hata moja ya mtu ambaye anatoka Tanganyika au *Tanzania Mainland* akamdharau mtu anayetoka Zanzibar Visiwani wala Zanzibar Visiwani akamdharau mtu ambaye anatoka *Tanzania Mainland* sote ni kitu kimoja.

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa, muda wako umeisha.

**MHE. AMEIR ABDALLAH AMEIR:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja asilimia mia moja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa kwa vile orodha yangu ni ndefu ni dakika tano tano sasa mnaofuata ili angalau mpate nafasi mlio wengi, jielekeze moja kwa moja. Niliahidi kuwaletea Bara sasa ni zamu ya Mheshimiwa Jackson Kiswaga na Mheshimwa Mwita Getere ajiandae.

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia mchana huu. Nafikiri kwansababu nilikaa Zanzibar ndiyo maana nimefuatia kuchangia baada ya watu wa Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama tunavyofahamu kwamba hali ya mazingira katika nchi yetu imeendelea kuharibika sana. Takwimu za dunia zinaonyesha kwamba joto katika miji mikubwa limeendelea kuongezeka sana. Tanzania kwa sababu bado tuna misitu mingi hatujaona yale matatizo makubwa. Nilikuwa na mambo mengi ya kuzungumza lakini kwa sababu ya muda nijielekeze tu moja kwa moja katika ushauri.

Mheshimiwa Spika, ushauri ambao nataka kutoa katika eneo hili la kutunza mazingira, kwanza elimu ya kutunza mazingira kwa Watanzania naomba itolewe kwa wingi sana kwa sababu hali inazidi kuwa mbaya. Sehemu nyingi ambazo zimeanza kuwa kame ni kwa sababu mazingira yameharibiwa mno ndiyo maana unakuta kwamba mimomonyoko inakuwa mikubwa, maji yameacha mkondo yameenda kwa wananchi. Nashauri elimu itolewe kwa wingi kwa sababu sioni kama Serikali inatilia mkazo sana eneo hili.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa kuna hii kawaida kwamba Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya wanafanya zoezi la kupanda miti kama 100 au 500 halafu vyombo vya habari vingi vinatangaza lakini hatutaki *popularity* ya aina hiyo. Namshauri Waziri wa Mazingira kwamba katika *KPA (Keep Performance Areas)* kwa hawa Wakuu wa Mikoa wape malengo ya kupanda miti kila mwaka na wapimwe kwa namna hiyo. Tunaona pale Tabora Mkuu wa Mkoa aliyekuwepo Bwana Mwanri ameubadilisha sana kwa sababu ali-*focus* sana katika kupanda miti. Kwa hiyo, kwa Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya iwe ni *KPA* yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo nataka kushauri katika kutunza mazingira tuongeze matumizi ya gesi lakini kama tutaweza tutoe ruzuku kwa vijijini. Kule vijijini tutoe ruzuku kidogo kwa sababu uwezo wa hawa watu wa vijijini kununua gesi ni kazi kubwa. Nashauri tufikirie kwa baadaye siyo sasa ili tutunze mazingira yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vilevile kumekuwa na ongezeko la kujenga kwenye miinuko katika miji, kwa mfano Iringa pale kuna miinuko lakini hata Morogoro pale Milima ya Uluguru unakuta watu wanajenga na Serikali ipo! Kwa nini Serikali isipige marufuku kwa sababu mazingira yanaendelea kuharibika na watu wanaangalia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia katika kutunza mazingira mashamba yaliyoko vijijini, kwa mfano kuna shamba pale

Uyole wakati niko pale Mbeya nilisikia watu wanasema hili shamba tunataka tuishauri Serikali ibadilishe kuwa viwanja, hapana! Siyo lazima tufanye hivyo. Unajua maeneo makubwa kama yale ni ya makimbilio, inaweza ikatokea vurugu huko mjini eneo kama lile linakuwa ni eneo la makimbilio. Kwa hiyo, wazo la kusema kwamba ufute shamba lililopo mjini siyo sawa. Kwani nani alisema mijini hatuwezi kuwa na mashamba, ni eneo zuri sana la makimbilio lakini ni *source* kubwa ya *oxygen*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo naliona sasa kumekuwa na ukataji mkubwa wa miti kiholela, watu wanachoma misitu lakini watu wanakata miti kiholela. Hawa Maafisa Misitu tumewaweka huko hawasimamii suala hili. Kwa hiyo, ni wajibu wetu kuhakikisha kwamba Maafisa hawa wanasimamia maana vinginevyo haya maeneo yatakwisha. Kwa mfano, mimi nina Kata za Kihanga na Wasa, miti kule imekuwa ikikatwa hovyoyovyoyo, Mkuu wa Wilaya na Afisa Misitu yupo na usiku wanasafirisha. Sasa mimi kama Mbunge siko tayari kuona misitu yangu inaharibika niondoke niache wananchi wakiwa katika hali ya ukame. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine Serikali iongeze maeneo ya uhifadhi. Tukifanya hivyo kwa kweli tutaweza kutunza mazingira na uharibifu wa mazingira tutaweza kuudhibiti. Kumekuwa na ukuaji wa miji, vijiji vinageuka kuwa miji na shughuli za kiuchumi zinaongezeka, kilimo cha kisasa kinaongezeka; hivi vitu vyote vinaharibu mazingira.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali iyazingatie haya niliyoshauri, nafikiri tukienda hivi tutakwenda vizuri. Ahsante sana kwa kunipa nafasi. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Jackson Kiswaga. Nilishakutaja Mheshimiwa Mwita Boniphace Getere, karibu sana, dakika tano.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Mimi nijielekeze tu kwenye suala la *NEMC*. Kwanza niwapongeze

Waziri wa Wizara hii, Mheshimiwa Jafo na mwenzake Chande na maafisa wake wote, wanafanyakazi nzuri na tunatumaini kwamba kazi yao itakuwa nzuri zaidi mbele tuendako. Mheshimiwa Jafo ni mzoefu, tuna uhakika ataendesha Wizara hii vizuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, sisi Watanzania wa Bara na Visiwani ni wamoja. Toka tumeunda Muungano wetu mwaka 1964 hatujaona kwamba tunabaguliwa. Isipokuwa kuna wanasiasa wenye uchochezi kwa matakwa yao lakini sisi ni wamoja. Kwa umoja wetu tuendeleo kupendana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna haja ya kushukuru sana Serikali ya Uingereza na huko tunakoenda tuendeleo kuwashukuru. Nasema hivyo kwa sababu gani? Kumbukumbu zinaonyesha mwaka Januari, 1964 wakati wa maasi ya lile Jeshi la *Tanganyika King's Rifles* tulizidiwa kabisa kwenye nchi yetu na pengine kipindi hicho Mwalimu angeondoka lakini kwa sababu wenzetu walitupa uhuru bila kinyongo alipoomba msaada walikuja wakatukomboa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwita Getere nadhani unge-*pick topic* nyingine.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, naendelea na agenda nyingine.

**SPIKA:** Ahsante.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, nizungumzie mambo ya *NEMC*. *NEMC* wanafanya *Environment Impact Assessment* ambayo ni Tathmini ya Mazingira lakini katika nchi yetu *NEMC* imekuwa kikwazo kikubwa sana cha maendeleo.

Mheshimiwa Spika, historia ya *NEMC* ilitoka Marekani mwaka 1969, wao walianzisha mambo haya baadaye wenyewe hata mikataba ya *NEMC* na mambo mengine ya mazingira hawaweki, lakini kwetu sisi *NEMC* imekuwa kikwazo

kikubwa sana. Naishauri Wizara na hasa watu wa *NEMC* tuangalie namna gani tuta-*handle* hii Tathimini za Mazingira kwenye mambo ya vijijini.

Mheshimiwa Spika, nataka kutoa mfano mmoja, leo ukitaka kuchimba kisima kijijini ni kazi ngumu sana. Kazi ngumu kuliko kawaida! Hata hivyo, vijijini huko tunapokwenda, mapipa ya mafuta ya ma-*petrol*/yamejaa kwenye majumba. Sasa sijui kipi tunataka kusaidia! Sijui tunachokisaidia ni kipi? Mabipa ya mafuta ya *petrol* na chupa zimejaa kwenye nyumba za watu na nyumba zinaungua, lakini leo mtu akitaka kujenga kisima hata *pump* moja ni kesi kubwa sana kuliko kawaida. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naishauri Wizara, mimi ni Mjumbe wa Kamati, tumezungumza kwenye Kamati kwamba tutungeneze utaratibu wa kuangalia tathmini ya mazingira kwenye miradi ambayo wananchi wana uwezo mdogo na wanaweza kuifanyia maendeleo. Tunacho-*encourage* hapa ni watu wapate maendeleo. Tunawasukuma watu wajenge wapate miradi ya kimaendeleo, lakini *NEMC* yenyewe inavunja haya maendeleo. Haileti hayo maendeleo.

Mheshimiwa Spika, tuna *stage* za *NEMC*, wana hatua nyingi za kufuata kwenye tathmini ya mazingira; kuna suala la *scoping*, kuna *screening*. *Screening* ndiyo ya kwanza, waangalie kama mazingira unayoyaona yanaweza kuathiri watu, wanyama na kadhalika?

Mheshimiwa Spika, leo hatua zote zinafuatwa. Ili upate kuchimba kisima cha mafuta, uwe na shilingi milioni tatu, shilingi milioni nne mpaka shilingi milioni 10. Unachimba saa ngapi? Mradi mdogo unahitaji kupata fedha; na fedha zenyewe wameelekeza kwa watu ambao ni wataalamu, waliopewa kufanya kazi hiyo. Wale wataalamu siyo kama Waingereza, siyo kama Wamarekani ni watu wengine wa nje; ukiwapa hela, hawana kitu cha upendo. Wanachohitaji ni hela. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana mradi wowote wa Tanzania ukifanyiwa tathmini ya kimazingira (*Environmental Impact Assessment*) hawaendi kufanya *review*. Hakuna *monitoring and review*. Wakishaandika kama wameuza, mkimalizana, wanaenda jumla, hawarudi tena. Watarudi kuja kusema oh, tunakufungia kwa sababu hujafanya jambo hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nawaomba Wizara ambayo ni ya Kamati ambayo nami nimo, kwamba waangalie hili jambo sana. Tumezungumza sana kwenye Kamati, waangalie namna ya kufanya, miradi midogo inayohitaji *screening*, inayoinahitaji tathmini ya mazingira ipunguziwe hiyo haja ili watu wapate mazingira ya kufanya kwenye jambo lao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine la kufanya ni sheria za mazingira. Kuna sheria inasema mita 200, kuna sheria ya maji mita 200, kuna sheria ya mita 60; sasa tueleweke kwamba tuna sheria gani tunatumia kwenye vyanzo vya maji? Ni mita 200 au ni mita 60? Sheria hizi za mazingira ziende kwenye kata, vijiji, vitongoji na kwenye halmashauri ili wananchi waweze kuona kwamba sheria hizi zinatumikaje kwenye jambo kama hili ambalo ni nzuri zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nilitaka kutoa hiyo historia ambayo ilikuwa imeipunguza, lakini nimeongea haya ambayo nimeeleweka.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwita Getere. Najua unaweza usiridhike kwa sababu hiyo, lakini nikwambie tu kwamba hata katika hotuba za Mwalimu, katika kitu kimoja ambacho anakiri kwamba ni *black spot* katika historia yetu, ni hilo la sisi kuja kusaidiwa na Waingereza baada ya kuwa tumepewa uhuru jana tu. Kwa hiyo, ndiyo maana hatupendi sana kulizungumzia, kwa sababu ni aibu. Ni kama mtu umeozeshwa mke, halafu umeshindwa, halafu tena una... ni



aibu kidogo. Ndiyo maana nikakuomba tusilizungumzie, maana yake... (*Kicheko*)

Maana tulipewa uhuru, halafu tukajikanyaga wenyewe, halafu tena ikabidi Waingereza warudi tena, sasa hayo jameshapitwa na wakati. Vinginevyo niko na wewe kwenye *NEMC* kujiangalia kwenye sheria zao za kuwezesha wananchi kuanzisha biashara fulani fulani ambazo zinahitaji tathmini ya athari za mazingira. Ni eneo lenye ukiritimba, lenye gharama kubwa, tunawaeleza kila wakati lakini huwa *NEMC* hawasikii.

Mheshimiwa Waziri *NEMC* hawasikii wasikudanganye. Katika watu wasiosikia ni *NEMC*. *NEMC* hawasikii; na wananisikia huko. Hawasikii hawa watu! *Petrol, diesel* ipo kila Kijiji; nchi hii ni kama ukiweka kiberiti inaweza ikalipuka yote, lakini hata kuweka utaratibu kule vijijini pakawa na vituo fulani fulani vya teknolojia fulani ambavyo vikaweza kutoa huduma hiyo, hawako tayari. Mpaka sijui atafute mtadhimini wa Chuo Kikuu, ana *degree* gani sijui aandike, afanye nini, hii biashara gani? (*Makofi*)

*NEMC* wabadilike, kama hawabadiliki, wajue kwamba sasa yuko Waziri mpya kijana, atawabadilisha.

Mheshimiwa Mwanaisha Ulenge, atafuatiwa na Mheshimiwa Issa Mchungahela.

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa nafasi hii ya kuchangia katika Wizara hii ya Makamu wa Rais, (Mazingira na Muungano). Awali ya yote nichukuwe fursa hii kuwapongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri, pamoja na Mwenyekiti wa Kamati husika. Naomba nichangie kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuna suala zima *disaster preparedness*. Tumesikia sasa hivi kwenye mitandao wakizungumzia suala nzima la *Cyclone* ya Jobo, lakini hii inatokana na sawa sawa na yaliyosemwa kwenye ripoti ya *Intergovernmental Panel on Climate to Change (IPCC)*

ambayo inazungumza suala zima la ongezeko la joto pamoja na ambazo zinaleta mvua nyingi, lakini imekuwa ni Mamlaka ya Hali ya Hewa peke yake inayoonekana inashikilia kidedea suala hili.

Mheshimiwa Spika, upande huu wa athari za mazingira zinazotokana na mvua nyingi na kupelekea mafuriko, upande huu wa Wizara hii ya Mazingira haitoi ushirikiano wa bega kwa bega na hali ya hewa kuhakikisha kwamba wananchi wanaandaliwa kwa hali kama hizi za mabadiliko ya hali ya nchi ili kuendelea kuishi salama hasa wananchi wanaoishi pembezoni mwa Bahari za Hindi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, jambo hili ni la muhimu sana kwa sababu imeshatokea, maeneo ya karibu na bahari yanamomonyoka. Kwa mfano, Chuo cha Mwalimu Julius Nyerere pale Kigamboni, ilitokea ndani ya *Dar es Salaam Road* mpaka kile chuo kikataka kuezuliwa. Kwa hiyo, suala hili ni muhimu kabisa, kuandaa wananchi waishio pembezoni mwa bahari ili kuweza kujikinga na vimbunga hivyo vinavyoweza kutokea.

Mheshimiwa Spika, naomba pia kuchangia kuhusiana na kumomonyoka kwa Kisiwa cha *Toten* kilichopo Mkoani Tanga. Tanga tumebarikiwa, tuna kisiwa kizuri na Mamlaka ya Bandari wanakitumia kisiwa kile, wametengeneza mnara unaoongoza meli unaoitwa mnara wa Ulenge juu ya kisiwa kile, lakini kisiwa kile kina *erode* na hakuna *measures* zozote ambazo zinachukuliwa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, naiomba Sekta ya Mazingira ikashirikiane na Mamlaka ya Bandari itengeneze *shoreline protections* kwenye bahari zetu ili kuendelea kuvikinga visiwa vyetu pamoja na maeneo yaliyoko kwenye mwambao wa bahari. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, naomba pia nichangie kuhusiana na suala nzima la *asbestos*. *NEMC* walishaweka hii sheria ya kwamba *asbestos* ni *harmful* kwa maisha ya binadamu, lakini

mpaka sasa yapo majengo mengi ambayo yameezekwa na *asbestos* na hata kwenye mabomba, *underground utilities* zipo ambazo ni za *asbestos*. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali ifanye *survey* ya kutosha ili kuweza kubaini majengo yote ambayo mpaka sasa yameezekwa na *asbestos* na itoe tamko rasmi kwa wanaoyamiliki ili kuweza kuezuliwa na kuangamiza *asbestos* zote nchini ili tuendelee kuishi tukiwa na afya njema. Ma-*technician* wetu, wahandisi wetu, wanakwenda kufanya kazi katika mazingira ambayo *asbestos* bado zipo. Ni hatari sana kwa afya zao. Naomba sana Waziri na Serikali ichukuwe hatua muhimu kwa ajili ya jambo hili. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine, naomba kuishauri sana Wizara ya Mazingira katika suala zima la ukataji miti ovyo. Tutafute njia mbadala ya kutengeneza mkaa. Zipo *research* nyingi ambazo zinaonyesha tunaweza kutumia *sold waste* kutengeneza mkaa, kama *briquette*. Hizi *sold waste* zitakapoondolewa kwenye miji yetu, maana yake bado Sekta ya Mazingira inanufaika kwa miji yetu kuwa misafi na salama, lakini wakati huo huo tunapata *energymbadala* ya kuzalisha moto badala ya kukata miti ovyo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, pia umuhimu wa sisi kutengeneza mkaa kwa kutumia *sold waste*, itawapelekea wanaweke wetu wa vijijini waendeleo kupika hali ya kuwa wako watanashati kwa sababu kuni zinawafanya wawe wachafu kutokana na moto. Kwa hiyo, naomba sana tufike wakati tutengeneze mkaa kutokana na takataka tunazozialisha katika majumba yetu.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naunga mkono hoja. (Makofi)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa *Eng.* Mwanaisha Ulenge. Ni kweli hizi *asbestos* zipo tena mengine kwenye majengo ya Serikali. Kwa hiyo, ni vizuri Mheshimiwa Waziri aingilie kati hili eneo. Kama ni kweli yana athari kwa maisha ya binadamu, basi tuchukulie hatua.

Mheshimiwa Issa Mchungahela, atafuatiwa na Mheshimiwa Latifa Juwakali.

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehema kwa kuniwezesha kuwa hai hivi leo na kuchangia hoja hii ambayo ni hoja muhimu sana. Pia nawashukuru wale wote waliowezesha kwa namna moja ama nyingine kunifanya nikachangia hivi leo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nataka nizungumzie hali halisi ya mazingira ambayo nafikiri kwa namna moja au nyingine Serikali haijafanya jitihada za kutosha sana kuangalia hiyo halisi na kuangalia jinsi gani ya kutatua tatizo hili la mazingira.

Mheshimiwa Spika, mfano katika mji wa Dar es Salaam, tafiti zinatonyesha kwamba tani 5,600 za uchafu zinazalishwa; na uchafu wenyewe umejikita sana kwenye takataka za *plastic*. Pia tafiti hizo hizo zinatuonyesha kwamba asilimia 30 mpaka 40 ya taka ngumu zinakuwa ndiyo peke yake zinaweza kupelekwa maeneo ya kutupa (*dump*) na dampo kwa Dar es Salaam liko moja tu, Pugu Kinyamwezi. Sasa ukiangalia asilimia iliyobakia ni takataka ambazo zenyewe hazina uhakika wa kwamba zinapelekwa wapi. Unaweza ukaona kwa jinsi gani hali ilivyokuwa ngumu hapo.

Mheshimiwa Spika, hali halisi pia inaonyesha kwamba kwenye *beach* za Mkoa wa Dar es Salaam kuna takataka takribani mifuko 150 mpaka mifuko 200 ambazo zinatolewa kila siku, yaani wale watu wanaojishughulisha na utoawaji wa taka, kila siku wanafanya kazi ya kutoa uchafu huo. Katika hali hiyo, tunahitaji kujielekeza sana kwenye jitihada ya kuzoa takataka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jitihada ambayo nayotaka ni-*stick*, ziko mbili ya kwanza kabisa ni kwenye suala la elimu. Tumejikita sana katika utatuzi wa kutengeneza miundombinu mikubwa mikubwa. Tnafikiria vitu vikubwa badala ya kufikiria vitu vidogo ambavyo vitatuwezesha kufanya suala hili kwa umakini kabisa. Kama tumeamua kutoa elimu, basi tuelekeze elimu yetu kwa sehemu kubwa kabisa kwa vijana, kwenye shule za msingi.

Mheshimiwa Spika, nashauri moja kwa moja tuwe na somo la mazingira. Lichukuliwe kama ni somo linafundishwa kuanzia Darasa la Kwanza, kwa sababu tunajua vijana wadogo ndio wanaoweza ku-*pick* suala lolote kwa uharaka zaidi. Wanajifunza kwa uharaka zaidi na kulitendea kazi; na kwa sababu wao ndio wenye nchi yao au dunia yao ya kesho; kwa sababu siyo dunia yetu, ni dunia yao wao, kwa hiyo, tukiwafundisha wao nafikiri itakuwa vizuri zaidi. Tutumie fedha nyingi katika eneo hili.

Mheshimiwa Spika, sehemu nyingine nashauri tuwamilikishe uchafu wale wanaotengeneza uchafu. Kama tutafanya jitihada hii, tutahakikisha kwamba mazingira yanakuwa safi. Hapa najaribu kuzungumzia kitu gani? Kwa mfano, tunajua kuna watu wanatengeneza maji, wanatengeneza *juice*, lakini kiuhalisia siyo kwamba wanatengeneza maji, isipokuwa wanatengeneza uchafu wa *plastic*, vile vifaa wanavyovitumia katika kuweka hayo maji au kuweka hivyo vitu vingine.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, lazima tufanye jitihada kuwamilikisha uchafu. Katika njia gani? Kuwaambia kwamba uchafu ule ni mali yao, wahakikishe kwamba kwa namna moja au nyingine, uchafu wowote utakaonekana sehemu yoyote ile unawahusu wao. Nao lazima wawajibike katika kuhakikisha uchafu ule wanauondoa. Kwa hiyo, njia mojawapo ni kuweka bei, kwa mfano bei ya maji shilingi 600, lakini iwekwe kama shilingi 100 iwe ni pesa ku-*retain* ule uchafu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mtu anayekuja kununua maji, ananunua kwa shilingi 600 lakini shilingi 100 ni gharama ya kutolea uchafu pale. Kwa hiyo, nafikiri kwa namna hiyo tunaweza kuwa na uhakika wa kuondoa uchafu ambao unazagaa kiholela.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ninalotaka kuzungumza ni kuhusu sera. Sera zetu lazima zihakikishe zinaangalia ajira za watu wa kutoa uchafu zinathaminiwa. Tuhakikishe kwamba kwa namna moja ama nyingine watoa uchafu wanaajiriwa kwa kuwawezesha kwenye miradi midogo midogo.

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Latifa Juwakali nilishakutaja, utafuatiwa na Mheshimiwa Anastazia Wambura.

**MHE. LATIFA KHAMIS JUWAKALI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia katika hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, (Muungano na Mazingira). Nami niungane na wenzangu kwa kuendelea kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa kazi kubwa ambayo anaendelea kuifanya.

Mheshimiwa Spika, pia naomba nichukuwe nafasi hii kumpongeza sana Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kusema kwamba ataendelea kuulinda na kuutetea Muungano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nami nataka niseme nasi vijana tuko nyuma yako mama, tutaendelea kuulinda, kuutetea kuupigania Muungano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kusema Muungano wetu huu ni tunu na tunasema tunu hulindwa, tunu hutetewa, tunu hupiganiwa; kwa hiyo, nasi kama Watanzania maana yake ni kwamba wajibu wetu ni kuendelea kuulinda kutetea na kupigania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba ninukuu maneno ya Rais wetu kipenzi chetu Hayati Dkt. John Joseph Pombe Magufuli alivyokuja kuliutubia Bunge letu hili la Kumi na Mbili. Alisema; "Muungano wa Tanzania ni Muungano wa hiari na umetokana na mambo makuu manne." Jambo la kwanza alisema, maono ya waasisi wa Taifa letu, ambaye ni Hayati Abeid Amani Karume pamoja na Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere; jambo la pili, alisema Muungano huu ulisababishwa na utengamano na ukaribu wa kijiografia kwa Tanzania Bara yaani Tanganyika na Tanzania Zanzibar na kwa sasa tunaita Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sipendi sana kuita Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar, napenda nitumie Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

**SPIKA:** Kazi iendelee. *(Kicheko)*

**MHE. LATIFA KHAMIS JUWAKALI:** Mheshimiwa Spika, jambo la tatu alisema kwamba uhusiano wa kidugu na urafiki baina na wananchi wa Zanzibar na Tanganyika. Sote tunaona, anayeishi Tanzania Bara na anayeishi Tanzania Zanzibar, karibu sote ni ndugu. Kama huna udugu wa kidamu, basi hata udugu wa kuoana.

Waheshimiwa Wabunge, waliotangulia humu, wengi wamejinasibu, wamesema, wapo ambao wanatoka Zanzibar, lakini wana wake Ukerewe, wameoa wengine Kigoma na maeneo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la nne lilikuwa ni uhusiano wa kirafiki na ukaribu uliokuwepo...

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, anayeongea sasa hivi, Mheshimiwa Latifa Juwakali ni Mbunge wa Viti Maalum, ambaye ameshawahi kukimbiza Mwenge wa Uhuru. Kwa hiyo, anajua vizuri majimbo yenu yote na hata kule Kongwa alifika. *(Makofi)*

Endelea kuchangia Mheshimiwa Latifa. Anaelewa maana ya Muungano ni nini?

**MHE. LATIFA KHAMIS JUWAKALI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Jambo la nne ni uhusiano wa kirafiki na ukaribu uliopo kati ya vyama vya TANU kwa upande wa Tanganyika na ACP kwa upande wa Zanzibar. Kwa mantiki hiyo, inaonyesha ni jinsi gani huu Muungano ulikuwa ni Muungano wa hiari na Muungano ambao umeweza kuwaunganisha baina ya pande mbili; Zanzibar na Tanzania Bara.

Mheshimiwa Spika, nimeanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Jana tulikuwa tuna kongamano pale na kongamano hili lilikuwa ni kuadhimisha miaka 57 ya Muungano, lakini yeye mwenyewe alikuwa ni shahidi, siyo matarajio kwamba wazee ndiyo watatangulia sisi vijana tutabakia, lakini hata hilo linawezekana, wazee wanaweza wakatangulia, vijana tukabakia au vijana tukatangulia na wazee wakabakia.

Mheshimiwa Spika, kuna kitu ambacho kinanisikitisha sana; leo nchi hii vijana wako wengi sana, lakini kama utakwenda katika vijana kumi uwasimamishe vijana watano wakuelezee historia au wakuambie wanaufahamu vipi Muungano, *it is so bad*, hawawezi kukuelezea historia ya Muungano. Kwa mantiki hii sasa...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. LATIFA KHAMIS JUWAKALI:** Mheshimiwa Spika, naomba uniongezee dakika moja.

**SPIKA:** Endelea.



**MHE. LATIFA KHAMIS JUWAKALI:** Mheshimiwa Spika, kwa mantiki hii, namwomba sana Mheshimiwa Waziri, mbali ya kazi nyingi ambazo anaendelea kuzifanya, waandae mpango maalum wa kuweza kuwasaidia vijana wetu ili waweze kuufahamu Muungano vizuri. Waswahili wanasema unachokijua ndicho unachoweza kukifafanua na ndiyo maana minong'ono mingi inakuwa huku, muda mwingine watu wanafuata mkumbo, vijana wanafuata mkumbo, maana yake kuna kero za Muungano, kuna faida za Muungano, hawaelewi. Kero zilikuwepo lakini nyingine zilishachanganuliwa.

Mheshimiwa Spika, hawa watu au vijana kama watakuwa wana uelewa wa kutosha itawasaidia wao sasa kusimama na kuweza kujenga hoja; kweli tuna Muungano, lakini kero zilikuwa hizi na faida ziko hizi. Naomba sana Mheshimiwa Waziri kama vijana wanasimamishwa kule shuleni, tunafanya *debates* za mada nyingine, hata na hii iwe miongoni mwa ajenda ya kuipeleka katika shule ili iweze kuwasaidia vijana wetu waweze kujua Muungano ni nini na kuweza kuusimamia na kuulinda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Latifa Juwakali kwa mchango wako mzuri.

Waheshimiwa Wabunge, nimesimama kwa kuwapa tangazo kidogo, maana tangazo hili ni muhimu sana. Wengi wenu mmekuwa mkiniuliza hivi mbona siku zinakwenda Mheshimiwa Waziri Mkuu hatuelewelewi kuhusu futari ya Waziri Mkuu. (*Makofi*)

Sasa naomba niwaambie kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu anawaalika kwa futari ambayo sasa anawaomba msiandae majumbani kwenu, kesho. (*Makofi*)

Baada ya kuhitimisha hoja ya kesho jioni, basi Futari ya Mheshimiwa Waziri Mkuu itafuata hapahapa katika viwanja vyetu. Nimeona niwatangazie mapema ili msiandae,

yaani kama unaandaa andaa daku, lakini futari usiandae nyumbani. Nadhani tumeelewana katika hilo. Pia Mheshimiwa Mchungaji Gwajima, unakaribishwa. (*Kicheko*)

Natangaza futari ya Waziri Mkuu ananiuliza na ya Spika lini? Tunakwenda kwa utaratibu, ngoja aanze Waziri Mkuu kwanza. (*Kicheko*)

Tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa heshima hiyo na kwa kweli kesho, basi kesho jioni mje na hijabu na kanzu kwa wingi kwenye *session* ya jioni. (*Kicheko/ Makofi*)

Ahsante sana. Mheshimiwa Anastazia Wambura nilishakutaja, halafu Mheshimiwa Maalim Mussa Hassan Mussa.

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia jioni hii.

Mheshimiwa Spika, nimeomba maalum kwa ajili ya wananchi wa Kata ya Mayanga katika Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara na ni kuhusu malalamiko makubwa ambayo yanatokana na uchafuzi wa mazingira unaotokana na Kiwanda cha Simenti cha Dangote. Nitakwenda moja kwa moja, labda kama muda utaruhusu basi naweza nikaongea jambo lingine.

Mheshimiwa Spika, haya ni malalamiko ya muda mrefu na kwa taarifa ambazo nimezipata ni kwamba hata *NEMC* walishawahi kufika Dangote pale na waliwaandikia barua ili waweze kurekebisha hiyo hali. Kiwanda hiki cha Dangote ni kiwanda ambacho kipo katika Kata ya Mayanga, Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara.

Mheshimiwa Spika, mwanzoni wakati hiki kiwanda kinajengwa, tuliambiwa kwamba kutakuwepo na *mechanism* ambayo itakuwa inazuia zile *pollutants* kufika kwenye mazingira ya wananchi. Kwa bahati mbaya sasa,

mwanzoni kilipoanza tukawa tunapata taarifa kwamba, nyakati za usiku unatoka moshi na vumbi lingi sana, tena wanasubiri nyakati za usiku ndipo hali hii inatokea, lakini imeendelea hivyo na baadaye sasa tunaona hata mchana hali hii inajitokeza.

Mheshimiwa Spika, sasa *NEMC* kwa taarifa hizo ni kwamba wameshapeleka barua Dangote, lakini mpaka sasa bado hali ni ileile. Kwa bahati mbaya ni kwamba wananchi wanapoonaa hali inazidi kuendelea wanaamua kwenda pale Dangote ili waonane na uongozi, lakini bahati mbaya tena zaidi ni kwamba wanazuliwa getini, hawawezi kuonana na uongozi.

Mheshimiwa Spika, ni ombi langu kwamba Waziri, Mheshimiwa Jafo pengine na Naibu wake, walifanyie kazi hili. Wafike pale waonane na wananchi ili waweze kuwaeleza hali halisi. Hata hivyo, naomba zaidi sana hatua za haraka zichukuliwe ili kuweza kunusuru mazingira haya ambayo yanachafuliwa. Kwa kweli hali ni mbaya sana.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa muda unaruhusu, nimpongeze sana Mheshimiwa Rais, mama Samia Suluhu Hassan, kwa kupata nafasi ya kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mujibu wa Katiba. Nimpongeze sana kwamba jana tumesikia ametoa msamaha kwa wafungwa 5,000 na hii ina *implication* kwenye mazingira ya Magereza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tumpongeze sana kwa sababu wafungwa wanaposongamana magerezani inaharibu pia mazingira ya magerezani na kuharibu pia afya zao. Kwa hiyo tunamshukuru sana na tunampongeza kwa kufanya jambo hili.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze pia...

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Wambura anasema Mheshimiwa Rais amesamehe

wafungwa, siyo wale waliofungwa juzi pale Uwanja wa Benjamin Mkapa, hapana; wafungwa. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Wambura, endelea, nilikuwa nasisitiza unachokisema.

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kutoa ufafanuzi; ni kweli wengine wasingeweza kunielewa.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii pia kumpongeza sana Dkt. Philip Mpango kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Makamu wa Rais na kwa kupitishwa kwa kura nyingi sana na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Jafo na Naibu wake; tumewaona wakipita katika maeneo ya machimbo na kusisitiza hali ya kuzuia uchafuzi wa mazingira. Kwa hiyo naomba waendelee na kasi hiyo.

Mheshimiwa Spika, kama muda upo, nizungumzie kidogo kuhusiana na mabadiliko ya tabianchi ambapo tunaona sasa hivi mafuriko yanatokea mara kwa mara, wakati mwingine pia madaraja, barabara zinakatika. Nitoe mapendekezo kwa Serikali, mipango miji; tumezoea kuona wenzetu wa mipango miji wanatandika jamvi la viwanja. Inaweza ikatoka wilaya moja hadi nyingine, hakuna nafasi hapo katikati ya kuruhusu *water sinks*.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nipendekeze kwamba, wanapopanga mipango miji na kukata viwanja basi wawe na tabia sasa ya kuona kwamba mafuriko yanaweza yakatokea, kwa hiyo waache sehemu ambazo mvua zikinyesha zitapokea maji kwa sababu sehemu kubwa itakuwa imefunikwa na mapaa ya nyumba.

Mheshimiwa Spika, kwenye upande wa miundombinu tubadilishe sasa *standards* tuongeze viwango vya barabara zetu, viwango vya madaraja, ili yaweze kuwa imara kuhimili mafuriko.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Anastazia Wambura. Mheshimiwa Maalim Mussa Hassan Mussa.

**MHE. MUSSA HASSAN MUSSA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba ya Wizara ambayo imewasilishwa asubuhi hii. Kwanza, nimpongeze sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mama Samia Suluhu Hassan, kwa namna ya maoni yake na uoni wake na maneno yake. Mheshimiwa Samia amenikosha sana kusema kwamba yeye na Hayati Dkt. Magufuli ni kitu kimoja. Hii ni kuonesha kwamba ile shughuli ambayo alikuwa anaifanya basi yeye ataiendeleza na kwa kweli yote ni mema.

Mheshimiwa Spika, jana tu nimemsikia Makamu wa Rais anasema kwamba hana msamaha na mtu yeyote ambaye atachezea Muungano wa Jamhuri ya Muungano. Sasa nataka nimseme Waziri, namsema kwa nia njema kabisa; muda mfupi tu kuteuliwa Waziri, Mheshimiwa Jafo, tayari amefanya ziara Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge, sisi tulikuwa tuna kitu choyo tunapoambiwa huyu ni Mbunge, pia ni Diwani katika halmashauri yake, kitu hiki kwetu hakipo. Athari yake ni nini? Mbunge anashindwa kushiriki kuona miradi ya maendeleo ndani ya jimbo lake, ile iko kwenye halmashauri na anayeshiriki pale ni Diwani, basi.

Mheshimiwa Spika, sasa katika kuweka mambo haya kuwa mema, tulitazame hilo. Kwa upande wa kwetu kule tutafanya hivyo lakini kwa sababu itakuwa ni sheria basi na hapa najaribu kuwachombeza Waheshimiwa Wabunge tufanye hivyo.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge, kama hilo halitoshi, tunapozungumza suala la Muungano tumekubaliana wote kwamba Muungano ni Tunu ya Nchi yetu na Muungano huu tunapoita Tanzania chanzo chake ni

Tanganyika na Zanzibar, bila Zanzibar kulikuwa hakuna neno Tanzania. Sasa neno Tanzania ni tunu na lazima tulidumishe lidumu.

Mheshimiwa Spika, cha msingi, Zanzibar imetoka wapi? Zanzibar huru imetoka kwenye Mapinduzi ya tarehe 12, Januari, 1964. Ukienda ndani, Zanzibar imetokana na nani? Wazanzibari watatu; Karume, Thabit Kombo, Hamid Ameir na mwingine anatiliwa kwamba yuko upande mmoja Bara, mmoja Zanzibar, lakini waliobakia wote ni watu kutoka Bara. Hizi tofauti zinatoka wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, waliofanya mapinduzi pale, kuna mtu anaitwa Edington Kisasi, Mchaga; Hamis Daruweshi, mtu wa Songea; Natepe, mtu wa Kusini Lindi; hao ndio waliofanya Mapinduzi ya Zanzibar na ikawa Zanzibar huru na Muungano umekuja kwa Zanzibar ambayo imeshakuwa huru na Tanganyika, ndiyo tukapata neno Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa vijana wenzangu, maana mimi bado kijana, nataka niwaambie; kama wazee wetu walifanya jitihada hiyo na nilikwishasema kwenye Bunge hili, kwamba barua imetoka tarehe 22, Aprili kwa marehemu mzee Lusinde ambaye yuko Dodoma, Mwenyezi Mungu amlaze mahali pema na mzee Moyo, wote wameshatangulia, wale kama ndio wameanzisha huu Muungano, sisi kwetu ni kuuendeleza. Sasa hii tofauti, huyu Mzanzibari, huyu nani, sasa sote hapa tuna jina moja, Watanzania. Mzanzibari au Muunguja na Mpemba ilikuwa pale miaka ya nyuma ya 1964, sasa sote ni Watanzania, tumeungana tuko katika nchi moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nataka kumwambia Ndugu yangu, Mheshimiwa Jafo; hebu atufanyie utaratibu katika uratibu wake wa Mfuko wa Jimbo. Wenzetu Bara wameshamaliza kutumia hela ya Mfuko wa Jimbo, sisi Zanzibar imetoka juzi baada ya yeye kwenda. Inazunguka sana. Hebu tuandae utaratibu wa kwamba ule Mfuko unapotoka sisi tuwe Zanzibar pale tuufanyie kazi, lakini umetoka juzi sisi tuko Bungeni, miezi mitatu.

Mheshimiwa Spika, ukimuuliza Mbunge wa *Mainland* huku atakwambia tayari amemaliza miradi yake. Sisi tuko hapa shughuli yenyewe bado, wengi wetu hatujaipokea.

Mheshimiwa Spika, huu muda wa leo, ni sawa. Nakushukuru sana na naunga mkono hoja; ahsante. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana kwa mchango wako mzuri Mheshimiwa Maalim Mussa.

Sasa mchangiaji wetu wa mwisho basi nimpe kutoka Pemba, Mheshimiwa Maryam Azan Mwinyi, Mbunge wa Viti Maalum, Pemba.

**MHE. MARYAM AZAN MWINYI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ambayo ni ya upendeleo, hasa kutoka Pemba. Kwa kuchangia hotuba ya Ofisi ya Makamu wa Rais ya Muungano, mimi hasa najikita katika mazingira.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Jamhuri ya Muungano imetoa mwongozo kufanya vikao katika taasisi mbili kutoka Zanzibar na kutoka Tanzania Bara ili vikao hivi viweze kuleta tija kwa Watanzania wote. Sasa tatizo ni hili ambalo vikao vinachelewa sana kufanywa katika Serikali zetu hizi mbili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vikao hivi vitasaidia kujadili pamoja mambo mengi na fursa nyingi za Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar, hasa kwenye miradi ya mazingira. Pia kuwe na ushirikiano wa kupatiwa taarifa ya Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar, vipi inanufaika katika mikataba ya mazingira inayoridhia ili taarifa hizo ziweze kuwasaidia wananchi wa Tanzania yote; Tanzania Zanzibar na Tanzania Bara.

Mheshimiwa Spika, wananchi hao waweze kufahamu fursa ambazo Serikali zetu zinaimarisha Muungano kwenye sekta ya mazingira. Kwa hiyo, tunamwomba Mheshimiwa Waziri katika Wizara hii alichukulie kuwa ni muhimu sana katika sekta hiyo ya kufanya vikao na kutoa taarifa katika nchi yetu

kwa Tanzania Bara na Tanzania Visiwani ili Muungano huu uzidi kudumu na kuimarishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana na naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Maryam Azan Mwinyi, tunakushukuru sana kwa mchango wako mzuri. Basi ukienda utusalimie Faida Bakari huko. *(Kicheko)*

Sasa moja kwa moja nimwite Mheshimiwa Naibu Waziri, ukitaka unaweza ukachangia hata hapohapo tu; una dakika kumi, halafu tumuachie Mheshimiwa Waziri, dakika 20.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa nafasi hii ya kutoa mawili, matatu kwa zile hoja ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge. Pia niwashukuru sana wale wote waliochangia katika mada hizi mbili, suala la Muungano na Mazingira kwenye Ofisi yetu. Nawashukuru sana kwa michango yenu mizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa muda siyo rafiki, naomba kwa ruhusa yako niende tu moja kwa moja kwa baadhi ya hoja ambazo zimetolewa na Wabunge, hasa kuhusu Muungano.

Mheshimiwa Spika, hoja ya kwanza ambayo imetolewa na Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud; Muungano umetimiza miaka 57. Pongezi zimepokelewa. Aidha, Serikali ya SMZ na Serikali ya SMT zinaendelea na jitihada za kutatua changamoto kumi za Muungano zilizobakia ambazo 15 tayari zimeshapatiwa ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, hoja yake ya pili ni ushauri; ametoa ushauri kuhusu kuimarisha na kudumisha Muungano. Ushauri umepokelewa. Aidha, Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan na Awamu ya Nane ya



Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya uongozi wa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi, zimeweka masuala hayo ya Muungano kwa nia moja vipaumbele vyake hivyo ni Serikali zote mbili kushirikiana katika kuzipatia ufumbuzi hizi kumi zilizobakia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hoja ambayo ameitoa Mheshimiwa Bakar Hamad Bakar kwamba kuenzi Muungano ni pamoja na kuwezesha viongozi wa Muungano huu, mfano Dkt. Omar Ali Juma; maoni yamepokelewa. Aidha, Serikali italifanyia kazi suala hili.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ambayo ameitoa Mheshimiwa Kassim Hassan Haji ni kuhusu Muungano wa Taasisi zetu za Zanzibar na zile za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama vile *TBS* na *ZBS* kule Zanzibar. Suala hili ushauri huu tumeuchukua kwa mikono miwili na hatua zimeanza huko nyuma kwasababu mwenyewe nilikuwepo *ZBS*, tumeshakaa vikao tofauti, mbalimbali kujadili suala hili hapa. Kwa hiyo, ushauri umechukuliwa na tutaufanyia kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia ipo hoja ya Mheshimiwa Mwanakhamis Kassim Said ambaye hoja yake alikuwa anatoa pongezi, pongezi hizo zimechukuliwa na zimezingatiwa na tutazifanyia kazi kwa kadri inavyowezekana.

Hoja nyingine ya Mheshimiwa Mwanakhamis, haikuwa zaidi nayo ni pongezi tu kwa Jamhuri ya Muungano na kudumisha Muungano wetu wa Tanzania.

Mheshimiwa Asia Abdugarimu Halamga, Mbunge Viti Maalum, pongezi zimepokelewa na tutazifanyia kazi. Suala linaloshughulikiwa na kamati ya pamoja ya *SMZ* na ya *SMT* zinashughulikiwa masuala ya muungano baada ya kukamilika Serikali itatoa taarifa kuhusu jambo hilo.

Mheshimiwa Spika, ipo hoja ya Mheshimiwa Omar Ali Omar Hafidh, yeye amesema tu Elimu ya Juu, sana sana

alizingumzia suala la mitaala kwamba hakuna mlingano mzuri kati ya mtaala unaotumika Zanzibar na ambao unatumika Tanzania Bara. Suala hili tumelichukua na tutalifanyia kazi, tutafuatilia kwa kadri inavyowezekana ili tuweze kulinganisha mitaala yetu hiyo, ili kusudi tija na mafanikio ya wanafunzi wetu yawe yanalingana. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, baada ya *summary* hiyo ambayo imetolewa na Waheshimiwa Wabunge katika Bunge lako hili Tukufu naomba tu niseme zipo changamoto kumi na tano ambazo zimeshapatiwa ufumbuzi na zimebakia changamoto kumi nazo kwa hakika karibuni kadri vikao vitakavyokaliwa na Serikali ufumbuzi wake utapatikana moja baada ya nyingine.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumze mambo mawili kuhusu muungano. Katika kipindi ambacho muungano unahitajiwa ama unahitajika zaidi Tanzania ni kipindi hiki. Hii ni kwasababu wapo maadui wengi wenye macho mabaya na makali wanaoutazama vibaya Muungano wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa hiyo, kipindi ambacho kinahitajika ni hiki, kwasababu hata wahenga wanasema Umoja ni Nguvu na Utengano ni Dhaifu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, na siku zote mbwa mwitu hula nyama ya kondoo aliyejitenga. Lakini jambo la pili, tuachane na wale watu ambao wana mawazo mgando ama fikra mgando kuhusu suala la muungano. Kwani hata ingekuwa ile tarehe 26 Aprili, 1964 wangeulizwa kuhusu Muungano basi wangejibu hayo hayo kwamba kwao Muungano usingefaa.

Mheshimiwa Spika, naomba niombe kwa Waheshimiwa Wabunge na Wananchi kwa jumla, mambo mawili tu; jambo la kwanza, kwa kuwa wapo watu wenye ujauzito wa mawazo kuhusu Muungano naomba tuwe madaktari wazuri sana wakuwafanyia tiba, upasuaji, taratibu kabisa ili wajifungue salama, wawe wanajua nini dhana ya muungano. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, lakini jambo la pili, ambalo naomba ni wale watu wenye *degree* zao, maarifa yao makubwa ambayo maarifa hayo tunatarajia yabakie ndani ya ubongo wao lakini kwa bahati mbaya maarifa hayo wanayahamisha na kuyapeleka kwenye matumbo yao. Ili kusudi kubomoa mwelekeo wa Jamhuri ya Muungano. Naomba watu hawa tuwaelimishe na naamini wataelimika inshallah.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo naomba nitoe shukrani kubwa kwa familia yangu, ambayo tulikesha pamoja katika kuandaa haya. Lakini pili nitoe shukrani kubwa sana kwa wapiga kura wangu wa Jimbo la Kojani kwa kuniwezesha kufika hapa leo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Nakushukuru sana, Mheshimiwa Naibu Waziri Chande, sasa nikuite Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Selemani Saidi Jafo, karibu sana uhitimishe hoja yako ili tuifanyie maamuzi, Mheshimiwa Waziri karibu sana.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, kwanza awali ya yote naomba kuchukua fursa hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu Mola ambaye ameniwezesha kuweza kuwasilisha hotuba hii hapa. Lakini hali kadhalika kusikiliza hoja za Wabunge, lakini pia kunipa uhai na afya njema. Jambo hilo ni kubwa sana kwangu na hakika Mwenyezi Mungu ahsante sana Mwenyezi Mungu wangu.

Mheshimiwa Spika, ningelipenda kuchukua fursa hii kumshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mama yetu Samia Suluhu Hassan kwa kuniamini kunipa dhamana ya kuhudumu katika Ofisi hii. Lakini nimshukuru Makamu wa Rais, Dkt. Isdor Mpango kwa maelekezo yake. Lakini kubwa zaidi naomba nimshukuru kwa dhati Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Majaliwa

Majaliwa, kwa maelekezo yake, Mheshimiwa Majaliwa ni mwalimu, naomba niwaambie kazi yake *professional* yake ni mwalimu lakini ni mwalimu wa kufundisha kweli kweli, Mheshimiwa Waziri Mkuu tunakushukuru sana sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini nikushukuru wewe kwa sababu umenipa fursa nimeweza kutoa hoja hapa lakini pia saa hizi kuweza kuhitimisha hoja yangu pamoja na Bunge lako Tukufu nakushukuru sana.

Mheshimiwa Spika, naomba kupeleka shukrani za dhiti kwa wazazi wangu, baba yangu mzee Saidi Ali Jafo Marehemu Mwenyezi Mungu ampatie pepo njema huko alipo lakini mama yangu mzazi Hadija Binti Mwalimu Madega kwa malezi mazuri sana ya kila siku na kuhakikisha kijana wao nafanya kazi kwa uadilifu. Ningelipenda kuchukua fursa hii kuishukuru sana familia yangu, Watoto wangu na Wake zangu wapenzi sana, nawapenda mno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, najua wakati mwingine wananimisi sana...

**SPIKA:** Jamani makofi haya yawe ya nia njema hayo.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:**...lakini kwa ajili ya majukumu ya Taifa letu ili liweze kusonga mbele.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, wangapi?

**SPIKA:** Na mmoja wa wake zake ni dada yangu, kwa hiyo shemeji yangu huyu bwana. *(Kicheko)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru sana Naibu wangu Hamad Hassan Chande kwa kazi kubwa ya kushirikiana ambapo tumefanya kazi kubwa kwa pamoja katika kipindi hiki kifupi cha kuhakikisha hotuba hii inafika hapa. Lakini nimshukuru Katibu Mkuu wangu sana

Mama yangu Mary Maganga kwa kazi kubwa, Naibu Katibu Mkuu Ndugu yangu Mohamed Abdul Hamis, lakini *Professor* Esnat ambaye yeye ndiyo Mwenyekiti wetu wa Bodi ya Wakurugenzi katika Baraza la Wahifadhi ya Mazingira, lakini Dkt. Samwel Mafungwa ambaye huyu ni Mtendaji Mkuu wa *NEMC*.

Mheshimiwa Spika, niwashukuru sana watendaji wote katika Ofisi ya Makamu ya Rais kwa kazi kubwa wanayofanya, hakika mmefanya kazi kubwa sana ya kujituma kipindi chote. Nipende kuchukua fursa hii kuwashukuru Kamati zangu za Bunge zile mbili zilizofanya kazi kubwa sana, Kamati ya Sheria na Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira. Lakini niwashukuru Wabunge wote waliochangia hapa ndani kwa michango yao mizuri sana. Wabunge wamekuwa mstari wa mbele kutusaidia sana kutuelekeza na kutushauri mambo mbalimbali hakika Wabunge tunawashukuru sana sana kwa michango yenu mizuri.

Mheshimiwa Spika, hoja yetu hii, nikushuru wewe kwasababu japo muda umekuwa mfupi lakini nimepata Wabunge wachangiaji kwa maneno takribani 26 na mmoja amechangia kwa maandishi. Hii inaonekana kwamba umetumia umahiri mkubwa sana kuhakikisha ndani ya muda mfupi wa Bunge wanapata fursa ya kuweza kuchangia hoja hii.

Mheshimiwa Spika, nimshukuru sana Naibu wangu, ameweza kutoa ufafanuzi katika maeneo mbalimbali hasa katika maeneo ya Muungano. Na hakika niseme kwamba kwa ujumla tumepokea maoni yote ya wajumbe na Wabunge wa Bunge hili. Lakini sisi jukumu letu kubwa sana ni kwenda kutekeleza kwa nguvu zote. Na bahati nzuri naomba niwahakikishie sisi wengine tutakuwa hatulali katika *agenda* hii.

Mheshimiwa Spika, tutahakikisha eneo la Muungano na Mazingira tunaenda kuweka *legacy* kama tulivyoweka huko nyuma katika maeneo mengine. Hili ni jukumu letu kubwa tunaenda kulifanya kwa nguvu zote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tumeweza kuona kwamba kulikuwa na suala zima la hoja kwamba Hospitali kuna suala zima la mikataba mingine inashindwa kusainiwa, tumeichukua hoja hii lakini naomba niwajulishe kwamba katika ule upande wa Hospitali ya Mnazi Mmoja na Ujenzi wa Barabara ya Chakechake mpaka Wete kule Pemba tayari jambo hili limeshafanyiwa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini niwaambie Waheshimiwa Wabunge licha ya haya mawili tayari yameshafanyiwa kazi lakini yote yaliyokuwa *pending* tutahakikisha na ndio maana nimefanya ziara mara mbili kule Zanzibar tayari kuhakikisha mambo yote yapo *pending* tunayafanyia kazi. Naomba muwe na imani ya kutosha kwamba tutaenda kuwashughulikia, changamoto zote za Muungano ambazo tunajua kwamba hili jambo litaweza kutatua matatizo ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, lakini kwenye suala zima la mfuko ule wa *TASAF* niwashukuru Wabunge wote wa Zanzibar, na juzi juzi nilikuwa natembelea miradi kule Zanzibar hasa miradi ya *TASAF* kwa kweli Miradi ya *TASAF* ya Zanzibar imefanya vizuri sana hasa katika upande wa majengo ya shule za sekondari na shule ya msingi. Lakini hali kadhalika vituo vya afya, na jukumu langu kubwa naomba niwahahakishie Wabunge mnaotoka upande wa Zanzibar katika upande wa miradi hii inayoelekea upande wa Zanzibar tutakuja kuisimamia kwa nguvu zote.

Mheshimiwa Spika, na miongoni mwa ziara yangu nitakuja kuifanya ni kutembelea miradi yote ya Muungano sambamba na miradi yote ya Mifuko ya Jimbo ambayo fedha zimepelekewa kwa ajili mfuko wa Jimbo. Na hili nitaomba Wabunge tushirikiane kwa pamoja nitakapokuja kule nitawajulisha tuweze kukagua miradi yetu ya Mfuko wa Jimbo uliokuwapo upande wa Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na ndiyo maana katika utekelezaji wa eneo hilo sasa hivi kiwango cha fedha kimeongezeka sasa kutoka shilingi bilioni 12 sasa Zanzibar katika kipindi

kinachofuata kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali yenye changamoto itapata takribani shilingi bilioni 36.7. Kwa hiyo, maeneo yote yenye changamoto tutahakikisha kwamba tunaenda kuyafanyia kazi. Kwa hiyo, zile sheria ndugu yangu ulizozungumza zote kwa kadri iwezekanavyo tutaenda kuzifanyia kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini katika suala zima la mfuko wa pamoja ni miongoni mwa kero au changamoto za muungano tutaenda kuzifanyia kazi, kwa hiyo ndugu zangu Wabunge naomba tuwe na subira tu katika maeneo hayo, yote tutaenda kuyafanyia kazi kwa kadri itakavyowezekana.

Mheshimiwa Spika, na katika upande wa Mazingira niwashukuru sana Wabunge wote mmejadili kwa kina *agenda* ya mazingira. Na hasa nikushukuru sana ulipozungumza suala zima ya ile mifuko mitatu ambayo ingeweza kutatua changamoto ya kimazingira, ni kweli mifuko hii ipo na bahati nzuri nchi mbalimbali wanatumia fursa hii ya mifuko hii. Wanatumia wanapata mafanikio makubwa sana na nikushukuru sana Mbunge mchango wako mkubwa sana, jambo hili tumelichukua kwa umoja wetu wote tutaenda kulifanyia kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, na hata hivyo, juhudi kubwa iliyofanyika mpaka hivi sasa kupitia *NEMC* na Wizarani hapa tumeshaanza kupata miradi mipya hivi sasa, takribani *tumeshasource* fedha zaidi ya Dola za Kimarekani Milioni Ishirini na Sita, Laki Tisa Arobaini na Saba, Mia Sita Arobaini ya Sita (\$26, 947,646) hii tayari ni kazi tayari imeshaanza kufanyika. Na nimetoa maelekezo kwa watendaji wangu pale nimewaambia sitaki watendaji wanaokaa bure bure nataka watendaji wanaofanya *resource mobilization*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nia yetu ni nini? Twende kupambana na suala zima la mabadiliko ya tabia nchi na eneo hili tutaenda kulifanyia kazi kwa nguvu zote. Na hata hivyo nitaomba sana wenzangu Waziri Wizara ya Fedha kama ulivyosema tutashirikiana kwa karibu. Vile vikwazo vyote

ambavyo vilikuwa ni changamoto kwa pamoja kama Serikali tutahakikisha suala zima la fedha zinazolingia basi ziweze kwenda kutekeleza miradi kama ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge aminini kwamba kipindi hiki tutahakikisha kwamba tunaenda kutekeleza utaratibu mzuri wa kwanza kupatikana fedha, la pili lakini kuhakikisha zile fedha zilizopatikana lazima ziende zikatekeleze Miradi ya Maendeleo. Hili ni jukumu letu kubwa tutaenda kulfanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, katika suala zima la mabadiliko ya tabia ya nchi tuseme kwamba tumejipanga na hasa maeneo ya fukwe ambayo sehemu zingine zimekatika. Na ndio maana Ofisi ya Makamu wa Rais imeanza kazi pale Dar es Salaam, eneo la barabara ya Barack Obama. Lakini hata hivyo kuna kazi kubwa inayoendelea kufanyika kule Pangani Tanga na maeneo mbalimbali hasa upande wa Zanzibar, ambao tumezungumza wazi kwamba kuna maeneo mengine yanamomonyoka, kwa hiyo ni jukumu letu kubwa kwamba tunahakikisha tunafanya kila liwezekanalo maeneo hasa yenye changamoto ya kimazingira twende tukalishughulikie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna yale maeneo ambayo yalizungumzwa wazi kwamba kuna baadhi ya maeneo hasa maeneo ya visiwa, visiwa ambavyo vipo hatarini katika kuzama na hili hatulitarajii ila tunaomba Mwenyezi Mungu atuepushe katika hilo. Kiwango cha maji kimeongezeka kweli katika bahari lakini kupitia Ofisi yetu tutajitahidi kufanya kila liwezekanalo kuhakikisha kupitia mifuko hii mitatu jinsi gani tunaweza kupata fedha za kusaidia maeneo yenye changamoto.

Mheshimiwa Spika, hili ndiyo jukumu letu kubwa tutaendelea kulfanyia, na hii nipende kusema kwamba ushauri wa kamati kama ulivyoshauri kama kwa ujumla wake tulivyosema kwamba tutajitahidi sana katika kuhakikisha kwamba tunafanyia kazi maeneo haya yote kwa ujumla



wake. Lengo ni kwamba wananchi wa maeneo ya Tanzania yote waweze kupata fursa ya kuona Serikali yao imeweza kuwahudumia kwa kadri ilivyoweza.

Mheshimiwa Spika, lakini kuna mambo mengi yamejitokeza na mambo haya imeonekana ni suala la elimu. Ni kweli elimu ni changamoto lakini katika maeneo yote mawili, upande wa Muungano kuelewa lakini upande wa Mazingira na ndiyo maana watu waliofuatilia jana tukio la jana tulifanya lile makusudi, lengo letu ni kwamba tuweze kutumia rasilimali chache katika upelekaji wa elimu. Tumeanza mwaka huu tumeweza kutoa elimu katika utaratibu wa makongamano lakini hata hivyo lengo letu kubwa ni kuhakikisha elimu hii tunaianza kuipandikiza kwa Watoto wetu wa shule za msingi na shule za sekondari.

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana nimeelekeza katika Ofisi yetu suala zima la muungano tunaenda kuendesha mashindano ya insha kwa wanafunzi wa Shule za Msingi na Shule za Sekondari. Na hao wanafunzi watakaofanya vizuri lengo ni tuwape zawadi nzuri. Lengo ni kwamba kupitia insha itasaidia sana kuweka *knowledge* ya watoto kuelewa suala zima la muungano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini katika suala zima, mpango kabambe wa *agenda* ya kuhakikisha kwamba suala la mazingira, Wabunge wote mliojadili suala la mazingira ni kweli tatizo la mazingira ni kubwa mno, lakini jambo hili lazima *awareness* iwe ya kutosha. Lakini tuwe na jinsi gani mkakati wa kutosha kila mmoja wetu aweze kushiriki, ndiyo maana kupitia Ofisi yetu mwaka huu nimezungumza katika hotuba yangu mnamo tarehe 5 Juni, Tanzania tunaenda kufanya kitu cha kwanza ambacho hakijawahi kufanyika nchini mwetu, hili ni jambo gani? Tunaenda *kuya-group* yale mambo yote mliyozungumza humu katika jambo moja inaitwa kampeni kabambe ya kimazingira ndani ya Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika kampeni hiyo hatuachi mtu, kampeni hiyo tunaenda kuishindanisha mikoa kwa viashiria vyote tutakavyoviweka. Mifuko ya plastiki, upandaji wa miti,

utengenezaji usafi. Kwa hiyo, mikoa yote itashindana. Tutashindanisha Halmashauri za Miji yote, Majiji yote, Halmashauri za Wilaya, tutashindanisha kata mpaka mitaa mpaka vijiji. Na tutataka tuwape Wabunge tuzo, Mbunge ambaye Kijiji chake kilikuwa cha kwanza Tanzania, hii ni kampeni kambambe ambayo tunaenda kuifanya Tanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, lakini tunaenda kuzishindanisha Wizara zote, Wizara ya Jenista Mhagama na Wizara ya Lukuvi yupi katika eneo lake alitunza mazingira mazuri. Kwa hiyo, Wizara zote zitashindana, Taasisi zote za Serikali zitashindana, Taasisi za, *Private Sector* zote zitashindana. Hii ni kampeni kambambe. Tunaenda kushindanisha *hotel* zote kuanzia *One Star to Five Star* mpaka *Guest House* ipi ilitunza mazingira mazuri. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, tunaenda kushindanisha vyuo vikuu vyote Tanzania ni chuo gani kilikuwa *the best* ndani ya Tanzania katika utunzaji wa mazingira. Tunaenda kushindanisha vyuo vya kati vyote vilivyoweza kutunza mazingira mazuri, tunaenda kushindanisha shule za Sekondari na Shule za Msingi. Hospitali za Rufaa za Mikoa, za Wilaya, vituo vya afya mpaka nani hii, katika upande huu wa elimu na upande wa afya watakaoshinda tunawapa *special bonus*.

Mheshimiwa Spika, naomba niwaambie Wabunge zile shule za sekondari zitakazoshinda tumekusudia tuwape magari maalum ya shule, shule kumi bora tunaenda kuzitafuta.

Kwa hiyo, Wabunge kazi kwenu tunataka tuwashangilie Wabunge kumi ambao shule zao kumi zimepata magari hapa hapa Bungeni jambo hili tunataka tulifanye, hii ni kampeni kabambe. Lakini tunaenda kushindanisha migodi yote ipi inatiliisha maji ya sumu kuharibu afya ya wananchi, kwa hiyo, tunaenda kushindanisha migodi yote na hali kadhalika tunaenda kushindanisha Hifadhi zetu zote. Tunataka tupate Hifadhi bora. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, lakini naomba niwaambie maeneo hayo yote na tutapata zaidi ya washindi 152, washindi hao tutawapeleka kwa ajili ya *Local Tourisms* tutawafanya kuwapeleka katika hifadhi mojawapo ya kitalii wakiwapo Wabunge maeneo yao waliyoshinda hii yote itakuwa ni *special* kazi ya Wizara hii. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, katika kampeni hii tutaenda kufanya jambo lingine kubwa katika kampeni kabambe. Suala zima la upandaji wa miti ya matunda katika taasisi zote tunaenda *ku-add value* katika *agenda* ya *nutrition* katika Taifa letu. Na nimesema hapa wazi kwamba katika zile shule zinazoshinda licha ya upatikanaji wa magari ya shule tutaenda kuwapa suala zima la madawati na vifaa vya kujifundishia katika maeneo yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, haya yote waliyojadili Wabunge haya yapo katika Kampeni Kabambe ya Kimazingira ambayo Tanzania tutaiendesha mpaka 2025 kitaeleweka ndani ya Tanzania. Nini dhamira yetu? Tunataka tuone kwamba wageni wanapokuja waseme Barani Afrika miongoni mwa nchi iliyotunza mazingira ni Tanzania. Tunataka tuthubutu kufanya hivyo. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge haya yote mliojadili ndugu zangu naomba ni, naomba yapo. Na tarehe 5 Juni, tutawaalika Wabunge wote katika suala zima la uzinduzi wa hiyo Kampeni Kabambe. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kampeni hii itakuwa na mabalozi maalum wakiwepo na Wabunge, tutawachagua Wabunge wawili, watakuwa mahiri, sijajua ni nani atakuwa, aidha Mheshimiwa Ester Bulaya ama ni nani sijajua ni nani. Hao Wabunge wawili na Mheshimiwa Kunambi pale anapiga debe kwa hiyo tutapata Wabunge wawili hao ni balozi. Lakini tutawachukua vijana wasanii wenye ushawishi mkubwa katika jamii kuwa mabalozi wetu katika suala zima la kampeni ya mazingira. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Spika, tutakuwa na watu ambao, watu ambao kutoka *Private Sector* ambao wanauwanda mpana wa kimazingira kushirikiana na Serikali katika agenda hii moja

tunataka tuweke katika *East Africa Community* Tanzania tunataka tuwe ikiwezekana watu wa mfano tunaopigiwa mfano katika upande wa mazingira. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba niwaambie Waheshimiwa Wabunge hoja zote hizi zote tumezija. Mlisema mambo ya *NEMC*, ni kweli *NEMC* kidogo ilikuwa ni tatizo lakini nimeanza kazi nao.

Mheshimiwa Spika, leo hii nimekutanisha wawekezaji wote waliokuwa na changamoto na ile inayoitwa *TAM* (Kibali cha Mazingira), watu wengine mpaka walikuwa wanalia pale wanasema wana miaka mitatu hawajapata kibali. Nimetoa maagizo nikasema haiwezekani shemeji yangu kwa mfano Ndugai anataka akaweke kituo cha mafuta pale Kongwa miezi sita hajapata kibali cha mazingira. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, watu wanapata *frustration*, watu wanataka kufanya uwekezaji lakini *NEMC* imekuwa kikwazo. Kwa hiyo, nimetoa maelekezo mahsusi, *tumei-categorize* miradi, *group A* na *group B*, hii yote tunataka tuibadilishe nchi yetu. Naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge hapa halali mtu, ni mkikimkiki mpaka kieleweke. Nataka watu waisome Tanzania ya mfano kwanza upande wa Muungano lakini upande wa mazingira, tunataka tusonge mbele. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, mwisho nimshukuru sana dada yangu Mheshimiwa Umy Mwalimu, mchakato huu wa bajeti katika Wizara hii alianza yeye. Naomba nimshukuru sana. Kipekee nimshukuru dada yangu, Mheshimiwa Jenista Mhagama, huyu mama Ndugu zangu anapata taabu sana, kipindi hiki cha Bunge sisemi lakini kama ndiyo nyie wengine mngekuwa mnapiga *dash* kila siku, kazi yake ni kubwa yuko *busy*. Hata usiku hawezi kupumzika, naomba nizungumze ukweli. Huyu mama naomba niwaambie, kama kazi hii angepewa Ndugu yangu Mheshimiwa Musukuma ndani ya siku hizi zote tunazokaa hapa naomba niwaambie katika yale mambo fulani asingeweza kabisa kwa kazi hii.

Mheshimiwa Jenista Mwenyezi Mungu akulipe sana. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo yote, sasa naomba niseme naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**  
Mheshimiwa Spika, naafiki. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imetolewa na imeungwa mkono kweli kweli. Tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa namna ulivyohitimisha hoja yako na namna ulivyotuhakikishia Waheshimiwa Wabunge kwamba mambo yataenda.

Naomba niwataarifu Waheshimiwa Wabunge kwamba nilikuwa na taarifa Mheshimiwa Waziri wa Fedha alikuwa amezidiwa na *stress* lakini sasa ameweza kuja. Baada ya lile goli moja la juzi hajaweza kufanya kazi kabisa. Mheshimiwa Mwigulu Nchemba yaliyopita yamepita bwana, tsubiri tarehe 8 Mei. Sasa kama saa hizi tu unaanza kuchanganyikiwa tarehe 8 itakuwaje bwana? *(Makofi/Kicheko)*

Basi tunaendelea Waheshimiwa Wabunge, Katibu.

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

#### **KAMATI YA MATUMIZI**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu.

**NDG. HUSSEIN ATHUMANI – KATIBU MEZANI:**

#### **MATUMIZI YA KAWAIDA**

#### **FUNGU 31 – OFISI YA MAKAMU WA RAIS**

Kifungu 1001 – *Administration & Human Recourse*  
*Division* .....Sh. 3,785,765,560

**MWENYEKITI:** Ni Mshahara wa Waziri, nina majina mawili tu hapa. Tuanze na Khalifa Mohamed Issa.

**MHE. KHALIFA MOHAMED ISSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwa kweli Mheshimiwa Waziri alipokuwa akihitimisha hoja yake mambo mengi kayaelezea.

Ninamuamini kaka yangu Mheshimiwa Jafo ni mtekelezaji lakini hata hivyo, nataka kujua tu kwamba kama nilivyosema katika mchango wangu Visiwa vile vya Zanzibar hasa vile vidogo vidogo viko hatarini sana kuzama na nilitaka kupata *commitment* yake tu kama nilivyomtaka mwanzo, ni lini yeye na wataalam wake wanaweza kuja kuona hiki nachozungumzia. Wataalam wanasema *seeing is believing*, kwa hiyo, aje aone ile athari ilivyo kwa kweli kumeathirika sana; Unguja na Pemba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilitaka *commitment* yake tu, sikusudii kukamata shilingi.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa. Mheshimiwa Waziri lini utakwenda kuangalia mambo ya Zanzibar.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nimshukuru sana Ndugu yangu kwa mchango mzuri lakini na kwa hoja yake hii nzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Inshaalah* Mungu akijaalia mara baada ya Ramadhan na kabla Bunge halijaisha nitafika kule kutembelea kwa upana wake zaidi. Nimesema baada ya Ramadhan kwa sababu kuna urojo kule una raha yake, ukienda wakati swaumu imeisha unaweza ukakaribishwa vizuri zaidi. Ahsante sana. (*Makofi/Kicheko*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri kwa ufafanuzi huo. Mheshimiwa Asya Mwadini.

**MHE. ASYA MWADINI MOHAMMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri alipokuja hapa mbele majibu yake yamejitosheleza kuhusiana na maswali yangu niliyoyapanga kumuuliza. Kwa hiyo, namshukuru sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Waziri hongera sana bwana, nadra kupata *approval rate* ya kiasi hiki. Kwa hiyo, hongera sana maelezo yako yameisafisha kila jambo. Naomba tumpigie makofi Mheshimiwa Waziri Jafo. (*Makofi*)

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 1002 – <i>Finance and Accounts Unit</i> .....	Sh. 371,217,000
Kifungu 1003 – <i>Policy and Planning Division</i> .....	Sh. 715,983,000
Kifungu 1004 – <i>Government Communication Unit</i> .....	Sh. 198,785,000
Kifungu 1005 – <i>Internal Audit Unit</i> .....	Sh. 242,024,000
Kifungu 1006 – <i>Procurement Management Unit</i> .....	Sh. 296,121,000
Kifungu 1007 – <i>Information and Communication Technology Unit</i> .....	Sh. 373,655,000
Kifungu 1008 – <i>Legal Services Unit</i> .....	Sh. 352,736,000
Kifungu 2001 – <i>Union Secretariat</i> .....	Sh. 808,046,000
Kifungu 5001 – <i>Environment</i> .....	Sh. 5,994,151,440

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

## **FUNGU 26 – MAKAMU WA RAIS**

Kifungu 1001 - *Administration and Human Resources Management*.....Sh. 8,719,077,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

## MIPANGO YA MAENDELEO

### FUNGU 31 - OFISI YA MAKAMU WA RAIS

Kifungu 1001 – <i>Administration &amp; Human Resources</i> <i>Division</i> .....	Sh. 3,880,000,000
Kifungu 5001 – <i>Environment</i> .....	Sh. 2,970,788,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. HUSSEIN ATHUMANI – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Matumizi imekamilisha kazi yake.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri kabla hatujarudi huku, ile milioni 400 tuliyokubaliana inakuwa *counterpart funds* ya huku itarekebishwa baadaye au ikoje hii? Kwenye Kamati ya Bajeti tulizungumzia suala hili sijui kama ulikuwepo au Waziri wa Fedha ndiyo anakumbuka vizuri zaidi? Tulikubaliana milioni 400 itakwenda Ofisi ya Makamu wa Rais kama ni sehemu ya *commitment* ya Tanzania kwa miradi hii ya maendeleo ambayo fedha zake ni za nje na hatukuwa na fedha ya ndani, kwenye Kamati ya Bajeti tukawa tumekubaliana kwamba mtawaongeza milioni 400 kwa ajili ya jambo hilo. Sijui tutakutana na wewe Waziri wa Fedha wakati huo au inakuwaje? Nafikiri mnakumbuka Mheshimiwa Jenista?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA NA WATU WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaikumbuka na tumeshaiwekea utaratibu na wakati wa Bajeti ya Wizara ya Fedha *addendum* ambayo itakuwa inaeleza kiasi hicho cha fedha ili kwenda kwenye ile *counter fund* kwa ajili ya fedha za mazingira za *development* itakuwa *considerable*. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana maana kwenye vitabu hivi haimo, kwa hiyo, tulitaka *commitment* hiyo ili wakati huo ukifika hiyo nayo iweze kupatikana kwa ajili ya Ofisi ya Makamu wa Rais.



Waheshimiwa Wabunge, Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Mheshimiwa Waziri taarifa.

## TAARIFA

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabla sijatoa hoja, napenda tu kuwasilisha kwako kwamba katika hiki kitabu chetu cha maendeleo hii milioni 400 ilishakuwa *considered* kwa maana kwamba ilishaingizwa katika hiki kitabu cha maendeleo, iko hapa katika *figure*.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kuwa Bunge lako Tukufu limekaa kama Kamati ya Matumizi na limekamilisha kazi yake. Hivyo, naomba taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, naafiki. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, hoja imetolewa na imeungwa mkono. Sasa naomba kama ilivyo ada niwahoji kwamba sasa mkubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2021/2022- Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira yalipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Wote wameafiki kabisa Bajeti hii. Kwa kweli kwa niaba ya Waheshimiwa Wabunge, niwapongeze sana Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kazi nzuri ambayo mmekuwa mkifanya, tunakutakia kila la kheri Mheshimiwa Waziri kwa bajeti hii kwa mwaka ujao wa fedha na wasaidizi wako wote kuanzia Katibu Mkuu na timu nzima. (*Makofi*)

Mazingira ni eneo ambalo linahitaji kutazamwa kipeke yake kabisa. Ni moja ya eneo ambalo kama ingekuwa tuna fedha za kutosha na za ziada tungeweza kuweka hela nyingi zaidi kwenye mazingira kwa sababu ni tatizo kubwa kila mahali, tatizo kabisa. Kama sisi wa Mikoa ya Dodoma, Shinyanga kwenye zawadi zako Mheshimiwa Waziri sijui kama tutabahatisha maana hali yetu si nzuri, haipendezi. Si Dodoma ile ambayo inatakiwa iwe kwa sababu juhudi za hifadhi ya mazingira zinatakiwa ziongezeke zaidi na zaidi na hasa kwanza kuzuia tu uharibifu, peke yake tu ni *plus* kubwa sana kwenye masuala ya mazingira. Kwa hiyo, tuko na ninyi katika jambo hili, tutasaidiana hatua kwa hatua.

Mwenyekiti wa Bodi ya *NEMC* mama yetu Profesa una kazi ya ziada. Hiyo *NEMC* uliyopewa mama ni shughuli pevu. Mimi ni mwana mazingira, nakumbuka wakati ule yuko Mheshimiwa January Makamba nilimuita ofisini kwangu yeye na Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu waliokuwepo na watu wa *NEMC*, nikazungumza nao sana masuala mbalimbali ambayo *NEMC* inakalia, mambo hayaendi na haibadiliki. Amekuja Mheshimiwa Simbachawene, amekuja Mheshimiwa Umy *NEMC* ni ile ile.

Kwa hiyo, *NEMC* ni tatizo, huo ndiyo ukweli kama alivyosema Waziri mpaka wawekezaji wengine wanatoa machozi, masharti magumu na ya ajabu ajabu. (*Makofi*)

Mimi ninayewaambia hayo ni mwana mazingira mwenzenu lakini siridhiki kabisa na utendaji wenu wa kazi. *NEMC* labda ifumuliwe ndiyo itakaa sawasawa kwa sababu hawasikii. Tumeshakaa nao huko pembeni *one to one* sisi wenyewe jamani hivi hatuwezi kwenda lakini wapi! Wakiritimba, wanageuza sijui kuwa nini na hivi mama ni

Profesa wanageuza *NEMC* kuwa ni *faculty* ya *some university* kwamba tafuta mtaalam aandike, andiko liende, lirudi wanasahisha, linarudi, linaenda, wanasahisha tena halafu wewe unaingia gharama, umtafute huyo sijui mwezeshaji na wao wenyewe *NEMC* uwalipie ndiyo waje waangalie *site* yako, waende wasahihishe tena, sasa hii *thesis* isiyoisha shida nini?

**MBUNGE FULANI:** Wizi huoi!

**SPIKA:** Sahisha rudisha, sahisha rudisha, mwaka hadi mwaka, yaani wamegeuza kabisa *NEMC* ni *academic institution* badala ya kuwa ni chombo cha uwezeshaji wa kuhakikisha mambo yanakwenda. Kwa miradi hiyo mikubwa tunaelewa kama ya gesi na *petrol* na mingine inayofanana na hiyo labda ya viwanda vikubwa, hata yenyewe nayo mnajipa *span* labda miezi sita mmevuka, kama mtu anawekeza anawekeza kama anaacha anaacha. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, mnajua nchi hii hata ukitaka kuchimba choo cha nyumbani kwako, unatakiwa upate tathmini ya athari ya mazingira? Mnajua kwa sheria ile au hamfahamu? Hata ukitaka kujenga shule ya msingi hamuwezi kujenga tu mnatakiwa muwe na hati ya tathmini ya athari ya mazingira ni kwamba tu Serikali haijabana vizuri lakini inatakiwa kwa kila jambo la *development* unalotaka kufanya kwa sababu litaathiri mazingira liwe na hati ya mambo hayo. Sasa kwa walivyo, hatuwezi kwenda namna hiyo, ni wakiritimba mno.

Kama hiyo ya mafuta, kila mahali chupa za mafuta zimejaa, mnaotembea vijijini si mnaona? Chupa za *petrol*, chupa za nini kila mahali zipo, kwa nini hivyo? Ni kwa sababu ya ukiritimba vinginevyo biashara hii ingefanyika kwa kutumia *technology* za kawaida watu wakamudu kuwekeza na Serikali ikapata kodi yake. Maana yale mafuta yote yanauzwa kodi ya Serikali hakuna kwa yule wa mwisho ambaye anamuuzia yule mwenye pikipiki, bodaboda na kitu cha namna hiyo, ni ukiritimba tu. (*Makofi*)

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri ukifikiri utaenda kupakapaka rangi *NEMC* tutarudi hapa mwakani na tutakuambia maneno haya haya, *NEMC* hawasikii. *NEMC* waache kuwa *academic institution* wabadilike. Profesa pale hujaenda *ku-extend arm* ya *academic*, hapana, ni kwa ajili ya *ku-facilitate* mambo yaende, ndiyo tunachotaka sisi kuona *results*. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, kwa kuwa mambo yetu yamekamilika, tena *within time*, nawashukuruni sana kwa ushirikiano, tumeenda vizuri, tumeshakamilisha kila jambo, kwa hatua hiyo basi, naomba niahirishe shughuli za Bunge hadi kesho saa 3.00 kamili asubuhi.

(Saa 11.45 Jioni Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumatano, Tarehe 28 Aprili, 2021 Saa Tatu Kamili Asubuhi)